JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

RIPOTI YA JUMLA YA UKAGUZI WA UFANISI KWA KIPINDI KINACHOISHIA MACHI, 2021

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU
WA HESABU ZA SERIKALI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Dira

Kuwa kituo bora cha ukaguzi wa hesabu katika sekta za umma

Dhamiri

Kutoa huduma za ukaguzi wa hesabu zenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma. Katika kutoa huduma zenye ubora, Ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:

Uadilifu

Kuwa taasisi adilifu inayotoa huduma bila upendeleo.

Weledi

Tunalenga kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu kwa kuzingatia taratibu bora.

Uaminifu

Tunahakikisha tuna kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala wa sheria.

Mkazo kwa watu

Tunalenga kufanikisha matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni nzuri wa kuhudumia wateja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.

Uvumbuzi

Kuwa taasisi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya taasisi.

Matumizi bora ya rasilimali

Kuwa taasisi inayothamini na kutumia kwa umakini mkubwa rasilimali za umma ilizokabidhiwa.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, DODOMA.
Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: +255 (026) 2321759, Nukushi: +255(026)2117527,
Baruapepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Kwa majibu, tafadhali taja:
Kumb. **CGA 319/421/01A/6** **28 Machi 2021**

Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
Chamwino,
40400 DODOMA.

YAH: KUWASILISHA RIPOTI YA JUMLA YA MWAKA YA UKAGUZI WA UFANISI NA UKAGUZI MAALUMU KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 MACHI 2021

Kwa mujibu wa Kifungu cha 143 (4) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara) na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008, nina furaha kuwasilisha Ripoti ya Jumla ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalumu kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi 2021.

Ripoti hii inajumuisha Ripoti 9 za Kaguzi za Ufanisi katika sekta ya elimu.

Ninawasilisha

Charles E. Kichere

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI ..... **VI**

ORODHA YA VIELELEZO ..... **X**

DIBAJI ..... **XIII**

SHUKRANI ..... **XVII**

MUHTASARI ..... **XIX**

SURA YA KWANZA **1**

UTANGULIZI **1**

1.1 Usuli wa ukaguzi wa ufanisi 1
1.2 Mamlaka ya kukagua 1
1.3 Madhumuni ya ripoti 2
1.4 Lengo Kuu la Ripoti 2
1.5 Umuhimu wa Elimu 3
1.6 Sababu za kufanyika Ukaguzi 4
1.7 Mchakato wa Udhibitisho wa Takwimu na Taarifa Zilizotolewa katika Ripoti 5
1.8 Muundo wa Ripoti 5

SURA YA PILI **7**

MFUMO WA ELIMU TANZANIA **7**

2.1 Utangulizi 7
2.2 Sera na Mfumo wa Kisheria Unaosimamia Utoaji wa Elimu 7
2.3 Mfumo wa Elimu Rasmi na Mafunzo Nchini 11
2.4 Ufadhili wa Utoaji wa Elimu 18

SURA YA TATU **21**

RASILIMALI KWA AJILI YA UTOAJI WA ELIMU **21**

3.1 Utangulizi 21
3.2 Maboresho Yaliyoonekana Katika Utoaji wa Elimu Nchini 21
3.3 Kupanga na Kuweka Bajeti ya Rasilimali kwa ajili ya Utoaji wa Elimu Nchini 24
3.4 Usambazaji na Utoaji wa Rasilimali kwa Huduma za Elimu 28
3.5 Upungufu wa Vifaa na zana kwa ajili ya Utoaji Elimu na Mafunzo 41
3.6 Ufadhili wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu 45

SURA YA NNE **48**

UDHIBITI WA UBORA WA ELIMU **48**

4.1 Utangulizi 48
4.2 Mifumo ya Udhibiti na Uhakiki Ubora kwa Elimu ya Msingi na Sekondari 48
4.3 Mifumo ya Udhibiti na Uhakiki wa Ubora kwenye Utoaji wa Elimu ya Juu ... 53

SURA YA TANO **58**

UTOAJI WA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI **58**

5.1 Utangulizi 58
5.2 Matokeo ya Ukaguzi 58

SURA YA SITA **78**

USIMAMIZI WA ELIMU KWA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUMU **78**

6.1 Utangulizi 78
6.2 Ugawaji na Uratibu wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia Elimu Maalumu 78
6.3 Mchango wa Wadhibiti Ubora katika Utoaji wa Elimu Maalumu 87
6.4 Utungaji na Usimamizi wa Mitihani kwa ajili ya Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu 94

SURA YA SABA 97

UTOAJI WA MAFUNZO KWA WALIMU KAZINI 97

7.1 Utangulizi 97
7.2 Msukumo wa Ukaguzi 97
7.3 Hoja za Ukaguzi 98

SURA YA NANE 119

UPATIKANAJI WA ELIMU NA MAFUNZO BORA YA UFUNDI STADI 119

8.1 Utangulizi 119
8.2 Kuna Upungufu Mkubwa wa Ujuzi kwenye Kada za Chini na Kati 119
8.3 Mfumo wa Udhibiti Ubora wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Haukuwa na Tija 130
8.4 Zifuatazo ni Sababu za Mapungufu Yaliyobainika 133
8.5 Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Kutopatiwa Fedha Inavyotakiwa 141
8.6 Kutokuwepo kwa Tija kwa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi 144

SURA YA TISA 146

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA ELIMU KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NA UTAFITI 146

9.1 Utangulizi 146
9.2 Mipango na Shughuli za Awali za Miradi 146
9.3 Uratibu wakati wa Utekelezaji wa Miradi ya Uimarishaji Uwezo wa Utafiti 151
9.4 Ufanisi wa Programu 153
9.5 Ufadhili wa Programu 160
9.6 Uendelevu wa Miradi katika Taasisi 171

SURA YA KUMI 173

MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU USIMAMIZI WA ULIPAJI NA UREJESHAJI WA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU 173

10.1 Utangulizi 173
10.2 Matokeo ya Ukaguzi 173
10.3 Sababu ya Udhaifu Uliojitokeza kwenye Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu 181
10.4 Athari za Mapungufu Yaliyobainika 188

SURA YA KUMI NA MOJA 191

URATIBU NA UFUATILIAJI WA UTOAJI WA ELIMU 191

11.1 Utangulizi 191
11.2 Matokeo ya Ukaguzi 191
11.3 Ufuatiliaji wa Shughuli za Utoaji wa Huduma ya Elimu Chini 197

SURA YA KUMI NA MBILI 207

HITIMISHO 207

12.1 UTANGULIZI 207
12.2 HITIMISHO LA JUMLA..... 207
12.3 HITIMISHO MAALUMU 208

SURA YA KUMI NA TATU 214

MAPENDEKEZO.....214

13.1 UTANGULIZI 214
13.2 MAPENDEKEZO MAALUMU YA UKAGUZI..... 214

ORODHA YA MAJEDWALI

Idadi ya Jedwali	Maelezo	Ukurasa
Jedwali 2.1	Ulinganisho wa Bajeti ya Jumla ya Serikali na ya Sekta ya Elimu	19
Jedwali 2.2	Bajeti ya Serikali Ikilinganishwa na Bajeti ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia	20
Jedwali 3.1	Bajeti ya Utoaji Elimu kwa Uhitaji Maalumu	25
Jedwali 3.2	Idadi ya Wanufaika wa Mikopo Waliopangwa Kupewa Ankara	26
Jedwali 3.3	Bajeti ya Sekta ya Elimu Ikilinganishwa na Bajeti ya Jumla ya Serikali	29
Jedwali 3.4	Jumla ya Bajeti na Kiasi Halisi Kilichotolewa kwa ajili ya Utoaji wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu kuanzia Mwaka 2014 - 2018	30
Jedwali 3.5	Bajeti Ikilinganisha na Fedha Zilizotolewa kwa ajili ya Miundombinu ya Shule za Msingi	30
Jedwali 3.6	Asilimia ya Kiasi Halisi Kilichotolewa kwenye Bajeti	31
Jedwali 3.7	Kiasi Kilichotolewa katika Asilimia kwa Miradi ya SIDA	34
Jedwali 3.8	Kiasi Kilichotengwa Ikilinganishwa na Kiasi Kilichopokelewa kuanzia Mwaka 2015/16 - 2019/20	35
Jedwali 3.9	Ugawaji wa Wafanyakazi miongoni mwa Wadau Muhimu	39
Jedwali 3.10	Vifaa ambavyo Havikuwepo katika Shule Zilizotembelewa	42
Jedwali 3.11	Uchambuzi wa Madawati katika Shule za Msingi Nchini, kuanzia Mwaka 2012 - 2018	43
Jedwali 3.12	Vifaa Vilivyopangwa Kununuliwa chini ya Programu Ndogo ya Malaria ya Kuboresha Maabara	44
Jedwali 3.13	Vyanzo vya Fedha za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuanzia Mwaka 2012/13 - 2015/16	45
Jedwali 4.1	Makundi ya Zana za Udhibiti na Uhakiki wa Ubora Zilizotengenezwa na Chuo Kikuu cha Ardhi kuanzia mwaka 2015 - 2020 kwa Ufadhili wa SIDA.	55
Jedwali 5.1	Mchanganuo wa Upatikanaji wa Madawati Nchini, kuanzia mwaka 2014 - 2018	61

Idadi ya Jedwali	Maelezo	Ukurasa
Jedwali 5.2	Fedha za Serikali Zilizotumika Kukarabati Shule Kongwe kwa Awamu ya IIII	64
Jedwali 5.3	Hali ya Uwiano wa Mwalimu kwa Mwanafunzi kwa Shue za Wanafunzi wenye Ulemavu wa Kuona	69
Jedwali 5.4	Hali ya Uwiano wa Mwalimu kwa Wanafunzi wenye Ulemavu wa Kusikia	70
Jedwali 5.5	Hali ya Uwiano wa Mwalimu kwa Wanafunzi wenye Ulemavu wa Akili	70
Jedwali 5.6:	Mabadiliko ya Uwiano wa Wanafunzi na Walimu, Madawati, na Madarasa kabla na baada ya Elimu ya Msingi na Sekondari Kutolewa Bure	75
Jedwali 5.7	Mabadiliko ya Uwiano wa Mwanafunzi na Mwalimu, Madawati na Madarasa kabla na baada ya Sera ya Elimu Bure	77
Jedwali 6.1:	Hali ya Vifaa Vilivyopo na Vinavyohitajika kwa Ajili ya Kujifunzia na Kufundishia Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu katika Shule Zilizotembelewa	79
Jedwali 6.2	Fedha Ziliotengwa na Serikali kwa ajili ya Elimu Maalumu (kiasi katika milioni – TSh.)	80
Jedwali 6.3	Kaguzi Zilizofanyika katika Shule za Msingi za Elimu Maalumu Zilizotembelewa	88
Jedwali 6.4	Shule za Elimu Maalumu Zilizowekwa Katika Mpango wa Kukaguliwa katika Kipindi cha Ukaguzi	90
Jedwali 6.5	Idadi ya Wathibiti-ubora wa Shule Ikilinganishwa na Idadi ya Shule za Elimu Maalumu katika Halmashauri	91
Jedwali 6.6	Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa ili Kuboresha Elimu Maalumu katika Shule Zilizotembelewa	93
Jedwali 6.7	Hali ya Kuzingatia Sifa za Wasimamizi Wanaosimamia Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu	95
Jedwali 7.1	Aina za Mafunzo Yaliyotolewa kwa Walimu	103
Jedwali 7.2	Maudhui ya Mafunzo Mbalimbali Yaliyotolewa	104
Jedwali 7.3	Fedha Zilizotolewa kwa ajili ya Mafunzo ya Huduma	110

Idadi ya Jedwali	Maelezo	Ukurasa
Jedwali 7.4	Bajeti ya Mafunzo katika TIE na ADEM (katika bilioni - Tsh.)	111
Jedwali 8.1	Ulinganifu wa Ujuzi kati ya Tanzania na Nchi zingine za Uchumi wa Kati	120
Jedwali 8:2	Mgawanyo wa Vyuo Vyenye Usajili wa Awali kwa Kanda	132
Jedwali 8.3	Idadi ya Kaguzi za Ubora Zilizofanywa kuanzia mwaka 2013/14 - 2018/19	133
Jedwali 8.4:	Uwiano wa Darasa kwa Mwanafunzi kwenye Vyuo Vilivyotembelewa	139
Jedwali 8.5	Mgawanyo wa Fedha za Bajeti kwa Makundi ya Vyuo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuanzia mwaka 2013 - 2019	143
Jedwali 8.6	Mgawanyo wa Fedha za Bajeti kwenye Kanda kuanzia mwaka 2013/14 - 2018/19	144
Jedwali 9.1	Vihatarishi Vilivyojirudia na Matokeo yake Hasi	147
Jedwali 9.2	Mabadiliko Makubwa ya Mradi na Changamoto Zilizotokana na Mabadiliko Hayo	150
Jedwali 9.3	Hali ya Utekelezaji wa Shughuli za Programu katika Tume ya Sayansi na Teknolojia	153
Jedwali 9.4	Orodha ya Shughuli na Fedha Zilizotumika lakini Hazioneshwi katika Mpango Mpya wa Mwaka	154
Jedwali 9.5	Kufanikiwa kwa Malengo ya Programu ya Jumla	155
Jedwali 9.6	Malengo Muhimu Yaliyochelewa Kufikiwa wakati wa Utekelezaji wa Programu za Kuimarisha Utafiti	156
Jedwali 9.7	Maeneo ya Utafiti Yaliyoimarika ikiwa ni Matokeo ya Kubadilishwa kwa Programu	158
Jedwali 9.8	Kiwango cha Maboresho ya Upatikanaji wa Mtandao kwa ajili ya Kupata Taarifa za Tafiti na Vifaa vya Mafunzo	159
Jedwali 9.9	Matumizi ya Fedha Chini ya Kiwango kwa Shughuli za Machapisho pamoja na Makongamano kwa Kipindi cha Miaka ya Fedha 2017/18 na 2018/19	170
Jedwali 9.10	Mambo Yanayoweza Kuathiri Uendelevu wa Miradi	171

Idadi ya Jedwali	Maelezo	Ukurasa
Jedwali 10.1	Idadi ya Wanufaika wa Mikopo na Mikopo Inayostahili Kulipwa kwa Mwaka	175
Jedwali 10.2	Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mikopo Inayostahili Kulipwa kwa Mwaka	177
Jedwali 10.3	Marejesho ambayo Hayakupunguzwa wakati wa Utoaji wa Taarifa ya Makusanyiko	178
Jedwali 10.4	Bakaa ya Mikopo kama Ilivyoripotiwa kwenye Kanzidata ya Mishahara ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Kanzidata ya Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo ya Bodi ya Mikopo	179
Jedwali 10.5	Idadi ya Wadhamini Waliotafutwa Ikilinganishwa na Jumla ya Idadi ya Wadaiwa Sugu wa Mikopo	185
Jedwali 11.1	Hali ya Ofisi za SIDO katika Suala la Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini	200
Jedwali 11.2	Mapungufu katika Kuripoti Maendeleo ya Programu	203

ORODHA YA VIELELEZO

Namba	Maelezo	Ukurasa
Kielelezo 2.1	Sheria Kuu Zinazosimamia Utoaji wa Elimu Nchini	9
Kielelezo 2.2	Muundo wa Mfumo Rasmi wa Elimu na Mafunzo Nchini Tanzania	12
Kielelezo 2.3	Uhusiano kati ya Watendaji Muhimu katika Sekta ya Elimu Tanzania	18
Kielelezo 3.1	Matumizi ya Fedha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi	36
Kielelezo 3.2	Upatikanaji wa Walimu kwa ajili ya Elimu na Mafunzo Bora ya Ufundi Stadi	38
Kielelezo 3.3	Upungufu wa Rasilimali-watu kwa ajili ya Elimu ya Mahitaji Maalumu	40
Kielelezo 4.1	Uwiano wa Wahakiki Ubora wa Elimu ya Wenye Mahitaji Maalumu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizotembelewa	49
Kielelezo 4.2	Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Wadhibiti Ubora wa Shule kutoka Shule 10 Zilizotembelewa katika Halmashauri 12	50
Kielelezo 5.1	Uchambuzi wa Idadi ya Wanafunzi Wanaokosa Madarasa katika Shule za Msingi Nchini kuanzia Mwaka 2014 - 2018	60
Kielelezo 5.2	Mchanganuo wa Upatikanji wa Vyoo kwenye Shule za Msingi Nchini kuanzia Mwaka 2014 - 2018	62
Kielelezo 5.3	Idadi ya Walimu wa Elimu ya Msingi ya Wenye Mahitaji Maalumu Waliopatiwa Mafunzo	66
Kielelezo 5.4:	Hali ya Walimu Waliopata Mafunzo kwenye Halmashauri Zilizotembelewa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19	67
Kielelezo 6.1	Idadi ya Walimu Waliopewa Mafunzo ya Elimu Maalumu kwa Shule za Msingi	86
Kielelezo 7.1	Hali ya Mafunzo ya Walimu katika ngazi ya Kitaifa	99
Kielelezo 7.2:	Hali ya Utoaji wa Mafunzo katika Mikoa Iliyotembelewa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19	100
Kielelelzo 7.3	Maofisa Waliopatiwa Mafunzo katika Halmashauri Zilizotembelewa kuanzia Mwaka2015/16 – 2018/19	101

Kielelezo 7.4	Asilimia ya Fedha Zilizopokelewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Zote Zilizotembelewa	113
Kielelezo 8.1	Ulinganifu wa Mahitaji na Udahili wa Wanafunzi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuanzia Mwaka 2013/14 -2017/18	121
Kielelezo 8.2	Idadi ya Waombaji Waliochaguliwa Kujiunga na Vyuo vya Elimu na Ufundi Stadi kuanzia Mwaka 2013 - 2018	122
Kielelezo 8.3	Kiwango cha Kufikiwa Makadirio ya Udahili wa Wanafunzi wa Kike kuanzia Mwaka 2013/14 – 2018/19	123
Kielelezo 8.4	Ulinganisho wa Uandikishaji wa Wanafunzi wa Kike na wa Kiume kwenye Fani Zinazoendana na Mpango wa Maendeleo	124
Kielelezo 8.4(a)	Mwenendo wa Udahili wa Wanafunzi wenye Ulemavu kwa Aina ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa Ulemavu kuanzia Mwaka 2013 - 2018	125
Kielelezo 8.4(b)	Mwenendo wa Udahili wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu kuanzia Mwaka 2013 - 2018[1]	126
Kielelezo 8. 5	Asilimia ya Udahili wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu Kulingana na Mtoahuduma	127
Kielelezo 8.6	Usambazaji wa Vituo vya Elimu ya Ufundi katika Kanda za Kijiografia Nchini	128
Kielelezo 8.7	Mwenendo wa Wanafunzi Waliodahiliwa kwenye Sekta Muhimu za Kiuchumi	130
Kielelezo 8.8	Hali ya Usajili wa Vyuo kwenye Kanda	131
Kielelezo 8.9	Mahitaji ya Walimu wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuanzia Mwaka 2013/14 - 2018/19	135
Kielelezo 8.10	Asilimia ya Walimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Wasio na Mafunzo ya Mbinu za Kufundishia	136
Kielelezo 8.11	Asilimia ya Madarasa Yaliyopo kwenye Vyuo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi	138
Kielelezo 8.12	Mahitaji, Uwepo, na Mapungufu ya Karakana kwenye Vyuo Vilivyotembelewa	140
Kielelezo 8.13	Mgawanyo wa Fedha za Kodi ya Maendeleo ya Ujuzi kwa ajili ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kunzia Mwaka 2014/15 - 2018/19 (bilioni Tsh.)	142

Kielelezo 9.1	Bajeti Iliyoidhinishwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	161
Kielelezo 9.2	Ucheleweshaji wa Utoaji wa Fedha za Programu	163
Kielelezo 9.3	Ukubwa wa Ucheleweshaji wa Kutuma Maombi ya Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Programu kuanzia Mwaka 2015/16 - 2019/20	164
Kielelezo 9.4	Utoaji wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Programu kuanzia Mwaka 2015/16 - 2019/20	165
Kielelezo 9.5	Asilimia ya Kiasi Kilichotengwa na Kutumika katika Kiwango cha Programu Ndogo kati ya Julai 2015 na Juni 2019	167
Kielelezo 9.6	Kiasi cha Ucheleweshaji wa Kulipa Posho za Wanafunzi	168
Kielelezo 9.7	Idadi ya Wanafunzi wa Shahada ya Umahiri ambao Walichelewa Kupata	169
Kielelezo 10.1	Mikopo Inayostahiki kwa kila Mwaka wa Kalenda Ikilinganishwa na Idadi ya Mikopo ya Uigizaji	176

DIBAJI

Ninayo furaha kuwasilisha Ripoti yangu ya Jumla ya Ukaguzi wa. Ripoti hii ya jumla inajumuisha ripoti 9 za ukaguzi wa ufanisi kuhusu utoaji wa elimu nchini. Wakaguliwa wakuu walikuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ; Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Taasisi ya Elimu Tanzania; Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi wa Elimu; na Baraza la Taifa la Mitihani. Wakaguliwa wengine waliohusika ni taasisi za utafiti na elimu ya juu, zikijumuisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania.

Ripoti hii inalenga kutoa taarifa kwa wadau (wabunge, maofisa wa serikali kuu na serikali za mitaa, wanahabari, wafadhili, na asasi za kiraia na zisizo za kiserikali kuhusiana na matokeo ya ukaguzi yaliyopo kwenye ripoti za ukaguzi wa ufanisi zilizofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali hadi kufikia Mwezi Machi, 2021. Ufafanuzi wa kina kuhusiana na taarifa zilizoandikwa kwa kifupi ndani ya ripoti hii unapatikana kwenye ripoti husika za kaguzi za ufanisi ambazo zilikabidhiwa kwa maofisa masuuli wa wizara na taasisi husika.

Ripoti hii inawasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara) na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008.

Chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila taarifa aliyotoa kwa mujibu wa Ibara Ndogo (2) ya Ibara iliyotajwa. Mara taarifa hiyo inapopokelewa, Rais

atamwelekeza Waziri husika kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kabla ya siku saba kupita toka kikao hicho cha Bunge kuanza. Ibara hiyo inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake kwa Spika wa Bunge iwapo Rais, kwa sababu zozote zile, atashindwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa Spika kama sheria inavyotaka.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 kumeimarisha uhuru wa utendaji wa Ofisi yangu katika kutimiza majukumu yake ya kikatiba. Uhuru wa utendaji wa Ofisi yangu utaniwezesha kupata taarifa na kuwa na udhibiti wa rasilimali zote zilizo chini ya Ofisi yangu, ikiwa ni pamoja na rasilimali-watu na fedha, ambazo zitaiwezesha Ofisi yangu kufanya kazi bila kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote, zikiwemo zile ninazozikagua.

Sheria hii imepanua mawanda ya ukaguzi kwa kunipa mamlaka ya kufanya ukaguzi wa ufanisi, ukaguzi wa utambuzi, ukaguzi wa mazingira, na ukaguzi maalumu. Aina hizi za ukaguzi ni zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za hesabu za fedha kama ambavyo tumekuwa tukifanya kwa miaka mingi.

Kimsingi, ripoti hii imeniwezesha kutoa maoni huru kwa Bunge kuhusiana na usahihi, uwajibikaji, uwazi, na uadilifu katika matumizi ya rasilimali za umma, hususani katika masuala ya utoaji wa huduma za elimu nchini. Ripoti hii imegusia zaidi kwenye maeneo ya usimamizi wa ubora wa elimu, usimamizi wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, utoaji wa mafunzo kwa walimu waliopo kazini, upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi, na utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Ripoti hii pia imegusia usimamizi wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu, utekelezaji wa programu za elimu kwa taasisi za utafiti na elimu ya juu, na uratibu na usimamizi wa wadau wanaohusika na utoaji wa elimu nchini.

Lengo kuu la kufanya aina hizi za ukaguzi ni kufanya tathmini ya matatizo yaliyobainishwa katika sekta husika, pamoja na kuangalia iwapo rasilimali zilizotengwa zimetumika kwa ufanisi kwa kuzingatia

uwekevu, tija, na ufanisi kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge kwenye maeneo yaliyotajwa.

Ni vizuri kufahamu kwamba wakati Ofisi yangu inafanya ukaguzi na kutoa ripoti ya utendaji wa serikali kuu, serikali za mitaa, na mashirika ya umma kulingana na sheria na taratibu zilizopo, wajibu wa kuhakikisha kuwa kuna ufanisi, uwekevu, na tija katika matumizi ya rasilimali za umma ni wa maofisa masuuli. Wakati huohuo, ni wajibu wa maofisa masuuli kuhakikisha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo niliyoyatoa yanatekelezwa kikamilifu.

Ni matarajio ya Bunge kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anahakiki usahihi wa taarifa za fedha na usimamizi wa rasilimali za umma katika serikali kuu, serikali za mitaa, na mashirika ya umma kuhusiana na tija na ufanisi kwenye utekelezaji wa programu mbalimbali za Serikali. Ofisi yangu inachangia kwa kutoa mapendekezo ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma. Kwa jinsi hiyo, serikali kuu, serikali za mitaa, mashirika ya umma, na Ofisi yangu kwa pamoja zinatoa mchango mkubwa kwa Bunge katika kuongeza na kujenga imani kwa wananchi kuhusu usimamizi wa rasilimali za umma. Ingawa majukumu yanatofautiana, lakini lengo ni moja kuhakikisha kunakua na usimamizi bora wa rasilimali.

Ili kukidhi matarajio ya wabunge na umma kwa ujumla, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya mapitio ya njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta ya umma. Aidha, Ofisi yangu inahakikisha ukaguzi wake unalenga na kuyapa kipaumbele maeneo muhimu yanayochangia au yanatarajiwa kuchangia maendeleo ya sekta ya umma hasa usimamizi wa masuala yahusuyo usalama wa wananchi wanapopata huduma mbalimbali. Hivyo, kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa rasilimali za umma.

Ninapenda kutambua juhudi kubwa ya wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa weledi na dhamira njema katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ikiwa pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi vya kutosha, mishahara duni, na wakati mwingine kufanya kazi kwenye maeneo yasiyofikika kirahisi.

Ni matumaini yangu kuwa Bunge litaona umuhimu wa taarifa zilizomo katika ripoti hii katika kuiwajibisha Serikali kuhusiana na jukumu lake la usimamizi wa rasilimali za umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania.

Charles E. Kichere
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
Dodoma, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
28 Machi, 2021

SHUKRANI

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioweka mazingira wezeshi kwangu kuweza kutimiza wajibu wangu wa kikatiba. Ninapenda kumshukuru kila mfanyakazi katika Ofisi yangu kwa jitihada zake ambazo zimeniwezesha kutoa ripoti kwa wakati. Ninalazimika kuishukuru familia yangu na familia za wafanyakazi katika Ofisi yangu kwa uvumilivu waliouonesha kipindi chote cha kutimiza wajibu huu wa kikatiba.

Ninapenda kuishukuru Serikali na Bunge letu tukufu kwa kuendelea kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Vilevile, shukrani za pekee ziende kwa jumuiya ya wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Uswidi (SNAO), Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Umoja wa Ulaya (EU), Ushirikiano wa Uswisi na Ujerumani (GFG Project) ukisimamiwa na Ushirikiano wa Kimataifa wa Ujerumani (GIZ), Benki ya Dunia kupitia Mpango wa Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP), pamoja na wengine wote waliotutakia mema ambao walichangia kwa njia moja au nyingine kwa nia ya kuleta mabadiliko katika Ofisi yangu. Mchango wao katika kuimarisha ujuzi wa wafanyakazi, mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano, na nyenzo mbalimbali umechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio yetu.

Halikadhalika, ninapenda kuwashukuru wadau wengine wote, ikiwa pamoja na maofisa masuuli wa taasisi nilizozikagua kwa kutoa mchango mkubwa na taarifa muhimu zilizohitajika kwa ajili ya uandaaji wa ripoti mahususi za ukaguzi wa ufanisi ambazo ndizo zimewezesha uandaaji wa ripoti hii ya jumla.

Shukrani za kipekee ziende kwa jamii ya wanataaluma na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka Vyuo Vikuu mbalimbali nchini, na maofisa wastaafu wa Serikali kwa michango yao ambayo iliboresha ripoti za ukaguzi wa ufanisi kupitia maoni na uhakiki walioufanya katika rasimu za ripoti.

Ninapenda pia kuishukuru Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu ambayo ripoti hii pamoja na ripoti nyingine binafsi za ukaguzi

zitawasilishwa kwa ajili ya uchambuzi, majadiliano, na kutoa maelekezo yake. Tunatarajia kuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu itatupa maboresho na mwelekeo utakaotokana na mjadala wa ripoti hizi.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru maofisa masuuli na watumishi wote wa taasisi za umma Tanzania nzima. Ninatambua pia mchango wa walipakodi ambao ripoti hii tunaitoa kwao. Mwenyezi Mungu awabariki nyote kadri mnavyojitoa katika kusimamia uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma nchini.

MUHTASARI

Utangulizi

Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Namba 11 ya Mwaka 2008 kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kufanya ukaguzi wa ufanisi kwenye sekta ya umma. Ukaguzi wa ufanisi unalenga kuboresha muundo wa uwajibikaji na utendaji wa taasisi za serikali. Pia, unatoa tathmini huru ya namna ambavyo taasisi hizo zinatumia rasilimali katika kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi.

Taarifa hii ya jumla ya ukaguzi wa ufanisi inaainisha mafanikio na mapungufu yaliyobainika, hitimisho, pamoja na mapendekezo katika Sekta ya Elimu nchini. Taarifa hii ya jumla ya ukaguzi wa ufanisi inatokana na Ripoti tisa za ukaguzi wa ufanisi juu ya Upatikanaji na Uwepo wa Miundombinu ya Shule za Msingi; Marejesho na Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Utoaji wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu; Utoaji wa Mafunzo ya Kujenga Uwezo kwa Walimu Walio Kazini; Utoaji wa Elimu na Mafunzo Bora ya Ufundi Stadi; Programu za Kuimarisha Uwezo wa Kufanya Utafiti kwa Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili na Ardhi, pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia zilizofanyika kati ya mwaka 2017 na 2020.

Kwa ujumla, ripoti hii inakusudia kusaidia wabunge, Serikali, vyombo vya habari, umma, na wadau wengine kuchukua maamuzi ya uhakika kwa lengo la kuongeza tija, ufanisi, na uwekevu katika utoaji wa elimu ya msingi, sekondari, ufundi stadi, na vyuo vikuu kwa umma. Ripoti hii ya jumla haikusudii kuwa mbadala wa ripoti tisa zilizofanywa na kutolewa katika miaka ya kifedha iliyotajwa. Msomaji anashauriwa kutegemea zaidi ripoti husika.

Mambo Makuu Yaliyobainika katika Ukaguzi

Utoaji wa Elimu bila Malipo (Darasa la I hadi Kidato cha IV)

Serikali iliwekeza kiasi kikubwa cha fedha katika utoaji wa elimu kwa kuanzisha elimu bure kuanzia ngazi ya elimu ya msingi hadi sekondari. Tangu kuanzishwa kwa elimu bure mwaka 2016, Serikali imetumia takribani shilingi za Kitanzania trilioni 1.096 hadi kufikia mwaka wa fedha

2019/20. Fedha hizi zimetumika kugharamia utoaji wa elimu ya msingi ikiwa ni pamoja na ukarabati na ujenzi wa miundombinu, rasilimali-watu pamoja na udhibiti na uhakiki wa ubora katika sekta ya elimu.

Kuanzishwa kwa Mpango wa Elimu Bure kumechangia ongezeko la wanafunzi na hivyo kupelekea haja ya kuongeza uwekezaji sambamba katika miundombinu, rasilimali-watu, vifaa vya maabara, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, na shughuli za udhibiti ubora wa elimu ambazo kwa pamoja huchangia katika utoaji wa elimu ya msingi, sekondari, na elimu ya juu yenye ubora uliokusudiwa. Kwa mfano, kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la saba kiliongezeka kutoka wanafunzi 8,298,282 hadi 10,460,785 sawa na ongezeko la asilimia 26. Idadi ya wanafunzi wa shule za sekondari iliongezeka kutoka 1,774,383 hadi 2,062,717 katika kipindi kama hicho sawa na ongezeko la asilimia 16.

Maboresho katika utoaji wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Chuo Kikuu

Uboreshaji na Ujenzi wa Miundombinu

Serikali imegharamia maboresho ya miundombinu katika shule za msingi na sekondari ambayo yameimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, Serikali imetumia takribani shilingi bilioni 326.1 kuboresha miundombinu ya shule kongwe 86 kati ya 89. Kwa sasa Serikali ipo katika awamu ya tatu ya maboresho hayo ambapo imetumia shilingi za Kitanzania bilioni 8.7 kukarabati shule kongwe 12.

Serikali imeongeza idadi ya madarasa kwa kujenga madarasa mapya 8,782 na hivyo kuyafanya yafikie 175,353 kutoka 166,571 yaliyokuwepo awali. Katika kipindi hicho, Serikali imejenga na kuboresha makazi ya walimu. Imejenga nyumba mpya 15,562. Uwekezaji huu umefanyika ili kuendana na ongezeko la wanafunzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na kuhakikisha kwamba wanafunzi wanajifunza katika mazingira yenye ubora na pia walimu wanaishi katika mazingira mazuri..

Aidha, Serikali imekarabati na pia kujenga majengo mapya ya maabara katika shule za sekondari na hivyo kuongeza idadi yake hadi kufikia 6,104 nchini. Mbali na ujenzi wa miundombinu, Serikali pia imeboresha miundombinu ya kujifunzia kwa kuzipatia shule zinazotoa elimu maalumu vifaa vipya 37,820 vya kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Vifaa hivi vilipelekwa katika shule 1,305 zinazotoa elimu maalumu kote nchini.

Utoaji wa Vitabu kwa Elimu ya Shule za Msingi

Katika kuhakikisha utoaji wa elimu bora, kwa miaka mitano iliyopita, Serikali ilizalisha na kusambaza vitabu 2,962,648 vya darasa la saba vya masomo yote, pamoja na mitaala 272,000 ya darasa la kwanza hadi la saba. Zaidi ya hayo, Serikali ilisambaza vitabu 25,452 vya wanafunzi wasioona katika shule mbalimbali nchini kote.

Ongezeko la Idadi ya Walimu

Katika kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi katika ngazi zote za elimu, Serikali imeajiri walimu ili kusaidia utoaji wa elimu katika elimu ya msingi na sekondari. Hadi sasa, idadi ya walimu wa shule za msingi na sekondari wamefikia 253,633 ambayo ni sawa na asilimia 75 ya mahitaji yote ya walimu nchini. Mbali na hilo, Serikali pia iliajiri wataalamu wa maabara 397 ambao walipelekwa katika shule za sekondari zinazofundisha masomo ya sayansi ili kuimarisha elimu kwa vitendo kwenye masomo kama vile fizikia, kemia na biolojia.

Kuimarisha Shughuli za Udhibiti wa Ubora wa Elimu

Katika kuhakikisha ubora wa elimu, Serikali ilitoa vyombo vya usafiri kuanzia ngazi ya mkoa hadi kata ili kurahisisha ukaguzi na usimamizi wa utoaji wa elimu bora katika maeneo hayo ya kiutawala. Jumla ya magari 38 yametolewa kwa Maofisa Elimu wa mikoa na magari 184 tayari yamenunuliwa na yanasubiri kusambazwa mikoani na katika halmashauri mbalimbali. Aidha, pikipiki 3,900 zimesambazwa kwa Maofisa Elimu kata ili kurahisisha shughuli za udhibiti wa ubora kwenye kata zao. Hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na: kuimarisha shughuli za udhibiti wa ubora wa elimu; kuajiri wadhibiti ubora wa elimu takribani 400 katika mwaka wa fedha 2019/20; na kujenga ofisi zipatazo 100 za wadhibiti ubora wa elimu nchini.

Aidha, Idara ya Udhibiti Ubora wa Elimu katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliweza kutembelea jumla ya taasisi za elimu 5,058 zikiwemo shule za msingi 3,953, shule za sekondari 1,089, na vyuo 16 vya ualimu,

sawa na asilimia 84.8 ya taasisi zote nchini zilizotakiwa kutembelewa na wadhibiti ubora wa elimu. Pia, Idara iliweza kufanya ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa wakati wa ukaguzi wa shule uliofanyika katika shule za awali na msingi 494 na shule za sekondari 75 ili kupima kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwao katika kaguzi zilizofanyika.

Kuimarisha Utoaji wa Elimu ya Juu

Katika kuimarisha utoaji wa elimu ya juu, juhudi za Serikali zimehakikisha kuna ongezeko la udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka wanafunzi 125,000 mwaka 2015 hadi wanafunzi 142,179 mwaka 2021. Ongezeko hili la udahili ni sawa na asilimia 14 ya wanafunzi wote waliodahiliwa mwaka 2015. Aidha, kumekuwa na ongezeko la jumla la kiwango cha mikopo ya wanafunzi wa vyuo vikuu ambayo imeongezeka kutoka shilingi za Kitanzania bilioni 373 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 462 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 24.

Pamoja na maboresho hayo yaliyofanywa na serikali katika sekta ya elimu, kaguzi zilizofanyika bado zilibaini uwepo wa mapungufu kadhaa kama yalivyoainishwa hapa chini. Ukaguzi umebaini mambo makuu saba ambayo ni matumizi ya rasilimali kwa ajili ya utoaji wa elimu; usimamizi usioridhisha wa ubora wa elimu; mapungufu katika usimamizi wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu; ujengaji uwezo usioridhisha kwa walimu walio kazini; na utoaji duni wa mafunzo ya ufundi stadi. Mambo mengine ni utekelezaji usioridhisha wa programu za tafiti katika taasisi za elimu ya juu; usimamizi usioridhisha wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; na uratibu na ufuatiliaji duni katika utoaji huduma za elimu nchini. Mambo haya yanafafanuliwa kwa kina hapa chini.

Ongezeko la Rasilimali kwa ajili ya Utoaji wa Elimu

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na ongezeko la fedha kwa ajili ya utoaji wa elimu ya msingi, sekondari, na vyuo vikuu. Kwa mfano, kati ya miaka ya fedha 2015/16 na 2019/20, Serikali iliweza kuongeza zaidi ya mara tatu ya fedha kutoka Sh. Bilioni 107 katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi Sh. Bilioni 382 katika mwaka wa fedha 2019/20 kugharamia uboreshaji wa miundombinu ya shule ya msingi na sekondari. Hali hii ilibainika pia katika kuwajengea uwezo walimu walio kazini na uimarishaji wa elimu na

mafunzo ya ufundi, ambapo maeneo haya yalipokea asilimia 25 na 46 ya bajeti zao za jumla, kwa mfuatano huo.

Ukaguzi ulibaini kwa ujumla kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha (2014/15 hadi 2016/17), Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ilikuwa ikipanga bajeti kuwezesha hatua ambazo zinaongeza utoaji wa elimu.

Mathalani, katika kipindi hicho, Serikali ilipanga kutumia Sh. Bilioni 815 kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu na ikafanikiwa kutoa jumla ya Sh. Bilioni 326. Ukaguzi ulibaini pia kuwa ukiachwa Mwaka wa Fedha 2017/18, kulikuwa na viwango tofauti vya bajeti na utoaji wa fedha kwa ajili ya utoaji wa elimu ya mahitaji maalumu, mipango ya kuwajengea uwezo walimu walio kazini, na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi.

Pamoja na ongezeko la fedha kwa ajili ya utoaji ekimu, baadhi ya maeneo yalikumbwa na uhaba wa bajeti. Upungufu huo wa fedha ulizorotesha utoaji wa huduma za elimu katika baadhi ya maeneo.
Kutolewa kwa fedha pungufu kulitokana na vipaumbele mbalimbali vya Serikali, elimu ikiwa mojawapo. Matokeo yake, shughuli kadhaa muhimu katika sekta ya elimu hazikutekelezwa. Shughuli zilizoathirika ni pamoja na upungufu wa madawati, kukosekana kwa vifaa vya kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu, ukosefu wa ukarabati wa miundombinu ya shule, na ukosefu wa mafunzo kwa walimu walio kazini.

Ukaguzi ulibaini pia kuwa kulikuwa na mgawanyo usiotosheleza wa walimu katika utoaji wa elimu ya msingi, sekondari, na elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Ukaguzi uligundua kuwa hakukuwa na uwiano wa kutosha wa mwalimu-mwanafunzi kwa elimu na mafunzo ya ufundi stadi ambapo uwiano wa sasa ni wanafunzi 79 kwa mwalimu 1, wakati mahitaji ya kawaida ni wanafunzi 16 kwa mwalimu 1. Upungufu pia ulibainika katika eneo la kuwajengea uwezo walimu walio kazini na wahakiki wa ubora, ambapo viwango vya upungufu vilikuwa kwa wastani wa asilimia 37 kwa walimu walioko makazini na upungufu wa asilimia 81 kwa wadhibiti ubora.

Uhaba wa rasilimali-watu katika sekta ya elimu ulisababishwa na utoaji pungufu wa fedha ili kuweza kuajiri na kusambaza wafanyakazi hususani walimu katika shule mbalimbali. Matokeo yake, kulikuwa na uwiano finyu wa walimu na wanafunzi. Hali hii iliathiri ufanisi katika utoaji wa elimu

nchini. Kwa kuongezea, vyuo vya ufundi stadi havikuweza kutambuliwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa sababu ya kuwa na idadi pungufu ya walimu.

Kwa upande wa mafanikio, Serikali ilipokea jumla ya asilimia 87 ya fedha (sawa na shilingi za Kitanzania bilioni 11.3) kutoka kwa washirika wa maendeleo waliokuwa wanafadhili utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha Ujuzi wa Kusoma, Kuandika, na Kuhesabu (LANES) kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia iliweza kukarabati shule 12 za zamani za sekondari ambapo Sh. 8,685,167,591 zilitumika kwa ajili ya ukarabati.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa taasisi za elimu ya juu ambazo zilikuwa zikitekeleza mpango wa kuimarisha utafiti uliofadhiliwa na Sida kati ya 2015/16 na 2019/20 zilipokea kiasi kikubwa cha fedha za programu zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zao.

Ukaguzi ulionesha kuwa vyuo vikuu 3 ambavyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Afya na Tiba Muhimbili (MUHAS), na Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU); pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa pamoja walipokea wastani wa asilimia 93 ya fedha zote, ambapo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Afya na Tiba Muhimbili walipokea asilimia 100 ya fedha zilizopangwa.

Usimamizi Usioridhisha wa Ubora wa Elimu

Ukaguzi uliofanyika ulibaini kuwepo kwa utekelezaji hafifu wa mipango iliyolenga kuweka usimamizi wenye tija wa mifumo ya udhibiti na uhakiki wa ubora kwa shule za msingi na sekondari. Kwa mfano, ukaguzi ulibaini kuwa kumekuwepo na uhaba wa wahakiki ubora kwa elimu ya wenye mahitaji maalumu huku kukiwa na ripoti za uwepo wa jumla ya wahakiki 98 pekee kati ya 1306 waliokuwa wakihitajika. Idadi hii ya wadhibiti ubora wa elimu ni sawa na asilimia 8 ya mahitaji yote. Zaidi, utekelezaji wa mapendekezo yaliyotokana na shughuli za uhakiki ubora kama ulivyofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni mdogo huku ikiripotiwa kuwa ni asilimia 39 pekee ya mapendekezo yote ndiyo

yalitekelezwa huku asilimia 61 ya mapendekezo hayo yakiwa hayajatekelezwa kabisa.

Kiwango kidogo cha utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na wahakiki ubora kilitokana na udhaifu wa idara za elimu katika kusimamia utekelezaji wa mapendezo ndani ya mamlaka za serikali za mitaa. Wahakiki ubora walikosa nguvu za kushawishi utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa.

Katika namna nyingine, shughuli za wahakiki ubora hazikuzingatia mambo mengine yahusuyo ubora katika sekta ya elimu hasa uwepo wa miundombinu sahihi, ambapo ni asilimia 5 pekee ya mapendekezo yote yaliyotolewa na wahakiki ubora yaligusia suala la miundombinu.

Kaguzi pia zilibaini kuwepo kwa utekelezaji hafifu wa shughuli zilizolenga kuimarisha uwezo wa taasisi za elimu ya juu kusimamia mifumo ya udhibiti na uhakiki ubora. Mifumo ya udhibiti ubora wa vikundi ya uvumbuzi katika Tume ya Sayansi na Teknolojia haikuundwa licha ya kwamba ilitarajiwa kuwa nyenzo ya kufuatilia matokeo ya uvumbuzi. Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba zana za uhakiki ubora ziliandaliwa lakini hazikuhuishwa katika taasisi ili kuwezesha usimamizi sahihi wa ubora katika utoaji wa elimu ya juu na hasa katika shughuli za utafiti. Zaidi ya hayo, hakukuwa na namna ya kufuatilia matumizi ya zana za udhibiti ubora zilizoandaliwa katika taasisi husika.

Kiwango kidogo cha shughuli za uhakiki ubora hatimaye kimeathiri ubora wa elimu ya msingi, sekondari, ufundi, pamoja na ya vyuo vikuu nchini. Kwa mfano, changamoto za miundombinu kama vile uchache wa madarasa na madawati imeendelea kuwepo licha ya miaka mingi ya kuzungumziwa katika taarifa za wakaguzi wa uhakiki ubora na hivyo kuathiri mazingira ya kufundishia na kujifunzia ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Matokeo yake, changamoto zinazopelekea kuwepo kwa mifumo dhaifu ya uhakiki ubora katika vyuo vikuu zimeendelea kuzalisha wahitimu waliokosa ujuzi muhimu unaotakiwa katika soko la sasa la ajira.

Mapungufu katika Usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na upungufu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Kwa mfano, asilimia 68 ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia[2] kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu vilivyohitajika havikuwepo katika shule za msingi 17 kati ya shule 18 zilizotembelewa. Kukosekana kwa utaratibu endelevu wa kugharamia elimu maalumu ndiyo sababu kubwa inayochangia upungufu huo. Kwa mfano, kiasi cha shilingi milioni 272 zilizotengwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia elimu maalumu ilibadilishwa matumizi na kutumika kwa ajili ya shughuli za mitihani ya darasa la nne na mashindano ya lugha ya Kingereza Afrika Mashariki.

Pia, ilibainika kulikuwa na upungufu wa mafunzo ya walimu wa elimu maalumu, na hata baada ya kuhitimu, walimu waliopatiwa mafunzo hawakupangwa kwenye shule za msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Kwa mwaka 2018, upungufu wa walimu wa elimu maalumu ulikuwa walimu 1968 (sawa na asilimia 44 ya mahitaji kwa ujumla). Kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2014 hadi 2018, Wizara iliweza kuzalisha walimu wa elimu maalumu 654. Hivyo, kama Wizara itaendelea kuzalisha walimu kwa kasi hiyo, inakadiriwa kwamba itachukua takribani miaka 12 kuweza kuondoa upungufu uliopo sasa kama hakutakuwa na mabadiliko. Sababu kubwa ya upungufu uliopo ni serikali ilikuwa na chuo kimoja tu cha ualimu wa elimu maalumu, yaani Chuo cha Ualimu Patandi, Arusha. Pia mgao/ugawaji wa walimu wa elimu maalumu haukuwa mzuri. Halmashauri 8 kati ya 12 hazikuwapangia kwenye shule za elimu maalumu jumla ya walimu 36 walioendelezwa katika taaluma hiyo.

Ukaguzi ulibaini kuwa kaguzi zinazofanywa na wadhibiti ubora wa shule wa Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia zilikuwa chache kinyume na Kifungu cha 12 cha Kiongozi cha Mkaguzi wa Shule cha Mwaka 2010, ambacho kinataka kila shule ikaguliwe walau mara moja kila mwaka. Mapitio ya ripoti za ukaguzi katika shule za msingi 18 yalibaini kuwa katika kipindi cha ukaguzi hakukuwa na shule hata moja iliyokaguliwa miaka yote kama inavyotakiwa. Hali hii ilisababishwa na ukweli kuwa vigezo

[2]Vifaa hivyo ni kama vile mashine za nukta nundu, Mashine ya kutoa nakala za nukta nundu, vifaa vya kuongeza mawimbi ya sauti na nyinginezo

vinavyotumika na wadhibiti ubora kuchagua shule za kuzikagua havikuhusisha elimu maalumu.

Ujengaji Uwezo Usioridhisha kwa Walimu Walio Kazini

Ukaguzi umebaini kuwa mafunzo kwa walimu yalifanyika kwa walimu wanaofundisha masomo ya ujuzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu wa darasa la kwanza na darasa la pili katika shule za msingi na kuwaacha walimu 147,027 wa masomo mengine na madaraja tofauti, idadi ambayo ni sawa na asilimia 82. Aidha, ilionekana kuwa walimu 75,127 sawa na asilimia 19 tu ya walimu waliopo katika shule za sekondari walilengwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 nchi nzima. Kadhalika, ukaguzi haukupata mpango wowote uliokusudiwa kwa ajili ya kuwajengea uwezo walimu katika shule za sekondari katika miaka ya fedha iliyofuata.

Ukaguzi umebaini pia kuwa walimu walio kazini mara chache walipata msaada wa maendeleo ya kitaalamu ama kupitia ziara za wadhibiti ubora au ushauri katika shule zao. Hii ilisababishwa na ukweli kwamba wathibiti ubora walikuwa wakiachwa nyuma katika suala la maarifa ikilinganishwa na walimu kutokana na kwamba baadhi ya mafunzo hayo yalitolewa kwanza kwa walimu kabla ya wathibiti ubora. Kwa hiyo, hali hii iliwanyima wathibiti ubora fursa ya kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Ukaguzi pia ulibaini kukosekana kwa mfumo wa maendeleo endelevu ya kitaaluma. Mfumo huo ulitarajiwa kutoa uhakika juu ya uendelevu na mwongozo wa wazi juu ya masuala ya kitaalamu katika utekelezaji wa mipango ya kujenga uwezo kwa walimu walio kazini.

Udhaifu wa kuwajengea uwezo walimu kimsingi ulitokana na kutotekelezwa kwa mkakati wa kitaifa wa kuwajengea walimu walio kazini uwezo na maendeleo ya kitaaluma. Kwa hiyo, kuwajengea uwezo walimu walio kazini kulitegemea zaidi miradi inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo nchini ambayo kwa upande wake iliwaacha walimu wengi bila maarifa ya kitaaluma kwa kuzingatia maudhui yote mawili, ujuzi wa kufundisha na uwezo wa somo husika.

Utoaji Usioridhisha wa Elimu na Mafunzo Bora ya Ufundi Stadi

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na pengo kubwa la ujuzi katika kada za ngazi za chini za mafundi na mafundi mchundo ambao linahitaji kujazwa katika kipindi cha miaka 13 ijayo. Inakadiriwa kuwa kazi za ujuzi mdogo kama vile waendeshaji wa mitambo na mashine unapaswa uongezeke kwa zaidi ya mara 4 kwa wastani ili Tanzania iwe na kiwango kiwango cha ujuzi sawa na nchi zingine zenye kipato cha kati.

Sababu za kuwepo kwa pengo la ujuzi wa kada za kati na chini ni pamoja na uwepo wa idadi ndogo, ambapo ni asilimia 20 tu ya waombaji ndio walichaguliwa kwa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Sababu zingine ni uwepo wa mafunzo yasiyotosheleza yanayotolewa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, na kutokuwepo kwa usawa katika usambazaji wa kijiografia wa vituo na vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

Ukaguzi pia ulibaini kuwa udahili wa programu za elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa makundi maalumu, kama vile wanawake, watu wenye ulemavu, na watu kutoka maeneo yenye vyuo vichache ulikuwa chini. Hii ilidhihirishwa na uwepo wa asilimia ndogo ya wanafunzi waliodahiliwa kutoka makundi hayo. Kwa mfano, ni asilimia 35 tu ya wanafunzi wa kike waliandikishwa ili kupata elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Zaidi ya hayo, ukaguzi ulibainisha kupungua kwa udahili wa wanafunzi wenye ulemavu kutokana na kutokuwepo kwa usawa kwenye mgawanyo kikanda wa vyuo vya ufundi stadi.

Kwa upande mwingine, ukaguzi umebaini kwamba vyuo vya ufundi vimeshindwa kukidhi viwango vya ubora unaohitajika. Hii ilitokana na kutokuwepo kwa utaratibu wenye tija wa kuhakikisha ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kutokana na kuwepo kwa ufuatiliaji usiokuwa na tija, upungufu wa walimu, na walimu kuwa katika vituo vya binafsi na serikali vinavyomilikiwa na serikali. Sababu zingine ni uwepo wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia isiyojitosheleza na iliyopitwa na wakati. Vilevile kulikuwepo na uhaba wa zana na vifaa vya kufundishia ambapo ni asilimia 57 tu ya zana za kufundishia zinazohitajika na vifaa vilipatikana katika vituo na vyuo vya elimu ya ufundi stadi vilivyotembelewa.

Aidha, ukaguzi ulibaini kwamba utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi ulipokea fedha chini ya kiwango na hivyo kutoweza kutimiza mahitaji ya utoaji wa huduma hiyo nchini. Theluthi moja ya fedha za kodi ya maendeleo ya ujuzi inatakiwa kuelekezwa katika utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2014/15 hadi 2014/18 ni kiasi cha shilingi bilioni 219.47 pekee kati ya shilingi bilioni 1,298 ndicho kilielekezwa katika utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 51 ya fedha zote za kodi ya maendeleo ya ujuzi zilizokusanywa katika kipindi hicho. Hii inamaanisha kuwa asilimia 49 iliyobaki ya kodi ya maendeleo ya ujuzi haikupelekwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kama inavyotakiwa kisheria.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kulikuwa na ucheleweshaji wa ugawaji wa fedha zilizokusanywa katika kanda na vituo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Ucheleweshaji huo ulikuwa kati ya siku 12 hadi 48. Ilibainika kuwa ucheleweshaji huo ulisababishwa hasa na ugawaji wa fedha za matumizi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ucheleweshaji huo uliathiri ununuzi wa vifaa vya mafunzo, na kwa upande mwingine uliathiri utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi uliofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haukuwa na ufanisi wa kutosha kuwezesha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kufanya maboresho muhimu katika utoaji wa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi.

Utekelezaji Hafifu wa Programu za Tafiti katika Taasisi za Elimu ya Juu

Kaguzi zilibaini kuwa upangaji wa awali wa shughuli za kuimarisha tafiti kwa taasisi za elimu ya juu (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Tume ya Sayansi na Teknolojia) hazikuratibiwa vizuri wala kutekelezwa vya kutosha. Ukaguzi ulionesha kuwa hatari zinazoweza kuathiri mafanikio ya programu hazikuangaliwa na hivyo kuathiri kufikiwa kwa malengo maalumu na ya jumla ya programu.

Kaguzi ziligundua kuwa malengo na viashiria vikuu vya utendaji vilivyobuniwa na waratibu wa programu havikuwa vya kweli na hivyo kupelekea asilimia 51 ya shughuli zilizotekelezwa kutokuwepo katika mipango iliyoidhinishwa. Kwa kuongezea, nyaraka za programu ambazo zilikuwa ni msingi wa utekelezaji wa programu katika taasisi husika hazikupitiwa upya ili kuendana na mabadiliko yaliyotokea wakati wa utekelezaji wa programu hizo. Udhaifu ulioonekana katika upangaji wa shughuli ulisababishwa na kuwepo kwa ushirikano mdogo na wadau tofauti kama vile mashirika mengine ya Serikali, taasisi za udhibiti wa elimu, mashirika ya kijamii, mashirika binafsi ya utafiti, na taasisi zingine za vyuo vikuu wakati wa uundaji wa mipango na muda wa utekelezaji.

Kaguzi zilibaini kuwa muda uliopangwa kukamilisha uidhinishaji haukushirikisha mamlaka zingine za utoaji idhini na waratibu wa programu ndogo. Kwa mfano, utekelezaji wa programu katika Tume ya Sayansi na Teknolojia haukupata ushirikiano wa kutosha kutoka katika taasisi za utafiti na taasisi za elimu ya juu.

Kaguzi pia zilibaini kuwa hakukuwa na utekelezaji kamili wa shughuli zilizopangwa, hususani utekelezaji wa programu katika Tume ya Sayansi na Teknolojia, ambapo mafanikio yalikuwa kwa asilimia 56 tu ya shughuli zilizopangwa. Kwa upande mwingine, vyuo vikuu viliweza kufikia kiwango cha kuridhisha cha malengo ya programu. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu ch Ardhi vilifikia asilimia 78 na 58 kwa mtiririko huo, kila kimoja katika malengo ya mipango yake ya programu. Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili nacho kilifanikisha malengo yake ya programu kwa kiwango cha kuridhisha.

Kutotekelezwa kwa ukamilifu shughuli zilizopangwa kulisababishwa na kuchelewa kufanikisha programu zinazototekelezwa na taasisi tofauti za utekelezaji. Ucheleweshaji wa shughuli za awali za programu uliathiri mafanikio ya programu kwa kuaathiri utekelezaji wa shughuli zingine zilizofuata. Vyuo vikuu vyote vitatu vilichelewesha kuidhinisha na kufanya shughuli za utafiti katika kozi za uzamivu. Ucheleweshaji wa idhini ulikuwa kati ya miezi 6 hadi 36 kwa kozi ya uzamivu kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; miezi 28 hadi 35 katika Chuo Kikuu cha Ardhi; na miezi 36 hadi 48 kwa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Hali hii ilipelekea kuathiri muda uliopangwa wa kuhitimu masomo ya umahiri.

Kaguzi ziligundua kuwa mtiririko wa fedha kutoka kwa wafadhili wa programu hadi kwa taasisi na vitengo vya utekelezaji ulikuwa mzuri na wa kutosha. Hata hivyo, shughuli ambazo zilikuwa zimepangiwa fedha hazikuwa na utaratibu mzuri wa utekelezaji wa matumizi. Kaguzi zilibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa kuomba fedha za programu kulingana na awamu za utoaji uliopangwa. Ucheleweshaji mkubwa ulibainika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kilichukua miezi mitano kuomba fedha huku Chuo Kikuu cha Ardhi kikichukua miezi 4 kutuma ombi la fedha.

Kaguzi ziligundua kuwa fedha za programu hazikutumika kikamilifu na kwa wakati kulingana na makubaliano ya programu. Fedha za programu zilitumika kwa wastani wa asilimia 65 katika Chuo Kikuu cha Ardhi sawa na shilingi 457,289,428; na wastani wa asilimia 49 kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakati makubaliano yalikuwa kufikia kiwango cha asilimia 70 ya matumizi. Sababu kuu ya viwango vya matumizi kuwa chini katika taasisi zote za utekelezaji ilikuwa ucheleweshaji wa kukamilika kwa shughuli za programu. Kulikuwa na mipango na ratiba za utekelezaji wa shughuli za programu isiyo na uhalisia. Vyuo vya elimu ya juu vilikuwa na malengo makubwa kwani shughuli nyingi zilipangwa kutekelezwa wakati wa programu.

Matokeo yake, si shughuli zote zilikamilishwa. Kulikuwa na shughuli zingine ambazo zililazimika kutegemea kukamilika kwa shughuli zingine za programu ndogo. Shughuli ambazo hazijakamilika zilisababisha matumizi yasiyokamilika ya fedha ambayo yalisababisha kuwe na kiwango kidogo cha matumizi ya jumla ya fedha za mradi.

Zaidi, ukaguzi uligundua kuwa viwango vya chini vya matumizi kwa baadhi ya shughuli vilisababisha fedha zipangiwe matumizi mengine. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Ardhi kilisababisha mrundikano wa zaidi ya shilingi milioni 300 zilizotokana na shughuli mbili katika miaka miwili ya kifedha hivyo kukilazimu Chuo kutumia fedha hizo kwa shughuli zingine za programu.

Kaguzi zilibaini kuwa utekelezaji duni wa shughuli zilizowekwa za programu ziliathiri mafanikio ya programu hiyo kwa viwango tofauti. Hii ilitokana na ukweli kwamba kila programu ilikuwa na malengo yake maalumu ambayo yalipaswa kutimizwa ili kufikia lengo kuu. Hata hivyo, malengo maalumu hayakufikiwa kwa asilimi 100 na hivyo matokeo

yaliyopangwa ambayo yameunganishwa na malengo mengine, hayakutimizwa kikamilifu na hivyo kuathiri kiwango ambacho mipango hiyo ingeweza kufikia malengo ya jumla.

Usimamizi Usioridhisha wa Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu haikuweza kufikia malengo yake katika ukusanyaji wa mikopo. Tathmini ya utendaji ilionesha kuwa ukusanyaji wa mikopo kwa kila mwaka unaofanywa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu dhidi ya mikopo inayostahili kurejeshwa kwa kuzingatia hesabu za jumla ilikuwa kati ya shilingi bilioni 330 (32%) na shilingi bilioni 465 (48%) kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2012/13 hadi 2016/17. Makusanyo yalikuwa asilimia 35 tu badala ya asilimia 70 iliyolengwa katika mwaka wa fedha 2013/14. Katika mwaka wa fedha 2016/17 ambao ulikuwa mwaka wa mwisho wa kutekeleza Mpango Mkakati wa wakati huo, Bodi iliweza kukusanya kwa asilimia 48 tu badala ya makusanyo ya asilimia 80 yaliyopangwa.

Ilibainika pia kuwa kwa miaka ya fedha 2014/15, 2015/16 na 2016/17, kiwango cha kutafuta wanufaika wa mikopo inayostahili kurejeshwa kiliongezeka kutoka asilimia 28 hadi asilimia 51 ya wanufaika. Hata hivyo, ongezeko hili halikulingana na idadi iliyoongezeka ya wanufaika wa mikopo inayostahili kurejeshwa kutoka 79,555 hadi kufikia 138,485 katika mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 51 ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Kwa mujibu wa kanzidata ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuhusu mikopo inayostahili kurejeshwa, kulikuwa na idadi ya mikopo inayostahili kurejeshwa ambayo haikukusanywa kwa muda mrefu. Matokeo ya ukaguzi yalionesha kuwa kuanzia mwaka 1994 hadi 2017 kulikuwa na jumla ya shilingi bilioni 801.3 za mikopo iliyokuwa haijalipwa.

Sababu za udhaifu uliobainika ni mapungufu katika kuunda na kutekeleza mikakati ya ukusanyaji, ukusanyaji hafifu wa ankara zilizotolewa, udhaifu katika kupanga na kuripoti matokeo ya ukaguzi kwa waajiri, na kanzidata ya walengwa wa mikopo ambayo haitumiki kikamilifu wakati wa kuandaa mipango kuhusu ukusanyaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika.

Hivyo, jumla ya makusanyo ya mikopo inayostahili ya shilingi bilioni 244 hayakufanyika katika mwaka wa fedha 2016/17. Kiasi hiki, ikiwa kingekusanywa, kingetumika kufadhili wanafunzi wengine wa elimu ya juu katika miaka inayofuata. Hii ina maana kwamba kulikuwa na idadi kadhaa ya wanafunzi wa elimu ya juu ambao walikosa mikopo.

Uratibu na Ufuatiliaji Duni katika Utoaji wa Huduma za Elimu Tanzania

Ukaguzi ulibaini uratibu duni miongoni mwa wahusika katika ngazi mbalimbali za utoaji wa elimu ikiwa pamoja na ngazi za wizara, mikoa, vyuo kikuu na shule hivyo kusababisha kutokuwepo mtiririko mzuri wa taarifa kati ya wizara na wadau wake. Wizara ya Elimu, Sayansi na teknolojia, na OR-TAMISEMI hawakuweka mipango ambayo ingeruhusu uratibu mzuri wa utoaji wa elimu katika ngazi za wilaya na mikoa katika utekelezaji wa shughuli za kielimu ambazo zingeruhusu kufikia malengo yaliyowekwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa uwepo wa uratibu duni katika ngazi mbalimbali za utendaji wa sekta ya elimu ulitokana na kukosekana kwa sera ya kitaifa katika kupanga na kutekeleza ukuzaji wa ujuzi ambao unaweza kuwezesha kubadilishana taarifa na kupunguza mwingiliano wa majukumu miongoni mwa wadau na wahusika wakuu.

Ukaguzi pia umebaini utendaji duni katika ufuatiliaji wa utendaji wa vyombo mbalimbali kama vile sekretarieti za mikoa, halmashauri, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu (ADEM), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), vyuo vikuu, na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) katika utoaji wa huduma za elimu nchini. Hii ilisababishwa na uwepo wa viashiria vikuu vya utendaji visivyo na tija inayoridhisha na kutokuwepo kwa kanzidata ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa ili kurahisisha ufuatiliaji.

Kwa upande mwingine, ilionekana kuwa njia za kufuatilia jinsi shughuli mbalimbali zilizofanywa kutoka ngazi ya vikundi hadi halmashauri zilikuwa hazifanani. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwepo kwa utoaji usioridhisha wa taarifa za matokeo ya ufuatiliaji na tathmini. Hii kwa kiasi kikubwa ilichangia kuwepo kwa kiwango kidogo cha utekelezaji wa mapendekezo

yanayotokana na shughuli za ufuatiliaji na tathmini na kupelekea uamuzi dhaifu juu ya shughuli mbalimbali katika utoaji wa elimu nchini.

Hitimisho la jumla

Kwa ujumla, kaguzi za ufanisi zilizofanyika zinatambua mchango wa Serikali katika kuiendeleza sekta ya elimu nchini. Hata hivyo, mambo yaliyobainika katika ripoti hizi zilizojumuishwa yanapelekea kuhitimisha kwamba Serikali bado haijasimamia kwa tija utoaji wa huduma katika sekta ya elimu kwa ngazi zote kuanzia elimu ya msingi, sekondari, ufundi hadi chuo kikuu.

Mapendekezo

Ili kuondoa kasoro zilizobainika katika utoaji wa elimu, yafuatayo ni mapendekezo ya msingi yanayoelekezwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa:

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia inapaswa:

1. Kuanzisha utaratibu endelevu wa kugharamia shughuli zote za elimu maalumu na kuhakikisha shughuli za mapitio ya mitaala, utunzi na usimamizi wa mitihani, udhibiti ubora wa shule, na mafunzo kwa walimu wa elimu maalumu zinapewa kipaumbele na kutengewa fedha katika bajeti.

2. Kuhakikisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaanzisha mfumo wa utambuzi wa wanufaika hatarishi wa mikopo na kuunganisha na mikakati ya ulipaji na urejeshaji wa mikopo ili kuongeza ufanisi katika utoaji na urejeshaji wa mikopo, hususani katika utambuzi wa wanufaika na utoaji wa mikopo.

3. Kuhakikisha taasisi za elimu ya juu nchini zinaboresha mifumo yao ya usimamizi wa rasilimali-fedha na kuanzisha utaratibu utakaowezesha maombi na utolewaji wa fedha kufanyika kwa wakati ili kuwezesha shughuli za utekelezaji wa kazi za programu kufanyika kwa wakati.

4. Kuhakikisha kuwa taasisi za elimu ya juu zinaboresha uwezo wao wa kusimamia miradi hasa katika usimamizi wa miradi inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo ili kupunguza ucheleweshaji na kushindwa kufikia malengo ya programu husika.

5. Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi ili kuhakikisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi inatoa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi; na

6. Kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi inaanzisha na kutekeleza mpango endelevu wa kuboresha majengo na upatikanaji wa vifaa vya kisasa katika vituo vyote vya kutolea elemu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

13.2.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais - TAMISEMI wanapaswa:

1. Kuhakikisha rasilimali zilizotengwa (fedha na watumishi wenye utaalamu) kwa ajili ya utoaji wa elimu na mafunzo zinatolewa kama ilivyopangwa na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa;

2. Kuanzisha mipango na taratibu za kuimarisha uratibu baina ya wahusika katika ngazi zote za utoaji elimu ili kuhakikisha taarifa zinafika kwa urasihisi katika ngazi zote za kiutendaji;

3. Kuimarisha uwajibikaji katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na wadhibiti ubora wa shule ili kuwezesha kuinua ubora katika utoaji wa elimu nchini;

4. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utendaji ya wahusika katika utoaji wa elimu; na

5. Kufuatilia kwa ukaribu na kutekeleza matumizi ya mafunzo ya mara kwa mara kwa wataalamu, huku msisitizo zaidi ukiwekwa katika kuhakikisha hatua endelevu zinawekwa kuwaendeleza walimu walio kazini.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa ukaguzi wa ufanisi

Ukaguzi wa ufanisi ni muhimu kwa sababu unalenga kuboresha uwajibikaji, uwazi na utendaji wa taasisi za Serikali ili wananchi wapate huduma bora, kwa wakati sahihi, na zinazolingana na thamani ya fedha zilizotumika. Vigezo kadhaa hutumika kuchagua maeneo yanayolengwa na ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi maalumu. Miongoni mwa mambo hayo ni malalamiko kutoka kwa wananchi na umuhimu wa eneo linaloangaliwa, pamoja na sababu za kijamii na kiuchumi.

Ukaguzi wa ufanisi unafanyika ili kufahamu iwapo shughuli, mipango, au miradi inayohusisha rasilimali za umma katika wizara, idara, serikali za mitaa, na mashirika yote ya umma imesimamiwa kwa kuzingatia uwekevu, tija na ufanisi. Uwekevu, tija na ufanisi unaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

- Uwekevu - Kupunguza gharama za rasilimali zinazotumika katika shughuli huku ukizingatiwa ubora, wakati, kiasi na bei sahihi;
- Ufanisi - Uhusiano kati ya matokeo kwa kuzingatia bidhaa, huduma, matokeo na rasilimali zilizotumika kuzalishia, ambapo ni kutumia rasilimali kwa uchache ambazo zitazalisha matokeo yaleyale kwa muda na ubora sahihi; na
- Tija - Kiwango ambacho malengo yamefikiwa na uhusiano kati ya malengo yaliyokusudiwa na matokeo halisi katika shughuli husika.

1.2 Mamlaka ya kukagua

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kisheria kufanya ukaguzi wa ufanisi kupitia Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008. Kifungu cha 28 cha Sheria hii kinaeleza kwamba “Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa lengo la kudhibitisha uwekevu, tija na ufanisi katika matumizi ya fedha au rasilimali za taasisi ya umma, anaweza kukagua, kuchunguza na kutoa ripoti, kadiri atakavyoona inafaa kuhusu:

a) Matumizi ya fedha na rasilimali za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa, na mamlaka zingine za serikali;

b) Utekelezaji wa majukumu ya maofisa masuuli, wakuu wa idara, na wakuu wa taasisi mbalimbali za umma; na

c) Utekelezaji wa matakwa ya sheria ya mazingira, kanuni, na sera ya ndani ya mazingira na viwango.

Ukaguzi wa ufanisi unalenga kuangalia iwapo malengo ya awali yaliyowekwa yamefikiwa. Kisha unaangalia iwapo uwekevu, tija na ufanisi umezingatiwa. Hatimaye, mapendekezo yanatolewa kwa ajili ya kuboresha maeneo yaliyoonekana kuwa na mapungufu.

1.3 Madhumuni ya ripoti

Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu waheshimiwa wabunge, Serikali, vyombo vya habari, umma, pamoja na wadau wengine ili waweze kufanya maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija na ufanisi katika shughuli za serikali.

Ripoti hii inabainisha masuala mbalimbali yaliyoonekana katika kaguzi za ufanisi dhidi ya yale yaliyotarajiwa katika utoaji wa huduma za elimu. Ripoti imetathmini utendaji wa sekta ya elimu ili kuwezesha utoaji wa maamuzi kuhusiana na rasilimali zilizotengwa na zilitolewa kwa sekta ya elimu; na uratibu baina ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na wadau muhimu katika sekta ya elimu. Aidha, Ripoti inatathmini kiwango cha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kufuatilia utendaji wa mawakala wa elimu na mamlaka za serikali za mitaa katika utoaji wa elimu.

1.4 Lengo Kuu la Ripoti

Taarifa imelenga kuwasilisha masuala yanayohusu utoaji wa elimu nchini ili kuboresha upatikanaji wake kwa wananchi wote. Taarifa imegusa rasilimali zinazoelekezwa kwenye elimu, ubora wa elimu, utoaji wa elimu ya msingi na sekondari, usimamizi wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, kuwajengea uwezo walimu walio kazini, utoaji wa

elimu na mafunzo ya ufundi stadi, utekelezaji wa mipango ya elimu katika vyuo vikuu, usimamizi wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu, na uratibu na uangalizi wa watendaji katika sekta ya elimu.

Hivyo, ripoti hii ya jumla inajumuisha upembuzi uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutoka katika kaguzi tisa za ufanisi katika sekta ya elimu ambazo ni:

(a) Upatikanaji na Utunzaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi Tanzania (2017);
(b) Usimamizi wa Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu (2018);
(c) Usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu (2019);
(d) Usimamizi wa Utoaji wa Mafunzo kwa Walimu walio Kazini (2020);
(e) Upatikanaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (2020);
(f) Kuimarisha Ushirikiano wa Utafiti na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2020);
(g) Kuimarisha Ushirikiano wa Utafiti na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (2020);
(h) Kuimarisha Ushirikiano wa Utafiti na Chuo Kikuu cha Ardhi (2020); na
(i) Uundaji wa Mifumo Bora ya Utafiti na Uvumbuzi Nchini kama Inavyotekelezwa na na Tume ya Sayansi na Teknolojia (2020).

1.5 Umuhimu wa Elimu

Elimu ni nyenzo inayowapa watu maarifa, ujuzi, mbinu, taarifa, na kuwawezesha kujua haki na wajibu wao katika familia, jamii na taifa. Mfumo wa elimu Tanzania hutekelezwa kwa kufuata vipindi vya miaka 7-4-2-3 ambayo ni miaka 7 ya elimu ya msingi, miaka 4 ya elimu ya sekondari, miaka 2 ya elimu ya sekondari ya juu, na miaka 3 ya elimu ya chuo kikuu.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995 iliweka muundo wa elimu rasmi katika viwango saba ambavyo ni:

i) Elimu ya awali - miaka miwili (umri wa miaka 5);
ii) Elimu ya msingi - darasa la i – vii (umri wa miaka 7);
iii) Elimu ya sekondari - kidato cha kwanza hadi cha nne (kwa miaka 4);

iv) Elimu ya sekondari - kidato cha 5 hadi cha 6 (kwa miaka 2);
v) Mafunzo ya ufundi stadi (kulingana na mpango husika);
vi) Elimu ya ufundi (kulingana na mpango husika); na
vii) Elimu ya juu - miaka 3 au zaidi (kulingana na mpango husika).

Elimu huleta uvumbuzi na ubunifu ambao unaweza kutokea watu wanapokuwa na ujuzi wa kutosha kujua jinsi ya kufanya kazi kwa kutumia teknolojia tofauti. Elimu hulipatia taifa rasilimali-watu wenye ujuzi wa kutosha, inakuza umoja wa kitaifa, na inainua uelewa wa umma. Hivyo, elimu ni nyenzo muhimu ya kufanikisha maendeleo endelevu kwa sababu inakuza maendeleo ya maarifa, ujuzi, na uelewa wa namna ya kukabiliana na mazingira. Pia, elimu inakuza maadili na hatua zinazohitajika kuwezesha kuwa na ulimwengu endelevu, ambao unahakikisha uhifadhi na utunzaji wa mazingira, kukuza usawa wa kijamii, na kuhimiza uchumi endelevu.

Sekta ya elimu inachangia kufanikisha Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA); Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya Mwaka 2025; pamoja na kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu kupitia utoaji wa elimu bora na yenye usawa ambayo inakuza fursa za kujifunza kwa maisha yote na kwa watu wote. Umuhimu wa elimu kwa maisha ya watu hauwezi kupuuzwa kwani ukosefu wa elimu husababisha matatizo ya kijamii kama vile maradhi, umaskini, na mizozo ya ndani ya nchi na jamii. Licha ya umuhimu wake kwa nchi, sekta ya elimu bado inakabiliwa na changamoto kadhaa hasa upatikanaji, ubora na idadi ya Watanzania wanaopata elimu rasmi au elimu ya msingi. Changamoto hizi zitajadiliwa katika sura zinazofuata za ripoti hii.

1.6 Sababu za kufanyika Ukaguzi

Licha ya juhudi kadhaa zilizofanywa na serikali kushughulikia changamoto mbalimbali katika sekta ya elimu, bado kuna changamoto ambazo zinahusiana na utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini; kuwepo kwa mazingira ya kujifunzia yasiyo rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi; kuwepo kwa wahitimu wachache wa ufundi stadi katika maeneo ya kazi; idadi kubwa ya wanafunzi madarasani, na idadi kubwa ya wanafunzi wenye sifa kutopata mikopo kwa muda husika au kutopata kabisa. Mambo haya yote yamekuwa chachu kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kufanya ukaguzi wa ufanisi katika eneo hili.

1.7 Mchakato wa Udhibitisho wa Takwimu na Taarifa Zilizotolewa katika Ripoti

Ukaguzi wa ufanisi ulifanywa kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya taasisi za ukaguzi juu ya ukaguzi wa ufanisi. Viwango hivyo vinaitaka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata ushahidi wa kutosha na unaofaa kuwa msingi mzuri wa matokeo, hitimisho, na mapendekezo kulingana na lengo au malengo ya ukaguzi.

Kwa kuzingatia kanuni za ukaguzi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi walipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao kuhusu matokeo ya ukaguzi na kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika rasimu ya taarifa hii.

1.8 Muundo wa Ripoti

Ripoti hii ina sura kumi na tatu zilizopangwa kama ifuatavyo:

i. *Sura ya kwanza* inatoa utangulizi kuhusu ukaguzi wa ufanisi, mamlaka na madhumuni ya ripoti kwa ujumla;

ii. *Sura ya pili* inatoa muhtasari kuhusu muundo wa usimamizi wa sekta ya elimu nchini Tanzania;

iii. *Sura ya tatu inatoa maelezo kuhusu rasilimali za utoaji wa elimu Tanzania*;

iv. *Sura ya nne inatoa matokeo ya ukaguzi kuhusu usimamizi wa ubora wa elimu Tanzania;*

v. *Sura ya tano* inatoa matokeo ya ukaguzi kuhusu utoaji wa elimu ya msingi na sekondari;

vi. *Sura ya sita inatoa matokeo ya ukaguzi kuhusu usimamizi wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu;*

vii. *Sura ya saba inatoa matokeo ya ukaguzi kuhusu utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini;*

viii. *Sura ya nane inatoa matokeo ya ukaguzi kuhusu utoaji wa elimu ya ufundi stadi;*

ix. *Sura ya tisa* inatoa matokeo ya ukaguzi kuhusu utekelezaji wa programu za elimu katika vyuo vikuu na taasisi za utafiti;

x. *Sura ya kumi* inatoa matokeo ya ukaguzi katika usimamizi wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu;

xi. *Sura ya kumi na moja* inatoa matokeo ya ukaguzi kuhusu uratibu na usimamizi wa wadau muhimu katika sekta ya elimu;

xii. *Sura ya kumi na mbili* inatoa hitimisho la jumla la ukaguzi;

xiii. *Sura ya kumi na tatu* inawasilisha mapendekezo kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhusu namna ya kuboresha utoaji wa elimu bora kwa wananchi.

SURA YA PILI

MFUMO WA ELIMU TANZANIA

2.1 Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo ya mfumo wa utoaji wa elimu nchini. Inawasilisha sera, mfumo wa kisheria, na mikakati ambayo yote kwa pamoja inasimamia utoaji wa elimu nchini. Sura hii pia inaonesha majukumu ya watendaji muhimu wanaohusika katika utoaji wa elimu. Vilevile, inashughulikia maelezo ya jumla ya sekta nzima ya elimu nchini.

2.2 Sera na Mfumo wa Kisheria Unaosimamia Utoaji wa Elimu

Sera, Sheria na Kanuni zinazoongoza utoaji wa elimu nchini Tanzania zimeelezewa hapa chini:

2.2.1 Sera za Utoaji Elimu

Kuna sera kuu 6 zinazosimamia utoaji wa elimu nchini kama ifuatavyo:

(a) Sera ya Elimu ya Mwaka 2014

Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 inatoa taarifa ya kukuza sekta ya elimu. Sera hii inahitaji uwepo wa mfumo madhubuti wa uchanganuzi wa elimu unaoweza kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu kwa wanafunzi na kupelekea uwepo wa idadi kubwa ya watu waliosoma vizuri na wenye maarifa ya kutosha katika nyanja tofauti za maisha. Inatoa maelekezo ambayo yanasisitiza uwepo wa miundombinu ya kutosha itayofanya mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia kwa makundi yote katika ngazi zote za elimu.

(b) Sera ya Elimu na Mafunzo Tanzania ya Mwaka 1995

Sera ya Elimu na Mafunzo Tanzania ya Mwaka 1995 ilikusudia kukuza ushirikiano katika utoaji wa elimu na mafunzo kupitia juhudi za makusudi za kuhamasisha mashirika binafsi kushiriki katika utoaji wa elimu. Zaidi, ililenga kuanzisha na kusimamia shule na taasisi zingine za elimu katika ngazi zote.

Aidha, Sera hii ilisisitiza utoaji wa elimu bora kupitia ukaguzi wa mitaala, uboreshaji wa usimamizi wa walimu, na uanzishaji na utumiaji wa mikakati sahihi katika tathmini ya ufaulu. Pia, ilikuwa na lengo la kuimarisha uhusiano wa elimu rasmi na isiyo rasmi kwa kuanzisha ulinganishaji wa maarifa na mwingiliano kati ya sekta hizi mbili ndogo za elimu.

(c) ***Sera ya Taifa kwa Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004***

Sera hii inaielekeza serikali, kwa kushirikiana na wadau, kutoa mazingira mazuri ya elimu-jumuishi itakayowahudumia watu wenye mahitaji maalumu. Kwa kuongezea, serikali kwa kushirikiana na wadau inatakiwa kuboresha vifaa na mafunzo kwa watu wenye ulemavu; kuchukua hatua kwa kuhakikisha majengo ya umma na vifaa vingine vinapatikana kwa watu wenye ulemavu; na kutoa msaada wa kitaalamu kwa wahitaji wenye ulemavu.

(d) Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ya Mwaka 2012

Lengo kuu la sera hii ni kuleta mfumo mzuri wa ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ambao unaweza kutatua changamoto za kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuchangia vyema maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya kitaifa.

Malengo maalumu ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kama yalivyoainishwa na Sera ni kuboresha umuhimu wa utoaji wa elimu ya mafunzo ya ufundi; kuanzisha mifumo itakayowezesha ushirikishaji wa sekta binafsi na wadau wengine katika uandaaji wa mipango ya ufundi stadi kulingana na mahitaji ya soko la ajira ya sasa na ya baadaye; kuongeza fursa za kujifunza katika viwango anuwai vya mafunzo ya elimu ya ufundi; na kuandaa programu za nje na kuboresha uwiano wa rasilimali zilizoelekezwa kwenye elimu rasmi na isiyo rasmi ya ufundi na ufundi stadi.

(e) Sera ya Elimu ya Juu ya Mwaka 1999

Miongoni mwa malengo ya sera ni pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi na kuongeza usawa katika udahili wa wanafunzi; na kupanua vyanzo vya ufadhili wa elimu ya juu na kukuza mfumo endelevu wa ufadhili wa elimu ya juu nchini.

(f) Sera ya Usimamizi wa Ajira ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 1999 (kama Ilivyorekebishwa Mwaka 2008)

Sera hii inayataka mashirika yote ya utumishi wa umma kuunda mipango ya mafunzo kulingana na mahitaji ya ujuzi kama ilivyoainishwa katika mipango yao ya rasilimali-watu kwa kuzingatia rasilimali zilizopo. Inayataka mashirika kutenga bajeti kwa shughuli zilizopangwa kutoka kwenye mgao wao wa bajeti wa kila mwaka.

2.2.2 Sheria Zinazosimamia Utoaji wa Elimu

Kuna sheria kuu tano ambazo hutumiwa kuongoza utoaji wa elimu nchini. Sheria hizi zinaelezwa kwenye **Kielelezo 2.1** hapa chini:

Kielelezo 2.1: Sheria Kuu Zinazosimamia Utoaji wa Elimu nchini



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Sheria Anuwai (2021)*

2.2.3 Mikakati na Mipango ya Utoaji wa Elimu

Serikali ina mipango na mikakati mikuu mitatu katika utoaji wa elimu nchini kama inavyofafanuliwa kwa kina hapa chini.

(a) Mpango wa Maendeleo wa Kitaifa (2016 /17 – 2020 /21)

Moja ya malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Kitaifa ni kujikita katika ubora wa utoaji wa elimu pamoja na hatua za kuimarisha mikakati, mipango, na sera kama hatua za kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995. Mpango huu ulilenga kutekeleza kwa ufanisi mpango kamili wa elimu bure. Aidha, mpango unakusudia kuboresha elimu ya juu kupitia ongezeko la wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu; upanuzi wa matumizi ya hali ya juu ya teknolojia ya habari na mawasiliano; na ongezeko kubwa la wahadhiri. Kwa ujumla, mpango huu ulilenga kuimarisha sekta ya elimu katika ngazi zote kupitia mipango na mikakati maalumu.

(b) Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (2016/17 - 2020/21)

Mpango huu unaelezea mipangilio ya taasisi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu, pamoja na uratibu na mifumo ya usimamizi wa sekta ya elimu nchini. Pia, unazijikita katika kuhakikisha upatikanaji sawa wa elimu na mafunzo kwa wote ikiwajumuisha wale walio katika hali duni zaidi; hitaji la juhudi iliyoimarishwa katika kuboresha ubora wa elimu katika ngazi zote; na chaguzi za kimkakati za ugawaji rasilimali kwa sekta ya elimu katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

(c) Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ujuzi (2016-2022)

Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ujuzi (MKKU) unatoa njia mpya ya kukuza ujuzi nchini. Kanuni zake za msingi ni kama vile mwitikio wa mahitaji, mabadiliko ya nguvu, mwelekeo wa matokeo, umakini, ujumuishaji, na ushirikishaji wa sekta mbalimbali katika utoaji wa elimu.

Mkakati huu unatumika kutimiza, kutekeleza, na kuleta pamoja kwa mara ya kwanza katika mkakati mmoja, mipango anuwai ya kukuza ujuzi. Hivyo, mkakati huu unashughulikia mlolongo mzima wa ujuzi wa kuajiriwa, kutoka njia zisizo rasmi hadi ukuzaji wa ujuzi rasmi; pamoja na ujifunzaji;

ujasiriamali, elimu ya ufundi na ufundi kabla ya ajira; elimu ya chuo kikuu; na uboreshaji wa stadi baada ya ajira kwa njia ya ujifunzaji endelevu.

2.3 Mfumo wa Elimu Rasmi na Mafunzo Nchini

Usimamizi wa mfumo wa elimu unatofautiana katika wizara mbili, yaani, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina jukumu la kuunda sera sahihi za elimu na kusimamia utekelezaji wake. Aidha, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina wajibu wa kutoa mafunzo na kuzalisha walimu wenye sifa pamoja na kuratibu elimu ya taifa ya ufundi. Taasisi zingine ni pamoja na Baraza la Mitihani la Tanzania, Taasisi ya Elimu Tanzania, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, na wakala wa maendeleo ya usimamizi wa elimu.

Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa upande mwingine ina jukumu la kusimamia utoaji wa elimu ya awali, msingi na sekondari ikiwa pamoja na udahili jumuishi, udumishaji shuleni, na kuhitimisha masomo; kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za kufundishia na kujifunzia ikiwa pamoja na vitabu, samani na miundombinu; na kusimamia uajiri na kuwapangia walimu shule.

2.3.1 Ngazi za Elimu Nchini

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995 ilitoa muundo wa mfumo rasmi wa elimu na mafunzo nchini katika ngazi saba ambazo zimeelezwa katika **Kielelezo 2.2**.

Kielelezo 2.2: Muundo wa Mfumo Rasmi wa Elimu na Mafunzo Nchini Tanzania

Elimu ya Awali	• Miaka 2 •Umri kati ya miaka 2-5 •hujifunza Afya ya Msingi
Elimu ya Msingi	•Miaka 7 • Inatoa Cheti cha Kumaliza Elimu ya Msingi •Hutolewa kwa watoto wote wa umri kati ya mika 7-12 •Mamlaka ya cheti-Baraza la Mitihani la Taifa
Elimu ya Sekondari	•Miaka minne ya Sekondari awali na 2 ya sekondari ya juu •Inatoa cheti cha kumaliza Elimu ya Sekondari •Mamlaka ya utoaji cheti ni Baraza la Mitihani
Elimu ya Ufundi	•Kati ya mwaka 1-3 kutegemean na kozi anuai •Inatoa cheti cha ufundi •Inpokea wanafunz waliomaliza elimu ya Msingi na kuendelea •Mamlaka ya uoaji cheti ni VETA
Elimu ya Taaluma	•kati ya mwaka 1-3 kutemean na kozi •inatoa Cheti cha taaluma cha Kitafa ngazi 5-8 •Mamlka ya utoaji cheti ni Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi'
Elimu ya Juu	•kati ya mika 3-5 kutegemeana na aina ya programu •Inapokea wanafunzi kutoka sekindari ya juu au elimu ya ufundi ngazi ya 8

Chanzo: Uchambuzi wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014

Mfumo wa elimu na mafunzo rasmi nchini ni kama unavyofafanuliwa hapa chini.

(a) Elimu ya awali

Elimu ya Awali – ni sehemu ya elimu ya msingi inayotolewa kwa wanafunzi wenye umri wa kuanzia miaka 5 hadi 6.
Malengo makuu ya elimu ya awali ni:

1) Kukuza uwezo wa mtoto kujifunza kwa kutenda;

2) Kukuza uwezo wa mtoto wa kuthamini na kuendeleza tamaduni zinazokubalika katika jamii;
3) Tambua watoto wenye mahitaji maalumu na kutafuta ufumbuzi unaofaa; na
4) Kumuendeleza mtoto kiroho na kimaadili.

(b) Elimu ya Msingi

Huu ni mzunguko wa elimu wa miaka saba, ambao ni lazima kwa watoto wote wenye umri wa miaka saba. Mwishoni mwa mzunguko huu, wanafunzi hujiandikisha katika elimu ya sekondari, mafunzo ya ufundi stadi au kuingia katika ulimwengu wa kazi.

Malengo makuu ya elimu ya msingi ni:

1) Kuendeleza uwezo wa kusoma, kuandika na ujuzi wa hesabu;
2) Kuendeleza watu ambao wanaweza kutambua matatizo na kutafuta ufumbuzi unaofaa zaidi kwa njia ya kidemokrasia na shirikishi;
3) Kukuza ujuzi wa kiufundi na vipaji miongoni mwa wanafunzi katika umri mdogo; na
4) Kuhimiza na kuimarisha uadilifu na uwajibikaji miongoni mwa watoto hadi vijana.

(c) Elimu ya Sekondari

Hii ni elimu rasmi inayotolewa kwa watu waliofanikiwa kumaliza miaka saba ya elimu ya msingi na kukidhi vigezo vinavyohitajika kwa elimu ya sekondari. Elimu ya sekondari imegawanyika katika ngazi mbili ambazo ni ngazi ya kawaida (kidato cha 1 hadi 4), na kiwango cha juu (kidato cha 5 na 6).

Elimu ya sekondari ya ngazi ya kawaida hudumu kwa miaka minne wakati sehemu ya kiwango cha juu hudumu kwa miaka miwili. Wanafunzi wanaomaliza elimu ya sekondari ya ngazi ya kawaida wanaweza kuendelea na hatua inayofuata ya elimu ya sekondari ya kiwango cha juu, au mafunzo ya ufundi stadi au elimu ya ufundi. Vilevile, kwa wanafunzi wanaomaliza sekondari ya kiwango cha juu wanaweza kuendelea na mafunzo ya ufundi stadi, elimu ya ufundi na/au elimu ya juu.

Lengo kuu la elimu ya sekondari ni:

1) Kuimarisha, kupanua, na kuendeleza uelewa wa kina wa mawazo na dhana zinazopatikana katika ngazi ya msingi;
2) Kuimarisha, kutambua na kuendeleza maadili ya kitamaduni ikiwa pamoja na umoja wa kitaifa, utambulisho, demokrasia, maadili, uadilifu wa kibinafsi, utayari wa kufanya kazi, haki za binadamu, desturi, mila, wajibu wa kiraia, na majukumu; na
3) Kuendeleza utayari wa elimu ya juu, mafunzo ya ufundi, elimu ya ufundi na kitaalamu, na kuwajengea hisia na uwezo wa kujisomea, kujiamini, na kujiendeleza katika maeneo mapya ya sayansi na teknolojia.

(d) Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Elimu ya ufundi stadi hutolewa baada ya elimu ya msingi na huhusu kozi za ushonaji, uchoraji, na useremala, n.k. na hudumu kwa hadi miaka minne na mwishoni mhitimu hupewa cheti cha uwezo. Wanafunzi waliofanikiwa wanaweza kujiunga na ulimwengu wa kazi au kuendelea na mafunzo zaidi.

(e) Elimu ya Ualimu na Elimu ya Mafunzo ya Ufundi

Elimu ya ufundi inahudhuriwa na wanafunzi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yanayohitaji viwango vya juu vya ujuzi, maarifa na uelewa na ambapo wanawajibika katika eneo lao la utaalamu. Elimu ya ufundi hutolewa na vyuo mbalimbali vya mafunzo ya ufundi nchini katika maeneo mbalimbali ya biashara na usimamizi, afya na sayansi shirikishi, benki, uhasibu, kilimo, mazingira, utalii n.k. Mwishoni mwa mafunzo, mwanafunzi hutunukiwa cheti au diploma katika nyanja husika ya masomo.

(f) Elimu ya Juu

Elimu ya juu inajumuisha elimu yote inayotolewa baada ya elimu ya sekondari ya ngazi ya juu ambayo hupelekea tuzo ya cheti, diploma na shahada.

2.3.2 Shughuli kuu Zinazofanywa na Watendaji Muhimu katika Sekta ya Elimu

Kazi hii inafanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania. Ni hatua ya awali ya mzunguko wa elimu nchini ambapo mahitaji ya kujifunza yanabainishwa na malengo yanawekwa pamoja na muundo wa kuongoza mchakato mzima wa utoaji wa elimu nchini. Mtaala, miongoni mwa mambo mengine, unabainisha kiwango cha elimu, muda utakaotumika katika kila ngazi, masomo yatakayofundishwa, mbinu zitakazotumika kufundishia, malengo ya kujifunza, matokeo, na maelekezo mengine muhimu ya elimu.

Huu ni mchakato ambapo mwingiliano kati ya wanafunzi na walimu kushiriki pamoja kuboresha maarifa yao hujidhihiridha. Kufundisha na kujifunza hufanyika kupitia mbinu mbalimbali lakini jambo muhimu ni mbinu shirikishi ambapo mwanafunzi h kitovu cha kujifunza na mwalimu kuwa mwezeshaji.

Mitaala ya kitaifa inategemea umahiri. Katika mfumo wa elimu nchini hii inafanywa katika kiwango cha shule chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI ambayo inahusika na usimamizi wa kila siku wa shule, na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hutoa mwongozo wa sera kupitia huduma bora na za uhakika

(a) Tathmini na Upimaji

Tathmini inahusu mchakato ambao maendeleo na mafanikio ya mwanafunzi hupimwa au kuhukumiwa kwa kufuata vigezo maalumu vya ubora. Inatoa taarifa juu ya kiwango ambacho matokeo/malengo yaliyokusudiwa ya kujifunza yanapatikana.

Tathmini inahusisha kukusanya na kuchambua taarifa kuhusu shughuli za programu, sifa, na matokeo. Hivyo, tathmini ya mtaala inahusisha kukusanya na kuchambua taarifa kutoka vyanzo vingi ili kuboresha kujifunza kwa mwanafunzi kwa njia endelevu.

Tathmini inafanywa kwa njia mbili tofauti, ya kwanza ni tathmini iliyofanyika wakati ujifunzaji ukiendelea ili kutathmini iwapo wanafunzi wanaelewa maarifa yaliyokusudiwa, na ni kwa madhumuni ya kuboresha

kujifunza. Hii ni aina ya tathmini ya muundo iliyoundwa na kusimamiwa na walimu kupitia vipimo vya mara kwa mara au mitihani.

Tathmini ya pili inafanywa ili kupima iwapo wanafunzi wamefikia malengo yaliyokusudiwa ya andalio la somo. Hii ni tathmini ya muhtasari uliofanywa mwishoni mwa programu fulani. Tathmini hii ya muhtasari katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu inafanyika kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania.

(b) Usajili na Idhibati

Usajili na uidhinishaji hufanywa na serikali kupitia mihimili mbalimbali kulingana na kiwango cha elimu. Shule za msingi na sekondari zinasajiliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia kamishna wa elimu ili kudhibitisha kuwa shule zilitimiza mahitaji ya msingi ya kufanya kazi ambazo ni pamoja na miundombinu kama vile madawati, madarasa, ofisi za walimu, uwanja wa michezo, mashimo ya vyoo, n.k.

Kwa elimu ya ufundi, usajili na uidhinishaji hufanywa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), ambalo hutoa idhini ya vyuo vya ufundi na ufundi stadi kufanya kazi na mara kwa mara kuangalia kama vinazingatia masharti na viwango vya usajili.

Katika ngazi ya chuo kikuu, jukumu la usajili na ithibati hufanyika kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU). Shughuli kuu zinazofanywa na Tume hii ni pamoja na:

(c) Udhibiti

Mwenendo wa tathmini ya mara kwa mara ya vyuo vikuu, mifumo yao, na programu ili kudhibiti mifumo ya uhakiki wa ubora katika vyuo vikuu vipya. Tume pia inathibitisha na kutathmini programu ili kuhakikisha uaminifu wao wa utambuzi wa sifa za vyuo vikuu zilizopatikana kutoka kwa taasisi za ndani na za nje kwa matumizi ya nchini.

2.3.3 Uhusiano baina ya Watendaji Muhimu

Kuna makundi makuu matatu ya watendaji wakuu katika utoaji wa elimu nchini. Makundi haya ya watendaji wakuu ni:

(a) Watungasera na wasimamizi wa sekta ya elimu
(b) Wasimamizi wa ngazi mbalimbali za elimu
(c) Watoahuduma

Makundi haya yanafafanuliwa kwa kina hapa chini.

(a) Watungasera na wasimamiaji wa elimu

Kundi hili linajumuisha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais - TAMISEMI zikiwa wizara mama zinazohusika moja kwa moja na elimu nchini. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ina jukumu la kutunga sera na miongozo ya kusimamia sekta za elimu wakati OR - TAMISEMI inawajibika kwa usimamizi wa kila siku wa shule.

(b) Wasimamizi na mamlaka ya kudhibitisha viwango mbalimbali vya Elimu

Kundi hili linahusisha taasisi mbalimbali za elimu zinazosimamia utekelezaji wa shughuli za elimu katika ngazi mbalimbali. Taasisi hizi ni pamoja na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Baraza la Mitihani la Tanzania, na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania inasimamia utoaji wa elimu katika ngazi ya chuo kikuu ili kuhakikisha kuwa kila chuo kikuu kinaanzishwa, kinaidhinishwa, na kinaendeshwa kulingana na viwango vilivyowekwa.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi lina jukumu la kuratibu na kusimamia vyuo vya ufundi na ufundi satdi ili kuhakikisha vinafanya kazi ndani ya mfumo na kwa viwango vilivyowekwa. Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi pia linahakikisha kuwa vyuo vya ufundi stadi vimesajiliwa, kuidhinishwa na kudumisha masharti ya idhini katika shughuli zao.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina jukumu la kubaini mafanikio ya malengo ya kujifunza kwa njia ya uchunguzi wa kina katika elimu ya msingi na sekondari, pamoja na elimu ya ualimu.

(c) Wasimamizi na mamlaka ya kudhibitisha viwango mbalimbali vya elimu

Kundi hii linajumuisha watoahuduma kama vile shule za msingi na sekondari, vituo vya mafunzo ya ufundi stadi, vyuo vikuu, na watoahuduma wengine za elimu. Hawa wanahusika kivitendo na utekelezaji halisi wa mafunzo na mitaala kwa wanafunzi. **Kielelezo 2.3** kinaelezea uhusiano uliopo kati ya watendaji hawa muhimu katika elimu.

Kielelezo 2.3 Uhusiano baina ya Watendaji Muhimu katika Sekta ya Elimu Nchini



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Sheria na Nyaraka Zinazoongoza Sekta ya Elimu*

2.4 Ufadhili wa Utoaji wa Elimu

Ufadhilli wa shughuli za elimu kimsingi hufanywa kupitia mgao toka serikalini na wadau wa maendeleo. Fedha hutengwa kwa ajili ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na taasisi zake au OR - TAMISEMI kupitia muundo wa kawaida wa mfumo wa bajeti.

Jedwali 2.1 linaonesha bajeti iliyotengwa kwa sekta ya elimu ili kutekeleza shughuli mbalimbali nchini. Bajeti za kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2013/14 hadi 2019/20 zilichambuliwa kwa asilimia ya bajeti yote ya serikali kama inavyoelezwa kwenye **Jedwali 2.1**.

Jedwali 2.1: Ulinganisho wa Bajeti ya Jumla ya Serikali na ile ya Sekta ya Elimu

Mwaka wa Fedha	Jumla ya Bajeti ya Taifa (Kiasi katika bilioni)	Bajeti ya Sekta ya Elimu (Kiasi katika bilioni)	Asilimia ya Bajeti ya Sekta ya Elimu kwenye Bajeti yote
2013/14	18,249	3,172	17
2014/15	19,853	3,465	17
2015/16	22,496	3,870	17
2016/17	29,540	2,958	10
2017/18	31,712	4,706	15
2018/19	32,475	3,212	10
2019/20	33,105	4,512	14

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Bajeti ya kila Mwaka katika Sekta ya Elimu (2021)*

Kwa kipindi cha miaka saba kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2019/20, bajeti ya sekta ya elimu ilikuwa kati ya asilimia 10 na 17 ya bajeti yote ya Serikali. Kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2016/17, bajeti ya sekta ya elimu ilibaki asilimia 17. Kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2019/20, bajeti ilibainika kushuka kati ya asilimia 10 mwaka 2016/17 na asilimia 15 mwaka 2017/18. Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilichambuliwa kwa miaka 7 kama inavyoelezewa katika **Jedwali 2.2**.

Jedwali 2.2: Bajeti ya Serikali Ikilinganishwa na Bajeti ya WEST

Mwaka wa Fedha	Jumla ya Bajeti ya Serikali	Bajeti ya WEST	Asilimia
	Kiasi katika Bilioni ya Shilingi		
2013/14	18,249	700	4
2014/15	19,853	799	4
2015/16	22,496	803	4
2016/17	29,500	1,094	4
2017/18	31,712	1,337	4
2018/19	32,500	1,407	4
2019/20	33,100	1,389	4

Chanzo: *Hotuba ya Uwasilishaji Bajeti Bungeni ya WEST kwa Mwaka wa Fedha Husika*

Jedwali 2.2 linaonesha kuwa kwa miaka saba ya fedha iliyopita, bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilidumishwa kwa asilimia 4 ikilinganishwa na bajeti nzima ya serikali. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2013/14 hadi 2019 kwa wastani, serekali iliweza kutoa takribani asilimia 95.4 ya bajeti iliyotengwa. Kiwango zaidi kilichotolewa kilikuwa asilimia 87 (mwaka 2018/19) na kiwango cha juu zaidi ni asilimia 114 (mwaka 2015/16).

SURA YA TATU

RASILIMALI KWA AJILI YA UTOAJI WA ELIMU

3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza utendaji katika upangaji na bajeti, ugawaji na usambazaji, ukusanyaji, na matumizi ya rasilimali katika utoaji wa elimu nchini. Rasilimali zilizojumuishwa katika sura hii ni pamoja na fedha, watumishi, na zana na vifaa muhimu kwa utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na utoaji wa elimu nchini.

Utoaji wa rasilimali katika sekta ya elimu hufanywa na Serikali kupitia wizara zinazohusika hasa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Rasilimali-fedha pia hupatikana kupitia fedha za wafadhili kwenye miradi maalumu.

3.2 Maboresho Yaliyoonekana Katika Utoaji wa Elimu Nchini

Kaguzi zilibaini uwekezaji wa kutosha ambao umekuwa ukifanywa na serikali katika kuboresha utoaji wa elimu ya msingi, sekondari, ufundi na chuo kikuu katika kipindi cha miaka 5 iliyopita.

3.2.1 Utoaji wa Elimu bila Malipo (Darasa la I hadi Kidato cha IV)

Serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha katika utoaji wa elimu kwa kuanzisha elimu bure kuanzia ngazi ya elimu ya msingi hadi sekondari. Tangu kuanzishwa kwa elimu bure mwaka 2016, Serikali imetumia takribani shilingi trilioni 1.096 hadi kufikia mwaka wa fedha 2019/20. Fedha hizi zimetumika kugharamia utoaji wa elimu ya msingi inayohusu maeneo mengi ikiwemo matengenezo ya miundombinu na maendeleo, rasilimali-watu, udhibiti wa ubora, na uhakika katika sekta ya elimu.

Kuanzishwa kwa Mpango wa Elimu Bure kumechangia ongezeko la idadi ya wanafunzi na hivyo haja ya kuongeza uwekezaji sambamba katika miundombinu, rasilimali-watu, vifaa vya maabara, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, na shughuli za uhakiki wa ubora ambazo zinaathiri utoaji wa elimu ya msingi, sekondari, na elimu ya juu. Kwa mfano, kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi darasa la kwanza hadi la saba kimeongezeka kutoka wanafunzi 8,298,282 hadi 10,460,785 sawa na ongezeko la asilimia

26. Idadi ya wanafunzi wa shule za sekondari imeongezeka kutoka 1,774,383 hadi 2,062,717 katika kipindi kama hicho.

3.2.2 Maboresho katika utoaji wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Elimu ya Juu

Uboreshaji na Ujenzi wa Miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari

Serikali imegharamia maboresho ya miundombinu katika shule za msingi na sekondari ambayo yameimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika utoaji wa elimu. Kwa mfano, Serikali imetumia takribani shilingi bilioni 326.1 kuboresha miundombinu ya shule kongwe 86 kati ya 89. Matumizi ya hivi karibuni yalikuwa awamu ya tatu ambapo Serikali ilitumia shilingi bilioni 8.7 kukarabati shule kongwe 12.

Serikali imeongeza idadi ya madarasa kwa kujenga mapya 8,782 na hivyo kuyafanya yafikie 166,571 kutoka 175,353 yaliyokuwepo. Katika kipindi hichohicho, Serikali imejenga nyumba mpya 15,562. Uwekezaji huu ulifanyika ili kuendana na ongezeko la ajira za walimu wa shule za msingi na sekondari pamoja na kuhakikisha kwamba wanafanya kazi na kuishi katika mazingira mazuri.

Aidha, Serikali imekarabati au kujenga majengo mapya ya maabara katika shule za sekondari na hivyo kuongeza idadi hadi kufikia 6,104 nchini. Mbali na ujenzi wa miundombinu, Serikali pia imeboresha miundombinu ya kujifunzia kwa kuzipatia shule zinazotoa elimu maalumu vifaa vipya 37,820 vya kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Vifaa hivi vilipelekwa katika shule 1,305 zinazotoa elimu maalumu kote nchini.

Utoaji wa Vitabu

Katika kuhakikisha utoaji wa elimu bora, kwa miaka mitano iliyopita, Serikali ilizalisha na kusambaza vitabu 2,962,648 vya darasa la saba pamoja na mitaala 272,000 ya darasa la kwanza hadi la saba. Zaidi ya hayo, Serikali ilisambaza vitabu 25,452 vya wanafunzi wasioona katika shule mbalimbali nchini kote.

Ongezeko la Idadi ya Walimu

Katika kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi katika ngazi zote za elimu, Serikali imeajiri walimu ili kusaidia utoaji wa elimu katika elimu ya msingi na sekondari. Hadi sasa, idadi ya walimu wa shule za msingi na sekondari wamefikia 253,633 ambayo ni sawa na asilimia 75 ya mahitaji yote ya walimu nchini. Mbali na hilo, Serikali pia imeajiri mafundi 397 wa maabara ambao walipelekwa katika shule za sekondari zinazofundisha masomo ya sayansi ili kuimarisha elimu kwa vitendo kwenye masomo kama vile fizikia, kemia na biolojia.

Kuimarisha Shughuli za Uhakikisho wa Ubora

Katika kuhakikisha ubora wa elimu Serikali ilitoa vyombo vya usafiri kuanzia ngazi ya mkoa hadi kata ili kurahisisha ukaguzi na usimamizi wa utoaji wa elimu bora katika maeneo yao ya kiutawala. Jumla ya magari 38 yametolewa kwa maofisa elimu wa mikoa na magari 184 tayari yamenunuliwa na yanasubiri kusambazwa mikoani na katika halmashauri. Aidha, pikipiki 3,900 zimesambazwa kwa maofisa elimu kata ili kurahisisha shughuli za udhibiti wa ubora kwenye kata zao. Hatua nyingine iliyochukuliwa na Serikali kuimarisha shughuli za uhakiki wa ubora ni kuajiri wahakiki ubora takribani 400 katika mwaka wa fedha 2019/20, pamoja na kujenga ofisi zipatazo 100 za wadhibiti ubora nchini.

Aidha, Idara ya Udhibiti Ubora wa Elimu katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliweza kutembelea jumla ya taasisi 5,058 zikiwemo shule za msingi 3,953, shule za sekondari 1,089, na vyuo vikuu 16, sawa na asilimia 84.8 ya taasisi zote nchini. Pia, Idara iliweza kufanya ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa wakati wa ukaguzi wa shule uliofanyika katika shule za chekechea na msingi 494 na shule za sekondari 75 ili kupima kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwao katika kaguzi zilizofanyika.

Kuimarisha Utoaji wa Elimu ya Juu

Katika kuimarisha utoaji wa elimu ya juu, juhudi za Serikali zimehakikisha kuna ongezeko la udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka 125,000 mwaka 2015 hadi wanafunzi 142,179 mwaka 2021. Ongezeko hili la udahili ni sawa na asilimia 14 ya wanafunzi wote waliodahiliwa mwaka 2015.

Aidha, kumekuwa na ongezeko la utoaji wa mikopo kwa wakati kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ambapo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, mgao wa mikopo umeongezeka kutoka shilingi bilioni 373 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 462 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 24.

3.3 Kupanga na Kuweka Bajeti ya Rasilimali kwa ajili ya Utoaji wa Elimu Nchini

3.3.1 Upangaji wa Bajeti Isiojitosheleza kwa ajili ya Utoaji wa Elimu Nchini

Licha ya umuhimu wa kupanga na kubajeti, kaguzi za ufanisi nne kati ya tisa zilizofanywa zilibaini kuwa kulikuwa na upangaji wa bajeti isiojitosheleza kwa ajili ya utoaji wa elimu. Maelezo ya kina kutoka katika kila ripoti yanaelezwa hapa chini.

Kulingana na ripoti inayohusu utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeweza kupanga bajeti ya utekelezaji wa shughuli za utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kipindi cha miaka miwili ya fedha ambayo ni 2014/15 na 2015/16. Hata hivyo, kiasi kilichotolewa kulingana na bajeti hakikutumika kwa shughuli zilizokusudiwa, badala yake kilitumika kutekeleza shughuli zingine za wizara. Wizara ilitoa kipaumbele cha chini kwenye kufadhili shughuli za utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Vivyohivyo, OR - TAMISEMI haikupanga bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za elimu kwa watu wenye mahitaji maalumu kwa kipindi cha miaka mitano.

Matokeo yake, wizara hizo mbili hazikuweza kuwa na udhibitisho wa bajeti kutekeleza shughuli zake na ziliendelea kutegemea fedha za wafadhili katika kutoa elimu ya mahitaji maalumu kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 3.1.**

Jedwali 3.1: Bajeti ya Utoaji Elimu kwa Mahitaji Maalumu

Mwaka wa Fedha	Bajeti	Kiasi halisi Kilichopokelewa	Asilimia ya kiasi Kilichotolewa
	Kiasi katika Bilioni ya Shilingi ya Tanzania		
2014/15	306	274	90
2015/16	1,098	359	33
2016/17	-	-	-
2017/18	-	-	-
2018/19	-	-	-

Chanzo: *Bajeti na Ripoti za Utendaji toka Wizara ya Elimu*

Jedwali 3.1 linaonesha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilipanga bajeti kwa miaka miwili ya 2014/15 na 2015/16. Kwa mwaka 2016/17 na 2018/19, Wizara haikujumuisha bajeti ya mahitaji ya elimu maalumu. Pia, kiasi kilichotolewa kilikuwa asilimia 90 na asilimia 33 ya kiwango kilichotengwa.

Kwa mujibu wa ripoti ya ufanisi kuhusu ujenzi wa uwezo wa walimu walio kazini, OR - TAMISEMI haikutenga bajeti kwa ajili ya kuwajengea uwezo walimu walio kazini kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2018/19. Wizara ilitegemea zaidi misaada kutoka nje. Hii ilipelekea mafunzo ya walimu waliopo kazini kufanywa kwa asilimia 17 ya walimu wote waliopo nchini kwa sababu ya kukosekana kwa fedha. Katika miaka yote minne, hakukuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kutoa mafunzo kwani yalitolewa kwa walimu 44,516 tu kati ya 259,274 (ambayo ni sawa na asilimia 17) ya walimu wote walio kazini nchini.

Aidha, kwa mujibu wa ripoti ya upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi nchini, kulikuwa na maboresho katika utoaji wa fedha kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari. Katika kipindi cha miaka mitatu kati ya mitano ya fedha, Wizara iliweza kutenga jumla ya Tsh Bilioni 815 na ikafanikiwa kutoa jumla ya TSh Bilioni 326. Ukaguzi ulibaini zaidi kwamba baada ya mwaka wa fedha 2017/18 kulikuwa na kiasi tofauti cha bajeti na fedha inayotolewa kwa ajili ya utoaji wa elimu ya wenye mahitaji maalumu, mafunzo ya kujenga uwezo kwa walimu walioko makazini pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya shule ya msingi.

Ilibainika pia kuwa OR - TAMISEMI haikuwa na taarifa juu ya rasilimali zilizopo na zinazohitajika (vifaa kama vile madawati na meza) kwa miundombinu ya shule za msingi. Hii ilitokana na ukosefu wa kanzidata ya hali ya miundombinu ya shule za msingi. Kama ingekuwa na kanzidata, wizara ingeweza kupanga bajeti inayojitosheleza.

Ripoti ya usimamizi wa ulipaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ilibainisha udhaifu katika kupanga na kutoa ankara kwa wanufaika wa mikopo wa elimu ya juu. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mpango-mkakati uliopitiwa ulibainisha kuwa shughuli za kimkakati kuhusu utoaji wa ankara kwa wanufaika wa mikopo haikupangwa kikamilifu. Hakukuwa na malengo yaliyotambuliwa katika mipango ya utoaji wa ankara. Kupitia mapitio ya mpango-mkakati, bodi haikuwa na mpango wa kutoa ankara za urejeshaji wa mikopo. Taarifa zaidi zimetolewa katika **Jedwali 3.2**.

Jedwali 3.2: Idadi ya Wanufaika wa Mikopo Waliopangwa Kupewa Ankara

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Wanufaika wa Mikopo Waliopangwa Kupewa Ankara	Idadi ya Wanufaika Waliopewa Ankara	Asilimia ya Waliopewa Ankara
2012/13	0	0	0
2013/14	0	6	0
2014/15	0	5	0
2015/16	0	56,672	-
2016/17	0	59,108	-

Chanzo: *Kanzidata ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya Utoaji Ankara*

Jedwali 3.2 linaonesha kuwa kuanzia mwaka 2012/13 - 2016/17, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu haikuweza kupanga utoaji wa ankara kwa wanufaika wa mikopo. Zaidi, kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2012/13 hadi 2014/15, idadi ya walengwa waliopatiwa ankara ilikuwa 6 na 5. Ilibainika kuwa ankara zilianza kutolewa mwaka 2015/16 na 2016/17. Ingawa Bodi ilianza kutoa ankara katika kipindi cha miaka miwili, utendaji wake haukuweza kutathminiwa kwa sababu haikuwa na malengo yaliyowekwa.

3.3.2 Sababu ya kupanga bajeti isiyojitosheleza katika utoaji wa elimu

Zifuatazo ni sababu za upangaji wa bajeti isiyojitosheleza katika utoaji wa elimu nchini:

(a) Kutoa kipaumbele cha chini kwenye elimu ya mahitaji maalumu na kutegemea wafadhili kufadhili shughuli zinazohusiana na utoaji wa elimu ya mahitaji maalumu. Fedha kutoka kwa wafadhili hazikuwa za uhakika na endelevu;

(b) Kiasi cha fedha kilichotolewa kwa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2015/16 na 2016/17 kilihamishiwa kwenye matumizi ya shughuli zingine wizarani;

(c) Kuhamisha jukumu la kuendesha mafunzo ya walimu walio kazini kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwenda Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi wa Elimu (WMUE) kulifanya Taasisi ya Elimu kutopanga bajeti kwa miaka miwili. Vilevile, kwa miaka 2017/18 na 2018/19, Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi wa Elimu haikutenga bajeti;

(d) Kutokufanya upembuzi unaojitosheleza wa mahitaji kabla ya upangaji wa bajeti. Hali hii ilionekana katika usimamizi wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Bodi haikuweza kupanga malengo katika utoaji wa ankara kwa wanufaika waliopatikana. Vivyohivyo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikufanya upembuzi wa mahitaji katika sekretarieti ya mkoa, mamlaka za serikali za mitaa, na ngazi za nchi kuhusiana na kuwajengea uwezo walimu walio kazini.

3.3.3 Madhara yanayotokana na upangaji wa bajeti isiyotosheleza katika utoaji wa elimu

Yafuatayo ni madhara yatokanayo na kupanga bajeti isiyotosheleza katika utoaji wa elimu nchini:

i. Walimu walio makazini hawakujengewa uwezo kupitia mafunzo. Mafunzo pekee yaliofanyika yalijikita zaidi kwa walimu wa darasa

la I na la II waliopangiwa bajeti. Walimu 179,341 (asilimia 82) waliokuwa shule za msingi, waliachwa.

ii. Miundombinu ya shule za msingi kutokufanyiwa ukarabati. Katika miaka ya fedha 2 kati ya 5 kuanzia mwaka 2012/13 hadi 2015/16 hakukuwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli za ukarabati. Hii ilipelekea kutotolewa kwa fedha kuanzia mwaka 2011/12 hadi 2015/16

iii. Katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliweza kukarabati shule kongwe za sekondari 12 ambapo kiasi cha shilingi 8,685,167,591 zilitumika.

iv. Kutokuwa na uhakika wa utolewaji wa mikopo endelevu kwa wanufaika wapya kutokana na kupanga, kuweka bajeti na utoaji wa ankara usiojitosheleza kwa wanufaika wa mikopo. Wahitaji wapya wa mikopo watakuwa katika hatari ya kushindwa kupata rasilimali zinazohitajika ili kuwawezesha kupata elimu ya juu. Hii ni licha ya juhudi za sasa za Serikali kuboresha urejeshaji wa mikopo na kutungwa kwa sheria ambayo iliongeza kiwango cha marejesho kutoka asilimia 8 hadi 15.

3.4 Usambazaji na Utoaji wa Rasilimali kwa Huduma za Elimu

Sehemu hii imegawanyika katika maeneo yafuatayo: utoaji wa fedha kwa huduma za elimu; ugawaji wa rasilimali-watu kwa ajili ya huduma za elimu; na utoaji wa vifaa na vitendeakazi kwa ajili ya huduma za elimu

3.4.1 Utoaji wa Fedha Usioridhisha kwa ajili ya Huduma za Elimu

Matokeo ya ukaguzi katika sehemu hii yalionesha kuwa utoaji wa fedha ulikuwa haujitoshelezi. Katika kipindi cha miaka 7 (yaani mwaka 2013 /14 - 2019/20), bajeti ya sekta ya elimu ilikuwa kati ya asilimia 10 na 17 ya bajeti yote ya Serikali kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 3.3.**

Jedwali 3.3: Bajeti ya Sekta ya Elimu Ikilinganishwa na Bajeti ya Jumla ya Serikali

Mwaka wa Fedha	Bajeti Taifa ya Jumla (Sh. Bilioni)	Bajeti ya Sekta ya Elimu (Sh. Bilioni)	Asilimia ya Bajeti ya Sekta ya Elimu kwenye Bajeti ya Jumla ya Taifa
2013/14	18,249	3,172	17
2014/15	19,853	3,465	17
2015/16	22,496	3,870	17
2016/17	29,540	2,958	10
2017/18	31,712	4,706	15
2018/19	32,475	3,212	10
2019/20	33,105	4,512	14

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Bajeti ya Mwaka ya Serikali kwa Sekta ya Elimu Mwaka 2021*

Jedwali 3.3 linaonesha kuwa kuanzia mwaka 2013/14, mwenendo ulionesha kupungua kwa mgao wa bajeti katika sekta ya elimu. Mgao mkubwa ulikuwa katika miaka ya fedha 2013/14 na 2015/16 ambapo jumla ya mgao ulikuwa ni asilimia 17 ya jumla ya bajeti yote ya Serikali wakati kiasi cha chini kilikuwa asilimia 10 katika miaka ya fedha 2016/17 na 2018/19.

Aidha, kwa kuzingatia kiasi halisi cha fedha zilizopelekwa, ukaguzi ulibaini kwamba kulikuwa na ongezeko katika utengaji wa fedha kwa ajili ya utoaji wa elimu ya msingi, sekondari na elimu ya ufundi. Kwa mfano kati ya miaka ya fedha 2015/16 na 2019/20 jumla ya kiasi halisi cha fedha iliyopelekwa kiliongezeka kwa mara tatu kuanzia TSh Bilioni 107 katika mwaka wa fedha 2015/16 hadi kufikia TSh Bilioni 382 katika mwaka wa fedha 2019/20 kugharamia utoaji wa elimu ya msingi.

Kwa kuzingatia ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, serikali iliweza kutoa asilimia 87 ya kiasi kilichopangwa. Chanzo cha fedha kwenye utekelezaji wa shughuli mbalimbali ni wadau wa maendeleo haswa wale ambao walikuwa wanafadhili mradi wa elimu wa ujuzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu. Mradi huu ulifadhili Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR – TAMISEMI. Utoaji wa fedha ni kama inavyoainishwa katika **Jedwali 3.4.**

Jedwali 3.4: Jumla ya Bajeti na Kiasi halisi Kilichotolewa kwa Elimu ya Mahitaji Maalumu kuanzia Mwaka 2014 – 2018 (Sh. Bilioni)

Year	Bajeti		Kiasi kilichotolewa		Asilimia Iliyotolewa	
	WEST	OR-TAMISEMI	WEST	OR-TAMISEMI	WEST	OR-TAMISEMI
2014/15	306	-	274	-	90	-
2015/16	2,070	254	1,331	190	64	75
2016/17	-	5,277	-	5,037	-	95
2017/18	4,966	761	4,320	761	87	100

Chanzo: *Bajeti ya WEST, OR-TAMISEMI na Mradi wa LANES kuanzia Mwaka 2014 - 2018*

Jedwali 3.4 linaonesha kuwa katika mwaka 2014/15, WEST ilipokea fedha nyingi zaidi kwa elimu ya mahitaji maalumu, ambapo asilimia 90 ya fedha zilizopangwa zilitolewa. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2017/18, OR-TAMISEMI ilipokea fedha kwa kiwango cha juu zaidi cha asilimia 100 kwa ajili ya kusaidia elimu ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Ripoti kuhusu upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi nchini ilibainisha kuwa, WEST kupitia Kurugenzi ya Uhakikisho wa Ubora ilikuwa na bajeti anuwai za utekelezaji wa shughuli zake kuanzia mwaka 2011/12 hadi 2015/16 kama inavyoainishwa katika **Jedwali 3.5.**

Jedwali 3.5: Bajeti Ukilinganisha na Fedha Zilizotolewa kwa ajili ya Miundombinu ya Shule za Msingi

Mwaka wa Fedha	Bajeti	Kiasi Kilichotolewa	Asilimia Iliyotolewa
	Kiasi katika Milioni za Shilingi		
2011/12	2,085	107	5
2012/13	1,230	340	28
2013/14	1,046	87	8
2014/15	1,606	583	36
2015/16	2,235	1777	80

Chanzo: *Wizara ya Elimu - Ripoti ya Kurugenzi ya Uhakiki wa Ubora (2017)*

Jedwali 3.5 linaonesha kuwa utoaji wa fedha umekuwa ukiongezeka kwa miaka kadhaa, isipokuwa mwaka 2013/14 ambapo ni asilimia 8 tu ndio ilitolewa ikilinganishwa na mwaka 2015/16 ambapo kiasi halisi

kilichotolewa kilikuwa asilimia 80 ya bajeti wakati kiwango cha chini kilikuwa asilimia 5 mwaka 2011/12.

Kwa upande mwingine, muhtasari wa fedha zilizotengwa na bajeti halisi iliyotolewa kwa shughuli zinazohusiana na kujengea uwezo walimu walio kazini zilichambuliwa kwa wizara mbili.

Kwa kulinganisha utekelezaji wa bajeti kati ya wizara mbili, ilionekana kuwa wizara hizo zilikuwa na tofauti katika utoaji wa fedha kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 3.6.**

Jedwali 3.6: Asilimia ya Kiasi Halisi Kilichotolewa kwenye Bajeti

Mwaka wa Fedha	Kiasi Kilichotolewa (%)			
	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19
WEST	80	57	42	28
OR-TAMISEMI	56	62	19	53

Source: *Mfumo wa Matumizi ya Muda wa Kati 'MTEF' kutoka OR-TAMISEMI na WEST kwa Kipindi cha Kuanzia Mwaka 2015/16 hadi 2018/19*

Jedwali 3.6 linaonesha kuwa utekelezaji wa bajeti ya WEST umekuwa ukipungua kwa miaka kadhaa, kutoka asilimia 80 ya bajeti mwaka 2015/16 hadi asilimia 28 mwaka 2018/19. Kwa upande mwingine, OR - TAMISEMI ilionekana kuwa na mwenendo thabiti zaidi, kwani ilipokea zaidi ya asilimia 50 ya bajeti yake isipokuwa kwa mwaka 2017/2018 ambayo ilipokea asilimia 19.

Kwa kuongezea, kulingana na ukaguzi wa ufanisi kwenye eneo la kuwajengea uwezo walimu walio kazini, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) na Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi wa Elimu (WMUE) kwa kushirikiana na WEST, ilihusika na mpango wa kuwajengea uwezo walimu walio kazini kwa ufadhili wa mradi wa ujuzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu (LANES) na UNICEF.

Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi Elimu (WMUE) ilipokea asilimia 25 tu ya bajeti yote ya shilingi bilioni 12.4 kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2018/19 wakati Taasisi ya Elimu Tanzania ilipokea asilimia 96 ya shilingi bilioni 13.47 kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2018/19.

Vilevile, ukaguzi wa ufanisi wa upatikanaji wa elimu bora ya ufundi na mafunzo ulibaini kuwa, katika kipindi cha miaka mitano, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilipokea asilimia 72 ya kiwango cha bajeti cha shilingi bilioni 176.6 kwa ajili ya elimu ya ufundi. Pia, kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ilipokea asilimia 46 tu ya bajeti ya shilingi bilioni 469.79.

VETA haikuweza kutekeleza shughuli zingine kama vile utoaji wa vifaa vya kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Pia, haikuhakikisha uwepo wa samani katika vituo vyenye uhitaji wa vifaa ili kutoa elimu ya ufundi kwa sababu ya utolewaji wa fedha isiojitosheleza.

Zaidi ya hayo, ripoti ya usimamizi wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ilionesha kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilikuwa na bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 2,590.02 kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18. Asilimia 39 ya bajeti yote katika miaka minne ilikuwa michango iliyotokana na ulipaji wa mkopo, wakati asilimia 61 ilikuwa mgao kutoka Serikalini.

3.4.2 Sababu ya Utoaji wa Fedha Usiojitosheleza katika Utoaji wa Elimu

Kwa mujibu wa ripoti zilizopitiwa, sababu kuu za utoaji wa fedha usiojitosheleza katika ufadhili wa utoaji wa elimu ni pamoja na:

(a) Vipaumbele shindani vya serikali

(b) Makusanyo ya fedha yasiyotosheleza kufadhili shughuli za utoaji wa elimu nchini; na

(i) Kukosekana kwa kipaumbele katika ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi. Hata hivyo, kwa miaka ya hivi karibuni, kipaumbele kimetolewa katika ukarabati wa shule kongwe za sekondari.

3.4.3 Matokeo ya Utoaji wa Fedha Usiotosheleza katika Utoaji wa Elimu

Kulikuwa na matokeo kadhaa yaliyotokana na utoaji fedha usiotosheleza ili kufanikisha utoaji wa elimu ikiwa ni pamoja na:

(i) Madawati yasiyotosheleza mahitaji ambayo kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2012 hadi 2016 takribani wanafunzi milioni 1.1 hawakuwa na madawati ya kutosha na hivyo kuathiri masomo yao;

(ii) Kutokutolewa kwa zana za kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu kama vile *themofomu*; printa ya nukta-nundu (braille embosser), mashine ya nukta-nundu (braille machine); na vifaa kwa ajili ya uchunguzi wa masikio (otoscope);

(iii) Kukosekana kwa vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika vyuo vya Ufundi Stadi. Pia, vifaa na zana muhimu kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia kama madawati, meza na miongozo ya kufundishia hazikupelekwa vyuoni;

(iv) Katika mwaka 2011/12, ni asilimia 43 tu ya kaguzi zilizopangwa zilifanywa na kurugenzi ya uhakiki wa ubora. Shughuli za ukaguzi ziliathiriwa na utolewaji finyu wa fedha;

(v) Kulikuwa na ukarabati hafifu wa miundombinu ya shule, na ujenzi usiotosheleza wa miundombinu mipya ya shule za msingi. Aidha, hakukuwa na idadi ya kutosha ya matundu ya vyoo, madarasa, ofisi za walimu, pamoja na ukarabati hafifu wa vifaa vilivyokuwepo;

(vi) Idadi isioridhisha ya walimu walio kazini walihudhuria mafunzo ya kujengewa uwezo ambao ni asilimia 18 tu ya walimu wote walio kazini.

3.4.4 Ugawaji na Matumizi ya Fedha katika Taasisi za Elimu ya Juu na Tume ya Sayansi na Teknolojia

Sehemu hii inawasilisha jinsi rasilimali-fedha zilivyosimamiwa katika programu zilizofadhiliwa na wadau wa maendeleo nchini. Ukaguzi ulihusu

mipango ya kuimarisha uwezo wa utafiti katika taasisi za elimu ya juu na utafti, ambazo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Chuo Kikuu cha Ardhi; Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili; na Tume ya Sayansi na Teknolojia .

Kwa kipindi cha miaka mitano ya programu kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20, SIDA ilitoa kiasi cha fedha kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa utafiti katika taasisi husika kama ifuatavyo:

- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilipokea asilimia 100 ya kiwango kilichopangwa;
- Chuo Kikuu cha Ardhi kilipokea asilimia 91 ya kiwango kilichopangwa;
- Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kilipokea asilimia 100 ya kiwango kilichopangwa; na
- Tume ya Sayansi na Teknolojia ilipokea asilimia 79 ya kiwango kilichopangwa.

Jedwali 3.7 linatoa muhtasari wa taarifa za kiwango cha bajeti kilichopangwa na kiasi kilichotolewa katika asilimia kwa kila taasisi.

Jedwali 3.7: Kiasi Kilichotolewa katika Asilimia kwa Miradi ya SIDA

Taasisi	**Asilimia Iliyotolewa**				
	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20
UDSM	100	108	110	51	165
ARU	100	100	100	100	50
MUHAS	100	88	111	125	116

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Ripoti za Malipo ya Miradi ya SIDA 2020*

Jedwali 3.7 linaonesha kuwa kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2017/18, vyuo vikuu vyote vilipokea asilimia 100 au zaidi ya bajeti isipokuwa mwaka 2016/17 ambapo Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kilipokea asilimia 88 tu ya kiwango kilichotengwa.

Katika miaka ya fedha 2018/19 na 2019/20, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi vilipokea takribani asilimia 50 ya bajeti kila moja kwa sababu zifuatazo:

Kwanza, Chuo Kikuu cha Ardhi, asilimia 50 ya fedha ilizuiwa na SIDA kwa sababu ya ucheleweshaji wa kuwasilisha ripoti ya utekelezaji ya mgawo wa kwanza ya mwaka wa fedha 2019/20. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kilipokea asilimia 100 ya kiwango kilichopangwa; Tume ya Sayansi na Teknolojia ilipokea asilimia 79 ya jumla ya bajeti kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20.

Pili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi vilichelewa kuomba malipo ya pili ya mwaka 2018/19 na hivyo kuifanya SIDA ichelewesha kutoa fedha. Utolewaji wa fedha uliozidi asilimia 100 ulisababishwa na utofauti katika viwango vya ubadilishaji fedha kati ya tarehe ya kutiwa saini kwa mkataba na wakati fedha zilipotolewa.

Maelezo ya kina kuhusu kiasi kilichotolewa kwa kila programu ndogo imetolewa katika **Jedwali 3.8**.

Jedwali 3.8: Kiasi Kilichotengwa Ikilinganishwa na Kiasi Kilichopokelewa kuanzia Mwaka 2015/16 hadi 2019/20

Programu ndogo	Kiasi Kilichotengwa	Kiasi Kilichopokelewa	Asilimia Iliyopokelewa
	Kiasi katika Milioni		
Ufadhili wa Utafiti	2,162	1,504	70
Usimamizi wa Utafiti	3,014	2,487	83
Mawasiliano ya Utafiti	2,635	2,357	89
Ufadhili wa Uvumbuzi	732	340	46
Mfumo wa Usimamizi wa Vituo vya Uvumbuzi	837	570	68
Gharama za utendaji	1,107	1,004	91
Jumla	**10,487**	**8,262**	**79**

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Bajeti za Mwaka za COSTECH, 2015/16 hadi 2019/20*

Jedwali 3.8 hapo juu linaonesha kuwa, kiwango cha juu (asilimia 91) kilichotolewa kilionekana katika gharama za utendaji na kiwango cha chini (asilimia 46) kilichotolewa kilionekana katika fedha za ubunifu. Sababu za fedha za uvumbuzi kutolewa kwa asilimia 46 tu ni kuchelewesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Ilibainika kuwa, hadi wakati wa ukaguzi mnamo Juni 2020, programu ndogo ilifanikiwa kutumia asilimia 54 tu ya bajeti. Matokeo yake, Tume ya Sayansi na Teknolojia ilikuwa na

fedha ambazo hazijatumika na kupelekea kuongezewa mwaka mmoja ili kukamilisha shughuli zilizosalia kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa.

3.4.5 Matumizi ya Fedha zilizotengwa chini ya Programu ya SIDA

Licha ya kutolewa kwa fedha, hakukuwa na ufanisi katika matumizi ya fedha zilizotolewa kama ilivyoainishwa katika taasisi mbili kati ya nne chini ya programu ya SIDA kama ilivyoainishwa kwenye **Kielelezo 3.1.**

Kielelezo 3.1: Matumizi ya Fedha katika Chuo cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi



Chanzo: *Ripoti za Utendaji za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi kuanzia Mwaka 2015/16 hadi 2018/19*

Kielelezo 3.1 kinaonesha kuwa kwa wastani, kiwango cha matumizi ya fedha iliyotolewa kilikuwa asilimia 49 tu kwa mwaka. Kwa miaka yote minne, matumizi ya vyuo vikuu vyote viwili yalikuwa chini ya asilimia 100.

Katika miaka mitatu kuanzia 2016/17 hadi 2018/19, uwezo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi katika matumizi ya fedha zilizotolewa ulikuwa chini ya asilimia 65. Matumizi ya kiwango cha juu (asilimia 98) yalibainika katika Chuo Kikuu cha Ardhi katika mwaka wa fedha 2015/16.

3.4.6 Sababu za Matumizi ya Fedha chini ya Kiwango katika Programu za SIDA

Sababu zilizobainika za matumizi chini ya kiwango ni pamoja na:

(a) Kuchelewa kuanza utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na hivyo kuathiri uwezo wa kutumia fedha zilizotolewa. Kulikuwa na ucheleweshaji wa udahili wa wanafunzi wa shahada za uzamili kama ilivyobainika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa upande wa Chuo kikuu cha Ardhi, sababu ilikuwa kuchelewesha uchapishaji na makongamano; na

(b) Kitengo cha usimamizi wa manunuzi kuchelewesha kukamilisha mchakato wa manunuzi kama ilivyoonekana katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hii ilitokana na kitengo cha usimamizi wa manunuzi kutokuwa na uwezo wa kusimamia ununuzi wa vifaa maalumu ambapo mchakato wa manunuzi wa baadhi ya vifaa ulianza upya kwa sababu ya mapungufu yaliyobainika.

3.4.7 Matokeo ya Matumizi ya Fedha chini ya Kiwango

Utumiaji wa fedha kwa kiwango cha chini ulipelekea madhara yafuatayo:

(a) Awamu ya fedha iliyosalia haikutolewa kwa sababu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi havikuweza kufikia kiwango cha asilimia 70 ya matumizi;

(c) Tume ya Sayansi na Technolojia haikukamilisha shughuli zilizopangwa chini ya programu na ililazimika kuomba kuongezewa mwaka mmoja ili kukamilisha matumizi kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa; na

(d) Kubadili matumizi ya fedha kwenda shughuli zilizotekelezwa vizuri na kupewa kipaumbele zaidi kama ilivyobainika katika Chuo Kikuu cha Ardhi ambapo fedha zilizotengwa kwa ajili ya makongamano na machapisho zilibadilishwa matumizi.

3.4.8 Ugawaji wa Rasilimali-watu katika Utoaji wa Elimu Bora

Miongoni mwa sababu zilizochangia utoaji duni wa elimu ni ugawaji mbaya wa rasilimali-watu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Kaguzi za ufanisi 4 kati ya 9 zilizofanywa zilibaini upangaji usiojitosheleza wa rasilimali-watu katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika utoaji wa elimu bora.

Ukaguzi ulibaini kuwa, hakukuwa na idadi ya kutosha ya walimu ili kuhakikisha kuna upatikanaji wa elimu bora ya ufundi stadi. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya ufundi Stadi na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hawakuwa na idadi ya kutosha ya walimu ili kutekeleza shughuli mbalimbali. **Kielelezo 3.2** kinaonesha hali ya upatikanaji wa walimu kwa ajili ya utoaji wa elimu bora ya ufundi stadi.

Kielelezo 3.2: Upatikanaji wa Walimu kwa ajili ya Elimu na Mafunzo Bora ya Ufundi Stadi



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu za Elimu ya Msingi Mwaka 2013/14-2017/18*

Kielelezo 3.2 kinaonesha kuwa licha ya kuongezeka kwa idadi ya walimu wanaohitajika, katika kipindi cha miaka sita, idadi ya walimu waliopo iliendelea kubaki ileile. Idadi isiyotosheleza ya walimu ilisababisha kuwepo

kwa uwiano mbovu wa wanafunzi na walimu katika elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi wa Mwaka 2013/14 - 2017/18, uwiano wa walimu na wanafunzi unatakiwa kuwa 16:1. Kinyume na inavopaswa, wastani wa uwiano katika kanda 12 za VETA ulibainika kuwa 79:1. Hii ilisababisha vyuo kadhaa vya VETA kutoidhinishwa kutokana na kutokidhi kigezo cha uwiano unaotakiwa.

Ripoti ya usimamizi wa ujengewaji uwezo wa walimu walio kazini ilibainisha mgawanyo usiotosheleza wa wafanyakazi wanaohusika na utoaji wa elimu. Kwa mujibu wa ripoti, upungufu wa wafanyakazi ulikuwa kati ya asilimia 14 na 49. **Jedwali 3.9** linatoa muhtasari wa upungufu huo.

Jedwali 3.9: Ugawaji wa Wafanyakazi miongoni mwa Wadau Muhimu

Idadi ya Wafanyakazi	WEST	OR-TAMISEMI	TET	WMUE
	Kurugenzi ya Mafunzo ya Walimu	Kurugenzi ya Utawala wa Elimu	Kituo cha Mitaala na Ufundishaji	Walimu
Wanaotakiwa	28	76	35	28
Waliopo	16	44	18	24
Upungufu (%)	43	42	49	14

Source: Takwimu za Hali ya Rasilimali-watu *(IKAMA: 2018/19)*

Jedwali 3.9 linaonesha kuwa wadau wote walikuwa na idadi ya watumishi isiyotosheleza. Upungufu mkubwa ulibainika katika Taasisi ya Elimu Tanzania ambayo ilikuwa na upungufu wa asilimia 49 wakati upungufu wa chini ulikuwa asilimia 14 katika WMUE.

Aidha, ukaguzi wa utendaji kuhusu usimamizi wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulibaini upungufu katika ugawaji wa rasilimali-watu katika wizara hizo mbili katika idara zao kama inavyoainishwa katika **Kielelezo 3.3**

Kielelezo 3.3: Upungufu wa Rasilimali-watu kwa ajili ya Elimu Maalumu



***Chanzo**: Hali ya Rasilimali-watu kutoka Wizara Husika (IKAMA: 2018/19)*

Kielelezo 3.3 kinaonesha kuwa, upungufu mkubwa wa rasilimali-watu wa asilimia 81 ulibainika katika ofisi za udhibiti ubora za kanda za WEST, na upungufu wa kiwango cha chini wa asilimia 20 ulibainika katika idara ya Sera ya Elimu ya Mahitaji Maalumu katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Kwa kuongezea, ripoti ya upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule ya msingi iliainisha kwamba, idara ya elimu katika halmashauri sita zilizotembelewa hazikuwa na wafanyakazi wenye ujuzi kama vile wahandisi na mafundi mchundo wanaohusika na miundombinu ya shule za msingi. Pia, katika mamlaka za serikali za mitaa, idara ya wahandisi ilikuwa na kazi nyingi kuliko uwezo wa watumishi ambazo ziliwazuia kutekeleza vyema jukumu walilopewa la kusimamia miundombinu ya shule ya msingi. Ilibainika zaidi kuwa, mara nyingi walitoa kipaumbele kwa majukumu mengine ambayo yalikuwa hayahusiani na usimamizi wa miundombinu ya shule za msingi.

Sababu kuu zilizopelekea mgawanyo wa rasilimali-watu usiojitosheleza katika utoaji wa elimu ni upungufu wa fedha kwa ajili ya kuwezesha kuajiri na ugawaji wa rasilimali-watu.

3.4.9 Matokeo ya Ugawaji wa Rasilimali Usiotosheleza kwa Utoaji wa Elimu

Matokeo yaliobainika yalikuwa ni pamoja na:

(a) Kutofikiwa kwa uwiano wa wanafunzi - walimu unaohitajika katika utoaji elimu na mafunzo ya ufundi stadi ambayo yaliathiri mchakato mzima wa utoaji wa elimu;
(b) Kuathiri ubora wa elimu inayotolewa kwa wanafunzi; na
(c) Kutoidhinishwa kwa vyuo vya Ufundi Stadi kwa sababu ya idadi ndogo ya walimu wanaotakiwa wenye ujuzi wa kufundisha.

3.5 Upungufu wa Vifaa na zana kwa ajili ya Utoaji Elimu na Mafunzo

Vifaa kama madawati, vifaa vya kufundishia, na vifaa vya kusaidia wanafunzi waenye na mahitaji maalumu ni muhimu katika kuhakikisha utoaji mzuri wa elimu bora. Ripoti 6 kati ya 9 zilizungumzia masuala yanayohusiana na ugawaji wa zana na vifaa vya utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kama ilivyoainishwa hapa chini.

Ukaguzi wa ufanisi juu ya upatikanaji wa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi umebaini kuwa, hakukuwa na miundombinu ya kutosha ya kufundishia na kujifunzia.

Kulingana na ripoti, katika vyuo vya VETA vilivyotembelewa, vifaa na mashine zilikuwa na upungufu wa wastani wa asilimia 57. Kwa mujibu wa rejista ya zana na vifaa, kulikuwa na upungufu wa zana za mafunzo kwa vitendo kwa wastani wa asilimia 54.

Zaidi ya hayo, ukaguzi wa utendaji juu ya elimu ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulibaini kuwa, hakukuwa na vifaa vya kutosha kwa shule za wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Uchambuzi uliofanywa kwenye vifaa na kumbukumbu za vifaa vya kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulibaini kuwa kulikuwa na pengo la asilimia 68 la vifaa na zana muhimu kati ya vifaa 3,785 vilivyohitajika katika shule 17 zilizochukuliwa sampuli ambazo zilidahili wanafunzi wenye

mahitaji maalumu. Kwa kuongezea, shule zingine zilikosa kabisa vifaa vinavyohitajika kama **Jedwali 3.10** linavyoeleza kwa muhtasari.

Jedwali 3.10: Vifaa Ambavyo Havikuwepo katika Shule Zilizotembelewa

Jina la Shule	Jina la Vifaa Ambavyo Havikuwepo
Themi	*Themofomu*, printa ya nukta-nundu
Kibena	*themofomu*, karatasi za nukta-nundu, printa ya nukta-nundu
Ilembula	Printa ya nukta-nundu, vifaa vya kupimia kiwango cha kusikia, odiometa, mikebe ya kutengenezea modi za sikio, vifaa vya kusaidia kusikia vya mfukoni, vifaa vya kufundishia kusikia, mita za kiwango cha sauti, seti ya televisheni, redio
Kambarage	*Rato*
Nyangao	Printa ya nukta-nundu, utari wa kusaidia kusikia, vifaa vya kusaidia kusikia vya nyuma ya sikio, vifaa vya kusaidia kusikia vya mfukoni, vifaa vya kufundishia kusikia, kipokezi
Mtama	Vipande vya plastiki ngumu, chemshabongo, rato, seti ya televisheni, redio
Mugeza Mseto	Printa ya nukta-nundu
Wailes	*Rato*
Kijitonyama	Mbao za nukta-nundu za PVC, printa za nukta-nundu, themofomu,
Hombolo Bwawani	Karatasi za nukta-nundu, mbao za nukta-nundu za PVC, printa ya nukta-nundu, themofomu, fimbo nyeupe za kupapasia watu wenye ulemavu wa macho, mbao za kuandikia watu wenye ulemavu wa macho
Mpunguzi	Vipande vya plastiki ngumu, rato, michezo ya mafumbo, seti ya televishemi, redio
Kaigara	Vipande vya plastiki ngumu, michezo ya mafumbo, rato, seti ya televisheni, redio

***Chanzo**: Kumbukumbu za Zana na Vifaa vya Shule (2019)*

Kwa kuongezea, ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na vyumba vya kutosha vya kuhifadhi na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia vilivyotolewa katika shule zilizotembelewa.

Sampuli ya shule nne zenye wanafunzi wenye matatizo ya kusikia (Kigwe Viziwi, Mtendeni, Kaigara na Meru) zilibainisha kuwa ni Kigwe Viziwi pekee ndiyo ilikuwa na chumba cha kupimia kiwango cha kusikia. Chumba cha kupimia kiwango cha kusikia ni muhimu ili kupata matokeo ya kuaminika wakati wa upimaji wa kiwango cha kusikia cha wanafunzi.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 29(3) ya Mitihani ya 2016 inamtaka waziri anayehusika na elimu kueleza njia ambayo watahiniwa wasioona watatumia katika kushiriki masomo ya hisabati na sayansi. Hata hivyo, WEST haikuandaa miongozo ya mitihani.

Vilevile, ukaguzi wa utendaji kuhusu usimamizi wa kuwajengea uwezo walimu walio kazini ulibaini ukosefu wa miongozo ya kufundishia na kujifunzia kwa walimu wa shule za msingi na sekondari.

Aidha, ripoti ya upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi ilibainisha kuwepo kwa uhaba wa madawati kama inavyooneshwa kwa kifupi katika **Jedwali 3.11**.

Jedwali 3.11: Uchambuzi wa Madawati katika Shule za Msingi Nchini kuanzia Mwaka 2012- 2018

Mwaka wa Fedha	Madawati Yaliyopo (katika elfu)	Madawati yanayokosekana (katika elfu)	Asilimia (%) ya Madawati Yanayohitajika
2014	1,960	813	30
2015	1,930	656	24
2016	1,980	368	13
2017	3,160	60	6
2018	2,960	402	12

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu za Madawati kutoka kwenye Ripoti za Maendeleo - OR-TAMISEM ya Mwaka 2019*

Jedwali 3.11 linaonesha upungufu wa madawati katika kipindi cha miaka yote mitano. Upungufu mkubwa ulibainika katika mwaka 2014 ambapo ulikuwa asilimia 30. Mwaka 2017 ulibainika kuwa mwaka ambao hali ya madawati ilikuwa bora. Hii ilisababishwa na uhamasishaji wa kitaifa wa kuhakikisha madarasa yana madawati ya kutosha.

Moja kati ya miradi minne ya kujenga uwezo wa utafiti uliripoti ukosefu wa vifaa na zana za kutosha katika uimarishaji wa uwezo wa utafiti. Kwa mujibu wa ripoti ya kujenga uwezo wa utafiti katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, katika mwaka wa fedha 2016/17, programu ndogo ya malaria ilipanga kununua vifaa vya maabara ya utafiti kama sehemu ya kuboresha maabara. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini hakuna kifaa kilichonunuliwa kama inavooneshwa katika **Jedwali 3.12.**

Jedwali 3.12: Vifaa Vilivyopangwa Kununuliwa chini ya Programu Ndogo ya Malaria ya Kuboresha Maabara

Mwaka wa Fedha	Bidha Itayonunuliwa	Tarehe iliopangwa	Mustakabali
2016/17	Jokofu (-80°C) na Kifukizi	Desemba 2019	Hakikununuliwa
	Ukarabati wa Vichunguza Wadudu	Desemba 2019	Hakikununuliwa
	Kilisha utando, kemikali na darubini ya kutenganisha	Februari 2020	Hakikununuliwa

Chanzo: *Mipango na Ripoti za Mwaka za MUHAS Julai 2015/16 - Juni 2018/19*

Jedwali 3.12 linaonesha vifaa vilivyopangwa kununuliwa lakini havikununuliwa. Hii ilipelekea lengo la kuboresha maabara kutotimizwa.

3.5.1 Sababu za Upungufu wa Vifaa na Zana katika Utoaji wa Elimu Nchini

Sababu kuu za zana na vifaa visivotosheleza zilikuwa:

(a) Upatikanaji duni wa vifaa, ambapo wanafunzi waliohitaji kufanyia kazi zao nje ya mazingira ya chuo kikuu hawakuweza kupata huduma ya mtandao; na

(b) Mgawanyo wa fedha usiotosheleza kuwezesha upatikanaji wa zana na vifaa na hivyo kuathiri upatikanaji wa madawati, zana za kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu, n.k.

3.5.2 Matokeo ya Zana na Vifaa Visivotosheleza katika Utoaji Elimu

Ukosefu wa zana na vifaa vya kutosha ulipelekea yafuatayo:

(a) Maabara hazikuboreshwa hivyo kuathiri shughuli za utafiti. Matokeo yake kulikuwa na ucheleweshaji wa kujenga uwezo wa utafiti kama ilivyokusudiwa. Hali hii ilibainika katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili;

(b) Utoaji wa elimu usiotosheleza kama ilivyokusudiwa. Iliripotiwa kuwa kulikosekana ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa sababu ya ukosefu wa vifaa vya kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu;

(c) Kukosekana kwa ithibati ya vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa muda mrefu kwa sababu ya kukosekana kwa zana na vifaa vya kutosha kuwezesha mafunzo; na

(d) Ukosefu wa programu nzuri ya kutafutia maarifa mtandaoni kwa wanafunzi wa elimu ya juu hivyo kusababisha matumizi ya 'google' na injini programu zingine kupitia simu zao za mkononi kutafutia maarifa badala ya programu zilizosajiliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

3.6 Ufadhili wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Ili kutekeleza shughuli zake za kila siku, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilihitaji ufadhili ili kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Wakati wa ukaguzi huu, Bodi ilikuwa na vyanzo kadhaa vya fedha kama inavyooneshwa katika **Jedwali 3.13**.

Jedwali 3.13: Vyanzo vya Fedha za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuanzia Mwaka 2012/13 hadi 2015/16

Vyanzo	Kiasi (katika Shilingi Bilioni)	Asilimia katika Bajeti ya Jumla
Fedha kutoka Serikalini	1,625.45	63
Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo	936.91	36
Mapato toka kwa wadau wa waendeleo	25.76	0.9
Mapato mengine	1.9	0.1
Jumla	**2,590.02**	100

Chanzo: *Kumbukumbu za Uhasibu za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuanzia Mwaka 2012/13 hadi 2015/16*

Jedwali 3.13 linaonesha kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilitegemea fedha kutoka serikalini ambayo ilichangia karibu theluthi mbili ya bajeti

yake ikifuatiwa na ulipaji na urejeshaji wa mikopo ambao mchango wake ulikuwa theluthi moja ya bajeti.

Licha ya utegemezi mkubwa kutoka serikalini, ripoti ya usimamizi wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu ilibainisha kuwa Bodi haikuwa na ufanisi katika mifumo ya kuhakikisha kuwa inakusanya fedha kupitia ulipaji na urejeshaji wa mikopo ili kupunguza utegemezi kwa serikali kuu.

Katika kipindi cha miaka mitano, Bodi imekusanya asilimia 40 tu (shilingi bilioni 199) kati ya shilingi bilioni 492. Halikadhalika, ripoti ilionesha udhaifu wa urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika wadaiwa. Ripoti imeonesha kuwa, kulikuwa na jumla ya wanufaika wa mkopo 112,922 wanaodaiwa shilingi bilioni 706.7. Yote haya yalichangia utegemezi mkubwa wa Bodi kwa serikali.

3.6.1 Sababu za Ulipaji na Urejeshaji Usioridhisha wa Mikopo

Sababu zilizobainika za ulipaji na urejeshaji usioridhisha wa mikopo zinajumuisha:

i. Kushindwa kutafuta idadi ya kutosha ya wanufaika wa mikopo ambapo ilibainika kuwa Bodi haikuweza kufuatilia angalau nusu ya mikopo inayostahili kulipya katika kipindi cha miaka minne;

ii. Bodi ilishindwa kuhakikisha wanufaika wa mikopo wanalipa mikopo kikamilifu. Ilibainika kuwepo kwa mikopo inayostaili kulipwa inayofikia shilingi bilioni 7 katika kipindi cha zaidi ya miaka mitano.

iii. Njia duni za ukusanyaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika wanadaiwa waliopatikana. Ilibainika kuwa Bodi ilikusanya bilioni 221 tu kati ya trilioni 2.4 kutoka kwa wadaiwa waliopatikana kwa miaka mitano ya fedha kuanzia mwaka 2012/13 hadi 2016/17

3.6.2 Matokeo ya Ulipaji na Urejeshaji Hafifu wa Mikopo

Yafuatayo ni matokeo yaliyotajwa ya ulipaji na urejeshaji hafifu wa mikopo:

i. Upatikanaji endelevu wa rasilimali kwa wanufaika wapya wa mikopo kuwa hatarini kwani Bodi haitakuwa na fedha za kutosha kuwakopesha wanafunzi wapya wanaostahili; na

ii. Utegemezi wa bajeti ya nyongeza kutoka serikali kuu kwa utendaji na shughuli endelevu za Bodi.

SURA YA NNE

UDHIBITI WA UBORA WA ELIMU

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha masuala yaliyobainika katika udhibiti wa ubora wa elimu nchini Tanzania. Sura hii pia inatoa mtazamo wa jumla wa masuala yaliyobainika kutoka katika kila ripoti mojamoja za kaguzi za ufanisi zilizohusika katika majumuisho ya ripoti hii. Kuna makundi mawili ya masuala makuu yaliyobainika, ambayo ni: uchambuzi wa mambo yaliyopo sasa yanayokwaza au yanayowezesha utoaji wa huduma bora za elimu, na uchambuzi wa ufanisi wa mifumo ya udhibiti na uhakiki ubora wa elimu nchini.

Kuhusiana na uwepo wa mambo yanayokwaza utoaji wa elimu bora, kipaumbele hasa kilikuwa katika kuchambua mifumo ya udhibiti na uhakiki ubora katika ngazi zote za elimu kuanzia elimu ya msingi, sekondari, ufundi na elimu ya juu. Masuala hayo yanajadiliwa hapa chini.

4.2 Mifumo ya Udhibiti na Uhakiki Ubora kwa Elimu ya Msingi na Sekondari

Sehemu hii inawasilisha udhaifu uliobainika katika ripoti za ukaguzi yanayohusiana na mifumo ya udhibiti na uhakiki ubora katika utoaji wa elimu ya msingi na sekondari.

4.2.1 Upungufu wa Wadhibiti na Wahakiki Ubora wenye Taaluma ya Elimu Maalumu

Mapitio ya taarifa ya ukaguzi wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulibaini kuwepo kwa upungufu wa wadhibiti na wahakiki ubora wenye taaluma ya elimu maalumu. Mapitio ya nyaraka za taarifa za wafanyakazi yalibaini kuwa ni wadhibiti na wahakiki ubora 98 tu ndio walikuwa na taaluma ya elimu maalumu.

Matokeo yake, wadhibiti na wahakiki ubora wengi ambao walikuwa wakifanya kazi za uhakiki na udhibiti ubora katika shule za msingi hawakuwa na utaalamu na ujuzi unaohitajika ili waweze kutathmini ipasavyo ufundishaji na ujifunzaji katika lugha za alama au kuhakiki

nyaraka zinazoandaliwa za ujifunzaji na ufundishaji. **Kielelezo 4.4** kinaonesha idadi ya wadhibitii na wahakiki ubora wa elimu maalumu waliopo katika halmashauri zilizotembelewa na timu ya ukaguzi.

Kielelezo 4.1: Uwiano wa Wahakiki Ubora wa Elimu Maalumu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizotembelewa



Chanzo: *Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Elimu Maalumu*

Kielelezo 4.1 kinaonesha kwamba kumekuwa na upungufu wa wahakiki ubora wa elimu maalumu katika baadhi ya halmashauri. Halmashauri iliyokuwa na uwiano mzuri zaidi kuliko zote ilikuwa ya Wilaya ya Wanging'ombe iliyokuwa na asilimia 50 ya wadhibiti ubora kwenye elimu maalumu kati ya wadhibiti ubora wote. Hata hivyo, licha ya kuwa na kiwango cha kuridhisha cha wahakiki ubora, bado baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa kama vile Wangingómbe, Bukoba, na Bahi hazikuwa na wadhibiti ubora wenye taaluma ya elimu maalumu.

Licha ya kuwa na wadhibiti ubora kwa kiwango cha hadi asilimia 50 katika Halmashauri za Wangingombe, Bukoba, na Bahi bado idadi kubwa ya wadhibiti hao hawakuwa na mafunzo na ujuzi wa kutosha wa elimu maalumu.

Mapitio zaidi ya ripoti hiyo yalibaini kwamba upungufu wa wadhibiti ubora wenye taaluma ya elimu maalumu ulisababishwa na idadi ndogo ya walimu wenye taaluma ya elimu maalumu ambao ndiyo huteuliwa kuwa wadhibiti ubora wa elimu maalumu.

Majadiliano zaidi na maofisa katika halmashauri zilizotembelewa yalibaini kwamba uchache wa walimu wa elimu maalumu ulitokana na uchache wa

taasisi za elimu na vyuo vinavyotoa mafunzo ya elimu maalumu. Ukaguzi ulibaini kwamba kulikuwepo na chuo kimoja pekee nchi nzima kilichokuwa kinatoa kozi za elimu maalumu katika ngazi ya elimu ya msingi, ambacho ni Patandi. Matokeo yake, udhibiti ubora usiotosheleza ulipelekea kuendelea kuwepo kwa changamoto katika utoaji wa elimu maalumu na hivyo kuathiri ubora wake.

4.2.2 Utekelezaji Hafifu wa Mapendekezo ya Wakaguzi wa Shule

Kwa mujibu wa muundo wa uongozi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, wadhibiti ubora katika ngazi ya wilaya wanawajibika kufanya ukaguzi katika shule za msingi na kutoa mapendekezo. Mahojiano yaliyofanywa na maofisa wa uhakiki ubora katika halmashauri nane yalibaini kwamba mapendekezo yaliyotolewa na wadhibiti ubora hayakutekelezwa kwa kiwango cha kutosha na Mamlaka husika za Serikali za Mitaa ambazo zipo chini ya OR-TAMISEMI. **Kielelezo 4.2** kinatoa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya wakaguzi katika mamlaka za serikali za mitaa.

Kielelezo 4.2: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Wadhibiti Ubora wa Shule katika Shule 10 Zilizotembelewa katika Halmashauri 12



Chanzo: *Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Elimu ya wenye Mahitaji Maalumu*

Kielelezo 4.2 kinaonesha kwamba asilimia 61 ya mapendekezo yaliyotolewa hayakutekelezwa ikimaanisha kwamba ni asilimia 39 pekee ya mapendekezo ndiyo yaliyotekelezwa kikamilifu. Kiwango kidogo cha utekelezaji wa mapendekezo kilitokana na kukosekana kwa mfumo thabiti

wa ufuatiliaji ambao ungeweza kuhakikisha kwamba mapendekezo yametekelezwa kikamilifu.

Kushindwa kutekelezwa kikamilifu kwa mapendekezo hayo kumeathiri mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Changamoto zilizokuwepo katika utoaji wa elimu maalumu zimedumu na zimeendelea kuwepo bila utatuzi na hivyo kuathiri ubora wa elimu maalumu.

4.2.3 Taarifa Pungufu za Ukaguzi wa Shule za Msingi

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu upatikanaji na uboreshaji wa miundombinu ya shule ulibaini kuwepo kwa taarifa pungufu kuhusu ukaguzi unaofanyika katika shule za msingi. Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ilitarajiwa kuwepo kanzidata ambayo ingehifadhi taarifa za ukaguzi wa miundombinu ya shule za msingi unaofanyika katika shule zote zilizosajiliwa nchini. Taarifa hizi zilikuwa muhimu kwa timu za ukaguzi na zilitarajiwa kuwa vigezo vya msingi wakati wa ukaguzi wa miundombinu.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikuweza kuimarisha kanzidata ya kuaminika na yenye taarifa hai zinazojumuisha mambo yote kuhusu ukaguzi kama vile aina, asili, uwepo, na matokeo ya ukaguzi uliofanyika.

Hali hii ilisababisha kukosekana kwa taarifa kuhusu ukaguzi uliofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, pamoja na kukosekana kwa mpango unaozingatia vihatarishi. Matokeo yake baadhi ya shule za msingi hazikukaguliwa wakati zingine zilikaguliwa mara kwa mara. Ukaguzi wa mara kwa mara kwa baadhi ya shule ulipelekea kutolewa kwa mapendekezo yanayojirudia katika kaguzi zilizotangulia.

4.2.4 Ukaguzi Hafifu wa Miundombinu ya Shule za Msingi

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu upatikanaji na uboreshaji wa miundombinu ya shule ulibaini kwamba ukaguzi wa shule haukuwa kamilifu wala unaozingatia mambo yote. Kulingana na ripoti, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inafanya ukaguzi wa shule na kutoa mapendekezo kuhusu marekebisho yanayohitajika kama sehemu ya hatua za uhakiki ubora wa

shule. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba asilimia 95 ya mapendekezo ya ukaguzi yaliegemea mambo yahusuyo taaluma na asilimia 5 pekee ikigusia mambo yahusuyo miundombinu.

Zaidi, ilibainika kwamba kaguzi hazikufanyika kwa ukamilifu kubaini kasoro katika majengo na hali ya miundombinu. Hivyo, mara nyingi mapendekezo yaligusia tu uboreshaji na usimamizi wa miundombinu kwa idadi ya miundombinu na si ubora wake.

Baada ya ukaguzi, wamiliki wa shule za msingi walihitaji kupewa taarifa kuhusu hali ya miundombinu katika shule zao. Hii iliwezesha waendeshaji wa shule kuwa na ufahamu wa mambo wanayotakiwa kuyafanyia kazi kuhusiana na uimara wa majengo, madawati, sakafu za madarasa, na usalama wa vyoo, pamoja na hali ya mazingira katika shule zao.

Mapitio ya ripoti yalibaini kwamba sababu kubwa iliyopelekea kuwa na kaguzi pungufu za miundombinu ya shule za msingi ni kuchelewa kutolewa fedha kwenda katika halmashauri husika. Fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya shughuli za ukaguzi zilicheleweshwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za ukaguzi.

Ukaguzi hafifu wa shule ulipelekea kutozingatiwa kwa viwango vya ubora vilivyowekwa. Hali hii iliathiri ufundishaji na ujifunzaji na hivyo kusababisha matokeo mabaya kwa mitihani ya mwisho ya shule za msingi.

4.2.5 Usimamizi Dhaifu wa Kanuni za Usajili wa Shule

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu upatikanaji na uboreshaji wa miundombinu ya shule ulibaini kuwepo kwa udhaifu katika kusimamia kanuni za usajili wa shule za msingi za serikali. Kulingana na ripoti hiyo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitakiwa kuhakikisha kwamba usajili wa shule za msingi unafuata hatua tatu ambazo ni kibali cha kujenga shule, ruhusa kwa mmiliki na msimamizi wa shule na usajili wa shule.

Ukaguzi ulibaini kwamba hatua za usajili wa shule zilifuatwa kwa ukamilifu pale ambapo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilikuwa ikisajili shule za watu binafsi. Hata hivyo, hali ilikuwa tofauti pale ambapo usajili ulihusu shule zinazomilikiwa na serikali. Usajili wa shule za serikali haukufuata kikamilifu hatua zinazostahili. Hivyo, shule zinazomilikiwa na serikali zilikuwa hazikidhi vigezo vingi vya usajili lakini ziliruhusiwa

kuendelea kufanya kazi. Vigezo vya muhimu zaidi vilihusu usimikaji wa majengo ya shule ambapo yalihusu uwasilishaji wa pendekezo la mradi, nakala za michoro ya majengo zilizothibitishwa na mhandisi wa wilaya, na ruhusa ya mkaguzi mkuu wa shule wa wilaya.

Sababu kubwa ya hali hii ni kwamba mmiliki na msajili wa shule ilikuwa taasisi moja (serikali). Mapitio ya majalada ya maombi ya usajili wa shule katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yalionesha kwamba Wizara haikuwa na namna thabiti ya kuhakikisha shule za serikali zinakidhi masharti ya usajili inayoyatoa. Hali hii ilipelekea wakaguzi wa shule kuwa washauri badala ya kuchukua hatua madhubuti kama inavyotakiwa na sheria. Matokeo yake, udhaifu uliobainika uliendelea kuwepo bila kufanyiwa kazi.

Udhaifu katika kusimamia kanuni wakati wa usajili wa shule ulipelekea kuwepo kwa shule za msingi na sekondari za serikali zinazoendeshwa bila kukidhi angalau vigezo vya msingi vya usajili. Hali hii iliathiri ubora wa elimu inayotolewa na shule ambazo zilikuwa na miundombinu chakavu.

4.3 Mifumo ya Udhibiti na Uhakiki wa Ubora kwenye Utoaji wa Elimu ya Juu

Sehemu hii inatoa muhtasari wa tathmini ya mifumo ya udhibiti ubora kwenye taasisi za elimu ya juu. Taarifa nne za ukaguzi wa ufanisi zilizotumika ni Taarifa kuhusu Programu ya Kujenga Uwezo wa Utafiti iliyofadhiliwa na Sida na kutekelezwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia. Muhtasari wa yaliyobainika kwenye ripoti hizo nne za ukaguzi wa ufanisi ni kama ifuatavyo.

4.3.1 Mifumo ya Uhakiki wa Shahada za Umahiri na Uzamivu

Kila chuo kikuu kilipaswa kuandaa na kutekeleza miongozo na sera za ubora wa shahada za umahiri na uzamivu. Taarifa ya ukaguzi wa ufanisi kwenye programu ya kujenga uwezo wa utafiti ilibainisha kuwa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kilifanikiwa kuandaa miongozo kwa ajili ya utekelezaji wa sera ya udhibiti na uhakiki wa ubora. Jambo hili lilipelekea Chuo hiki kukipandisha hadhi kitengo cha uhakiki ubora na kukifanya kurugenzi kamili ya uhakiki ubora mnamo mwaka 2017.

Kurugenzi hii imekuwa ikiratibu idara na vitengo vya chuo kuhusiana na uhakiki wa ubora wa programu za shahada za umahiri na uzamivu kabla ya kupelekwa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania kwa ajili ya kupatiwa ithibati.

Taarifa ya ukaguzi ya programu wa programu ya kujenga uwezo wa utafiti kwenye taasisi za elimu ya juu ilibainisha kuwa programu hii ilikisaidia Chuo Kikuu cha Ardhi kuimarisha kitengo cha udhibiti ubora kwenye utoaji wa shahada za umahiri na uzamivu. Katika Chuo Kikuu Cha Ardhi, programu hii ilihusika kwenye kuandaa na kununua vifaa kwa ajili ya udhibiti ubora wa shahada za umahiri na uzamivu.

Katika Chuo Kikuu cha Ardhi, programu hii ilisaidia mambo mawili. Jambo la kwanza lilikuwa ununuzi wa vifaa na madodoso kwa ajili ya kusaidia kuboresha ubora wa shahada za umahiri na uzamivu, kama vile programu ya kudhibiti wizi wa maarifa ya watu wengine. Jambo la pili lilikuwa kufundisha matumizi ya vifaa na madodoso kwa ajili ya uhakiki na udhibiti ubora.

4.3.2 Ukosefu wa Mifumo ya Udhibiti Ubora wa Vituo vya Uvumbuzi

Kati ya mambo yaliyotakiwa kutekelezwa kwenye programu ya kujenga uwezo wa utafiti katika Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ilikuwa uanzishaji wa vituo vya uvumbuzi kweye ofisi za mikoa ambazo vilitarajiwa ziwe chachu ya maendeleo ya uvumbuzi ambayo ni matokeo ya tafiti zilizofanyika. Hata hivyo, tumebaini kuwa ofisi nyingi za Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogovidogo hazina mifumo ya udhibiti ubora wa vituo vya uvumbuzi pamoja na zana za kufanya ufuatiliaji na tathmini. Vilevile, ofisi za mikoa za SIDO hazikuwa na muundo kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa utendaji wa vituo vya uvumbuzi.

Maelezo yaliyotolewa na maofisa wa Tume ya Sayansi na Teknolojia wakati wa ukaguzi huu yalitanabaisha kuwa sababu kubwa ni kukosekana kwa mwongozo wa ufuatiliaji na tathmini katika ngazi ya mkoa. Hili limepelekea kuhatarisha uendelevu wa vituo vya uvumbuzi kwa kuwa kazi nyingi zinazofanywa na vituo hivyo zinahitaji ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba matokeo yalikokusudiwa yanapatikana.

4.3.3 Zana (Madodoso) za Udhibiti Ubora Ziliandaliwa kwa Ukamilifu

Mapitio ya taarifa ya ukaguzi wa ufanisi kwenye programu ya kujenga uwezo wa utafiti ya Chuo Kikuu cha Ardhi yalibaini kuwa moja ya malengo lilikuwa kuandaa zana za udhibiti ubora. Ukaguzi umebaini kuwa kati ya zana 10 zilizotakiwa kutengenezwa, Chuo kilifanikiwa kuandaa zana 27 kuanzia mwaka 2018. Jambo hili limefanya Chuo kufanikwa kukamilisha malengo waliyojiwekea kwa asilimia 170.

Jedwali 4.1 linaonesha aina ya zana za udhibiti ubora zilizoandliwa na Chuo Kikuu cha Ardhi kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 kama matokeo chanya ya programu ya kujenga uwezo wa utafiti chuoni.

Jedwali 4.1: Makundi ya Zana za Udhibiti na Uhakiki Ubora Ziliandaliwa na Chuo Kikuu cha Ardhi kuanzia Mwaka 2015 hadi 2020 kwa Ufadhili wa SIDA

Kundi	Idadi	Asilimia ya Zana Zote
Zana za Udhibiti/Uhakiki wa Tafiti	9	33
Zana za Udhibiti/Uhakiki wa Utawala	10	37
Zana za Udhibiti/Uhakiki Ubora wa Mitihani na Mafunzo	8	30
Jumla	**27**	**100**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kwenye Programu ya Kujenga Uwezo wa Utafiti, Chuo Kikuu cha Ardhi*

Jedwali 4.1 linaonesha jumla ya zana 27 za udhibiti ubora ambazo zimeandaliwa na Chuo Kikuu cha Ardhi kati ya mwaka 2015 na 2020**.** Zana 9 kati ya 27 zilikuwa zinahusika na uhakiki wa ubora wa tafiti. Zana 18 zilikuwa zinahusiana na mambo mengine ya kitaaluma kama vile utawala, mitihani, na ufundishaji.

4.3.4 Matumizi Yasiyoridhisha ya Zana za Udhibiti Ubora

Waraka wa uanzishaji wa mradi ulitaka kitengo cha udhibiti ubora kusimamia kisayansi utekelezaji wa udhibiti ubora katika Chuo Kikuu cha Ardhi. Hii ilifanyika ili kukuza viwango vya taaluma na kufanikisha matokeo ya utafiti na mafunzo.

Hata hivyo ukaguzi ulibaini kuwa zana za utafiti hasa zile zililzolenga kuboresha uwezo kwenye tafiti hazikusimamiwa inavyotakiwa. Ukaguzi ulibaini kuwa zana iliyotumika mara kwa mara ilikuwa programu ya kubaini wizi wa maarifa ikifuatiwa na tathmini ya ufundishaji.

Vilevile, sera ya udhibiti ubora ya Chuo Kikuu cha Ardhi inakitaka kitengo cha udhibiti ubora kufanya ukaguzi wa ubora ili kubaini iwapo taasisi inafuata na inatekeleza taaratibu za udhibiti ubora. Zaidi, ukaguzi umebaini kuwa kaguzi za ubora hazikufanyika ili kutambua kiwango cha utekelezaji wa zana za upimaji wa ubora. Vilevile, ukaguzi umebaini kuwa kaguzi za ubora hazikufanyika ili kupima namna ambavyo zana za ubora zilitumika.

Aidha, taarifa ya ukaguzi wa kujenga uwezo wa utafiti wa Tume ya Sayansi na Teknolojia inabainisha kwamba modeli ya ufuatiliaji na tathmini ya vituo vya uvumbuzi havikutumiwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia pamoja na kwamba ilikuwa imeshatengenezwa. Maelezo yaliyotolewa ni kwamba ilikuwa inasubiri kuandaliwa kwa miongozo ya utekelezaji.

Vilevile, kutotumika kwa zana zilizoandaliwa za udhibiti ubora katika Chuo Kikuu cha Ardhi kumekwamisha utekelezaji wa malengo ya programu kwa kuwa upimaji wa ubora kwenye tafiti za shahada za umahiri na uzamivu haukunyika.

4.3.5 Kukosekana kwa Mbinu za Ufuatiliaji wa Matumizi ya Zana za Udhibiti Ubora Zilizoandaliwa

Ili kuhakikisha kuwa zana zilizoandaliwa zinatumika kikamilifu na matokeo yake yanapatikana, Chuo Kikuu cha Ardhi kilitakiwa kuhakikisha kinatengeneza mbinu kwa ajili ya ufuatiliaji wa namna zana hizo zinavyotumika. Jambo hili lilitarajiwa ili kuwa na uhakika kuwa lengo la kukuza ubora limefikiwa kwenye maeneo ambayo huduma zimetolewa hususani kwenye maeneo ya utafiti ambayo ndiyo yalikuwa malengo ya programu. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba hakukuwepo ufanisi kwenye eneo hili kwani zana za ufuatiliaji ubora ziliandaliwa kisha kuachwa bila kutumika. Mapitio ya Kitabu cha Udhibiti Ubora cha Chuo Kikuu cha Ardhi yalibaini kuwa hakukuwa na mbinu za namna ya kufanya ufuatiliaji wa zana za udhibiti ubora. Hali hii ilisababishwa na kukosekana

kwa ufuatiliaji wa karibu wa maofisa wa programu kwenye matokeo yaliyokusudiwa hivyo kusababisha kushindwa kutathmini kiwango cha matumizi ya zana za udhibiti ubora. Hali hii ilihatarisha kufikiwa kwa malengo makuu ya programu ya kuhakikisha kuwa kunakuwepo tafiti zenye ubora wa hali ya juu.

SURA YA TANO

UTOAJI WA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya ukaguzi kuhusu utoaji wa elimu ya msingi na sekondari nchini. Matokeo hayo ya ukaguzi yamegawanywa katika makundi matatu ambayo ni mazingira na miundombinu ya shule; walimu na mbinu za kufundishia; na usimamizi wa shule za msingi na sekondari.

Ripoti tatu za ukaguzi wa ufanisi zilitumika kuhitimisha masuala yanayoshughulikia utoaji wa elimu ya msingi na sekondari. Ripoti hizi ni pamoja na ukaguzi wa ufanisi kuhusu utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini; usimamizi wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu; na upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi nchini.

Watendaji wakuu ambao wanahusika katika utoaji wa elimu ya msingi na sekondari ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo inawajibika kuunda, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa sera za elimu. Aidha, wizara hii inawajibika kutoa mafunzo ya walimu kupitia usimamizi wa utendaji wa vyuo vya ualimu vya umma pamoja. Mtendaji mwingine ni O-TAMISEMI ambayo ina jukumu la kuratibu usimamizi wa shule za msingi kupitia Idara ya Uratibu wa Elimu ya Msingi pamoja na mamlaka za serikali za mitaa. TAMISEMI kupitia wakurugenzi wa wilaya inapaswa kuhakikisha kuwa shule zote za msingi zinakuwa na mazingira mazuri na salama ya kufundishia na kujifunzia.

5.2 Matokeo ya Ukaguzi

Ukaguzi uliofanywa umeleta matokeo katika maeneo matano ambayo ni uwepo wa miundombinu duni ya shule na mazingira ya kujifunza; uandaaji wa walimu wa shule za msingi na sekondari na mbinu za kufundishia; usimamizi usioridhisha wa shule katika utoaji wa elimu ya msingi na sekondari; ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa elimu ya msingi na sekondari; na matokeo ya elimu bila malipo katika utoaji wa elimu nchini. Matokeo haya yanajadiliwa kwa kina hapa chini.

5.2.1 Uwepo wa Miundombinu Duni ya Shule Pamoja na Mazingira ya Kujifunzia

Ukaguzi wa ufanisi uliofanyika ulibaini kuwepo kwa mazingira na miundombinu duni katika utoaji wa elimu ya msingi na sekondari. Mapungufu yalipimwa kwa kuzingatia uwepo wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, na madawati katika shule za msingi na sekondari. Pia, mazingira ya kujifunzia kwa walimu walio kazini yalizingatiwa. Yale yaliyobainika katika kipengele hiki yamejadiliwa hapa chini.

a) Upungufu wa Madarasa kwenye Shule za Msingi

Ukaguzi wa ufanisi juu ya upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi ulibaini kuwa hakukuwa na vyumba vya madarasa vya kutosheleza wanafunzi wote wa shule za msingi. Kwa mujibu wa ukaguzi na uchambuzi wa takwimu zilizopo, ilibainika kuwa kulikuwa na wanafunzi milioni 10.11 ambao waliandikishwa katika shule za msingi za umma wakati vyumba vya madarasa vilivyokuwepo nchini kote vilikuwa 118,255 badala ya 252,791 hadi kufikia mwaka 2018. Hii ilifanya wastani wa uwiano wa wanafunzi kwa darasa kukaa nchini kote kuwa 76 badala ya wanafunzi 40.

Kulingana na ripoti hiyohiyo, katika miaka mitano mfululizo ya fedha kuanzia 2014/15 hadi 2017/18, wastani wa wanafunzi milioni 5.13 ambao ni sawa na asilimi 51 hawakuwa na vyumba vya madarasa. Hali hii ilikuwa na athari katika utoaji wa elimu bora ya shule za msingi nchini. **Kielelezo 5.1** kinatoa muhtasari wa takwimu hizi.

Kielelezo 5.1: Uchambuzi wa Idadi ya Wanafunzi Wanaokosa Madarasa katika Shule za Msingi Nchini Kuanzia Mwaka 2014-2018



	2014	2015	2016	2017	2018
Idadi ya Wanafunzi ('000,000)	8.22	8.30	8.63	8.96	10.11
Idadi ya Wanafunzi Waliokosa Vyumba vya Madarasa ('000,000)	3.81	3.67	6.27	5.68	6.23

Chanzo: *Takwimu za Elimu ya Msingi kuanzia Mwaka 2014-2018 kutoka Open.data.go.tz*

Kielelezo 5.1 kinaonesha kuwa mwelekeo wa idadi ya wanafunzi kukosa vyumba vya madarasa uliongezeka kutoka milioni 3.81 hadi 6.23 kuanzia mwaka 2014 hadi 2018. Hii ilichangiwa na udahili mkubwa wa wanafunzi wa shule za msingi kuanzia mwaka 2014 hadi 2018. Kwa kiasi kikubwa, udahili mkubwa wa wanafunzi ulichangiwa na kuanza kwa mpango wa elimu ya msingi bila malipo.

Kwa mfano, iliripotiwa kwamba idadi ya wanafunzi wanaokosa madarasa ni kati ya asilimia 33 katika Wilaya ya Mbulu hadi kufikia asilimia 69 Mkoani Geita. Uchunguzi zaidi ulionesha kuwa, wastani wa uwiano wa wanafunzi kwa darasa katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa ulikuwa 1:86 wakati uwiano wa kitaifa ni 1:76 katika mwaka 2018. Uchambuzi wa wakaguzi katika ripoti hiyo ulionesha kuwa katika mamlaka ya serikali za mitaa zilizotembelewa, wastani wa wanafunzi 22,864 (sawa na asilimi 53) hawakuwa na vyumba vya madarasa.

b) Utoaji wa Madawati kwa Shule za Msingi

Kwa mujibu wa ukaguzi wa ufanisi juu ya upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi nchini, licha ya juhudi za serikali kuhakikisha kunakuwa na madawati ya kutosha katika kila shule ya msingi, bado kulikuwa na wanafunzi milioni 1.1 ambao hawakuwa na madawati katika shule za msingi kote nchini. **Jedwali 5.1** linaonesha kwa ufupi idadi

ya wanafunzi waliokuwa wakisoma bila madawati kuanzia mwaka 2014 hadi 2018.

Jedwali 5.1: Mchanganuo wa Upatikanaji wa Madawati Nchini kuanzia Mwaka 2014-2018[3]

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Wanafunzi (Maelfu)	Madawati Yaliyopo (Maelfu)	Madawati Yanayopungua (Maelfu)	Idadi ya Wanafunzi Wasio na Madawati (Maelfu)	Asilimia ya Madawati Yanayohitajika
2014	8,220	1,960	813	2,440	30
2015	8,300	1,930	656	1,970	24
2016	8,250	1,980	368	1,100	13
2017	9,310	3,160	60	180	6
2018	10,110	2,960	402	1,200	11

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu kutoka TAMISEMI za Miaka 2014-2018*

Jedwali 5.1 linaonesha kuwa, idadi ya wanafunzi wanaokosa madawati imepungua kutoka milioni 2.44 hadi 1.20 kuanzia mwaka 2014 hadi 2018 kwa mtiririko huo. Hii inamaanisha kuwa uhaba umepungua kutoka asilimia 30 mwaka 2014 hadi asilimia 11 mwaka 2018.

Ripoti hiyo ilipambanua zaidi kwamba madawati yanayopatikana yanaweza kuchukua wanafunzi milioni 8.90 wakati vyumba vya madarasa vilikuwa 118,255 ambavyo vina uwezo wa kuchukua wanafunzi milioni 4.73 huku wakibaki wanafunzi milioni 5.38 ambao ama walikosa vyumba vya madarasa au kukosekana kwa madawati 402,840 kwenye vyumba vya madarasa yaliyokuwepo. Aidha, ukaguzi huo pia ulionesha kuwa hali ya kukosa madawati katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa ilikuwa kati ya asilimia 37 na 69.

c) Upungufu wa Matundu ya Vyoo kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi

Ukaguzi wa ufanisi juu ya upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi nchini ulionesha kuwa wastani wa wanafunzi milioni 5.24 nchini hawakuwa na matundu ya vyoo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2014 - 2018. Hadi wakati wa ukaguzi huu, wanafunzi milioni 5.39 ambao ni sawa na asilimia 65 ya wanafunzi wote nchini hawakuwa na matundu ya vyoo. Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa matundu ya vyoo 265,519 nchini kote.

[3] Mahesabu yamefanyika kwa kuzingatia kuwa dawati moja wanakaa wanafunzi watatu.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwepo kwa uhaba mkubwa zaidi wa matundu ya vyoo kwa shule za msingi. Uwiano wa mwanafunzi kwa choo kwa wavulana ulikuwa 1:57 na wasichana 1:56 kinyume na kiwango cha uwiano kinachotakiwa cha mwanafunzi na choo cha 1:25 kwa wavulana na 1:20 kwa wasichana. **Kielelezo 5.2** kinatoa muhtasari wa maelezo haya.

Kielelezo 5.2: Mchanganuo wa Upatikanaji wa Matundu ya Vyoo kwenye Shule za Msingi Nchini kuanzia Mwaka 2014-2018



	2014	2015	2016	2017	2018
Idadi ya Wanafunzi ('000,000)	8.22	8.30	8.63	8.96	10.11
Idadi ya Wanafunzi Waliokosa Vyoo ('000,000)	5.13	5.26	5.39	5.68	6.31

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Takwimu za TAMISEMI kuanzia Mwaka 2014-2018*

Kielelezo 5.2 kinaonesha kuwa idadi ya wanafunzi waliokosa vyoo iliongezeka kutoka milioni 5.13 katika mwaka 2014 hadi milioni 6.31 mwaka 2018. Ripoti hiyo ilionesha zaidi kuwa wanafunzi milioni 5.36 ambao sawa na asilimia 62 ya wanafunzi wote nchini hawakuwa na matundu ya vyoo. Hii ilisababishwa na ukosefu wa matundu ya vyoo 311,956 nchini kote.

Katika ngazi ya mamlaka za serikali za mitaa, uwiano wa chini wa wanafunzi kwa choo uilikuwa 1:28 wakati kiwango cha juu kilikuwa 1:79. Ukaguzi ulionesha kuwa halmashauri za Mpwapwa, Mpanda na Geita zilikabiliwa na upungufu mkubwa wa matundu ya vyoo kuanzia asilimia 73 hadi 75, hali iliyosababisha kuwa na wastani wa uwiano wa 1:55 katika Halmashauri sita zilizotembelewa. Mamlaka zote sita za serikali za mitaa zilizotembelewa hazikuzingatia uwiano wa kawaida wa choo kwa wanafunzi.

d) Upatikanaji wa Vituo vya Walimu na Vifaa kwa Shule za Msingi na Sekondari

Kwa mujibu wa ukaguzi wa ufanisi kuhusu utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini, ilibainika kuwa vituo vya mafunzo ya walimu vilikuwa katika hali mbaya. Katika mikoa mitano iliyotembelewa wakati wa ukaguzi, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa vituo vya mafunzo ya walimu vilivyopo havikuwa vikifanya kazi.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya ukaguzi, majengo mengi yalitumika kwa matumizi mengine yasiyotarajiwa kama vile vituo vya masomo, au maduka. Kwa mfano, kituo cha walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Karatu Mkoani Arusha kinatumika kama stoo ya shule; na Kituo cha Nyerere katika Manispaa ya Singida kinatumika kama ukumbi wa mikutano wa Manispaa na Kituo cha Mitihani ya Kufuzu. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato, jengo la kituo cha walimu kimegeuzwa kituo cha uchapishaji cha halmshauri; na kituo cha walimu cha Mji wa Geita kinatumika kama kituo cha masomo za ziada kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Pia, ukaguzi wa ufanisi kuhusu utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulibainika kuwa kulikuwa na mapungufu katika kuhifadhi na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia vilivyotolewa katika shule za msingi zilizotembelewa. Mathalani, shule nne (4) zilizotembelewa za wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia za Kigwe Viziwi, Mtendeni, Kaigara, na Meru, ni shule moja tu ya Kigwe Viziwi ndiyo ilikuwa na chumba kinachohitajika cha kupima sauti ili kutoa matokeo ya kuaminika wakati wa kupima kiwango cha kusikia cha wanafunzi.

e) Ukarabati Mkubwa wa Shule Kongwe za Sekondari

Pamoja na changamoto za upungufu wa fedha za serikali katika ukarabati wa miundombinu ya shule hasa za msingi, serikali imechukua hatua za makusudi kuboresha hali ya miundombinu katika shule za sekondari, hasa kwa kufanya ukarabati wa shule kongwe. Shule kongwe nyingi za serikali zilikuwa na miundombinu chakavu iliyohitaji ukarabati. **Jedwali 5.2** linaonesha fedha zilizotumika kukarabati shule kongwe za serikali katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Jedwali 5.2: Fedha za Serikali Zilizotumika Kukarabati Shule Kongwe kwa Awamu ya IIII

Jina la Shule	Mkoa	Fedha Zilizotumika (Sh.)
Sekondari ya Wasichana Weruweru	Kilimanjaro	749,179,604
Sekondari ya Sumbawanga	Rukwa	757,456,854
Sekondari ya Pamba	Mwanza	423,702,556
Sekondari ya Wasichana Mtwara	Mtwara	776,605,047
Sekondari ya Mbeya	Mbeya	795,419,022
Sekondari ya Mawenzi	Kilimanjaro	750,332,637
Sekondari ya Mara	Mara	896,468,635
Sekondari ya Lyamungu	Kagera	799,443,156
Sekondari ya Ifunda	Iringa	767,543,970
Sekondari ya Arusha	Arusha	699,129,180
Sekondari ya Machame	Kilimanjaro	847,658,579
Sekondari ya Kibasila	Dar es Salaam	422,228,351
Jumla		**8,685,167,591**

Chanzo: *Taarifa ya Ukaguzi wa Fedha - Wizara ya Elimu Mwaka 2019/20*

Jedwali 5.2 linaonesha kuwa kumekuwa na matumizi yanayoridhisha ya fedha za serikali kwa kuzifanyia ukarabati mkubwa shule kongwe za serikali nchini. Kwa ujumla, serikali imetumia jumla ya TSh 8,685,167,591 kwa ajili ya kufanyia ukarabati wa shule kongwe katika mikoa 10 katika mwaka wa fedha 2019/20.

Katika awamu hii ya 3, jumla ya shule kongwe 12 za serikali zimekarabatiwa. Kwa wastani, kila shule ilipokea jumla ya shilingi 723,763,966 za shughuli za ukarabati, huku fedha nyingi zikielekezwa mkoa wa Kilimanjaro ambao ulipokea jumla ya shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya shule zake tatu. Ukarabati huu mkubwa uliofanyika umechangia kwa kiwango kikubwa kuboresha miundombinu wa shule hizo kongwe. **Picha 5.1** inaonesha majengo ya Shule ya Sekondari Kibaha ikiwa moja ya shule kongwe zilizofanyiwa ukarabati mkubwa.

Picha 5.1: Ukarabati Mkubwa wa Mabweni na Madarasa katika Shule ya Sekondari Kibaha

5.2.2 Utoaji wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari na Mbinu za Kufundishia

Sehemu hii inatoa matokeo kutoka kwenye taarifa tatu za ukaguzi wa ufanisi ambazo ni Ukaguzi wa Ufanisi wa Utoaji wa Mafunzo ya Walimu Walio Kazini; Usimamizi wa Utoaji wa Elimu Maalumu; na Upatikanaji na Utunzaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi. Matokeo haya ya ukaguzi yanategemea kiwango cha utoaji wa huduma ya walimu wa shule za msingi na sekondari pamoja na mbinu za kufundishia. Sehemu hii inalenga kutoa muhtasari juu ya kiwango cha mafunzo yanayotolewa kwa walimu; uwiano kati ya wanafunzi kwa mwalimu; na upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia.

(a) Upungufu wa Idadi ya Walimu Waliopokea Mafunzo ya Elimu ya Maalumu katika Shule za Msingi za Wenye Mahitaji Maalumu

Kwa mujibu wa ukaguzi wa ufanisi wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, licha ya ukweli kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilikuwa na chuo kilichokuwa na uwezo wa kudahili walimu 300 wa elimu maalumu kwa mwaka, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2014 hadi 2018, Wizara ilizalisha wastani wa walimu 131 tu wenye taaluma ya elimu maalumu kwa mwaka. Mwelekeo wa kuzalisha walimu wa shule za msingi katika kipindi hicho ni kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo 5.3.**

Kielelezo 5.3: Idadi ya Walimu wa Elimu ya Msingi Wenye Mahitaji Maalumu Waliopata Mafunzo



Chanzo: *Orodha ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia y Walimu Waliopatiwa Mafunzo*

Kielelezo 5.3 kinaonesha kuwa kiwango cha juu cha walimu wa elimu maalumu waliopata mafunzo ilikuwa 201 kwa mwaka 2015. Kwa miaka 2016 na 2017 idadi ilipungua hadi 160 na 100 mtawalia. Upungufu huu wa walimu waliopata mafunzo ulisababishwa na kupungua kwa fedha za Mradi wa LANES ambazo kwa kiasi kikubwa zilikuwa zikifadhili mafunzo haya ya walimu.

(b) Mafunzo Yasiyotosheleza kwa Walimu wa Shule za Msingi Walio Kazini

Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa idadi ndogo ya walimu walio kazini waliopata mafunzo kwa shule za sekondari kitaifa isipokuwa kwa walimu wa shule za msingi walio kazini. Taarifa ya mafunzo ya walimu walio kazini kitaifa zilichambuliwa kwa kuzingatia idadi ya chini zaidi iliyolengwa ya walimu 2 walio kazini katika daraja la chini kwenye shule za msingi nchini kote kama ilivyowekwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na TAMISEMI, pamoja na lengo la kufikia kiwango cha chini cha walimu 4 walio kazini kutoka kila shule ya sekondari kama ilivyowekwa na Programu ya Kuboresha Hali ya Wanafunzi na Walimu (STEP).

Ukaguzi uligundua kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2018/19, Wizara hizi mbili zilifanikiwa kutoa mafunzo kwa jumla ya walimu 31,824 kati ya walimu 32,314 wa shule za msingi ambao ni sawa na asilimia 98 ya lengo. Pia, mafunzo kwa walimu walio kazini yalitolewa katika mwaka wa fedha 2015/16 pekee chini ya mradi wa STEP. Hii ni licha ya ukweli

kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ililenga kutoa mafunzo kwa walimu wasiopungua 4 wa masomo ya hisabati, biolojia, Kiingereza na Kiswahili kutoka kila shule nchini.

Hata hivyo, mafunzo ya ndani yaliyotolewa yalikuwa ni kwa ajili ya walimu waliofundisha ujuzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) kwa darasa la kwanza na la pili na si kwa walimu waliofundisha masomo mengine. Madhara yake, kikwazo kikubwa cha utoaji wa mafunzo kwa ngazi ya kitaifa kilikuwa uwiano mkubwa wa walimu walio kazini kufikia 147,027 waliofundisha masomo mengine ambayo ni sawa na asilimia 82 ya walimu 179,341 walio shule za msingi ambao hawakupatiwa mafunzo.

Pia, kulingana na ripoti hiyo hakukuwa na idadi ya kutosha ya walimu wa shule za msingi na sekondari ambao walipewa mafunzo katika mikoa iliyotembelewa. Kwa mfano, malengo ya mafunzo hayakufikiwa katika mikoa 4 kati ya 5 iliyotembelewa kwa shule za sekondari. Pia, kulikuwa na idadi duni ya walimu wa shule za msingi na sekondari ambao walipatiwa mafunzo katika halmashauri zilizotembelewa. **Kielelezo 5.4** kinatoa muhtasari wa idadi ya walimu walio kazini ambao walipatiwa mafunzo katika shule za msingi na sekondari kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Kielelezo 5.4: Hali ya Walimu Waliopata Mafunzo kwenye Halmashauri Zilizotembelewa kwa Mwaka 2018/19



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Taarifa za Mafunzo kutoka Halmashauri Zilizotembelewa kwa Mwaka 2019*

(c) Utoaji wa Malezi kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari

Malezi kwa walimu wa shule za msingi na sekondari yalitolewa mara chache na maofisa watendaji wa kata na wakuu wa shule. Hiyo ilithibitishwa kupitia mahojiano yaliyofanywa na jumla ya wakuu wa shule na walimu 40 katika halmashauri zilizotembelewa kwamba mfumo wa ushauri kwa walimu walio kazini haukufanya kazi kwa ufanisi.

Ukaguzi kuhusu ujengaji kwa uwezo kwa walimu waliopo kazini uliripoti kwamba ni shule 4 tu kati ya shule 40 za msingi na sekondari zilizotembelewa zilikuwa na maingiliano kwa njia ambayo walimu wasio na uzoefu walipatiwa msaada wa kitaalamu kutoka kwa walimu wakuu na walimu wenye ujuzi walioteuliwa.

(d) Utoaji wa Mafunzo kwa Walimu Walio Kazini Haukuzingatia Masomo Yote

Ukaguzi ulibaini kuwa mafunzo yalifikishwa zaidi kwa walimu walio kazini hasa waliounganishwa na masomo ya kufundisha katika viwango vya chini, wengi wao wakiwa walimu wa darasa la I hadi IV. Vivyohivyo, masomo mengine zaidi ya kusoma, kuandika na kuhesabu kwa madarasa la juu (IV-VII) yalitolewa kwa sehemu katika baadhi ya shule wakati katika shule zingine hayakutolewa kabisa. Masomo ya kufundisha ambayo hayakuwa na miongozo ya walimu katika shule nyingi za msingi ni pamoja na hisabati, Kiswahili, na Kiingereza. Hii ni licha ya ufaulu duni wa wanafunzi katika masomo hayo matatu katika miaka minne iliyopita kwa mujibu wa ripoti za Baraza la Mitihani la Tanzania.

Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa kulikuwa na jumla ya walimu walio kazini 538 na 597 katika shule za msingi na sekondari mtawalia ambao walipata mafunzo hususani katika masomo ya hisabati kuanzia Disemba 2019 hadi Februari 2020.

(e) Uwiano wa Mwalimu kwa Wanafunzi kwa Wanafunzi Wenye Ulemavu wa Kuona

Kulikuwa na mgawanyo duni wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kwa shule za msingi za wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Ukaguzi wa

ufanisi juu ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulibaini kuwa kulikuwa na uwiano duni wa wanafunzi kwa mwalimu katika shule za msingi zilizotembelewa za wenye mahitaji maalumu, ambapo idadi ya walimu wanaohitajika ilikuwa ndogo ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi waliodahiliwa.

Pia, ripoti hiyo ilibaini kuwa katika shule za msingi zilizotembelewa za wanafunzi wenye ulemavu wa kuona, uwiano unaohitajika wa mwalimu-wanafunzi ulikuwa tofauti na uwiano unaohitajika wa 1:5. **Jedwali 5.3** linatoa muhtasari hali ya uwiano.

Jedwali 5.3: Hali ya Uwiano wa Mwalimu kwa Mwanafunzi kwa Shule za Wanafunzi wenye Ulemavu wa Kuona

Jina la Shule	Idadi ya Wanafunzi	Idadi ya Walimu	Uwiano Halisi
Hombolo Bwawani	10	4	1:3
Kijitonyama	6	2	1:3
Themi	60	12	1:5
Ilembula	6	1	1:6
Nyangao	25	4	1:6
Kibena	27	3	1:9
Mugeza Mseto	48	5	1:10

***Chanzo**: Uchambuzi wa Wakaguzi na Taarifa Zilizokusanywa kutoka Shule Zilizotembelewa*

Jedwali 5.3 linaonesha kuwa hali mbaya zaidi kwenye uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi ilikuwa katika shule za msingi za Mugeza Mseto (1:10). Wakati hali ilikuwa nzuri katika Shule ya Hombolo Bwawani, ambapo uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi ulikuwa 1:2. Hii inaashiria kuwepo kwa mzigo mzito kwa walimu au muda mchache wa kuwahudumia wanafunzi.

(f) Uwiano wa Mwalimu kwa Wanafunzi wa Ulemavu wa Kusikia

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu utoaji wa elimu ya wenye mahitaji maalumu pia ulibaini kuwa katika Shule za Msingi za Mtendeni na Kigwe Viziwi, mwalimu mmoja alifundisha kati ya wanafunzi 9 na 18 mtawalia, ambao ni juu ya uwiano unaohitajika wa 1:7. **Jedwali 5.4** linatoa muhtasari uwiano katika shule za msingi zilizotembelewa zenye wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia.

Jedwali 5.4: Hali ya Uwiano wa Mwalimu kwa Wanafunzi Wenye Ulemavu wa Kusikia

Jina la Shule	Idadi ya Wanafunzi	Idadi ya Walimu	Uwiano Halisi
Kaigara	51	0	0
Meru	60	12	1:5
Ilembula	6	1	1:6
Mtendeni	27	3	1:9
Kigwe Viziwi	106	6	1:18

Chanzo: *Uchambuzi wa WakaguziKutoka KWenye Taarifa za Shule Zilizotembelewa*

Jedwali 5.4 linaonesha kuwa uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia ulikuwa mdogo zaidi katika Shule ya Msingi Kaigara ambapo hakukuwa na mwalimu wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu licha ya kudahili wanafunzi 51 wenye ulemavu wa kusikia. Hata hivyo, hali ilikuwa nzuri katika Shule ya Msingi Meru ambapo uwiano ulikuwa 1:5 ambao ni wa kawaida na kigezo rasmi cha uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi.

(g) Uwiano wa Mwalimu kwa Wanafunzi wenye Ulemavu wa Akili

Ilibainika kuwa katika shule za msingi zilizotembelewa zenye wanafunzi wenye ulemavu wa akili, uwiano unaohitajika wa mwalimu-wanafunzi kwa ulemavu wa akili ulikuwa wa juu ya uwiano unaohitajika wa 1:5. **Jedwali 5.5** linatoa muhtasari wa maelezo haya**.**

Jedwali 5.5: Hali ya Uwiano wa Mwalimu kwa Wanafunzi wenye Ulemavu wa Akili

Jina la Shule	Idadi ya Wanafunzi	Idadi ya Walimu	Uwiano Halisi
Ilembula	42	0	0
Mpunguzi	14	2	1:7
Mpilipili	27	3	1:9
Kaloleni	75	6	1:13
Wailes	60	4	1:15
Mtama	15	1	1:15
Tumaini	46	3	1:15
Kaigara	34	2	1:17

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa kutoka Shule Zilizotembelewa (mwaka 2020)*

Jedwali 5.5 linaonesha kuwa, shule zote zilikuwa na uwiano wa juu zaidi wa walimu kwa wanafunzi kuliko uwiano unaohitajika wa 1:5. Hali ilikuwa mbaya zaidi katika Shule ya Msingi Ilembula ambayo ilidahili wanafunzi 42 wenye ulemavu wa akili, ingawa hakukuwa na mwalimu yeyote aliyebobea wa ulemavu wa akili.

(h) Upungufu wa Vifaa katika Shule za Msingi kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Kulikuwa na upungufu katika ugawaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa shule za msingi na sekondari. Ukaguzi ulibaini upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari zilizotembelewa.

Ukaguzi wa ufanisi wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulibaini kuwa kulikuwa na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama mashine za nukta-nundu, michezo ya mafumbo, vifaa vya kusaidia kusikia vya nyuma ya sikio na modi za kusaidia kusikia kwa shule za msingi za wanafunzi wenye mahitaji maalumu nchini. Ukaguzi ulibaini pia kwa mwaka 2017, Wizara kupitia mradi wa LANES ulisambaza vifaa 18,778 vya kujifunzia na kufundishia elimu maalumu.

Katika shule 18 za msingi za wenye mahitaji maalumu zilizotembelewa, kulikuwa na upungufu wa vifaa vya kufundishia, vifaa vya kujifunzia, na vifaa vya kuwasaidia wenye ulemavu vipatavyo 2,566. Mahitaji ya jumla ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi zilizotembelewa yalikuwa ni vifaa 3,785 wakati idadi ya vifaa vilivyopo ilikuwa 1,219.

Uhaba wa jumla wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na vifaa vya kuwasaidia walio na ulemavu ilikuwa asilimia 68 katika shule 17 za msingi zilizotembelewa. Kiwango cha chini kabisa kilikuwa katika Shule ya Msingi Mtama Mkoani Lindi ambayo haikuwa na kifaa chochote cha kusaidia wanafunzi wenye ulemavu. Kwa kuongezea, ukaguzi ulibaini kuwa vifaa vya kujifunzia vilivyotolewa kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi havikuwa rahisi kutumika. Kwa mfano, vitabu vilivyotolewa kwa wanafunzi walemavu wa kuona vilikuwa na picha za kawaida na zilichapishwa pande zote mbili. Hii ilifanya iwe ngumu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu

kusoma kwa urahisi. Taarifa za kina zimetolewa katika sura ya 6 ya ripoti hii.

(i) Vifaa Pungufu vya Kujifunzia kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari Walio Kazini

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikuandaa miongozo, vifaa vya kujifunzia, na mipango na miundo ya kutosha ya utoaji mzuri wa mafunzo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari. Kwa mfano, ilibainika kuwa kulikuwa na upungufu katika uandaaji wa vifaa vya kujifunzia kama vile vitabu na miongozo.

Pia, ilibainika kuwa miongozo ya mafunzo na vifaa vya kujifunzia haikuchapishwa kwa idadi ya kutosha na kusambazwa inavyopaswa. Katika halmashauri zilizotembelewa, moduli za mafunzo zilipatikana kwa uchache katika baadhi ya shule za msingi na sekondari wakati katika shule zingine hazikuwepo kabisa.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa moduli za kujisomea ambazo zilizosambazwa kwa shule za msingi ni zile tu za kusoma, kuandika na kuhesabu. Hakukuwa na moduli za kujisomea kwa walimu ambao walifundisha masomo mengine katika kiwango cha juu cha shule za msingi wala kwa walimu katika shule za sekondari.

5.2.3 Usimamizi Usioridhisha wa Shule katika Utoaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini; usimamizi wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu; na upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi ilibaini kuwa kulikuwa na usimamizi duni katika shule za msingi zilizotembelewa kwa namna ambayo usajili wa shule, usimamizi wa mali, ufadhili, na uhakiki wa ubora haukufanywa vizuri. Ufafanuzi wa kina unatolewa kama ifuatavyo.

(a) Shule Zilizosajiliwa bila Kukidhi Vigezo vya Msingi

Ukaguzi wa ufanisi wa upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi ulibaini kwamba asilimia 94 ya shule za msingi 17,165 nchini hazikusajiliwa na Wizara ya Elimu. Shule za msingi za umma ambazo zilisajiliwa na ofisa elimu wa mkoa kwa niaba ya kamishna wa elimu zilisajiliwa bila kukidhi vigezo vya msingi vya usajili. Kwa mujibu wa Miongozo ya Wizara ya Elimu ya Mwaka 1982, vigezo vya msingi vya kusajili shule ni pamoja na ujenzi wa majengo ya shule na angalau vyumba 6 vya madarasa na uwepo wa madawati ya kutosha.

Uchambuzi wa matokeo ya ukaguzi wa shule 11 za msingi zinazomilikiwa na serikali zilizotembelewa, ni shule mbili tu ndizo zilikidhi vigezo vya msingi vya usajili wakati shule za msingi tisa hazikupaswa kufanya kazi kwa kuwa hazikukidhi mahitaji ya miundombinu ya shule.

Chanzo cha shule za msingi kusajiliwa bila kukidhi vigezo vya msingi ni udhaifu katika ukasimishaji wa usajili wa shule za msingi za umma kwa mamlaka za serikali za mitaa kinyume na Sheria ya Elimu, Sura ya 353 na marekebisho yake. Wizara haikupaswa kukabidhi jukumu lake la msingi kwa TAMISEMI. Hii ilisababisha kuwa na shule za msingi ambazo hazikuwa na vifaa vya kutosha.

(b) Kukosekana kwa Taratibu Maalumu za Matengenezo ya Vifaa vya Kufundishia, Kujifunzia na Kuwasaidia Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Ukaguzi wa ufanisi juu ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulibaini kulikuwa na udhaifu katika usimamizi wa mali za shule za msingi kwa ajili ya utoaji wa elimu. Hii ilitokana na ukweli kwamba, hakukuwa na utaratibu wa utunzaji na matengenezo ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, ambao ni wanafunzi wenye ulemavu wa kuona, kusikia, na akili.

Mapitio ya bajeti za kila mwaka yalionesha kuwa Wizara zote mbili hazikuandaa bajeti ya matengenezo ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia elimu maalumu. Mnamo Mei 2018, walimu 253 wa elimu maalumu walifundishwa jinsi ya kutunza na kutengeneza vifaa vya kusaidia wanafunzi wenye ulemavu wa kuona na kusikia. Hata hivyo, ilibainika

kuwa mafunzo yaliyotolewa kwa walimu kwa shule za msingi zilizotembelewa yalikuwa ya matengenezo madogo na si matengenezo makubwa ya vifaa vya kusaidia wanafunzi wenye ulemavu.

Hali hii ilisababishwa na kutokuwepo kwa kumbukumbu za vifaa vilivyoharibika na jumla ya vifaa vya kusaidia wenye ulemavu vilivyopo shuleni. Utunzaji huo wa kumbukumbu ulikuwa muhimu kwa ufuatiliaji na kuamua ni lini au vifaa vipi vilihitaji matengenezo. Pia, idadi ndogo ya wataalamu wa kukarabati vifaa ilichangia kuwapo kwa vifaa ambavyo havijatengenezwa shuleni.

(c) Ufadhili wa Kutosha wa Elimu ya Msingi

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulibaini kuwepo kwa upungufu wa fedha kwa elimu ya msingi ambapo fedha zilizotolewa ama zilitolewa kidogo au hazikutolewa kabisa ikilinganishwa na kiasi kilichoombwa au kupangiwa bajeti na hivyo kutowezesha utekelezaji wa shughuli yoyote.

Zaidi ya hilo, bajeti iliyopangwa kwa shughuli za elimu haikuzingatia mambo yote muhimu ya elimu. Kwa mfano, mapitio ya bajeti za mwaka za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI na ripoti za utendaji kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2014/15 hadi 2017/18 yalibaini kuwa bajeti za TAMISEMI hazikujumuisha fedha za ununuzi wa vifaa vya kusaidia wanafunzi wenye ulemavu na mafunzo ya walimu kwa shule za maalumu.

TAMISEMI kupitia mamlaka zake za serikali za mitaa imekuwa ikitenga fedha zisizotosheleza katika sekta ya elimu hivyo kuzifanya shule zishindwe kufikia malengo yaliyokusudiwa na ahadi zilizowekwa na serikali kupitia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu. **Jedwali 5.6** linaonesha viwango vya bajeti vilivyopangwa kwenye sekta ya elimu kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2019/20.

Jedwali 5.6: Bajeti ya Elimu Ikilinganishwa na Bajeti Kuu ya Serikali

Mwaka wa Fedha	Jumla ya Bajeti ya Serikali Tsh. (Bilioni)	Bajeti ya Sekta ya Elimu (Tsh. Bilioni)	Asilimia ya Bajeti kwenye Sekta ya Elimu
2016/17	29,540	2,958	10
2017/18	31,712	4,706	15
2018/19	32,475	3,212	10
2019/20	33,105	4,512	14

Chanzo: *Bajeti ya Serikali na Mpango wa Muda Mfupi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mwaka 2020*

Jedwali 5.6 linaonesha kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20, mwelekeo unaonesha kuwa kulikuwa na mabadiliko kidogo ya utoaji wa fedha kwa sekta ya elimu. Kiwango cha juu zaidi kilikuwa katika mwaka 2017/18 ambapo jumla ya fedha iliyotengwa ilikuwa asilimia 15 ya bajeti nzima wakati malipo ya kiwango cha chini kilikuwa asilimia 10 ya bajeti yote.

5.2.4 Ufuatiliaji wa Utoaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini ilibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeweza kufanya ziara 3 kati ya 4 kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2018/19. Mapitio ya ripoti za pamoja za ufuatiliaji kwa miaka 2017 na 2018 yalibaini udhaifu katika utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini. Maeneo ambayo yanahitaji maboresho ni pamoja na utoaji wa mafunzo kwa walimu wa masomo yasiyo ya sayansi, na kukosekana kwa mafunzo ya kujenga uwezo juu ya elimu-jumuishi. Kwa mfano, kuna haja ya kutoa mafunzo ya usimamizi wa maendeleo ya tabia za wanafunzi.

Sababu za udhaifu uliotajwa hapo juu zilitokana na kutokuwepo kwa mipango na mfumo wa mafunzo kazini kuanzia ngazi ya wilaya hadi ngazi za taifa. Kwa upande mwingine, walimu wengi waliripotiwa kuwa na maarifa kidogo ya namna ya kutekeleza mbinu mpya zinazotegemea uwezo wa mwalimu katika kufundisha.

Kwa sababu hiyo, wanafunzi waliohitimu walikuwa na maarifa ya kinadharia zaidi kuliko ujuzi wa kuwawesha kutumia maarifa

waliyoyapata. Ingawa udhaifu uliogunduliwa wakati wa kufanya ufuatiliaji wa pamoja ulitarajiwa kujadiliwa na maazimio kufanywa katika Mapitio ya Pamoja ya Sekta ya Elimu, uhakiki wa Ripoti ya Mapitio ya Sekta ya Elimu ulionesha kuwa maazimio ya jinsi ya kukomesha changamoto zilizoonekana katika ufuatiliaji wa pamoja hayakutolewa.

Aidha, ukaguzi wa ufanisi kuhusu upatikanaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI zilipaswa kuwa na kanzidata ya kitaifa inayofaa ya uimarishaji na utunzaji wa miundombinu ya shule za msingi. Hii ingewezesha ufuatiliaji wa shughuli zote 60 zinazohitajika kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa miundombinu ya shule za msingi nchini.
Ukaguzi pia ulibaini udhaifu kwenye utunzaji wa taarifa wakati wa kuchambua sababu za kwa nini baadhi ya shule zilikuwa na miundombinu duni. Sababu zilizobainika ni pamoja na ukosefu wa taarifa za kutosha kuhusu shule zilizosajiliwa, zilizokaguliwa, na ambazo hazijakaguliwa; pamoja na kanzidata isiyofaa ya rasilimali zilizopo na zinazohitajika.

5.2.5 Matokeo ya Sera ya Elimu Bure katika Utoaji wa Elimu Nchini

Kufuatia kuanzishwa kwa sera ya elimu bila malipo mwaka 2016, kumekuwa na ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi. Katika mwaka 2015, jumla ya wanafunzi 8,298,282 waliandikishwa katika shule za msingi na hivyo idadi kuongezeka hadi kufikia wanafunzi 10,460,785 mwaka 2020, ambalo ni ongezeko asilimia 26.

Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa, kufuatia ongezeko la idadi ya wanafunzi walioadahiliwa katika shule za msingi, kumekuwa na msukumo mkubwa wa kuongeza rasilimali katika utoaji wa elimu na hasa katika shule za msingi. Hali hii inadhihirishwa na kubadilika kwa uwiano wa mwanafunzi na mwalimu, na darasa na madawati kabla na baada ya elimu bure. Mabadiliko ya uwiano ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali 5.7**.

Jedwali 5.7: Mabadiliko ya Uwiano wa Mwanafunzi na Mwalimu, Madawati na Madarasa kabla na baada ya Sera ya Elimu Bure

Uwiano	Kabla ya elimu bure (2015)	Baada ya elimu bure (2020)
Idadi ya wanafunzi (I-VII)	8,298,282	10,460,785
Wanafunzi na walimu	42	61
Wanafunzi na vyumba vya madarasa	72	81
Wanafunzi na madawati	4	4

Chanzo: *Takwimu Rasmi za Elimu ya Msingi kwa Miaka 2015-2010)*

Jedwali 5.7 linaonesha kwa ujumla kuwa, kumekuwa na ongezeko la idadi ya wanafunzi na kupungua kwa uwiano wa wanafunzi na walimu, na madarasa na madawati na kusababisha uhitaji zaidi wa rasilimali za kuwezesha utoaji wa elimu ya msingi. Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa (darasa I-VII) imeongezeka kwa asilimia 26 kutoka takribani milioni 8.3 kabla ya elimu bure hadi takribani milioni 10.5 baada ya elimu bure.

Jedwali 5.7 pia linaonesha kumekuwa na mabadiliko ya uwiano wa mwanafunzi kwa mwalimu kutoka wanafunzi 42 kwa mwalimu mmoja hadi kufikia wanafunzi 62 kwa mwalimu mmoja.
Zaidi ya hilo, mabadiliko pia yameonekana katika uwiano wa wanafunzi kwa chumba cha darasa kutoka wanafunzi 72 kwa chumba kimoja cha darasa kabla ya elimu bure hadi kufikia wanafunzi 81 kwa chumba kimoja cha darasa baada ya elimu bure.

Kwa upande mwingine, hakukuwa na mabadiliko katika uwiano wa wanafunzi na madawati, ambapo kabla na baada ya elimu bure uwiano umebaki kuwa wa wanafunzi 4 kwa dawati moja. Mapitio ya ripoti ya sekta ya elimu yameonesha kuwa sababu ya kutokuwa na mabadiliko katika uwiano wa wanafunzi na madawati ni kampeni ya kitaifa ya kutengeneza madawati iliyofanyika mwaka 2017-2018.

Ongezeko la uhitaji wa walimu, madarasa na madawati, umepelekea ongezeko la uhitaji wa rasilimali-fedha ili kufikia kiwango ambacho kitatengeneza mazingira rafiki ya utoaji wa elimu ya msingi yenye ubora wa kiwango cha juu.

SURA YA SITA

USIMAMIZI WA ELIMU KWA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUMU

6.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi uliofanyika kuhusu usimamizi wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi nchini kwa kulenga wanafunzi wenye ulemavu wa akili, kuona, na kusikia.

Matokeo haya ya ukaguzi yamegawanyika katika makundi matatu ambayo ni ugawaji na uratibu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalumu; mchango wa shughuli za wadhibiti ubora wa shule katika kuboresha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu; na utungaji na usimamizi wa mitihani ya taifa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu Mwaka 2019 imetumika kufanya majumuisho ya matokeo ya ukaguzi yanayoelezwa katika sura hii. Wakaguliwa wakuu walikuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na OR-TAMISEMI. Wadau wengine ni pamoja na Baraza la Mitihani la Tanzania, na mamlaka za serikali za mitaa na tawala za mikoa. Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi ni kama yanavyoelezwa kwa kina hapa chini.

6.2 Ugawaji na Uratibu wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia Elimu Maalumu

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na O-TAMISEMI hazijaweza kuratibu na kugawa vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia elimu maalumu. Hali hii inathibishwa katika maeneo yafuatayo:

6.2.1 Upungufu wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia kwenye Shule Zenye Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Mapitio ya orodha za vifaa katika shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu zilizotembelewa yalibaini kuwa shule 17 kati ya 18 zilikuwa na upungufu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalumu kama inavyooneshwa kwenye **Jedwari 6.1.**

Jedwali 6.1: Hali ya Vifaa Vilivyopo na Vinavyohitajika kwa ajili ya Kufundishia na Kujifunzia Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu katika Shule Zilizotembelewa

Jina la shule	Idadi ya Vifaa Vilivyopo	Idadi ya Vifaa Vinavyohitajika	Upungufu	Asilimia ya Upungufu
Mtama	0	60	60	100
Mpunguzi	1	52	51	98
Kambarage	5	119	114	96
Kibena	35	255	220	86
Mtendeni	16	118	102	86
Wailes	19	89	70	79
Ilembula	117	541	424	78
Tumaini	48	153	105	69
Mpilili	28	84	56	67
Kigwe Viziwi	154	451	297	66
Kaigara	49	132	82	62
Mgeza Mseto	258	682	424	62
Kaloleni	107	269	162	60
Nyangao	229	489	260	53
Kijitonyama	35	64	29	46
Hombolo bwawani	42	122	42	34
Themi	76	105	29	28
Meru	HA[4]	HA	HA	HA
TOTAL	**1,219**	**3,785**	**2,566**	**68**

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Kumbukumbu za Vifaa vya Shule*

Jedwali 6.1 linaonesha kuwa, upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ulikuwa wa asilimia 68 katika shule za msingi 18 zilizotembelewa. Shule za Msingi Themi, Hombolo Bwawani na Kijitonyama ambazo ni asilimia 17 ya shule zilizotembelewa, zilikuwa na upungufu wa chini ya asilimia 50 wakati Shule ya Msingi Mtama haikuwa na kifaa chochote kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Hali hii ilisababishwa na mambo yafuatayo:

Sababu za Upungufu wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia Kwenye Shule zenye Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

[4] Taarifa za shule ya msingi Meru kuhusu idadi ya vifaa vilivyopo haikuwasilishwa kwa wakaguzi.

i. Upungufu wa Mipango na Bajeti kwa Shughuli za Elimu Maalumu

Mapitio ya bajeti na ripoti za utekelezaji za mwaka za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2017/18 yalibaini kuwa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na mafunzo ya walimu wa elimu maalumu zinategemea sana fedha za wafadhili ambazo si endelevu.

Kwa kipindi cha ukaguzi, Wizara zote mbili hazikuweza kujumuisha shughuli za elimu maalumu katika mipango yao ya mwaka na bajeti. Badala yake, shughuli hizo za elimu maalumu zilijumuishwa kwenye programu ya kusoma kuandika na kuhesabu. Hata hivyo, programu hiyo haikuweza kukidhi mahitaji yote ya elimu maalumu. **Jedwali 6.2** linaonesha bajeti iliyotengwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI kwa ajili ya shughuli za elimu maalumu.

Jedwali 6.2: Fedha Zilizotengwa na Serikali kwa ajili ya Elimu Maalumu (kiasi katika milioni za Tsh.)

Chanzo cha Fedha	Miaka	WEST		OR-TAMISEMI	
		Bajeti	Fedha Iliyotolewa	Bajeti	Fedha Iliyotolewa
Serikali ya Tanzania	2014/15	306	274	Hakuna	Hakuna
	2015/16	1,098	359	Hakuna	Hakuna
	2016/17	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
	2017/18	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
Jumla ndogo 1		**1,404**	**633**	Hakuna	Hakuna
Programu ya LANES	2014/15	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
	2015/16	972	972	254	190
	2016/17	Hakuna	Hakuna	5,277	5,037
	2017/18	4,966	4,320	761	761
Jumla ndogo 2		**5,938**	**5,292**	**6,292**	**5,988**
Jumla Kuu (Jumla ndogo 1 na2)		**7,342**	**5,925**	**6,292**	**5,988**

Chanzo: *Bajeti ya WEST na OR-TAMISEMI Mwaka 2014/15 hadi 2017/2018*

Jedwali 6.2 linaonesha kuwa kwa kipindi cha ukaguzi OR-TAMISEMI hazikutenga wala kupanga bajeti ya fedha za serikali kwa ajili ya shughuli za elimu maalumu. Shughuli za elimu maalumu zilifadhiliwa kwa kiasi kidogo na mradi wa LANES. Pia, **Jedwali 6.2** linaonesha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitenga kiasi cha shilingi milioni 1,404 kwa ajili ya shughuli za elimu maalumu katika miaka ya fedha 2014/15 na

2015/16, ingawa ni shilingi milioni 633 tu ndizo zilitolewa kwa ajili ya shughuli hizo.

Ukaguzi pia ulibaini kuwa kati ya shilingi milioni 633 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya elimu maalumu, shilingi milioni 272 zilibadilishiwa matumizi na badala yake kutumika kwa ajili ya shughuli za mitihani ya darasa la nne, na mashindano ya lugha ya Kingereza katika Jumuiya ya Afrika mashariki.

ii. Ukosefu wa Tathmini ya Mahitaji

Mapitio ya majalada ya elimu maalumu na majalada ya manunuzi yalionesha kuwa hakukuwa na tathmini yoyote ya mahitaji iliyofanyika ili kubaini mahitaji kwa kila kundi la wanafunzi wenye ulemavu katika shule za msingi. Ukosefu wa tathmini ya mahitaji ya elimu maalumu ilipelekea kukosekana kwa taarifa muhimu kama vile idadi halisi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, na vifaa vya kufundishia na kujifunzia vilivyopo na vinavyohitajika kwa ajili ya elimu maalumu katika ngazi ya taifa.

6.2.2 Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia havikuwa Rafiki kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Uhakiki uliofanyika katika shule za elimu maalumu zilizochaguliwa ulibaini kuwa, vitabu vya wanafunzi wenye ulemavu wa kuona vilikuwa na picha za kawaida ambazo wanafunzi wenye ulemavu wa kuona hawawezi kuziona kama inavyooneshwa katika **Picha 6.1**.



Picha 6.1: *Vitabu kwa Ajili ya Wanafunzi wenye Ulemavu wa Kuona Vikiwa na Picha za Kawaida (Picha ilipigwa katika Shule ya Msingi Themi Arusha, tarehe 12/09/2018)*

Uchunguzi zaidi uliofanywa na wakaguzi ulibaini kuwa vitabu hivyo pia vilikuwa vimechapwa kwa nukta-nundu mbele na nyuma ya kurasa za karatasi. Hali hii ilisababisha mwingiliano wa maandishi katika pande hizo mbili za karatasi na hivyo kusababisha wanafunzi washindwe kusoma maandishi kwa ufasaha. Sampuli ya vitabu vilivyochapishwa kwa nukta-nundu mbele na nyuma ya karatasi inaoneshwa katika **Picha 6.2**.



Picha 6.2: *Kurasa za Vitabu vya Nukta-nundu Vilivyochapwa Mbele na Nyuma ya Kurasa (Picha ilipigwa katika Shule ya Msingi Themi, Arusha, tarehe 12/09/2018)*

Suala la kuchapishwa vitabu mbele na nyuma ya karatasi lilitajwa katika taarifa ya ukaguzi ya wadhibiti ubora wa shule ya tarehe 19 Mei 2017. Taarifa hiyo ilipendekeza kuwa vitabu vya nukta-nundu vichapishwe upande mmoja wa karatasi ili kuepuka mwingiliano wa maneno na kupunguza mkanganyiko wa kusoma maandishi hayo kwa wanafunzi wenye ulemavu wa kuona. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi huu hakukuwa na mabadiliko yoyote.

6.2.3 Upungufu wa Vyumba vya Stoo kwa Ajili ya Kuhifadhi Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia katika Shule Zilizotembelewa

Katika uhakiki wa shule nne zenye wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia za Kigwe Viziwi, Mtendeni, Kaigara na Meru ilibainika kuwa ni Shule ya Msingi Kigwe Viziwi tu ndiyo ilikuwa na chumba maalumu kwa ajili ya kuhifadhia kifaa kinachosaidia kupima kiwango cha usikivu kwa watu wenye ulemavu wa kusikia (audiometer). Chumba hiki ni muhimu kwenye upimaji wa uwezo wa kusikia kwani kinasaidia kutoa matokeo ya uhakika. Kwa mfano, katika Shule ya Msingi Mtendeni ilionekana kuwa ofisi moja ya mwalimu inatumika kama stoo ya kuhifadhia vifaa vya kupimia kama inavyooneshwa katika **Picha 6.3**.

Picha 6.3: *Ofisi ya Mwalimu wa Elimu Maalumu Ikitumika kama Chumba cha Kuhifadhi Vifaa na Kupima Wanafunzi Wenye Ulemavu wa Kusikia (Picha ilipigwa na wakaguzi katika Shule ya Msingi Mtendeni katika Wilaya ya Ilala, tarehe 20/08/2018)*

Ukosefu wa chumba maalumu kwa ajili ya kuhifadhi vifaa hivyo maalumu kulitokana na kushindwa kutathmini mahitaji na kutenga fedha kwa ajili ya elimu maalumu kama ilivyoelezwa katika kipengele **6.2.1(i)**.

6.2.4 Mapungufu katika Utaratibu wa Matengenezo ya Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Ukaguzi ulibaini kuwa OR-TAMISEMI na Wizara ya Elimu hazikuwa na utaratibu wa matengenezo ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Mapitio ya bajeti za mwaka yalibaini kuwa wizara zote hazikutenga bajeti kwa ajili ya matengenezo ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia elimu maalumu.

Mapitio ya taarifa za mafunzo za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilibaini kuwa kwa kipindi cha mwezi Mei 2018, Wizara kupitia programu ya kusoma, kuandika na kuhesabu iliendesha mafunzo kwa walimu 253 wa elimu maalumu ili kuwajengea uwezo wa kufanya matengenezo ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenye ulemavu wa kuona na kusikia. Hata hivyo, baadhi ya walimu waliohudhuria mafunzo hayo walipofanya mahojiano na wakaguzi walieleza kuwa ujuzi walioupata kupitia mafunzo hayo ulilenga kuwapatia uwezo wa kufanya matengenezo

madogomadogo. Hivyo, kwa matengenezo makubwa ya vifaa, shule zilipaswa kutafuta wataalamu wengine wenye ujuzi zaidi.

Vilevile, ilibainika kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilikuwa na mafundi wawili tu waliokuwa na uwezo wa kufanya matengenezo makubwa ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Hali hii imesabisha uwepo wa idadi kubwa ya vifaa vibovu, kwa mfano uwepo wa mashine mbovu za nukta-nundu 115 na za kunakili maandishi ya nukta-nundu 2 katika Shule za Msingi Hombolo Bwawani, Ilembula, Nyangao na Mugeza Mseto, kama inavyooneshwa katika **Picha 6.4**.

Hombolo, tarehe 23/01/2019

Nyangao, tarehe 11/12/2018

Mugeza Mseto, tarehe 08/01/2019

Ilembula, tarehe 27/09/2018

Picha 6.4: Mashine Mbovu za Nukta-nundu na za Kunakili Maandishi ya Nukta-nundu (*Picha ilipigwa na wakaguzi katika shule tofauti na tarehe tofauti kama inavyooneshwa*)

Ilibainika pia kuwa wizara zote mbili hazikuwa na taarifa za uhakika kuhusu idadi ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia ambavyo ni vibovu na vilihitaji matengenezo.

Hali hii ilisababishwa na dodoso linalotumiwa na OR-TAMISEMI kukusanya taarifa za shule za msingi halikuhusisha taarifa kuhusu hali ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia elimu maalumu.

Uwepo wa vifaa vibovu vya kujifunzia na kufundishia elimu maalumu kulisababisha upotevu wa fedha za umma kwa sababu vifaa hivyo vingeweza kutengenezwa na kutumika. Kuachwa bila matengenezo kwa muda mrefu huongeza uchakavu ambao unaweza kufanya vishindwe kutengenezeka kabisa.

6.2.5 Idadi Pungufu ya Walimu wa Elimu Maalumu katika Shule Zenye Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu

Kifungu cha 4.2 cha Mpango wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2009 hadi 2017 unaitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI kuviongezea uwezo vyuo vya ualimu ili viweze kutoa mafunzo ya elimu jumuishi kwa lengo la kuongeza idadi ya walimu wenye taaluma ya elimu maalumu nchini. Tathmini iliyofanyika kuhusu utoshelevu wa walimu wenye taaluma ya elimu maalumu nchini ilibaini yafuatayo:

i. Idadi ndogo ya walimu waliopewa mafunzo ya elimu maalumu katika kipindi cha ukaguzi

Ukaguzi ulibaini kuwa, japokuwa makadirio yanaonesha uhitaji wa walimu wa elimu maalumu katika shule za msingi nchini ni walimu 4,428, hadi wakati ukaguzi unafanyika idadi ya walimu wa elimu maalumu katika shule za msingi ilikuwa 2,460, sawa na upungufu wa walimu 1968 ambao ni asilimia 44 .

Upungufu huu ulitokana na kasi ndogo ya kuzalisha walimu wa elimu maalumu[5]. Hii ni kwa sababu serikali ilikuwa na chuo kimoja tu cha kuwaandaa walimu wa elimu maalumu wa shule za msingi nchini yaani Chuo cha Ualimu Patandi Arusha.

Ingawa Chuo cha Ualimu Patandi kilikuwa na uwezo wa kudahili walimu 300 kwa mwaka, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilizalisha walimu

[5] Taarifa za mafunzo za kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2018/19

wa elimu maalumu 654 tu katika kipindi cha kuanzia mwaka 2014 hadi 2018 sawa na wastani wa kuzalisha walimu 131 kwa mwaka. Kwa kiwango hiki cha uzalishaji, inakadiriwa itachukua takribani miaka 15 kwa Wizara kuondoa upungufu wa walimu 1968 wa elimu maalumu, kama hali itabaki kama ilivyo. Mwenendo wa kuzalisha walimu wa elimu maalumu katika shule za msingi kwa miaka mitano iliyopita ni kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo 6.1.**

Kielelezo 6.1: Idadi ya Walimu Waliopewa Mafunzo ya Elimu Maalumu kwa Shule za Msingi



Chanzo: *Orodha ya Walimu wa Elimu Maalumu ya WEST*

Kielelezo 6.1 kinaonesha kuwa idadi kubwa ya walimu wa elimu maalumu waliozalishwa ilikuwa 201 mwaka 2015. Katika miaka 2016 na 2017, idadi ilipungua kufikia chini ya 160, na katika mwaka 2018 idadi ilikuwa chini ya 100.

Kwa upande mwingine, mapitio ya kanzidata ya walimu maalumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na taarifa za mafunzo kwa kipindi cha miaka minne yalibaini kuwa walimu wa elimu maalumu 1,508 ambao ni asilimia 61 ya walimu wote wa elimu maalumu, hawakupatiwa mafunzo ya muda mfupi kuanzia mwaka 2014 hadi 2018. Makadirio ya idadi ya walimu wa elimu maalumu nchini ni 2,460; kati ya hao walimu 952 tu ndio walipewa mafunzo ya muda mfupi, ambayo yalitolewa na Wizara ya Elimu au OR-TAMISEMI kuanzia mwaka 2014 hadi 2018.

ii. Mapungufu katika Uhamisho kwa Walimu Walioendelezwa katika Taaluma ya Elimu Maalumu

Mapitio ya taarifa za mafunzo ya walimu katika halmashauri zilizotembelewa yalionesha kuwa halmashauri 8 kati ya 12 hazikuwahamisha walimu walioendelezwa katika taaluma ya elimu

maalumu kwenda katika shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Idadi ilikuwa kubwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ambapo ilikuwa na walimu 9 ambao walikuwa wanasubiri uhamisho.

Katika ngazi ya taifa, mapitio ya orodha ya walimu wa elimu maalumu katika Ofisi ya Taifa ya OR-TAMISEMI yalionesha kuwa walimu 611 walioendelezwa katika taaluma ya elimu maalumu walikuwa bado hawajahamishwa kwenda shule za elimu maalumu. Maofisa elimu maalumu waliohojiwa katika halmashauri husika walieleza kuwa suala la kushindwa kuhamisha walimu linatokana na changamoto za kifedha.

6.2.6 Uratibu Duni katika Utoaji wa Elimu Maalumu

Kwa mujibu wa Kipengele 3.2.3 cha Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Serikali ilipaswa kuratibu wizara, taasisi, na wakala zake zenye jukumu la kusimamia masuala ya elimu, ikijumuisha elimu maalumu.

Mapitio ya ripoti mbalimbali ilionesha kuwa hakukuwa na uratibu mzuri katika ugawaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia elimu maalumu kwa sababu halmashauri na OR-TAMISEMI hawakupeana taarifa kuhusu idadi ya walimu wa elimu maalumu. Baadhi ya taarifa zilizopatikana katika shule hazikuwepo katika ngazi ya wilaya.

Ukaguzi ulibaini pia kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI hawakuratibu vizuri jitahada zao za kununua na kusambaza vifaa vya kujifunzia na kufundishia elimu maalumu kwa udhamini wa mradi wa LANES. Kutokana na kukosekana kwa mawasiliano ili kujua idadi na aina ya vifaa vilivyokuwa vinahijika zaidi, wizara zote mbili zilinunua vifaa vya aina zinazofanana, na wakati mwingine, vifaa vingine vilivyokuwa vinahitajika havikununuliwa kabisa.

6.3 Mchango wa Wadhibiti Ubora katika Utoaji wa Elimu Maalumu

Tathmini ya uwezo wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kutekeleza shughuli za udhibiti ubora wa shule ilibaini upungufu katika kufanya kaguzi na kutekeleza mapendekezo yanayotolewa ili kuboresha shughuli za elimu maalumu. Katika tathmini hiyo mambo yafuatayo yalibainika:

6.3.1 Upungufu wa kaguzi zilizofanyika katika shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu

Mapitio ya taarifa za kaguzi zilizofanyika katika shule 18 zilizotembelewa yalionesha kuwa shule hizo zilikuwa hazikaguliwi mara kwa mara. Hii ni kinyume na Kipengele cha 12 cha Mwongozo wa Ukaguzi wa Shule wa Mwaka 2010, ambao unataka kila shule ikaguliwe mara moja kila mwaka wa masomo.

Jedwali 6.3 linaonesha taarifa kuhusu idadi ya kaguzi zilizofanyika katika elimu maalumu kwenye shule za msingi zilizotembelewa. Taarifa hizo ni kwa miaka minne ya fedha kuanzia 2014/15 hadi 2017/2018.

Jedwali 6.3: Kaguzi Zilizofanyika katika Shule za Msingi za Elimu Maalumu Zilizotembelewa

Shule	Hali ya Kaguzi (✓ = Imefanyika × = Haijafanyika HA= Haihusiki)				Jumla ya idadi ya kaguzi
	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18	
Kaloleni	✓	✓	×	✓	3
Themi	×	✓	✓	✓	3
Mtendeni	×	✓	✓	✓	3
Tumaini	✓	✓	×	✓	3
Mugeza Mseto	✓	✓	✓	×	3
Meru	×	✓	×	✓	2
Ilembula	×	×	✓	✓	2
Kijitonyama	×	✓	×	✓	2
Mpunguzi	×	×	✓	✓	2
Kambarage	×	×	×	✓	1
Kibena	×	×	✓	×	1
Wailes	×	×	×	✓	1
Mpilipili	✓	×	×	×	1
Kaigara	×	✓	×	×	1
Hombolo Bwawani	×	✓	×	×	1
Kigwe Viziwi	×	✓	×	×	1
Nyangao	×	×	×	×	0
Mtama[6]	HA	HA	HA	×	0
Asilimia ya kaguzi	**24**	**59**	**35**	**56**	

[6] Katika Shule ya Msingi Mtama, Kitengo cha Elimu Maalumu kilianzishwa mwaka 2018, hivyo taarifa za miaka ya nyuma kuhusu wanafunzi wa elimu maalumu hazikuwepo.

Shule	Hali ya Kaguzi (✓ = Imefanyika × = Haijafanyika HA= Haihusiki)				Jumla ya idadi ya kaguzi
	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18	
kwa Mwaka					

Chanzo: *Taarifa za Kaguzi za Shule kwa Kipindi cha kuanzia Mwaka 2014/2015 hadi 2017/2018*

Jedwali 6.3 linaonesha kuwa, kwa kipindi cha miaka minne ya fedha kuanzia 2014/15 hadi 2017/18, hakuna shule yeyote ya elimu maalumu iliyokaguliwa kila mwaka. Shule 5 tu kati ya 18 zilikaguliwa angalau mara tatu au mbili katika kipindi cha miaka minne. Shule zingine zote zilikaguliwa mara moja au mbili. Kwa upande wa Shule ya Msingi Nyangao hali haikuwa ya kuridhisha kwa kiwango kikubwa kwa sababu kwa kipindi chote cha miaka minne haikuwahi kukaguliwa.

Sababu za upungufu wa kaguzi zilizofanyika katika shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu

Mapitio ya taarifa za kaguzi za shule za elimu maalumu na ofisi za wadhibiti ubora wa shule katika wilaya zilizotembelewa zilionesha kuwa hakukuwa na utaratibu mzuri wa kuchagua shule za elimu maalumu ili zikaguliwe. Hii ilitokana na sababu kuwa vigezo vilivyotumika kuchagua shule ili zikaguliwe havikuhusisha mambo ya elimu maalumu, na wadhibiti ubora wa shule hizo hawakuwa na taaluma ya elimu maalumu. Masuala haya yanaelezwa kwa kina kama ifuatavyo:

i. Vigezo vya Kuchagua Shule za Kukaguliwa Havikuhusisha Masuala ya Elimu Maalumu

Ilibainika kuwa wadhibiti ubora wa shule walikuwa wakichagua shule za kwenda kuzikagua kwa kuzingatia matokeo ya mtihani wa taifa wa darasa la saba. Hivyo, kwa shule ambazo zilikuwa na kitengo[7] cha elimu maalumu, hazikukaguliwa kwa kuwa, matokeo ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu yalikuwa yakitolewa kwa ujumla na wanafunzi wa kawaida ambao hawakuwa na ulemavu.

[7] Shule ya msingi ya kawaida yenye kitengo cha wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Hali hii ilipelekea wanafunzi wenye mahitaji maalumu, kwa uchache wao, uhalisia wa matokeo yao kutoonekana kwa sababu ya matokeo mazuri ya wanafunzi ambao si walemavu. Ufuatiliaji wa karibu ulihitajika ili kuibua changamoto za wanafunzi wenye mahitaji maalumu. **Jedwali 6.4** inaonesha shule za elimu maalumu zilizowekwa kwenye mpango wa kukaguliwa.

Jedwali 6.4: Shule za Elimu Maalumu Zilizowekwa katika Mpango wa Kukaguliwa katika Kipindi cha Ukaguzi

Jina la Halmashauri	Idadi ya shule za elimu maalumu	Miaka na shule zilizowekwa kwenye mpango wa ukaguzi							
		2014/15		2015/16		2016/17		2017/18	
		Shule kwenye mpango	(%) Shule kwenye mpango	Shule kwenye mpango	(%) Shule kwenye mpango	Shule kwenye mpango	(%) Shule kwenye mpango	Shule kwenye mpango	(%) Shule kwenye mpango
Jiji la Arusha	6	4	67	4	67	2	33	2	33
Njombe Mji	5	0	0	2	40	1	20	2	40
Wanging'ombe	1	0	0	1	100	1	100	0	0
Temeke	14	2	14	4	29	2	14	3	21
Kinondoni	6	4	67	2	33	2	33	1	17
Ilala	14	5	36	10	71	8	57	0	0
Lindi	1	1	100	0	0	0	0	0	0
Lindi	3	0	0	0	0	0	0	0	0
Bukoba	3	2	67	2	67	1	33	1	33
Muleba	5	0	0	1	20	1	20	0	0
Dodoma	7	3	43	3	43	4	57	3	43
Bahi	2	1	50	1	50	2	100	0	0
Jumla	**67**	**22**	**33**	**30**	**45**	**24**	**36**	**12**	**18**

Chanzo: *Mipango ya Ukaguzi ya Wadhibiti Ubora wa Shule kuanzia Mwaka 2014 hadi 2018*

Kama inavyoonekana katika **Jedwali 6.4**, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi na Wanging'ombe zilikuwa zimewekwa kwenye mpango mara nyingi zaidi, kwa asilimia mia moja kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2016/17. Pia, Halmashauri ya Wilaya ya Bahi iliweka kwenye mpango wa

ukaguzi shule zote kwa mwaka 2016/17 tu kwa sababu ilikuwa na idadi ndogo ya shule za elimu maalumu. Kwa mwaka 2017/18, kiwango cha juu cha kuweka shule maalumu katika mpango wa ukaguzi kilikuwa asilimia 43.

Kwa kipindi chote cha miaka minne tangu 2014/15 hadi 2017/18, kiwango cha shule maalumu kuhusishwa katika mipango ya ukaguzi kwa ujumla kilikuwa kati ya asilimia 18 na 45. Kiwango kikubwa kilikuwa mwaka 2015/16 na kiwango cha chini zaidi kilikuwa mwaka 2017/18.

ii. Upungufu wa Idadi ya Wadhibiti Ubora wa Shule wenye Taaluma ya Elimu Maalumu

Mapitio ya orodha ya wadhibiti ubora wa shule za msingi ilionesha kuwa, idadi ya wadhibiti ubora wa shule ni 1306, ambapo kati ya hao 98 tu (sawa na asilimia 8) ndio walikuwa na taaluma ya elimu maalumu. **Jedwali 6.5** linaonesha idadi ya wadhibiti ubora katika halmashauri, wadhibiti ubora wenye taaluma ya elimu maalumu, na idadi ya shule za elimu maalumu.

Jedwali 6.5: Idadi ya wadhibiti Ubora wa Shule Ikilinganishwa na Idadi ya Shule za Elimu Maalumu katika Halmashauri

Jina la Halmashauri	Idadi ya Wadhibiti Ubora wa Shule	Wadhibiti Ubora wa Shule wenye Taaluma ya Elimu Maalumu	Idadi ya Shule Maalumu
Manispaa ya Temeke	20	2	14
Manispaa ya Ilala	22	3	14
Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni	20	2	6
Halmashauri ya Jiji la Dodoma	8	1	7
Halmashauri ya Jiji la Arusha	11	1	6
Halmashauri ya Wilaya ya Muleba	2	0	5
Halmashauri ya	6	0	5

Jina la Halmashauri	Idadi ya Wadhibiti Ubora wa Shule	Wadhibiti Ubora wa Shule wenye Taaluma ya Elimu Maalumu	Idadi ya Shule Maalumu
Mji Njombe			
Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe	6	3	1
Halmashauri ya Wilaya ya Lindi	5	0	3
Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba	3	1	3
Halmashauri ya Wilaya ya Bahi	8	2	2
Halmashauri ya Manispaa ya Lindi	4	0	1

Chanzo: *Ofisi za wadhibiti ubora wa shule katika halmashauri*

Jedwali 6.5 inaonesha upungufu wa wadhibiti ubora wa shule wenye taaluma ya elimu maalumu. Halmashauri ya Mji Njombe, Manispaa ya Lindi, Wilaya ya Lindi, na Wilaya ya Muleba hazikuwa na wadhibiti ubora wa shule wenye taaluma ya elimu maalumu ingawa wana shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Halmashauri zilizobaki zilikuwa na angalau mthibiti ubora mmoja mwenye taaluma ya elimu maalumu ikilinganishwa na idadi ya shule za elimu maalumu.

6.2.2 Utekelezaji Hafifu wa Mapendekezo ya Wadhibiti Ubora wa Shule

Kwa mujibu wa muundo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, wadhibiti ubora wa shule ngazi ya halmashauri wana jukumu la kukagua shule za msingi na kutoa mapendekezo ili kuleta maboresho.

Mahojiano na wadhibiti ubora wa shule katika halmashauri zilizotembelewa yalibaini kuwa, halmashauri na OR-TAMISEMI huwa hawatekelezi ipasavyo mapendekezo yanayotolewa kwenye kaguzi zao za shule. Pia, mapitio ya taarifa za ukaguzi wa shule za msingi zilizotembelewa yalionesha kuwa idadi ndogo ya mapendekezo ilitekelezwa ipasavyo, kama inavyooneshwa katika **Jedwali 6.6.**

Jedwali 6.6: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa ili Kuboresha Elimu Maalumu katika Shule Zilizotembelewa

Jina la shule	Hali ya Utekelezaji			Asilimia ya mapendekezo yasiyo tekelezwa
	Mapendekezo yaliyotolewa kuhusu elimu maalumu	Mapendekezo yaliyo tekelezwa	Mapendekezo yasiyo tekelezwa	
Hombolo	1	1	0	0
Mtendeni	4	3	1	25
Themi	7	4	3	43
Mugeza Mseto	6	3	3	50
Kaloleni	9	3	6	67
Ilembula	4	1	3	75
Kambarage	1	0	1	100
Kibena	1	0	1	100
Kaigara	3	0	3	100
Kigwe Viziwi	2	0	2	100
Jumla	**38**	**15**	**23**	**61**

Chanzo: *Uchamuzi wa Taarifa za Kaguzi Zinazofanywa na Wadhibiti Ubora wa Shule*

Jedwali 6.6 linaonesha kuwa kati ya mapendekezo 38 ambayo yalitolewa kuhusu kuboresha elimu maalumu, ni mapendekezo 15 tu ndiyo yalitekelezwa. Mapendekezo 23 ambayo ni sawa na asilimia 61 ya mapendekezo yote yaliyotolewa hayakutekelezwa ipasavyo.

Kushindwa kutekeleza mapendekezo ipasavyo kulichangiwa na kukosekana kwa utaratibu wa kuhakikisha mapendekezo yanatekelezwa na hivyo kuweza kusababisha upotevu wa rasilimali za serikali zinazotumika kuhakikisha ukaguzi unafanyika. Pia, kushindwa kutekeleza mapendekezo ipasavyo kunasababisha kutokuwepo kwa maboresho katika kufundisha na kujifunza wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

6.4 Utungaji na Usimamizi wa Mitihani kwa ajili ya Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania hawatungi na kusimamia ipasavyo mitihani kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Hii ni kwa sababu zifuatazo:

6.4.1 Kukosekana kwa Mwongozo wa Namna ambavyo Wanafunzi wenye Ulemavu wa Kuona Watafanya Mitihani kwa Masomo ya Hisabati na Sayansi

Kanuni ya 29(3) ya Kanuni za Mitihani za Mwaka 2016 inamtaka waziri wa elimu kuandaa namna bora ambayo itawawezesha wanafunzi wenye ulemavu wa kuona kufanya mitihani ya masomo ya hisabati na sayansi.

Mahojiano na maofisa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yalibaini kuwa Wizara haikuandaa namna bora ya kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu wa kuona kufanya mitihani ya masomo ya hisabati na sayansi. Hali hii inawanyima fursa wanafunzi hao kutumia vifaa wezeshi kama vile abakasi ambavyo huwasaidia wakati wa kukokotoa mahesabu.
Walimu wa elimu maalumu katika Shule za Msingi Mugeza Mseto, Kibena, Ilembura na Nyangao waliohojiwa walionesha kuwa kukosekana kwa namna bora ya kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu wa kuona kufanya mitihani ya hisabati na sayansi ni changamoto kubwa kwa wanafunzi hao, kwa sababu hawawezi kukokotoa hesabu kwa namna ya kawaida kama wanafunzi wengine, na hivyo matokeo yao katika masomo hayo huwa si mazuri.
Mapitio ya matokeo ya mitihani ya wanafunzi wenye ulemavu wa kuona yalibaini kuwa, wastani wa ufaulu wa wanafunzi hao huwa ni daraja “D” kwenye somo la hisabati, na daraja “C’ kwenye somo la sayansi.

6.4.2: Usimamizi wa Mitihani Usioridhisha kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Waraka wa Serikali Na. 11 wa Mwaka 2011 unataka wasimamizi wa mitihani wawe na uelewa na taaluma ya kila aina ya ulemavu ili kusaidia urahisi wa mawasiliano na watahiniwa wenye mahitaji maalumu.
Mapitio ya taarifa za utekelezaji wa mitihani kutoka kwenye halmashauri zilizotembelewa yalionesha kuwa wasimamizi waliosimamia wanafunzi wa elimu maalumu hawakuwa na taaluma na uelewa wa elimu maalumu.

Jedwali 6.7 ilionesha hali ya sifa za wasimamizi wanaosimamia mtihani wa kumaliza elimu ya msingi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Jedwali 6.7: Hali ya Uzingatiaji wa Sifa za Wasimamizi Wanaosimamia Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Jina la Shule	Mwaka wa Mtihani wa Darasa VII ✓ = Walifuata X = Hawakufuata HA[8]=Haihusiki				
	2014	2015	2016	2017	2018
Kaloleni	X	X	HA	HA	HA
Meru	X	X	X	✓	✓
Mugeza Mseto	HA	HA	✓	✓	✓
Mpilipili	HA	X	HA	X	HA
Themi	HA	HA	HA	✓	✓
Ilembula	HA	HA	HA	✓	HA
Kibena	HA	HA	HA	X	HA
Nyangao	X	HA	X	X	✓
Kigwe Viziwi	✓	✓	✓	✓	✓
Hombolo	✓	HA	HA	HA	X

Chanzo: *Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mitihani Mwaka 2014 Hadi 2018*

Jedwali 6.7 linaonesha kuwa, kwa miaka yote mitano kuanzia mwaka 2014 hadi 2018, kulikuwa na wanafunzi waliosimamiwa na wasimamizi wasiokuwa na taaluma ya elimu maalumu. Ni Shule ya Msingi Kigwe Viziwi tu ndiyo ilisimamiwa na wasimamizi wenye taaluma ya elimu maalumu kwa kipindi chote cha ukaguzi. Hali hii inatokana na Kigwe Viziwi kuwa shule maalumu kwa wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia.

Hali ya shule kusimamiwa na wasimamizi wasio na taaluma ya elimu maalumu hupelekea wasimamizi kushindwa kuwasiliana vizuri na watainiwa, hivyo kushindwa kuwasaidia wanapokuwa na shida. Wakati mwingine, wasimamizi huhitaji msaada kutoka kwa walimu, kitendo kinachoweza kuhatarisha mazingira ya mtihani unavyofanyika.

[8]Inamaanisha kuwa, katika shule husika hakukuwa na wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanaofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka huo.

6.4.3 Usahihishaji wa Mitihani Haukuzingatia Ipasavyo Mahitaji Maalumu

Waraka wa Serikali Na.11 wa Mwaka 2011 unaelekeza usahihishaji wa mitihani kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu uhusishe walimu wenye taaluma ya elimu maalumu.

Hata hivyo, ukaguzi uliofanya ulibaini kuwa usahihishaji wa mitihani ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu haukuzingatia ipasavyo mahitaji maalumu ya wanafunzi hao. Hii ni kwa sababu hakukuwa na ushahidi wowote kudhibitisha kuwa walimu maalumu walihusishwa katika kusahihisha mitihani ya wanafunzi wenye ulemavu wa akili na kusikia.

Pia, ilibainika kuwa usahihishaji wa mitihani ya wanafunzi wenye ulemavu wa kuona ulihusisha kwanza kutafsiri mitihani ya wanafunzi hao kutoka nukta-nundu kwenda lugha ya kawaida kabla ya kuanza kusahihishwa. Hali hii haina ulazima na ingeweza kuepukwa kwa kuhakikisha kuna idadi ya kutosha ya walimu wa elimu maalumu ili kuwezesha mitihani hiyo kusahihishwa moja kwa moja na walimu wenye taaluma ya elimu maalumu ya kusoma nukta-nundu kwa wanafunzi wenye ulemavu wa kuona.

SURA YA SABA

UTOAJI WA MAFUNZO KWA WALIMU KAZINI

7.1 Utangulizi

Sura hii inahusu matokeo ya ukaguzi wa ufanisi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuwajengea uwezo walimu walio kazini.

Ujengaji uwezo kwa walimu walio kazini ni utaratibu wa kimkakati wa kuwapatia walimu maarifa na ujuzi unaowasaidia kuboresha mbinu za kufundisha na kusaidia wanafunzi kujifunza kwa ubora. Kuwajengea walimu uwezo kumegawanyika katika aina kuu mbili. Aina hizi ni pamoja na utoaji wa mafunzo, semina, warsha, na ulezi wa kitaaluma. Aina nyingine ya ujengaji wa uwezo ni kupitia utoaji wa miongozo, na machapisho mbalimbali yanayosaidia ukuaji endelevu wa taaluma ya walimu.

Mwongozo wa Taifa wa Mtaala wa Elimu Msingi na Elimu ya Ualimu unasisitiza umuhimu wa kuwajengea uwezo walimu. Mwongozo unaeleza kuwa ili kutekeleza mtaala na kuboresha sekta ya elimu, walimu ni nguzo muhimu, hivyo ni muhimu walimu walio kazini kupatiwa mafunzo ya ziada na maarifa ili kuwajengea uwezo hasa katika mbinu za kufundishia.

7.2 Msukumo wa Ukaguzi

Ingawa Serikali imefanya juhudi nyingi katika kuimarisha maarifa na ujuzi wa walimu walio kazini, bado kumekuwepo na changamoto kadhaa zinazoonekana kuhusiana na kuwajengea uwezo walimu walio kazini. Chanagamoto hizi zilipelekea Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa ufanisi katika programu za kuwajengea uwezo walimu walio kazini.

Baadhi ya changamoto zilizosababisha ukaguzi huu ni pamoja na mafunzo kutolewa kwa walimu wachache na kiasi cha bajeti finyu ambacho kimekuwa kikitengwa ili kuwajengea uwezo walimu walio kazini.

7.3 Hoja za Ukaguzi

Sehemu hii inaeleza hoja kuu za ukaguzi kuhusiana na ufanisi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuwajengea uwezo walimu walio kazini.

7.3.1 Kiwango Kisichoridhisha cha Kuwajengea Uwezo Walimu Walio Kazini

Ingawa Serikali ilifikia lengo ililojiwekea la kuwajengea uwezo walimu kwa asilimia 98, ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI zilijiwekea lengo la kuwajengea uwezo walimu 32,314 ambao ni sawa na asilimia 18 tu ya walimu 179,341 wa shule za msingi kaika kipindi cha kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2018/19.

Halikadhalika ukaguzi ulibaini kuwa mafunzo yaliyotolewa kwa walimu walio kazini yalijikita zaidi katika ufundishaji wa kusoma, kuandika na kuhesabu kwa darasa la I na la II. Takribani walimu 147,027 hawakupatiwa mafunzo. Hawa ni walimu wanaofundisha masomo mengine kuanzia darasa la IV-VII, ambao ni sawa na asilimia 82 ya walimu wote.

Kupitia mradi wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu inayofadhiliwa na Uswidi (LANES) na Programu ya Uboreshaji wa Elimu (EQUIP), Serikali ilijiwekea lengo la kuwajengea uwezo walimu 2 katika kila shule kote nchini hususani walimu wanaofundisha darasa la kwanza hadi la tatu. Katika ngazi ya sekondari, kwa kupitia programu ya STEP, Serikali ilikusudia kuwapa mafunzo walimu 4 kutoka kila shule kote nchini. Ukaguzi ulibaini kuwa utoaji wa mafunzo ulikuwa na mapungufu yafuatayo.

(i) Idadi Ndogo ya Walimu wa Sekondari Ndio Waliopatiwa Mafunzo

Ukaguzi ulibaini kwamba mafunzo kwa walimu wa sekondari yalitolewa kitaifa kwa mwaka wa fedha 2015/16 pekee kupitia programu ya uboreshaji wa elimu ya sekondari ambayo ilikuwa sehemu ya mkamkati wa Matokeo Makubwa Sasa. Hata hivyo, mafunzo hayo yalitolewa kwa walimu wa masomo ya Kiswahili, Kiingereza, hisabati, na biolojia tu. Walimu wanaofundisha masomo mengine tofauti na hayo hawakupatiwa mafunzo.

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na mwendelezo wa programu kwa kipindi cha miaka iliyofuatia kutokana na kukosekana kwa mipango endelevu katika utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini. **Kielelezo 7.1** kinatoa muhtasari wa hali ya mafunzo ngazi ya taifa.

Kielelezo 7.1: Hali ya Mafunzo ya Walimu Ngazi ya Taifa



Chanzo: *Takwimu za Elimu ya Msingi (2015-2018), Mpango wa Kuimarisha Walimu wa Wanafunzi (Ripoti za STEP, 2016) na Ripoti za Mafunzo kutoka ADEM*

Ingawa lengo lilifikiwa katika kuwajengea uwezo walimu wa shule za msingi, idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo ilikuwa ya walimu wa madarasa ya awali, la kwanza na la pili pekee. Kwa upande wa elimu ya sekondari, takribani asilimia 77 ya walimu waliokusudiwa walijengewa uwezo. Halikadhalika ilionekana kuwa asilimia 19 ya walimu wote wa sekondari wapatao 75,127 ndio walikusudiwa kujengewa uwezo katika kipindi cha mwaka 2015/16 kote nchini. Ukaguzi ulibaini kuwa kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2018/19 hakukuwa na programu yoyote ya kitaifa iliyojielekeza kuwajengea uwezo walimu wa shule za sekondari.

(ii) Idadi Ndogo ya Walimu Walipatiwa Mafunzo katika Mikoa Iliyotembelewa

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu (TEA) pamoja na Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu (ADEM) Serikalini kwa shule za msingi ilifanikiwa kufikia lengo la kuwajengea uwezo walimu kutoka mikoa miwili (2) kati ya mikoa mitano (5) iliyotembelewa, sawa na asilimia 40. Kwa upande wa sekondari, katika mikoa iliyotembelewa lengo la kuwajengea uwezo walimu lilifikiwa katika mkoa mmoja tu sawa na silimia 20. Mikoa ambayo haikufikia lengo kwa upande wa shule za msingi ni Arusha, Katavi na Geita ilihali katika sekondari mkoa pekee uliofikia lengo ni Katavi huku iliyosalia ikiwa haijafikia lengo kama inavyoonekana katika **Kielelezo 7.2**.

Kielelezo 7.2: Hali ya Utoaji wa Mafunzo katika Mikoa Iliyotembelewa(2018/19)



***Chanzo**: Takwimu za Elimu Msingi (2015-2018) na Taarifa za Elimu za Mikoa (2015/16-2018/19)*

Kielelezo 7.2 kinaonesha kwamba ukiachilia Mikoa ya Geita, Katavi na Arusha ambako malengo ya kuwajenga uwezo walimu yalifikiwa kwa kiwango cha chini ya asilimia 50, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI walifanikiwa kufikia malengo ya kuwajengea uwezo walimu katika mikoa ya Singida na Lindi.

Sababu za kutofikia lengo katika mikoa tajwa ni pamoja na wawezeshaji wa mikoa ambao walitakiwa warithishe maarifa hayo katika ngazi za chini hawakuelekeza wajibu wao ipasavyo. Hii ilitokana na uratibu usioridhisha katika ngazi za wilaya hadi kata ili kutoa fursa kwa wawezeshaji kutoa mafunzo kwa walimu.

Mchanganuo kama huo pia ulifanyika kwa viongozi wa elimu katika ngazi za kata na wilaya waliopatiwa mafunzo. Viongozi hawa ni pamoja na waratibu elimu kata, maofisa elimu na maofisa taaluma wa wilaya. Matokeo ya uchambuzi huo yanaonekana katika **Kielelezo 7.3.**

Kielelelzo 7.3: Maofisa Waliopatiwa Mafunzo katika Halmashauri Zilizotembelewa kuanzia Mwaka 2015/16-2018/19)



***Chanzo**: Mchanganuo wa Taarifaza Mafunzo katika Halmashauri Zilizotembelewa Mwaka 2019*

Kielelezo 7.3 kinaonesha idadi ya jumla ya maofisa waliokusudiwa kujengewa uwezo ikilinganishwa na idadi halisi ya waliopatiwa mafunzo katika halmashauri 10 zilizotembelewa. Kielelezo kinaonesha kwamba zaidi ya robo tatu ya maofisa wote katika halmshauri hizo walipatiwa mafunzo.

(iii) Ujengaji Uwezo kwa Walimu Haukufanyika kwa Masomo Yote

Mapitio ya taarifa mbalimbali za mafunzo kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na OR-TAMISEMI yalibaini kwamba mafunzo mengi yaliyotolewa katika kipindi hiki yalihusu zaidi stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu na si kwa masomo yote ya ufundishaji. Mafunzo haya yaliyotolewa

zaidi kwa walimu waliofundisha masomo hayo katika shule za msingi na hivyo kuwaacha bila kupatiwa mafunzo walimu wengi wanaofundisha masomo mengine kuanzia darasa la III-VII.

Hata hivyo, mapitio ya taarifa za Programu ya Kuboresha Hali ya Wanafunzi na Walimu yalibaini kuwa jumla ya walimu walio kazini 538 wa shule za msingi na walimu 597 wa sekondari walipatiwa mafunzo katika somo la hisabati.

Pia, jumla ya walimu 134 wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu mbalimbali za ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Aidha, walimu 186 walipatiwa mafunzo ya namna ya kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kutumia zana za kiteknolojia.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa progamu mbalimbali za kuwapatia walimu mafunzo hazikuzingatia masomo mengine yanayofundishwa katika shule za msingi na sekondari. Baadhi ya masomo yakiwemo ya maarifa ya jamii na masomo ya sanaa kama vile historia na jiografia hayakuhusishwa katika mafunzo. Ikizingatiwa kwamba katika baadhi ya masomo kama Kiswahili na Kiingereza kumekuwa na mada mpya kama vile ukalimani na tafsiri pamoja na mada ya uchumi wa kimazingira katika somo la uchumi ni muhimu walimu wa masomo hayo wakapatiwa mafunzo ili kuongeza maarifa katika ufundishaji wao.

Jedwali 7.1 linatoa muhtasari wa programu nne ambazo zilitekelezwa katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2018/19. Kwa kupitia programu hizi ukaguzi ulibaini kuwa mafunzo yaliyotolewa yalijikita katika maeneo ya umahiri wa masomo machache.

Jedwali 7.1: Aina za Mafunzo yaliyotolewa kwa Walimu

Jina la Programu	Lengo	Waliokusudiwa
LANES	Kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa KKK kwa watoto wa kati ya miaka 5 na 13. Kuboresha usimamizi wa sekta ya elimu na kuongeza ushiriki wa jamii katika kuinua kiwango cha kusoma, kuandika na kuhesabu	Walimu wa shule za msingi
EQUIP-T	Kuinua ufundishaji na ujifunzaji katika hatua za awali za elimu ya msingi kwa kuwajengea uwezo walimu, walimu wakuu, na waratibu elimu kata	Walimu wa shule za msingi
TUSOME PAMOJA	Kuinua kiwango cha elimu ya msingi katika madarasa ya chini; kuimarisha umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunza; na kuinua kiwango cha ushiriki wa wazazi katika masuala ya elimu	Walimu wa shule za msingi
STEP	Kuimarisha mafunzo kwa walimu wanaofundisha masomo ya sayansi, hisabati, Kiingereza na Kiswahili	Walimu wa shule za msingi

***Chanzo**: Taarifa za Utekelezaji wa Programu Nne kuanzia Mwaka 2015-2018*

Ukaguzi ulibaini kuwa sababu za kuweka msisitizo zaidi katika kutoa mafunzo ya kusoma, kuandika na kuhesabu ni mahitaji ya miradi iliyofadhiliwa na mashirika mbalimbali. Kutokana na hali hiyo, walimu wengi ambao hawakupatiwa mafunzo wanakosa umahiri katika mbinu mpya za kufundishia hasa katika kufundisha na kufikia malengo ya mitaala mipya ya ufundishaji kwa kuzingatia umahiri, na kufahamu mabadiliko mbalimbali yanayotokea katika ufundishaji na mabadiliko ya kiteknolojia.

(iv) Ujengaji wa Uwezo Uliofanyika Haukuzingatia Mahitaji yote ya Kitaaluma

Mafunzo yaliyotolewa kwa walimu walio kazini hayakujumuisha mahitaji yote ya kitaaluma ya walimu. Ukaguzi ulibaini kuwa mafunzo yaliyotolewa kwa walimu walio kazini hayakuzingatia baadhi ya mahitaji ya kitaaluma kama inavyoonekana katika **Jedwali 7.2.**

Jedwali 7.2: Maudhui ya Mafunzo Mbalimbali Yaliyotolewa

Programu	Mahitaji ya Kitaaluma				
	Mbinu za Ufundishaji	Maarifa ya somo husika	Upimaji	Udhibiti wa Darasa	Uongozi wa Shule
LANES	√	√	x	x	√
EQUIP-T	√	√	x	√	√
TUSOME PAMOJA	√	√	x	X	√
STEP	√	√	x	x	x

Chanzo: *Mapitio ya Taarifa za Mafunzo kuanzia Mwaka 2015/16-2018/19*

Katika programu zote nne zilizotekelezwa nchini, ukaguzi ullibaini kwamba kulikuwepo na mafunzo yaliyohusu mbinu za kufundshia mtaala ulioboreshwa unaozingatia umahiri katika kufundisha na kujifunza. Hata hivyo, pamoja na kwamba walimu wanafahamu kuwepo kwa mtaala mpya ambao mwanafunzi ni shabaha ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mapitio ya taarifa za ukaguzi yalibaini bado kuna mapungufu katika ufundishaji kwa kutumia mbinu zinazobainishwa katika utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa.

Sababu kubwa iliyopelekea udhaifu katika utekelezaji wa mtaala ni pamoja na wingi wa wanafunzi katika madarasa hivyo kupelekea ugumu kwa walimu kutumia mbinu shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Picha 7.1: Mrundikano wa zaidi ya wanafunzi 150 katika darasa moja kama ilivyoshuhudiwa na timu ya ukaguzi katika Shule ya Msingi Ukombozi katika Halamshauri ya Mji wa Geita (Picha ilipigwa tarehe 14.01.2020)

Baaadhi ya sababu zilizopelekea mafunzo yaliyotolewa yasizingatie mahitaji yote kitaaluma ni pamoja na zifuatazo:

7.3.2 Walimu Walio Kazini Hawapatiwi Mafunzo Endelevu ya Kitaaluma

Ukaguzi ulibaini kuwa ni nadra sana walimu walio kazini walipatiwa mafunzo endeleveu ya kitaaluma kupitia usaidizi wa wadhibiti ubora wa shule. Hii ni kutokana na kwamba wadhibiti ubora nao wamekuwa hawapatiwi mafunzo hayo kwa wakati. Hali hii inawafanya wawe nyuma kimaarifa ikilinganishwa na baadhi ya walimu waliopata fursa ya kuhudhuria mafunzo. Hili hii ilisababisha wadhibiti ubora kushindwa kutekleza majukumu yao ya kuwasaidia walimu kuendana na mabadiliko mbalimbali yanajitokeza katika utekelezaji wa mtaala.

Utoaji wa usaidizi wa kitaaluma ulisababishwa na mambo makuu yafuatayo:

(i) Usaidizi wa kitaaluma kupitia wadhibiti ubora ulifanyika kwa nadra

Ukaguzi ulibaini kuwa ingawa katika shughuli za kawaida, wadhibiti ubora wanapaswa kuwapa walimu msaada wa kitaaluma ili kuinua uelewa wao katika mambo mbalimbali ya taaluma ya ualimu, msaada huo huo haukuwa ukitolewa ipasavyo na wadhibiti ubora.

Katika halmashauri kumi zilizotembelewa, wadhibiti ubora walikiri kuwa usaidizi huo haufanyiki ipasavyo na umekuwa ukitolewa mara chache kupitia mijadala kati ya walimu na wadhibiti ubora ambayo ilijielekeza zaidi katika kuboresha mbinu za ufundishaji.

Hali hii inatokana na mafunzo mengi yalianza kutolewa kwanza kwa walimu kabla ya wadhibiti ubora na hivyo kupelelea wadhibiti ubora kubaki nyuma kimaarifa. Pia, muda unaotengwa kwa ajili ya shughuli za udhibiti ubora kwa shule ni mchache kuweza kupata fursa ya kuendesha mijadala na walimu kuhusu ufundshaji. Hii inatokana na idadi ndogo iliyopo ya wadhibiti ubora ikilinganishwa na idadi ya shule wazozihudumia katika eneo husika.

(ii) Ushauri wa kitaaluma haukutolewa vyema na waratibu elimu na wakuu wa shule

Ukaguzi ulibaini kuwa ujengaji wa uwezo kwa njia ya ushauri elekezi kwa walimu wasio na uzoefu haukuwa unafanyika vyema. Hii ni kutokana na kutokuwepo kwa mfumo wa kuwasaidia walimu wapya au wasio na uzoefu katika kuelewa mazingira ya kazi na kupata mbinu bora za kumudu madarasa yao ipasavyo. Hili lilithibitika kupitia mahojiano kati ya timu ya ukaguzi na walimu wakuu 40 wa shule mbalimbali katika halmshauri 10 zilizotembelewa.

Ukaguzi ulibaini kuwa ni katika shule 4 tu kati ya shule 40 za msingi na sekondari zilizotembelewa ndio ambazo kulikuwa na usaidizi wa kitaaluma kwa njia ya ushauri wa kitaaluma kutoka kwa walimu wakuu na walimu wengine wenye uzoefu zaidi.

Hata hivyo katika shule hizo ambazo usaidizi wa kitaaluma ulikuwepo, timu ya kaguzi ilibaini baadhi ya kasoro. Kasoro hizo ni pamoja na usaidizi kutofanyika kimwendelezo. Hakukuwa na mpango maalumu wa kuhakikisha kuwa utaratibu huo unakuwa edelelevu. Pia, hakukuwa na mfumo ulioweza kubaini iwapo walimu walikokuwa wakipatiwa usaidizi wamemudu vyema maeneo husika waliyokuwa wanapatiwa usaidizi huo.

Mapitio ya kumbukumbu za shughuli za waratibu elimu kata yalionesha kuwa wamekuwa wakitembelea shule zilizoko ndani ya maeneo yao ya

kiuongozi lakini shughuli zao za kufuatilia maendeleo ya shule hayakuhusisha kuwajengea uwezo walimu kwa njia ya ushauri au majadiliano.

Sababu za kutokuwepo kwa huduma saidizi za ushauri wa kitaaluma kwa walimu walio kazini ni pamoja na wasimamizi wa utekelezaji wa mitaala kuanzia ngazi ya shule kutofanya uchambuzi wa kina kuhusu mahitaji mahususi ya kitaaluma ya walimu ili kubaini maeneo yenye changamoto na yanayohitaji usaidizi wa ndani ya shule. Sababu nyingine ni kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haijatoa mwongozo wa namna usaidizi huu wa kitaaluma kuanzia ngazi ya shule utakavyofanyika na kutoa taarifa kwa ajili ya maboresho.

Kutokana na hali hiyo, walimu wameshindwa kuendana na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia; matokeo yake maarifa yao ya mbinu za kufundishia katika baadhi ya maeneo kupitwa na wakati.

7.3.3 Kukosekana kwa Mipango Endelevu ya Kuwajengea Uwezo walimu walio Kazini

Sera ya Elimu ya Mwaka 1995 inazielekeza Wizara ya Elimu na OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa mafunzo kwa walimu kazini yanatolewa kwa ulazima. Hii itapelekea kuwepo kwa ukuaji endelevu wa kitaaluma kwa walimu na hivyo kuinua kiwango cha ubora na weledi.

Ukaguzi ulibaini kukosekana kwa mpango endelevu wa mafunzo kwa walimu kazini. Pamoja na kuwa katika hatua za kuandaliwa, mpango huo utahakikisha kuna mwendelezo na utatoa mwelekeo bayana kuhusu masuala ya kitaalamu katika kutoa programu za mafunzo ya ujenzi wa uwezo kwa walimu walio kazini.

Pamoja na kujumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu (ESDP 2016/17-2020/21) wa Wizara ya Elimu, mipango ya kuwajengea uwezo walimu walio kazini kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI ilitegemea zaidi programu zinazofadhiliwa na wadau wa maendeleo kama vile mradi wa kusoma, kuandika na kuhesabu (LANES), programu ya uwezeshaji wa walimu (EQIUP-T), na TUSOME PAMOJA. Ukaguzi katika halmashauri 10 zilizotembelewa ulibaini udhaifu katika vipaumbele vya mipango amabapo hakukuwa na shughuli za utoaji wa

mafunzo kwa walimu walio kazini zilizowekwa katika mipango ya mwaka ya halmashauri hizo.

Kutokana na hali hiyo, walimu wamekuwa wakiajiriwa na wengi wao huanza kutekeleza majukumu yao bila kupatiwa hata mafunzo karibishi au usaidizi elekezi ambao ungewasaidia kujua namna mbalimbali za kukabiliana na changamoto za kitaaluma katika mazingira halisi ya kazi.

7.3.4 Kukosekana kwa Mkakati wa Kitaifa wa Kuwajengea Uwezo Walimu Walio Kazini

Maofisa katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI walionesha kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye jukumu la kuandaa sera na miongozo mbalimbali ya kielimu haikuwa imeandaa mpango endelevu wa mafunzo kwa walimu kazini hadi wakati wa ukaguzi huu.

Kukosekana kwa mpango wa mafunzo endelevu kwa walimu kunatokana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikutumia ipasavyo matokeo ya mapitio ya Mpango wa Maendeleo ya Taaluma ya Ualimu uliopita (TDMS, 2008-2013) ili kuandaa mpango mpya baada ya ule wa mwanzo muda wake kumalizika.

Kukosekana kwa mpango-mkakati wa kuwajengea uwezo walimu kumepelekea suala la kuwajengea uwezo walimu kutopewa kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu (ESDP 2017/18 - 2020/21).

7.3.5 Kukosekana kwa Mikakati Endelevu ya Kibajeti Kusaidia Ujengaji Uwezo kwa Walimu

Sera ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 1999 (na maboresho ya mwaka 2008) inaelekeza OR-TAMISEMI ihakikishe inabuni mipango na kutenga bajeti kwa ajili ya kuwajengea uwezo walimu. Hata hivyo, mapitio ya bajeti kutoka OR-TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, sekretarieti za mikoa na halmashauri mbalimbali zilizotembelewa yamebaini kwamba hakukuwa na bajeti ya kutosha iliyotengwa kwa ajili ya mafunzo kwa walimu walio kazini isipikuwa sehemu kubwa ya bajeti ya mafunzo kwa walimu ilitokana na michango ya wafadhili. Ufafanuzi zaidi ni kama inavyoelezwa hapa chini.

(i) ***Kiwango cha bajeti kisichoridhisha katika kuwajengea uwezo walimu walio kazini***

Ilibainishwa kuwa, kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2018/19, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI zilitenga bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 19.9 kwa ajili ya kuwajengea uwezo walimu walio kazini. Kupitia bajeti hiyo, Serikali ilikusudia kujengea uwezo walimu 32,314 walio kazini wanaofundisha madarasa ya awali na msingi (awali na darasa la I-IV) . Bajeti hiyo ilitosha kuwezesha kufikia lengo kwa sababu walimu 31,824 walio kazini sawa na asilimia 98.4 walipatiwa mafunzo ya kujengewa uwezo.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa idadi iliyokusudiwa ya walimu kwa ajili ya mafunzo ilikuwa asilimia 18 tu ya jumla ya walimu 179,341 wa shule za msingi. Bajeti iliyotengwa iliwezesha kufikia lengo lililowekwa, ingawa walimu 147,027 sawa na asilimia 82 ya walimu wote wa shule za msingi wanaofundisha madarasa ya juu (darasa la V-VII) waliachwa bila kupewa mafunzo. **Jedwali 7.3** linatoa muhtasari wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za mafunzo kupitia mpango wa LANES kati ya miaka ya fedha 2015/16 na 2018/19.

Jedwali 7.3: Fedha Zilizotolewa kwa ajili ya Mafunzo ya Walimu Walio Kazini

Mwaka wa Fedha	Bajeti Iliyotengwa (kwa bilioni Tsh)	Shughuli za Mafunzo	Chanzo cha Fedha
2015/2016	5.4	Maandalizi ya vifaa vya mafunzo na kupanga mafunzo	Chanzo cha Nje (GPE-LANES)
2016/2017	7.0	Utoaji wa mafunzo kwa wakufunzi wa wakufunzi na kushusha chini kwa walimu wa darasa la I-III	Chanzo cha Nje (GPE-LANES)
2017/2018	5.3	Utoaji wa mafunzo ya walimu walio kazini wa darasa la awali, na	Chanzo cha Nje (GPE-LANES)

Mwaka wa Fedha	Bajeti Iliyotengwa (kwa bilioni Tsh)	Shughuli za Mafunzo	Chanzo cha Fedha
		daraja la I-II kuhusu mtaala uliofanyiwa marekebisho	
	2.2	Utoaji wa mafunzo kwa walimu wa darasa la I-IV kuhusu elimu wanafunzi wenye mahitaji maalumu	Chanzo cha Nje (GPE-LANES)
2018/2019	Hakuna	Hakuna	Hakuna

Chanzo: *Bajeti* ya Wizara *ya Elimu, Sayansi na Teknolojia* kwa Miaka *2016/17 na 2018/19*

Jedwali 7.3 linaonesha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilikuwa imetenga bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 19.9 kwa ajili ya mafunzo ya walimu walio kazini lakini wizara ilijielekeza zaidi kutoa mafunzo kwa walimu wa awali na darasa la I-IV hasa kwa stadi za kusoma, kuandika, na kuhesabu. Licha ya jitihada hizo za Serikali, hakukuwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya masomo mengine ambayo hatimaye yangechangia kuongeza uwezo wa walimu wote walio kazini. Uamuzi huu ni kinyume na Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu – II, ambao unazitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI kuanzisha, kuendeleza, na kuhamasisha rasilimali kwa ajili ya kuwajengea uwezo walimu wa shule za msingi na sekondari.

Sababu ya bajeti isiyotosheleza kuhudumia kuwajengea uwezo walimu wengi zaidi walio kazini ni ukweli kwamba hakukuwa na mpango endelevu wa kitaifa wa kujenga uwezo ambao ulijumuisha walimu wote. Badala yake kuwajengea uwezo walimu kulitegemea zaidi miradi inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo kama vile LANES, EQUIP-T na TUSOME PAMOJA ambayo miongoni mwa mambo mengine ilitenga fedha kwa ajili ya mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu walio kazini.

Utegemezi wa fedha za wadau wa mendeleo una uwezekano wa kuathiri uendelevu wa matokeo ya mafunzo ya ujenzi wa uwezo ambayo tayari yameshatolewa kwa walimu walio kazini.

(ii) ***Bajeti Zisizoridhisha za Ujenzi wa Uwezo katika Taasisi ya Elimu Tanzania na Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu***

Mapitio ya taarifa za upangaji wa bajeti na mafunzo za Taasisi ya Elimu Tanzania ulionesha kuwa katika miaka ya fedha 2015/16 na 2016/17, shilingi bilioni 1.0 na shilingi bilioni 11.9, mtawalia zilitengwa kwa ajili ya mafunzo ya mfunzo kazini.

Hata hivyo, katika miaka wa fedha 2017/2018 na 2018/19, Taasisi ya Elimu Tanzania haikupanga bajeti ya mafunzo, hivyo hakukuwa na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya mafunzo ya walimu walio kazini kwa miaka hiyo miwili ya fedha.

Sababu za Taasisi ya Elimu Tanzania kutokuwa na fedha za bajeti ya mafunzo katika miaka ya fedha 2017/18 na 2018/19 ni jukumu la kuendesha mafunzo kwa walimu walio kazini kukasimiwa kwa Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu. Kutokana na ushirikiano huu, kiasi cha shilingi bilioni 25.4 kwa miaka hii miwili ilitengewa Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu.

Jedwali 7.4: Bajeti ya Mafunzo katika TET na ADEM (katika Bilioni ya Shilingi)

Mwaka wa Fedha	TET		ADEM	
	Kiasi cha Bajeti	Kiasi Halisi	Kiasi cha Bajeti	Kiasi cha Bajeti
2015/16	1.1	12.3	0	0
2016/17	1.0	11.9	0	0
2017/18	0	0	26.4	25.4
2018/19	0	0	0	0

Chanzo: *Ripoti za Mafunzo kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania na Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu, 2019*

Jedwali 7.4 linaonesha kuwa katika miaka ya fedha 2015/16 na 2016/17, Taasisi ya Elimu Tanzania ilipanga na kutumia shilingi bilioni 24.2. Kiasi hiki kilikuwa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa walimu walio kazini, lakini hali ilikuwa tofauti katika miaka miwili iliyofuata ya fedha ambapo hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo. Kwa upande mwingine, Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu ilipanga bajeti na kutumia shilingi bilioni 25.4 kwa ajili ya mafunzo ya walimu walio kazini kwa mwaka wa

fedha 2017/18, lakini mwaka wa fedha 2018/19 hakuna taasisi kati mbili iliyotenga fedha kwa ajili ya mafunzo ya walimu kazini.

Kukosekana kwa uendelevu wa kibajeti na utengaji wa fedha katika Taasisi ya Elimu Tanzania na Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu kulitokana na ukweli kwamba jukumu la kuratibu na kutoa mafunzo ya walimu kazini lilikuwa chini ya Mamlaka ya Elimu Tanzania. Baadaye, Taasisi ya Elimu Tanzania iliendesha mafunzo kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI kwa miaka 2015/16 na 2016/17, lakini katika miaka iliyofuata jukumu hilo lilikasimiwa kwa Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu na hivyo fedha zilielekezwa kwa Wakala.

1. ***Kutokuwepo kwa Fedha za Bajeti kwa ajili ya Mafunzo ya Kuwajengea Uwezo Walimu Walio Kazini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa***

Kupitia ukaguzi wa Mpango wa Utekelezaji wa Mwaka kutoka katika sekretarieti 5 za mikoa na mamlaka 10 za serikali za mitaa zilizotembelewa, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa zilipokea zaidi ya nusu ya kiasi cha bajeti. Hata hivyo, hakuna fedha zilizotengwa kugharimia mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu walio kazini.

Kielelezo 7.4 kinaonesha wastani wa asilimia ya fedha zilizopokelewa kama sehemu ya bajeti zilizotengwa katika mamlaka za serikali za mitaa zote zilizotembelewa na katika shule za msingi na sekondari kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2018/19. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wastani wa fedha zilizopokelewa ni zaidi ya asilimia 65 kwa mamlaka zote za serikali za mitaa zilizotembelewa.

Kielelezo 7.4: Asilimia ya Fedha Zilizopokelewa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zote Zilizotembelewa



***Chanzo**: Bajeti za idara husika katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa kuanzia 2015/16-2018/19*

Ilibainika zaidi kuwa sababu ya kutotengwa fedha kwa ajili ya utoaji wa mafunzo ya kujenga uwezo ni ukosefu wa kipaumbele kilichowekwa katika mamlaka husika za serikali za mitaa.

Hata hivyo, katika mamlaka zote za serikali za mitaa zilizotembelewa, timu ya ukaguzi haikupewa ushahidi wa kuthibitisha kuingizwa kwa shughuli hizi katika makadirio yao ya bajeti hata katika hatua za awali za maandalizi ya bajeti.

7.3.4 Mifumo na Michakato Isiyotosheleza ya Utoaji wa Mafunzo kwa Walimu walio Kazini

Maofisa wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI na sekretariaeti 5 za mikoa pamoja na mamlaka 10 za serikali za mitaa zilizotembelewa walionesha kuwa Wizara hazikuwa zimeandaa ipasavyo miongozo, vifaa vya kujifunzia, programu, na miundo kwa ajili ya utoaji bora wa mafunzo kwa walimu walio kazini. Suala hili linafanunuliwa kama yafuatayo:

(i) Kutofanya Kazi kwa Vituo vya Walimu

Timu ya ukaguzi ilishuhudia kutokuwepo au kutofanya kazi kwa vituo vya walimu vilivyokuwepo. Vituo hivi vya walimu vilitapaswa kutumika ili kuhakikisha utambuzi mzuri wa miundo na michakato ya ufundishaji bora.

Katika mikoa hiyo 5 iliyotembelewa, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa vituo vya walimu vinavyopatikana katika mikoa mingi havikuwa vinafanya kazi

ya kama vituo vya mafunzo kwa walimu walio kazini. Majengo mengi yalitumika kwa matumizi mengine yasiyotarajiwa kama vile vituo vya masomo ya jioni na maduka. **Picha 7.1** inatoa mifano ya vituao ambavyo vilitumika kwa madhumuni mengine:

Picha 7.2(a): Kituo cha walimu kilichopo Wilaya ya Karatu (Arusha) kilichotumika kama stoo ya shule.

Picha 7.2(b): Uendeshaji Kituo cha Walimu cha Nyerere katika Manispaa ya Singida MC kikitumika kama ukumbi wa mkutano wa manispaa na kituo cha masomo ya maarifa (QT).

Picha 7.2(c): Jengo la kituo cha walimu lililopo Halmashauri ya Wilaya Chato ambalo limegeuzwa kituo cha uchapishaji cha halmashauri.

Picha 7.2(d): Jengo la kituo cha walimu lililopo Halmashauri ya Mji Geita ambalo linatumika kama kituo cha masomo ya ziada kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Ukaguzi ulibaini kuwa katika mamlaka zote 10 za serikali za mitaa zilizotembelewa, kati ya vituo 32, ni kituo kimoja tu kijulikanacho kama

Ukaguzi ulibaini kuwa katika mamlaka zote 10 za serikali za mitaa zilizotembelewa, kati ya vituo 32, ni kituo kimoja tu kijulikanacho kama Leganga katika Halmashauri ya Wilaya Meru ndicho kilionekana kufanya kazi na kusaidia shughuli zinazohusiana na mafunzo ya walimu kama ilivyokusudiwa. **Picha 7.3(a)** inaonesha Kituo cha Leganga na walimu wakiwa ndani wakifanya shughuli mbalimbali.

Picha 7.3(a): Jengo la Kituo cha Walimu Leganga kama lilivyoonekana katika Kata ya USA River katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru.

Picha 7.3(b) Uboreshaji wa vifaa vya kufundishia unaofanywa na walimu walio kazini wanaohudhuria Kituo cha Walimu kwa ajili ya kujijengea uwezo

Maofisa wa Wakala wa Maendeleo ya Usimamizi wa Elimu, Taasisi ya Elimu Tanzania, OR-TAMISEMI, na maofisa elimu kata katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa walieleza kuwa sababu ya vituo vya walimu kutofanya kazi ipasavyo ni kutokuwepo kwa wafanyakazi waliopangiwa mahsusi kuratibu na kuwezesha uendeshaji wa vituo hivyo.

taarifa, na ushiriki wenye tija katika kupanga shughuli zinazohusiana na mafunzo ya walimu walio kazini (Sera ya Elimu, 1995).

Ilibainika kuwa uratibu ulifanyika kupitia mifumo ya majadiliano. Katika ngazi ya kitaifa, mifumo hii hujumuisha vikundi-kazi vya wataalamu na Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu; na kupitia ziara za pamoja za ufuatiliaji, na Mapitio ya Pamoja ya Sekta ya Elimu.

Ripoti za robo mwaka za vikundi-kazi vya wataalamu na kamati za maendeleo ya sekta ya elimu (TWGs na ESDC: 2015-2018) zilionesha kuwepo kwa uratibu usioridhisha katika ngazi zote za uendeshaji.

Hii ni kwa sababu ya vikao vyao havikufanyika kama kawaida, ambapo walitakiwa kukutana kila robo mwaka. Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa mambo yanayohusiana na INSET hayakujadiliwa vizuri na kupitisha maamuzi katika mikutano michache ambayo ilifanyika.

Udhaifu katika uratibu ulidhihirishwa na matukio mawili tofauti ambayo yote kwa pamoja yaliathiri ufanisi wa mipango ya kujenga uwezo uliyoanzishwa. Matukio hayo mawili ni:

1. ***Uwepo wa Programu Zisizoratibiwa za Kujenga Uwezo wa Walimu Walio Kazini***

Maofisa wa OR-TAMISEMI, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Taasisi ya Elimu Tanzania, na Wakala wa Usimamizi wa Maendeleo ya Elimu walionesha kuwa kulikuwa na baadhi ya programu ambazo zilitekelezwa bila kuwashirikisha au kuwataarifu wadau muhimu ili watekeleze majukumu yao. Hali hii ilithibitishwa kupitia ukaguzi wa ripoti ya Kikao-kazi cha Mapitio ya Pamoja ya Sekta ya Elimu (2018). Ripoti hiyo ilionesha kuwepo kwa asasi za kiraia ambazo zimekuwa zikitoa aina tofauti za mafunzo kwa walimu walio kazini.

Vilevile, maofisa kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania walithibitisha kuwa programu nyingi zilihuishwa bila kuwajulisha maofisa wa Taasisi hiyo waliopewa mamlaka na Sheria ya Taasisi ya Elimu Tanzania Na. 13 ya Mwaka 1975. Timu ya ukaguzi ilibaini kulikuwa na mafunzo mbalimbali yaliyotolewa na asasi mbalimbali za kiraia katika miaka minne iliyopita. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo walimu katika maeneo

waliopewa mamlaka na Sheria ya Taasisi ya Elimu Tanzania Na. 13 ya Mwaka 1975. Timu ya ukaguzi ilibaini kulikuwa na mafunzo mbalimbali yaliyotolewa na asasi mbalimbali za kiraia katika miaka minne iliyopita. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo walimu katika maeneo mbalimbali, ingawa mafunzo haya hayakuidhinishwa na Taasisi ya Elimu Tanzania kama ilivyotakiwa.

Maofisa wa OR-TAMISEMI walieleza kuwa sababu za mafunzo haya kutekelezwa bila kuhusishwa Taasisi ya Elimu Tanzania ni kutokana na mafunzo haya kimsingi kulenga mikoa au mamlaka mahususi za serikali za mitaa. Kwa kuzingatia hayo, programu hizi zilifanywa kati ya sekretarieti za mkoa au mamlaka husika za serikali za mitaa.

Kwa hiyo, mafunzo hayo yaliyotolewa hayakufanana kutokana na moduli zilizotumika hazikuidhinishwa kabla na Taasisi ya Elimu Tanzania. Matokeo yake, kulikuwa na mbinu tofauti za kufundishia na uelewa wa masuala muhimu katika kufundisha kama vile andalio la somo na upimaji wa wanafunzi wa wanafunzi.

(ii) Utekelezaji Usioridhisha wa Mkabala wa Michakato ya Kujenga Uwezo katika Mazingira ya Shule

Uchambuzi uliofanywa na timu ya ukaguzi ulionesha kuwa mbinu inayotumika haifanyi kazi vizuri katika ngazi za shule. Mafunzo hayo hayakuendeshwa katika ngazi za shule kwenye nyanja mbalimbali. Miongoni mwa mambo yaliyotajwa ni kukosekana kwa taratibu za utekelezaji na motisha ili kuhakikisha kuwa walimu waliopata mafunzo watawafundisha wenzao.

Kwa hiyo, mafunzo yaliyopangwa kuendeshwa kwa siku nne hadi tano yalitolewa haraka kwa siku moja au mbili kwa kutumia saa mbili kila siku ambayo kwa kiasi kikubwa yalipunguza uhalali wa maudhui yaliyowasilishwa.

7.3.7 Kutokuwepo kwa Miongozo ya Kitaifa ya Mafunzo

Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu (2016/17-2020/21) unaitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuandaa na kugawa miongozo ya utoaji wa mafunzo ya kujenga uwezo na kusaidia walimu wote walio kazini. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatakiwa pia kuhakikisha kuwa miongozo iliyobuniwa inatumiwa na watekelezaji wakati wa maandalizi na utoaji wa mafunzo.

Maofisa wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI walionesha kuwa kukosekana kwa Mwongozo wa Kitaifa wa Maendeleo Endelevu ya Kitaaluma (CPD) kulitokana na kukosekana kwa mwendelezo wa mkakati uliomalizika mwaka 2013. Kukosekana kwa Mwongozo wa Kitaifa wa Maendeleo Endelevu ya Kitaaluma kwa walimu kumesababisha utoaji wa zimamoto wa mafunzo ya kujenga uwezo ambayo yanalenga wigo finyu kimawanda, masomo ya kufundishia yaliyohusika, na mahitaji mengine ya kitaaluma kwa walimu.

a) Mipango ya Mafunzo na Vifaa vya Kujifunzia Visivyotosheleza

Sheria ya Uanzishaji wa Taasisi ya Elimu Tanzania Na. 13 ya Mwaka 1975 (Sura ya 142 kama ilivyorekebishwa mwaka 2002) inaitaka Taasisi ya Elimu Tanzania kusanifu, kukuza, na kufanya mapitio ya programu za mafunzo zinazotolewa kwa walimu walio kazini ikiwa pamoja na kuandaa vifaa vya kujifunzia kama vile vitabu na miongozo.

Maofisa wa Taasisi ya Elimu Tanzania wanaofanya kazi chini ya kitengo cha mafunzo ya mitaala walionesha kuwa kwa kushirikiana na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) waliandaa mwongozo wa kitaifa wa maendeleo endelevu ya kitaaluma kwa walimu walio kazini. Mwongozo huu ulipaswa kutumiwa na programu zingine zote zilizokusudiwa kwa walimu walio kazini. Hata hivyo, mwongozo huo haujaidhinishwa kwa matumizi ya wizara na wadau wengine wa elimu. Katika kukabiliana na hili, maofisa wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia walionesha kuwa mwongozo huo iko katika hatua za mwisho za kuidhinishwa. Hata hivyo, maofisa hao hawakuweza kutoa hati yoyote kwa timu ya ukaguzi ili kuthibitisha majibu yao.

SURA YA NANE

UPATIKANAJI WA ELIMU NA MAFUNZO BORA YA UFUNDI STADI

8.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa Mpango wa Kuendeleza Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi wa Mwaka 2013/14-2017/18, elimu na mafunzo ya ufundi stadi ni mfumo unaolengo kuwapatia wanaojifunza ujuzi na maarifa ili waweze kuwa sehemu ya soko la ajira.

Elimu na mafunzo ya ufundi stadi inaiwezesha nchi kufikia malengo ya Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano wa Mwaka 2016/17-2020/21 na kutekeleza vema sera ya maendeleo ya viwanda.

Jukumu la usimamizi wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi ni la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Lengo la ukaguzi huu lilikuwa kufanya tathmini endapo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilihakikisha kwamba Watanzania wanapata elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi ili kukuza maendeleo ya ujuzi na kukidhi mahitaji ya soko la ajira.

Hivyo, sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi kama yalivyoainishwa kwenye malengo ya ukaguzi, hususani kwenye upatikanaji wa ujuzi unaohitajika pamoja na upatikanaji wa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi. Hali inayohusu uwepo wa ujuzi unaotakiwa inaelezewa vema kwa kuangalia ombwe la ujuzi kwenye kada za chini na za kati. Sura hii vilevile, inachambua matokeo kuhusu uwepo wa tija kwenye mfumo wa udhibiti ubora kwenye utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Vilevile, inaangazia tija kwenye ugawaji wa fedha pamoja na utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini kuhusu upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini. Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi huu.

8.2 Kuna Upungufu Mkubwa wa Ujuzi kwenye Kada za Chini na Kati

Katika uchumi wa Tanzania kuna pengo kubwa la ujuzi kati ya kada za chini na kati (mafundi na mafundi mchundo) ikilinganishwa na kada ya juu ya wataalamu. Ukaguzi umebaini kwamba kuna upungufu mkubwa wa

wataalamu hasa kwenye kada za chini ambao unatakiwa kujazwa katika kipindi cha miaka 13 ijayo ili kuwezesha nchi kubakia kwenye uchumi wa kati.

Jedwali 8.1 linaonesha ulinganifu wa upungufu wa ujuzi kati ya Tanzania na nchi zingine za uchumi wa kati. Ukaguzi umebaini kwamba uwiano kati ya wataalamu, kada ya kati, na kada ya chini za ujuzi ni 1:0.7:1.2. Uwiano huu ni mdogo ikilinganishwa na unaotakiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Teknolojia (UNESCO) ambao ni 1:5:25. Kwa ujumla, uwiano wa watu wenye ujuzi ni 1:5:30 kulinganisha na ule wa nchi za uchumi wa kati ambao ni 1:3:5.

Jedwali 8.1: Ulinganifu wa Ujuzi kati ya Tanzania na Nchi Zingine za Uchumi wa Kati

Kiwango cha Ujuzi	Kundi la Kazi	Uwiano wa Wafanyakazi na Idadi ya Watu kwa Asilimia		Utofauti wa Ujuzi kati ya Tanzania na Nchi za Uchumi wa kati	Wastani wa Utofauti kati ya Tanzania na Nchi za Uchumi wa Kati
		Tanzania	Nchi za uchumi wa kati		
Chini	Waendesha Mitambo	1.3	5.66	Mara 4	Mara 0.6
	Nyinginezo	82.4	48.14	Mara 0.6	
Kiashiria cha mlinganyo wa wafanyakazi wenye ujuzi		1:5:30	1:3:5		

***Chanzo**: Uchambuzi wa wakaguzi kutoka kwenye Mpango wa Maendeleo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (2013/14-2017/18) na Mpango wa Taifa wa Kuendeleza Ujuzi (2016/17–2025/26), 2019*

Jedwali 8.1 linaonesha kwamba kada za chini zinatakiwa kuongezeka mara nne zaidi ili kuwezesha nchi kusalia kwenye uchumi wa kati. Ukaguzi ulichambua upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya ujuzi wa mafundi mchundo na kubaini yafuatayo.

8.2.1 Upatikanaji Usiotosheleza wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilishindwa kufikia lengo la kudahili wanafunzi 1,012,967 wa elimu na mafunzo ya

ufundi stadi mwaka 2017/18 kwa kudahili wanafunzi 119,184 ambao ni upungufu wa wanafunzi 893,783 wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

Kielelezo 8.1: Ulinganifu wa Mahitaji na Udahili wa Wanafunzi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (2013/14 -2017/18)



***Chanzo**: Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Mpango wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Taarifa ya Ufanisi wa Sekta ya Elimu, 2020*

Kielelezo 8.1 kinaonesha kuwa udahili wa wanafunzi wa Elimu na Mafunzo ya ufundi stadi ulipungua kwa asilimia 8.4 kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2017/18.

Ukaguzi ulibaini kwamba sababu kubwa ya kushindwa kuhimili upungufu huu ilikuwa kukosekana kwa mikakati na mipango endelevu ya kuhakikisha kuwa kunakuwepo na upatikanaji wa elimu ya ufundi iliyojitosheleza.

8.2.2 Waombaji Wachache Walichaguliwa Kujiunga na Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Ukaguzi ulibaini kwamba kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2018/19 waombaji 25,370 ndio waliochaguliwa kujiunga na elimu na mafunzo ya ufundi stadi kati ya 105,709 ambayo ni sawa na asilimia 23 tu ya waombaji wote.

Kielelezo 8.2: Idadi ya Waombaji Waliochaguliwa Kujiunga na Vyuo vya Ufundi Stadi (2012/13 - 2017/18)



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Takwimu za Maombi na Udahili 2020*

Kielelezo 8.2 kinaonesha kwamba kiwango cha juu cha udahili cha asilimia 43 kilikuwa mwaka 2018 na kiwango cha chini cha udahili cha asilimia 9 kilikuwa mwaka 2014. Ukaguzi umebaini kwamba sababu kubwa ya kuwepo kwa udahili wa chini ni uwezo mdogo wa udahili wa vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi, uhaba wa rasilimali-watu kama walimu, idadi ndogo ya madarasa, karakana, malazi, pamoja na mgawanyo usio na uwiano wa vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

8.2.3 Utoaji Mafunzo Usiojitoseheleza kwa Wanafunzi wa Makundi Maalumu

Ukaguzi ulibaini kwamba kulikuwa na udahili wa kiwango cha chini wa wanafunzi wa makundi maalumu kama wanawake, watu wenye ulemavu, pamoja na wale wanaotoka kwenye maeneo yasiyo na vyuo vya ufundi kama inavyojadiliwa hapa chini.

(a) Wanafunzi wa Kike Wachache Walidahiliwa

Udahili wa wanafunzi wa kike ulitakiwa kufikia malengo ya asilimia 50 mwaka 2017/18. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba udahili wa wanafunzi wa kike ulifikia asilimia 35 tu hadi mwaka 2017/18 ambapo ilikuwa chini ya asilimia 50 iliyotakiwa kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo 8.3**.

Kielelezo 8.3. Kiwango cha Kufikiwa Makadirio ya Udahili wa Wanafunzi wa Kike (2013/14 – 2018/19)



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Takwimu Za Elimu Msingi 2020*

Kielelezo 8.3 kinaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2013/14, udahili wa wanafunzi wa kike ulikuwa asilimia 39 ikilinganishwa na lengo la asilimia 47 mwaka 2014/15. Hii inamaanisha kuwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilishindwa kufikia lengo la asilimia 50 la udahili wa wanafunzi wa kike.

(a) Udahili Mdogo wa Wanafunzi wa Kike katika Fani Zinazoendana na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano

Ukaguzi ulibaini kuwa wanafunzi wa kike walidahiliwa zaidi katika fani zilizopo kwenye sekta ya utalii na hoteli wakati sekta ya usafirishaji na ujenzi ilikuwa na uwiano mdogo wa wanafunzi wa kike ikilinganishwa na wanafunzi wa kiume.

Ukaguzi ulibaini, kupitia mahojiano na wakurugenzi wa kanda na wakuu wa vyuo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, kwamba udahili wa wanafunzi wa kike ulikuwa wa chini katika sekta za biashara na ujenzi pamoja na zile zinazohusiana na mpango wa miaka mitano wa maendeleo wa taifa.

Kielelezo 8:4 kinatoa ulinganisho baina ya udahili wa wanafunzi wa kike na wa kiume kwenye fani zinazoendana na soko la ajira. Ukaguzi ulibaini kuwa udahili wa wanafunzi wa kiume ulikuwa wa juu kwenye sekta nne ambazo ni kilimo, uchukuzi, ujenzi na nishati wakati udahili wa wanafunzi wa kike ukiwa wa juu kwenye sekta mbili ambazo ni utalii na ukarimu pamoja na teknolojia ya Mawasiliano na Habari (TEHAMA).

Kielelezo 8:4: Ulinganisho wa Udahili wa Wanafunzi wa Kike na wa Kiume kwenye Fani Zinazoendana na Mpango wa Maendeleo



Chanzo:*Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Takwimu za Udahili* (2019)

Kulingana na **kielelezo 8.4** katika sekta ya Kilimo uwiano wa wanawake ulikuwa asilimia 47, wakati sekta ya usafiri ikiwa asilimia 11 ikilinganishwa na sekta ya nishati ambapo udahili wa wanafunzi wa kike ulikuwa asilimia 17. Ukaguzi ulibaini kuwa katika sekta za utalii na ukarimu udahili wa wanafunzi wa kike ulikuwa asilimia 70, na vilevile katika habari na mawasiliano udahili wa wanawake ulikuwa asilimia 54.

Ukaguzi ulibaini kuwa udahili mdogo wa wanafunzi wa kike katika sekta hizi ulitokana na ukosefu wa mkakati wa wazi wa namna ya kutekeleza lengo lililokusudiwa la kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike katika elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

(b) Udahili Mdogo wa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu

Ukaguzi ulibaini kuwa udahili wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulipungua kwa asilimia 64 kati ya mwaka 2013 na 2018. **Kielelezo 8.4(a)** na **Kielelezo 8.4(b)** vinaonesha mwenendo wa udahili wa wanafunzi wenye

mahitaji maalumu kwa makundi katika vyuo na vituo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Kwa ujumla, vielelezo hivyo vinaonesha kuwa udahili wa wanafunzi kwenye elimu na mafunzo ya ufundi stadi ulipungua kimakundi na aina ya uhitaji maalumu.

Ukaguzi ulibaini pia kuwa udahili wa watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) ulikuwa chini ya asilimia 81, ukifuatiwa na watu wenye ulemavu wa kusikia ambapo udahili ulipungua kwa asilimia 80, wakati kwa upande wa watu wenye ulemavu wa akili na wale wenye usonji udahili uliongezeka kwa asilimia 5 na 14 mtawalia.

Kilezo 8.4 (a): Mwenendo wa Udahili wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu kwa Aina ya Ulemavu, 2013 -2018[9]



Chanzo:*Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Kitabu cha Takwimu cha Elimu ya Ufundi kwa Kipindi cha 2013 – 2018*

Kielelezo 8.4(a) kinaonesha kuwa kulikuwa na udahili wa juu wa wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia ikilinganishwa na aina zingine za ulemavu. Wanafunzi wenye usonji walikuwa na uandikishaji wa chini zaidi katika vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

[9] Albino, Usonji, Vipofu na Viziwi

Kielelezo 8.4 (b): Mwenendo wa Uandikishaji wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu 2013 -2018[10]



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka Kijitabu cha Data za Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa Kipindi cha 2013 - 2018*

Kielelezo 8.4(b) wanafunzi wenye changamoto za kimwili wana kiwango cha juu cha udahili ikilinganishwa na aina zingine za ulemavu zilizochambuliwa. Hata hivyo, uchambuzi wa mwenendo unaonesha kuwa kumekuwa na kupungua kwa udahili kwa miaka mingi.

(c) Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Ilidahili Idadi Ndogo ya Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

Uchambuzi zaidi wa udahili ulionesha kuwa, asilimia 99 ya wanafunzi wenye ulemavu walidahiliwa katika vyuo vingine vya elimu ya ufundi stadi wakati Mamlaka ya Elimu na Mafunzo Stadi ilidahili asilimia 1 tu ya wanafunzi wote.

Kielelezo 8.5 kinaonesha asilimia ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu waliodahiliwa na watoa huduma. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa udahili wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ulifanywa na watoahuduma wengine wakati Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilidahili asilimia moja tu ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Kielelezo 8.5: Asilimia ya Udahili wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu Kulingana na Mtoahuduma



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Mfumo wa Usimamizi wa Sekta ya Elimu (2013-2018)*

Kielelezo 8.5 kinaonesha kwamba, mashirika ya kidini yalikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu waliodahiliwa ikilinganishwa na watoahuduma wengine kama Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ambayo ilikuwa na asilimia ndogo ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa, asilimia 99 ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu walidahiliwa katika vyuo vingine vya elimu ya ufundi wakati vyuo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi vilidahili asilimia 1 tu ya wanafunzi wote.

Ukaguzi ulibaini kuwa sababu za udahili mdogo wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu zilikuwa ni ukosefu wa zana na miundombinu rafiki kwa watu wenye mahitaji maalumu kama vile vifaa vya kusaidia kujifunzia; kukosekana kwa walimu wa kutosha na wenye ujuzi wa kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu; kukosekana kwa mpango wa utekelezaji jumuishi wa wanafunzi kutoka makundi yenye mahitaji maalumu katika elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

(d) Kutokuwepo kwa Usawa katika Mtawanyo wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Kwa mujibu wa Mpango wa Nne na wa Tano wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi wa 2012/19 hadi 2016/17 na 2018/19-2022/23, ili kuhakikisha upatikanaji elimu ya ufundi wenye usawa, moja ya malengo ilikuwa kuhakikisha usawa kwenye ujengaji wa vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

Kielelezo 8.6 kinaonesha kutokuwepo kwa usawa kwenye mtawanyo wa vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi katika kanda nchini. Ukaguzi ulibaini kuwa ukanda wa kaskazini ulikuwa na asilimia 26 ya vituo vya elimu nchini, kanda ya magharibi ilikuwa na kiwango cha chini zaidi kwa sababu ilikuwa na asilimia 6 tu ya vituo vya utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi vilivyopo. Hii inaonesha ukosefu wa usawa katika mtawanyo wa vyuo vya elimu ya ufundi katika kanda mbalimbali nchini.

Kielelezo 8.6: Mtawanyo wa Vituo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika Kanda za Kijiografia Nchini



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Takwimu za Elimu ya Msingi (2013-2018)*

Kielelezo 8.6 kinaonesha kwamba, ukanda wa kaskazini ulikuwa na asilimia 26 ya vyuo vyote wakati kanda ya magharibi ulikuwa na asilimia 6 tu ya vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Hali hii huathiri udahili wa wanafunzi katika fani za elimu ya ufundi na mafunzo stadi kwenye maeneo mengi ya nchi.

(e) Kusuasua kwa Maboresho ya Miundombinu

Kwa mujibu wa Mpango wa Nne wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi moja ya vipaumbele kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa elimu ya ufundi ilikuwa kujenga vhuo kimoja cha ufundi katika wilaya 25 zilizobainishwa.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilifanikiwa kujenga vyuo vitatu vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi vya wilaya. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ilifanikiwa kuboresha karakana 8 tu kati ya karakana 25 zilipangwa kufanyiwa maboresho.

Aidha, Mamlaka ilifanikiwa kukarabati vyuo sita vya maendeleo ya jamii kati ya vyuo 25. Ukaguzi ulibaini kuwa sababu ya kutofikia malengo hayo ilikuwa kukosekana kwa ufanisi katika ugawaji wa fedha.

8.2.4 Matokeo Mchanganyiko kwenye Udahili wa Wanafunzi wa Elimu ya Ufundi katika Fani Zinazoendana na Mpango wa Maendeleo ya Uchumi.

Kwa mujibu wa Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Ujuzi (2016/17-2025/26), Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (I na II), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilipaswa kuhakikisha kuwa wanafunzi wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi wanafunzi wanadahiliwa kwa wingi katika fani zinazoendana na vipaumbele vya taifa kama vile kilimo, ujenzi, madini, na TEHAMA.

Kielelezo 8.7 kinatoa mwenendo wa udahili wa wanafunzi kwenye elimu na mafunzo ya ufundi stadi na sekta muhimu za kiuchumi. Ukaguzi ulibaini kuwa udahili katika kilimo na usindikaji wa chakula uliongezeka, wakati udahili katika TEHAMA ulipungua. Aidha, udahili katika sekta ya ujenzi uliongezeka huku udahili katika sekta ya madini ukipungua.

Kielelezo 8.7: Mwenendo wa Wanafunzi Waliodahiliwa kwenye Sekta Muhimu za Kiuchumi



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Elimu (2019)*

Kielelezo 8.7 kinaonesha mwenendo wa udahili wa wanafunzi katika sekta muhimu za kiuchumi katika Kanda za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi zilizotembelewa. Uchambuzi unaonesha kuwa kulikuwa na kupungua kwa udahili wa wanafunzi katika fani zilizopewa kipaumbele na Mkakati wa Maendeleo wa Taifa. Kulingana na mahojiano na maofisa katika vyuo vilivyotembelewa, sababu kubwa ilikuwa kubadilika kwa machaguo ya wanafunzi.

8.3 Mfumo wa Udhibiti Ubora wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Haukuwa na Tija

Ukaguzi ulibaini kwamba mfumo wa udhibiti wa ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi ulikuwa na mapungufu kama yanavyoainishwa hapa chini.

8.3.1 Idadi kubwa ya vyuo havikukidhi Ubora Unaotakiwa

Mpango wa Maendeleo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi wa Mwaka 2013/14 hadi 2017/18 uliitaka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Stadi kuhakikisha kuwa idadi ya vyuo vya ufundi vilivyopata usajili wa kudumu ndani ya miaka mitatu vinaongezeka kutoka asilimia 25 kwa mwaka 2011/12 hadi asilimia 75 mwaka 2017/18. Pia, ukaguzi umebaini kuwa kuanzia mwaka 2013/14 hadi mwaka 2018/19, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilishindwa kuhakikisha kuwa asilimia 75 ya vyuo hivyo vinapata ithibati ifikapo mwaka 2017/18.

Kielelezo 8.8 kinaonesha usajili wa vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi katika kanda ambapo ni asilimia tisa tu ndivyo vilipata usajili kamili.

Kielelezo 8.8: Hali ya Usajili wa Vyuo Kwenye Kanda



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Taarifa za Usajili, 2020*

Kama inavyonekana kwenye **Kielelezo 8.8,** ukaguzi umebaini kuwa idadi ya vyuo kati ya asilimia 81 hadi 92 vilikuwa na usajili wa muda kwenye kanda zilizotembelewa. Sababu kubwa ya vyuo vingi kubaki kwenye usajili wa muda zilikuwa ni kukosekana kwa walimu wa kutosha; kutofanyika ukaguzi wa ubora; ukosefu wa vifaa; na uhaba wa madarasa na karakana.

8.3.2 Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Vilisalia kwenye Usajili wa Muda kwa Kipindi Kirefu

Vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi vilipaswa kupata ithibati ndani ya miezi sita baada ya kupatiwa usajili wa kudumu na vikishindwa kufanya hivyo ndani ya miaka mitano vilitakiwa kufutiwa usajili.

Ukaguzi ulibaini kuwa asilimia 56 ya vyuo hivi vilisalia kwenye usajili wa muda kwa zaidi ya miaka mitano. Vilevile, vyuo vyote 650 vilivyosajiliwa vilishindwa kupata usajili wa kudumu ndani ya miaka mitano.

Jedwali 8:2 Mgawanyo wa Vyuo vyenye Usajili wa Awali kwa Kanda

Kanda	Idadi ya vyuo vyenye usajili wa awali	Idadi ya Vyuo vilivyosalia kwenye Usajili wa awali kwa miaka 5	Asilimia ya vyuo vilivyokaa kwenye usajili wa awali kwa Zaidi ya miaka 5
Dar es Salaam	106	78	74
Kaskazini	100	72	72
Mashariki	44	28	64
Nyanda za Juu	94	56	60
Kusini Mashariki	19	11	58
Kusini Magharibi	50	26	52
Kati	56	25	45
Ziwa	98	27	28
Mashariki	22	5	23

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Taarifa za Ithibati za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (2019)*

Jedwali 8.2 linaonesha kuwa kwa zaidi ya asilimia 56 ya vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi ambavyo vilikuwa na usajili wa muda vilisalia katika hali hiyo kwa muda wa zaidi ya miaka mitano. Kanda ya Dar es Salaam ilikuwa na asilimia 78, kanda ya kaskazini ilikuwa na asilimia 72, wakati kanda ya ziwa ilikuwa na asilimia 28.

8.4 Zifuatazo ni Sababu za Mapungufu Yaliyobainika

8.4.1 Ofisi za Kanda Zilifanya Ufuatiliaji Hafifu wa Ubora

Ofisi za kanda zilitakiwa kufanya ufuatiliji wa kudhibiti ubora kwa vyuo vyote vya ufundi stadi. Ukaguzi ulibaini kuwa ufuatiliaji wa ubora kwa watoahuduma ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi haukufanyika kama inavyotakiwa. Ukaguzi wa ubora wa mafunzo ulifanyika kwenye vyuo vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi tu na kuacha vile vinavyomilikiwa na watu au taasisi binafsi. Hali hii ilichangia vyuo kutokutekeleza masharti ya usajili na ithibati.

8.4.2 Kufanyika kwa Idadi Ndogo ya Ukaguzi wa Ubora

Kwa mujibu wa Mpango wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi wa mwaka 2018/2019 hadi 2022/2023, asilimia 50 ya vyuo vilivyosajiliwa vinatakiwa kufanyiwa ukaguzi wa ubora kila mwaka kwa lengo la kupima ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi wanayotolewa.

Jedwali 8.3 linaonesha idadi ya kaguzi za elimu na mafunzo ya ufundi stadi zilizofanyika katika kipindi cha kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2018/19**.** Ukaguzi ulibaini kwamba ni asimia 13 tu ya watoahuduma ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi 650 waliosajiliwa ndio waliofanyiwa ukaguzi wa ubora kati ya mwaka 2013/14-2018/19.

Jedwali 8.3: Idadi ya Kaguzi za Ubora Zilizofanywa kati ya mwaka 2013/14-2018/19

Mwaka wa Fedha	Idadi ya Vyuo	Idadi ya Vyuo ambavyo Havikufanyiwa Kaguzi za Ubora
2013/14	760	760
2014/15	898	898
2015/16	877	877
2016/17	448	448
2017/18	655	655
2018/19	650	563

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakagzui kutoka kwenye Taarifa za Ukaguzi wa Ubora Mwaka 2019*

Jedwali 8.3 linaonesha kuwa tangu mwaka 2013/14 hadi 2018/19 kaguzi za ubora zilifanywa kanda ya kaskazini ambapo vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi 87 vilikaguliwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa sababu ya kutokufanyika kwa ukaguzi ni kutokuwepo kwa kitengo kinachojitegemea cha ukaguzi wa ubora kilichotakiwa kuwa chini ya Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Hali hii ilisababibisha kutokuwepo kwa uimarishaji endelevu wa ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi na kuongezeka kwa matukio ya kutofikiwa kwa viwango vya ubora.

8.4.3 Mapitio ya Mitaala Hayakufanyikwa kama Ilivyotarajiwa

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Ubora wa Maandalizi ya Kusajiliwa na Kupewa Ithibati wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, mitaala hutakiwa kufanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitano ili iendane na mahitaji ya soko.

Ukaguzi ulibaini kuwa mitaala 42 kati ya 80 ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi iliyomaliza muda wake mwezi Mei 2018 ilikuwa haijafanyiwa mapitio hadi wakati wa ukaguzi huu. Sababu iliyopelekea mitaala hiyo kutofanyiwa mapitio ni kutokufanyika kwa utafiti wa mahitaji ya soko kwa wakati kwa ajili ya kutumika kwenye mapitio ya mitaala hiyo. Kutokufanyika kwa mapitio ya mitaala kutapelekea mitaala hiyo kutokwenda na wakati pamoja na kushindwa kukidhi mahitaji ya ajira na jamii ya wakati uliopo.

8.4.4 Idadi ya Walimu Isiyotosha kwa ajili ya Kuhakikisha Ubora wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Kwa Mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ya Mwaka 2012, moja ya mambo yanayosabibisha kupungua kwa ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa kwenye vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi ni ukosefu wa walimu wenye uwezo na ubora unaotakiwa kama ambavyo inaelezwa hapa chini.

(i) Uhaba wa Walimu wa Elimu na Mafunzo na Ufundi Stadi

Ukaguzi ulibaini kwamba kuna uhaba wa walimu wenye ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. **Kielelezo 8.9** kinaonesha mahitaji pamoja na

idadi ya walimu waliopo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2019/20. Ukaguzi umebaini kwamba idadi ya walimu waliopo ni ndogo kuliko mahitaji hivyo kupelekea kuwepo kwa uhaba mkubwa wa walimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Kielelezo 8.9: Mahitaji ya Walimu wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (2013/14 - 2018/19)



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Mpango wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Takwimu za Elimu ya Awali (2013/14-2017/18)*

Kielelezo 8.9 kinaonesha kwamba uhaba wa walimu umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka asilimia 42 mwaka 2013/14 hadi kufikia asilimia 69 mwaka 2018/19.

(ii) Uwiano Usioridhisha wa Wanafunzi na Walimu wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi wa Mwaka 2013/14-2017/18, uwiano wa wanafunzi kwa walimu ulitakiwa uwe 16:1. Ukaguzi umebaini kwamba uwiano wa wanafunzi kwa walimu katika vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi satdi ulikuwa mdogo. Kwa mfano, uwiano wa wanafunzi kwa walimu katika Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Dar es Salaam ulikuwa 154:1. Katika Chuo cha Hoteli na Utalii Njiro uwiano ulikuwa mdogo wa 7:1. Hali hii imesababishwa na uwezo mdogo wa Chuo cha Ualimu wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro kuandaa walimu wa kutosha.

(iii) Walimu wa Ufundi Stadi Kutokuwa na Mafunzo ya Mbinu za Kufundishia

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi(2013/14-2017/18), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloji na Mafunzo ya Ufundi Stadi kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilitakiwa kuhakikisha kuwa asilimia 75 ya walimu wamepitia mafunzo ya mbinu za kufundishia kuanzia mwaka 2015/16 na kufikia asilimia 100 mwaka 2017/18.

Kielelezo 8.10 kinaonesha asilimia ya walimu ambao hawakupata mafunzo ya mbinu za kufundishia kwa kila kanda. Kielelezo kinaonesha kwamba walimu wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi katika kila kanda hawakuwa na mafunzo ya mbinu za kufundishia.

Kielelezo 8.10: Asilimia ya Walimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Wasio na Mafunzo ya Mbinu za Kufundishia



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Vitabu vya Takwimu vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (2019)*

Kielelezo 8.10 kinaonesha kwamba Kanda ya Kaskazini ilikuwa na asilimia 85 ya walimu wasiokuwa na mafunzo ya mbinu za kufundishia, Kanda ya Mashariki ilikuwa na asilimia 78, Kusini Magharibi ilikuwa na asilimia 66 wakati Dar as Salaam ilikuwa na asilimia 25. Sababu kubwa iliyopelekea hali hii ni uwezo mdogo wa Chuo cha Ualimu wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro kudahili wanafunzi. Kwa sasa Chuo kina uwezo wa kudahili asilimia moja tu ya walimu wenye uhitaji wa mbinu za kufundishia.

8.4.5 Uhaba wa Vifaa na Miundombinu ya Kufundishia na Kujifunzia

Kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi wa Mwaka 2016-2022 wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Teknolojia, uwepo wa zana na vifaa vyenye ubora ni jambo la msingi katika utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Timu ya ukaguzi ilibaini yafuatayo kuhusiana na uwepo, hali na utumikaji wa zana na vifaa vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

(a) Uhaba wa vifaa kwenye vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi

Ukaguzi ulibaini kwamba kulikuwa na upungufu wa asilimia 46 wa vifaa vya kufundishia kwenye vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Arusha kilikuwa na upungufu wa asilimia 76 wakati Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Ulyankulu kilikuwa na asilimia 31 ambao ndio uhaba wa kiwango cha chini. Aidha, zaidi ya asilimia 75 ya programu za mafunzo zilikuwa na uhaba wa vifaa vinavyohitajika.

(b) Uhaba wa zana za kufundishia kwenye vyuo vya elimu na mfunzo ya ufundi stadi

Ukaguzi ulibaini kwamba kulikuwa na uhaba wa zana za kufundishia kwenye vyuo vilivyotembelewa ambapo vyuo vyote vilikuwa na asilimia 46 ya zana zinazohitajika.

(c) Uhaba wa madarasa kwa katika vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi

Viwango vya elimu ya ufundi vinataka kila programu ya elimu ya ufundi stadi kuwa na karakana kwa ajili ya mazoezi kwa vitendo pamoja na darasa litakalotumika kwa ajili ya mafunzo ya nadharia. Ukaguzi ulibaini kuwa vyuo vyote vya ufundi vilivyotembelewa vilikuwa na upungufu wa madarasa wa asilimia 29 kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo 8.11**.

Kielelezo 8.11: Asilimia ya Madarasa Yaliyopo kwenye Vyuo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Mfumo wa Taarifa wa Sekta ya Elimu 2019*

Kielelezo 8.11 kinaonesha kuwa kwenye vyuo vilivyotembelewa kulikuwa na upungufu wa madarasa. Chuo cha Ufundi Stadi Mkoa wa Mwanza kilikuwa na upungufu wa asilimia 47 ya madarasa yanayohitajika; na Chuo cha Ufundi Stadi cha Shinyanga kilikuwa na upungufu wa asilimia 50. Hata hivyo, Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mtwara, Tabora na Kipawa vilikuwa na utoshelevu wa madarasa yanayohitajika kwa asilimia 100.

Vilevile, uwiano wa mwanafunzi kwa darasa ulitofautiana baina ya vyuo vilivyotembelewa. Chuo cha Ufundi Stadi Arusha kilikuwa na uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi wa 1:598 ambao ulikuwa mkubwa ikilinganishwa na vyuo vingine, wakati Chuo cha Ufundi Stadi Ulyankulu kilikuwa na uwiano mdogo wa 1:51. **Jedwali 8.4** linaonesha uwiano wa darasa kwa wanafunzi.

Jedwali 8.4: Uwiano wa Darasa kwa Mwanafunzi kwenye Vyuo vya Elimu na Ufundi Stadi Vilivyotembelewa

Jina la Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi	Idadi Iliyopo	Idadi ya Wanafunzi	Uwiano wa Darasa kwa Mwanafunzi
Arusha	4	2392	1:598
Shinyanga	5	2238	1:448
Mbeya	5	1539	1:308
Kipawa -	5	1010	1:202
Kihonda	15	2834	1:189
Mtwara	21	2389	1:114
Tabora	13	1222	1:94
Mwanza	14	1122	1:80
Ulyankulu	7	357	1:51
Njiro	5	98	1:20

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Mfumo wa Taarifa wa Sekta ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi*

Jedwali 8.4 linaonesha kuwa uwiano wa darasa kwa mwanafunzi ulikuwa mkubwa katika Chuo cha Ufundi Stadi Arusha kikiwa na uwiano wa 1:598 wakati Chuo cha Ufundi Stadi cha Ulyankulu kilikuwa na uwiano wa 1:51 ambao ulikuwa wa kiwango cha chini ikilinganishwa na vyuo vingine.

8.4.6 Uhaba wa Karakana kwa ajili ya Mafunzo kwa Vitendo

Uchambuzi wa vitabu vya takwimu vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ulionesha kwamba kulikuwa na mahitaji ya karakana kwenye vyuo vyote vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Hali hii pia ilidhihirika wakati wa mahojiano na maofisa kwenye vyuo vya ufundi vilivyotembelewa.

Wakati wa ziara ya wakaguzi kwenye Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Wilaya ya Busekelo, ilibainika kwamba kuna vyumba ambavyo vilitumika kama karakana ila havikukidhi viwango vinavyotakiwa vya karakana.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kwamba kuna vyuo ambavyo vilikuwa vinafanya kazi bila uwepo wa karakana za kutosha kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

Kielelezo 8.12 kinalinganisha uhitaji, uwepo na upungufu wa karakana kwenye vyuo vya ufundi vilivyotembelewa.

Kielelezo 8.12: Mahitaji, Uwepo na Upungufu wa Karakana kwenye Vyuo Vilivyotembelewa



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Mfumo wa Taarifa wa Sekta ya Elimu (2019)*

Kielelezo 8.12 kinaonesha kwamba upungufu wa karakana kwenye vyuo vilivyotembelewa ulikuwa kati ya karakana 2 hadi 11. Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Tabora ndicho kilikuwa na uhaba mkubwa wa karakana.

Pamoja na hayo, ukaguzi ulibaini kwamba uwiano wa karakana ulitofautiana kati ya chuo kimoja na kingine. Chuo cha Ufundi cha Kipawa ndicho kilikuwa na uwiano mkubwa wa 1:505 zaidi huku Chuo cha Ulyankulu kikiwa na uwiano mdogo zaidi wa 1:51. Upungufu wa karakana unasababisha wanafunzi kushindwa kujifunza kwa vitendo.

(d) Ukosefu wa Vifaa kwa Wanafunzi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi wenye Mahitaji Maalumu

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu wa Taifa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi inatakiwa kuhakikisha uwepo wa miundombinu na vifaa sahihi na jumuishi vya kufundishia na kujifunzia.

Ukaguzi ulibaini kwamba vyuo vyote vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi havikuwa na vifaa vya kujifunzia kwa watu wenye mahitaji maalumu ili kuweza kudahili wanafunzi hao. Vilevile, ukaguzi ulibaini uwepo wa karakana na majengo ambayo hayakuwa rafiki kwa watu wenye mahitaji maalumu.

Sababu kubwa iliyopelekea Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kushindwa kudahili wanafunzi wenye mahitaji maalumu ni kutoandaa mipango inayotekelezeka kwa ajili ya kundi hili.

8.5 Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Kutopatiwa Fedha Inavyotakiwa

Ukaguzi umebaini kwamba kazi zilizohusisha elimu na mafunzo ya ufundi stadi hazikutengewa fedha ili kuweza kutekelezwa kikamilifu kama ifuatavyo.

8.5.1 Mgawanyo na Mapato ya Kodi ya Maendeleo ya Ujuzi Usiokidhi Mahitaji

Theluthi moja ya mapato ya kodi ya ujuzi yaliyopatikana kutoka kwenye makusanyo ya kodi ya maendeleo ya ujuzi hutakiwa kuwekwa kwenye mfuko wa mafunzo ya ufundi stadi ili kutumika kwa shughuli zinazohusu elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

Kielelezo 8.13 kinaonesha kiasi cha makusanyo ya theluthi moja ya kodi ya maendeleo ya ujuzi, kiasi walichopewa Mamlaka ya Elimu na Ufundi Stadi na tofauti ya mgawanyo kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2018/19. Ukaguzi ulibaini kwamba kiasi walichopewa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kilikuwa kidogo tofauti na sheria ilivyotaka.

Kielelezo 8.13: Mgawanyo wa Fedha za Kodi ya Maendeleo ya Ujuzi kwa ajili ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuanzia Mwaka 2014/15-2018/19 (Bilioni ya Shilingi)



Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Taarifa za Makusanyo za Mamlaka ya Mapato Tanzania na Bajeti za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuanzia Mwaka 2014/15-2018/19*

Kielelezo 8.13 kinaonesha kuwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilipokea asilimia 51 tu ya fedha zote ilizotakiwa kupewa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2014/15 hadi 2018/19. Vilevile, mgawanyo huu wa mapato haukuonekana kuimarika mwaka baada ya mwaka.

Matokeo ya kupungua kwa mgao wa fedha yalikuwa kudhoofika kwa uwezo wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kufikia malengo yake kama vile kupanua upatakinaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na kukosekana kwa fedha za kuboresha uwezo wa walimu kupitia mafunzo mabalimbali ya mafunzo ya vitendo kwenye maeneo tofauti kama vile viwandani.

8.5.2 Uchelewashaji wa Fedha kwenye Kanda na Vyuo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Ukaguzi ulibaini kwamba fedha zilizopelekwa kwenye vyuo kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2018/19 zilicheleweshwa kwa

muda wa kati ya siku 12 hadi 48. Vilevile, ukaguzi ulibaini kwamba uchelewaji huu ulitokana na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuchelewa kupeleka fedha makao makuu ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Ucheleweshaji huu uliathiri manunuzi ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia ambayo pia iliathiri utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

8.5.3 Mfumo Dhaifu wa Mgawanyo wa Fedha kwa Vyuo vya Elimu ya Ufundi Stadi

Timu ya ukaguzi ilichambua mgawanyo wa fedha kwenda vyuo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na kubaini kwamba kuanzia mwaka 2013 hadi 2019 tofauti kati ya chuo kimoja na kingine ilikuwa asilimia 49. **Jedwali 8.5** linaonesha mgawanyo wa fedha za kodi ya kuendeleza ujuzi katika vyuo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Jedwali 8.5: Mgawanyo wa Fedha za Bajeti kwa Makundi ya Vyuo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (2013-2019)

Jina la Chuo	Bajeti (Sh. Bilioni)	Mgawanyo (Sh. Bilioni)	Tofauti (Sh. Bilioni)	Tofauti (Asilimia)
Vyuo vyenye Hadhi ya Mkoa				
Mtwara	5.8	4.9	0.8	15
Tabora	4.6	4.6	0.07	2
Shinyanga	6.4	6.3	0.5	1
Mwanza	5.2	5.1	0	0
Mbeya	5.7	5.8	-0.169	-3
Vyuo vyenye Hadhi ya Wilaya				
Busekelo	0.47	0.46	14,205,597	3
Vyuo vya Ufudi Stadi				
Arusha	4.5	4.4	0.8	2
Ulyankulu	4.5	4.4	0.08	2
Vyuo vya Ufundi Maalumu				
Chuo cha TEHAMA - Kipawa	4.8	2.4	2.3	49
Chuo cha Utalii na Hoteli Njiro	8.0	8.0	0	0

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Bajeti na Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2019*

Jedwali 8.5 linabainisha kwamba vyuo vya mikoa vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ndivyo ambavyo havikupatiwa fedha zinazotokana na kodi ya kuendeleza ujuzi. **Jedwali 8.6** linaonesha matokeo ya mgawanyo wa fedha kwa ofisi za kanda.

Jedwali 8.6: Mgawanyo wa Fedha za Bajeti kwenye Kanda (2013/14-2018/19)

Jina la Kanda	Fedha Walizopatiwa (Kwa Sh. Bilioni)	Matumizi (Kwa Sh. Bilioni)	Tofauti (Sh. Bilioni)	Tofauti (Aslimia)
Dar es Salaam	2.7	3.7	1	37
Kusini Mashariki	3.3	3.6	0.3	9
Ziwa	3.1	3.2	0.1	3
Mashariki	3.4	3.4	0	0
Kusini Magharini	4.3	4	-0.05	-1
Mashariki	3.6	3.5	-0.1	-3
Kaskazini	4.5	3.5	-1	-22

Chanzo: *Uchambuzi wa Wakaguzi kutoka kwenye Bajeti na Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti Mwaka 2019*

Kielelezo 8.6 kinaonesha kwamba matumizi ya fedha zilizopelekwa kwenye kanda yalikuwa kati ya asilimia 22 na 37. Sababu kubwa iliyopelekea tofauti ya matumizi ni ugawaji wa fedha uliotegemea zaidi udahili wa wanafunzi na fedha za bajeti za miaka ya nyuma na hakukuwa na ugawaji wa fedha ambao uliendana na mahitaji halisi ya chuo.

8.6 Kutokuwepo kwa Tija kwa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikufanya kwa uhakika ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Wizara ya Elimu ilifanya tathmini na ufuatiliaji kwa kutegemea taarifa zilizopelekwa kwake na mamlaka yenyewe. Wizara ilizitumia taarifa hizo kutoa majumuisho ya utendaji wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

8.6.1 Udhaifu katika ufuatiaji na tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu, hususani kwenye elimu na mafunzo ya ufund stadi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatakiwa kuandaa mfumo wa ufuatiliaji kuhusu upatikanaji wa elimu yenye ubora ngazi ya taifa yenye viashiria vya upimaji. Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikuweza kufanya ufuatiliaji na tathmini ka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuhusu Ubora wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Hii ni kwa sababu Wizara haikuwahi kufanya ufuatiliaji na tathmini yake kwenye eneo la upatikanaji wa eimu na mafunzo ya ufundi stadi.

8.6.2.Viashiria vya upimaji havikuandaliwa na kutumiwa ipasavyo

Kwa mujibu wa Mpango wa Kuendeleza Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi wa Mwaka 2013/14-2017/18 na Mpango wa Maendeleo ya Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilitakiwa kuaanda mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini wenye viashiria vya upimaji.

Ukaguzi umebaini kwamba Mpango wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi wa Mwaka 2013/14-2017/18 haukuwa na viashiria vya upimaji ili kupima utekelezaji wa malengo makuu ya taasisi kuhusu upatikanaji yenye tija wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba Mpango wa Mamlaka wa miaka mitano ulikuwa na viashiria vya Upimaji kuhusu maendeleo ya upatikanaji wa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kupitia mapitio ya taarifa za mwaka za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwamba viashiria vya upimaji vilivyomo kwenye mpango mkakati wa shirika havikutumiwa kwenye utoaji na upashanaji taarifa kuhusu upatikanaji wa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi yanayotakiwa.

SURA YA TISA

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA ELIMU KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NA UTAFITI

9.1 Utangulizi

Sehemu hii inawasilisha masuala yaliyobainika kutoka katika taarifa nne za ukaguzi wa ufanisi katika sekta ya elimu. Mambo yaliyobainika yamejikita katika utekelezaji wa programu za elimu hususani uimarishaji wa uwezo wa kufanya utafiti katika taasisi za elimu ya juu ikijumuisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Chuo Kikuu cha Ardhi, pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia.

Taarifa hizo nne za ukaguzi zilizotumika katika majumuisho ya sehemu hii ni Uimarishaji Uwezo wa Utafiti katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Uimarishaji Uwezo wa Utafiti katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili; Uimarishaji Uwezo wa Utafiti katika Chuo Kikuu cha Ardhi; na Ujengaji wa Mifumo ya Kuwezesha Tafiti Zinazoendana na Mazingira na zenye Ubora wa Hali ya Juu katika Tume ya Sayansi na Teknolojia.

Sehemu hii mahususi inajikita katika kujumuisha mambo yote yaliyobainika katika tathmini za mipango ya miradi na mipango ya awali, uratibu wakati wa utekelezaji wa miradi husika, ufanisi katika utekelezaji wa miradi, upatikanaji wa fedha kwa shughuli za miradi, pamoja na mwendelezo wa miradi husika katika taasisi hizo. Madhaifu yaliyobainika yanawasilishwa hapa chini.

9.2 Mipango na Shughuli za Awali za Miradi

Mapitio ya ripoti binafsi za ukaguzi wa ufanisi yalibaini kwamba, shughuli za awali za utekelezaji wa miradi ya elimu katika taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, na Ardhi, pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia haikuratibiwa na kutekelezwa kwa kiwango cha kutosha. Udhaifu uliobainika unawasilishwa hapa chini.

9.1.1 Uchambuzi hafifu wa vihatarishi wakati wa kuandaa mipango ya miradi

Utekelezaji wa miradi katika taasisi za elimu ya juu unahitaji uchambuzi wa kutosha wa vihatarishi ili kulinda rasilimali dhidi ya matumizi mabaya na kuepuka kutopatikana kwa thamani ya fedha. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba utekelezaji wa miradi katika taasisi husika haukuambatana na uchambuzi wa kutosha wa vihatarishi. **Jedwali 9.1** linaonesha vihatarishi vilivyojirudia katika taasisi tofauti na ambavyo havikuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa miradi katika taasisi[11] nne husika na hivyo kuathiri matokeo ya mradi.

Jedwali 9.1: Vihatarishi vilivyojirudia na matokeo yake hasi

Vihatarishi Vilivyosahaulika	Utokeaji wake	Madhara ya Muda Mfupi
Tume ya Vyuo Vikuu kuchelewa kuidhinisha mitaala	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Chuo Kikuu cha Ardhi Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	• Kuchelewa kwa matokeo ya Miradi • Kutopatikana kwa matokeo ya mradi
Wanafunzi kutoweza kumaliza masomo kwa wakati	Chuo Kikuu cha Ardhi Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	• Kuchelewa kwa matokeo ya mradi
Wanafunzi kuacha masomo	Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	• Kutofikiwa kwa malengo ya mradi
Kutopokea maombi kwa kozi zilizoanzishwa	Chuo Kikuu cha Ardhi Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili	• Kutofikiwa kwa malengo ya mradi • Kukosekana kwa thamani ya fedha
Mwamko mdogo wa jamii kutumia matokeo ya tafiti	Chuo Kikuu cha Ardhi Tume ya Sayansi na Teknolojia	• Kutofikiwa kwa malengo ya mradi

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi kwa Programu ya Uimarishaji Uwezo wa Kufanya Tafiti katika Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Ardhi, na Muhimbili na Tume ya Sayansi na Teknolojia*

[11] Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ardhi, pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia

Jedwali 9.1 linaonesha vihatarishi mbalimbali ambavyo vilishindwa kubainishwa na kuweza kuathiri kufikiwa kwa malengo mahususi na malengo ya jumla ya mradi wakati wa utekelezaji wa shughuli za mradi. Kuchelewa kuidhinishwa kwa mitaala kulikofanywa na Tume ya Vyuo Vikuu kulikuwa moja ya vihatarishi vilivyojibainisha katika vyuo vikuu vyote vitatu vilivyoshiriki mradi wa uimarishaji uwezo wa kufanya utafiti. Moja ya madhara ambayo yalijitokeza katika sehemu nyingi ni kuchelewa au kutofikiwa kwa malengo mahususi au ya jumla ya mradi katika taasisi zote nne zilizotekeleza miradi husika.

9.1.2 Kuandaa Viashiria na Malengo Yasiyo na Uhalisia

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu uimarishaji uwezo wa utafiti katika Tume ya Sayansi na Teknolojia ulibaini kwamba malengo ya awali ya mradi yalijumuisha malengo na viashiria ambavyo havikuwa na uhalisia na kujumuishwa katika shughuli ambazo zilishindwa kufanyika kikamilifu. Kwa mfano, programu ya uimarishaji wa uwezo wa utafiti katika Tume ya Sayansi na Teknolojia ilinuia kuongeza ripoti za miradi ya masomo ya shahada ya uzamivu kutoka mbili hadi tatu kwa kila mwaka hadi mwezi Juni mwaka 2018 lakini lengo hilo halikuweza kufikiwa. Upangaji huu haukuweza kufanywa vizuri kwa kuwa, hata kama kusingekuwepo na ucheleweshaji wa kuanza kwa miradi, lengo hili lisingefikiwa kwa kuwa ilitarajiwa kuchukua miaka miwili hadi mitatu kwa watafiti kuanza kutoa ripoti na matokeo mengine yakiwemo machapisho.

Zaidi, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili hakikuweka malengo ya kupima ufikiwaji wa namna ya kuimarisha ujuzi katika kukabili malaria. Ukaguzi ulibaini kwamba malengo yaliyowekwa hayakufikiwa kwa kuwa wakati wa uaandaji wa mipango ya mradi, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kiliweka makadirio ya juu kupita kiasi, kwa mfano malengo ya idadi ya machapisho kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye makongamano.

Aidha, ukaguzi wa programu ya kuimarisha uwezo wa kiutafiti katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili ulibaini kwamba malengo ya kuwa na kiwango cha juu cha tafiti mbili zinazopeana taarifa kupitia kituo hiki kwa kila mwaka hayakuwa na uhalisia. Hii ni kwa kuwa, malengo yaliyowekwa hayakuzingatia kazi zingine kama za manunuzi katika nyanja

za ukusanyaji na usimamizi na uandaaji wa sera ya kupeana taarifa, mambo ambayo yalitakiwa kufanyika kwa wakati mmoja.

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu programu ya uimarishaji uwezo wa kufanya utafiti katika Tume ya Sayansi na Teknolojia ulibaini kwamba, uandaaji wa malengo na viashiria visivyo na uhalisia ulitokana na waandaji wa mradi kuwa na matarajio ya juu kuhusu matokeo ya mradi. Ukaguzi ulibaini zaidi kwamba malengo na viashiria visivyo na uhalisia vimechangia kuzuia upimaji wa kiwango ambacho Tume imefanikiwa kutimiza malengo ya mradi uliotekelezwa. Suala hili pia limepelekea kuwa na utofauti wa malengo kati ya SIDA na Tume ya Sayansi na Teknolojia katika utekelezaji wa tafiti za shahada ya uzamivu.

9.1.3 Kutopitiwa kwa nyaraka za uanzishaji wa mradi

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu mradi wa uimarishaji uwezo wa kiutafiti katika Chuo Kikuu cha Ardhi pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia ulibaini kwamba taasisi hizo hazikufanya mapitio ya nyaraka za mradi ili kuweza kuwa na malengo yaliyoendana na uhalisia na kufanya makubaliano yaliyoafikiwa kutokana na mikataba kuwa na uhalisia.

Sehemu ya 4 ya Mwongozo wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uswidi kuhusu usimamizi wa misaada unataka vitengo vinavyotekeleza miradi kupitia upya makubaliano kuhusu majukumu na wajibu na kuzingatia mipango ya masuala yaliyokubaliwa wakati wa maandalizi. Hata hivyo, timu ya wakaguzi ilibaini kwamba nyaraka za uanzishaji wa mradi hazikupitiwa na Chuo Kikuu cha Ardhi pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia ili kujumuisha mabadiliko yoyote makubwa licha ya kuwepo kwa mabadiliko hayo makubwa yaliyotokea wakati wa utekelezaji wa mradi. **Jedwali 9.2** linaonesha baadhi ya changamoto kubwa zilizojitokeza wakati wa utekelezaji pamoja na madhara yake kwenye mradi.

Jedwali 9.2: Mabadiliko Makubwa ya Mradi na Changamoto Zilizotokana na Mabadiliko Hayo

Chuo/Taasisi	Shughuli ya Mradi	Mabadiliko yaliyojitokeza	Sababu za Mabadiliko
Chuo Kikuu cha Ardhi	Kuandaa na kuidhinisha mitaala wa shahada za uzamivu	Muda wa kuidhinisha mitaala ya shahada za uzamivu	Taratibu za uidhinishaji wa mitaala husika
Tume ya Sayansi na Teknolojia	Manunuzi na ufungaji wa mfumo wa usimamizi wa fedha	Muda wa manunuzi na ufungaji wa mfumo	Taratibu za manunuzi
Chuo Kikuu cha Ardhi	Kuandaa na kuidhinisha mitaala ya shahada za umahiri	Muda wa kuidhinisha mitaala ya shahada za umahiri	Taratibu za uidhinishaji wa mitaala husika
Tume ya Sayansi na Teknolojia	Kuanzishwa kwa hifadhi ya usimamizi wa tafiti	Muda wa uanzishaji	Kusuasua kwa mwenendo wa wanafunzi
Chuo Kikuu cha Ardhi	Kufanyika kwa tafiti	Muda wa kukamilika kwa tafiti	Kuchelewa kwa ukusanyaji wa data na uandaaji wa ripoti
Chuo Kikuu cha Ardhi	Mafunzo ya masomo ya uzamili	Muda wa wanafunzi kuhitimu masomo	Kusuasua kwa mwenendo wa wanafunzi
Chuo Kikuu cha Ardhi	Shughuli za huduma za kitaalamu kwa jamii	Namna ya kutekeleza huduma za kitaalamu kwa jamii	Bajeti ndogo ya kazi husika

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Programu za Kuimarisha Uwezo wa Kufanya Utafiti katika Chuo Kikuu cha Ardhi na Tume ya Sayansi na Teknolojia*

Jedwali 9.2 linaonesha kwamba kulikuwa na mabadiliko saba ambayo yalijitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli za miradi na hivyo kupelekea uhitaji wa kupitiwa upya ili kutathmini hatua zilizofikiwa au matokeo ya mradi ili kupunguza athari za kufikiwa kwa lengo zima la mradi. Baadhi ya mabadiliko makubwa yaliyojitokeza ni muda wa uidhinishaji wa mitaala ya shahada za umahiri na uzamivu, muda wa wanafunzi kuhitimu masomo, na kuanzishwa kwa usimamizi wa hifadhi ya

tafiti. Mabadiliko haya yameleta na yameendelea kuleta changamoto ya ufikiwaji wa malengo ya mradi.

Mabadiliko hayo yaliyojitokeza yaliathiri kiwango ambacho mradi ulifikia malengo yake kiufanisi, kwa tija na kiuwekevu wakati wa utekelezaji wa miradi kwa Chuo Kikuu cha Ardhi pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mfano, katika Chuo Kikuu cha Ardhi, programu haikuweza kufikia tarehe ya mwisho ya kufanya mahafali ya wanafunzi wa shahada ya uzamivu na hivyo kuwa na uchelewaji wa miezi 19 hadi kufikia muda wa kutoa ripoti za utafiti kwa kila programu ya mradi. Zaidi, mradi haukufanikiwa kupata idhini ya mitaala ya shahada za uzamili kutoka Tume ya Vyuo Vikuu hadi wakati wa kufunga mradi ulipofika.

9.3 Uratibu wakati wa Utekelezaji wa Miradi ya Uimarishaji Uwezo wa Utafiti

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu utekelezaji wa programu ya uimarishaji uwezo wa kufanya utafiti katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili ulibaini kuwepo kwa uratibu hafifu kati ya mamlaka zilizihusika na uidhinishaji katika mfumo uliopo wa kuidhinisha mitaala katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kuanzia katika ngazi ya idara hadi Baraza la Seneti la Chuo. Ilibainika kwamba uratibu hafifu katika ngazi ya mamlaka zinazohusika na uidhinishaji ilikuwa sababu kubwa ya kutoanzishwa kwa kozi mbili za shahada ya umahiri zilizohitajika.

Kulingana na lengo namba tatu la andiko la mradi, katika kipindi cha mwaka 2015/16 hadi mwaka 2019/20, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kilitakiwa kuanzisha kozi mbili za shahada ya umahiri zinazohusiana na maeneo ya kipaumbele katika sekta ya afya. Hata hivyo, kutokana na uratibu hafifu na mamlaka zinazohusika na uidhinishaji, Chuo kilishindwa kuanzisha shahada hizo.

Ukaguzi uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili ulibaini kuwepo kwa uratibu hafifu kwa shughuli za utafiti kulikotokana na utekelezaji hafifu wa namna zilizowekwa za kupeana matokeo ya utafiti. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kilipanga na kuandaa machapisho ya kisera kama namna ya kupeleka matokeo ya utafiti kwa kutafsiri matokeo ya utafiti kuwa machapisho ya kisera. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kwamba idadi ya

machapisho ya kisera yaliyoandaliwa wakati wa kipindi kilichotekeleza mradi hayakuwa toshelevu.

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu uimarishaji wa uwezo wa utafiti katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulibaini kwamba kulikuwa na uratibu hafifu wa taarifa za wanafunzi. Ukaguzi ulibaini kwamba uratibu wa taarifa ulichukua muda mrefu kukamilika. Hii ilitokana na kwamba mradi mmoja wa utafiti ulijumuisha nyanja nyingi ambazo zilifanywa na wanafunzi tofauti.

Ukaguzi pia ulibaini kwamba uratibu hafifu wa taarifa za wanafunzi ulitokana na kukosekana kwa uimarishaji wa mitandao ya ushirikiano katika ngazi ya mikoa na kimataifa ili kurahisisha upatikanaji na kupeana taarifa kati ya nchi shiriki zinazofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uswidi katika mradi husika.

Ukaguzi wa ufanisi kwa mradi wa kujenga mifumo ya ufanyaji tafiti bora na bunifu ulibaini kuwepo kwa uratibu hafifu wa ushirikiano kati ya vituo vya uvumbuzi, taasisi za utafiti, pamoja na vyuo vya elimu ya juu. Ilitarajiwa kwamba Tume ya Sayansi na Teknolojia pamoja na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogovidogo iunde muunganiko na ushirikiano kati ya vituo, taasisi za elimu ya juu, na taasisi za utafiti na maendeleo. Kutokana na nyaraka zilizopitiwa, ilibainika kwamba jitihada zilifanywa kuhakikisha kwamba kila kituo cha uvumbuzi kimeunganishwa na taasisi za elimu ya juu na za utafiti.

Ukaguzi wa ufanisi ulibaini kwamba Tume ya Sayansi na Teknolojia ilikuwa imeandaa Mfumo wa Kiutafiti na Kiuvumbuzi katika vituo vya uvumbuzi. Hata hivyo, mfumo huo wa ushirikiano uliopendekezwa kati ya taasisi za elimu, taasisi za utafiti na vituo haukuweza kuhuishwa katika taasisi husika. Badala yake, matokeo ya mapendekezo ndiyo yaliweza kufanya kazi katika muda mfupi. Mapitio ya ripoti za mwaka za miradi kwa kipindi cha mwaka kuanzia 2017/18 hadi 2018/19 yalibaini kwamba Tume ya Sayansi na Teknolojia ilianza majadiliano na jitihada za ushirikiano kati ya pande zote zinazohusika katika kuboresha ushindani kati ya vituo vya uvumbuzi.

Ukaguzi ulibaini pia kwamba hakukuwa na muunganiko imara na endelevu kati ya vyuo vikuu, taasisi za utafiti na maendeleo, na vituo vya uvumbuzi.

Vyuo vikuu vilikuwa vimejikita zaidi katika kazi za ushauri wa kitaalamu kwa kuwa wengi wao hawakuwa na miundombinu ya kuunga mkono na kushirikiana na vituo vya uvumbuzi.

Katika namna inayofanana, ukaguzi wa ufanisi katika Tume ya Sayansi na Teknolojia ulibaini kuwepo kwa uratibu duni wa shughuli za utafiti kulikosababishwa na upeanaji hafifu kwa taarifa za mapema kati ya vituo vya uvumbuzi kuhusu ratiba za maonesho na makongamano.

9.4 Ufanisi wa Programu

Mapitio ya ripoti nne za ukaguzi wa ufanisi yalibaini kuwa, taasisi nne za kiutendaji zilikuwa na viwango tofauti vya utendaji na ufikiwaji wa malengo. Kufikiwa kwa malengo kunasaidia kujua kiwango cha ufanisi katika kufikia malengo yaliyowekwa. Sehemu zifuatazo zinatoa muhtasari wa matokeo makuu na inaonesha kwa kiwango gani mipango hiyo imeweza kufikiwa kwa ufanisi.

9.4.1 Utekelezaji usiokamilika wa shughuli za programu iliyopangwa

Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi katika Tume ya Sayansi na Teknolojia ilibaini kuwa utekelezaji wa shughuli za programu haukukamilika na idadi kubwa ya shughuli hazikutekelezwa kabisa na mpango huo. Hii ilibainika katika kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za programu yaani kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20 isipokuwa mwaka wa fedha 2018/19 ambapo zaidi ya nusu ya shughuli za programu zilitekelezwa. **Jedwali 9.3** linaonesha hali ya utekelezaji wa shughuli za programu katika Tume ya Sayansi na Teknolojia.

Jedwali 9.3: Hali ya Utekelezaji wa Shughuli za Programu katika Tume ya Sayansi na Teknolojia

Mwaka wa Fedha	Shughuli Zote Zilizopangwa	Zilizotekelezwa	Zisizotekelezwa
2015/16	8	3	5
2016/17	11	5	6
2017/18	10	5	5
2018/19	12	10	2
Jumla	**41**	**23(56%)**	**18(44%)**

Chanzo: *Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Programu ya Kuimarisha Utafiti katika Tume ya Sayansi na Teknolojia*

Jedwali 9.3 linaonesha kuwa, kwa jumla, karibu asilimia 56 ya jumla ya shughuli zilizopangwa kati ya mwaka wa fedha 2015/16 na 2018/19 zilitekelezwa. Shughuli nyingi zilitekelezwa wakati wa mwaka wa fedha 2018/19 ambapo shughuli 10 kati ya 12 zilizopangwa zilitekelezwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa, utekelezaji usioridhisha wa shughuli zilizopangwa ulichangiwa na tabia ya kuhamishia shughuli mwaka unaofuata ambazo hazijatekelezwa katika mwaka uliopita. Ukaguzi pia uliripoti kuwa, utekelezaji usioridhisha wa shughuli zilizopangwa ulitokana na kuwa na viashiria visivyoendani na uhalisia katika kufikiwa kwa mipango ya utekelezaji iliyowekwa.

Jedwali 9.4: Orodha ya Shughuli na Fedha Zilizotumika lakini Hazioneshwi katika Mpango Mpya wa Mwaka

Mwaka wa Fedha	Shughuli Zilizotekelezwa lakini Hazionyeshwi katika Bajeti kwa Mwaka wa Fedha Husika	Aina ya Gharama	Matumizi ya Gharama Jumla (Sh.)
2017/18	Kuboresha mfumo wa usimamizi wa fedha	Mshauri	101,530,191
2018/19	Mafunzo ya uongozi wa Tume ya Sayansi na Teknolojia juu ya Mabadiliko ya Usimamizi katika Taasisi ya UONGOZI	Usafiri/chakula	27,637,500
	Watumishi wawili kupata mafunzo ya mawasiliano ya kisayansi	Usafiri wa anga, malipo ya kujikimu ya kila siku	57,900,750
Jumla			**187,068,441**

Chanzo: Mipango ya Mwaka na Taarifa za Fedha Zilizokaguliwa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Miaka ya Fedha kuanzia 2015/16 hadi 2018/19

Jedwali 9.4 linaonesha shughuli zilizofanywa lakini hazikuwepo katika bajeti ya miaka 2017/18 na 2018/19. Ilibainika kuwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ilitumia shilingi 187,068,441 katika kipindi hiki kwa shughuli ambazo hazikuwepo katika mipango ya kila mwaka. Utekelezaji wa shughuli za ziada ulipelekea kuwepo kwa tofauti kati ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa na shughuli halisi zilizopangwa katika kila mwaka husika.

9.4.2 Vyuo vikuu vilifanikiwa kufikia kiwango kinachoridhisha cha malengo ya Programu za Kuimarisha Utafiti

Ukaguzi unaohusu utekelezaji wa miradi ya utafiti katika vyuo vikuu vitatu ulibaini kwamba kulikuwa na utendaji wa kuridhisha kwa kuzingatia mafanikio ya jumla ya malengo ya miradi kama yalivyotekelezwa katika vyuo vikuu vitatu pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia. **Jedwali 9.5** linawasilisha matokeo ya uchambuzi huo.

Jedwali 9.5: Kufanikiwa kwa Malengo ya Programu ya Jumla

Taasisi	Kiwango cha Mafanikio (asilimia)
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	78
Chuo Kikuu cha Ardhi	58
Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili	Toshelevu
Tume ya Sayansi na Teknolojia	Toshelevu

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi wa Kuimarisha Uwezo wa Utafiti za Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tume ya Sayansi na Teknolojia na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili*

Jedwali 9.5 linaonesha mafanikio makubwa ya malengo ya programu wakati wa utekelezaji wa programu ya kuimarisha uwezo wa utafiti katika vyuo vikuu vitatu pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia. Wakati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ardhi vilifanikiwa kufikia asilimia 78 na 58 mtawalia ya malengo yao ya mpango, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Tume ya Sayansi na Teknolojia waliweza kufikia kiwango cha kuridhisha cha malengo yao.

Mapitio ya kila ripoti inaonesha kuwa kulikuwa na mfumo mzuri wa kusimamia matumizi ya fedha katika taasisi zote ambazo zilihitaji matumizi kabla ya kuomba fedha kwa matumizi yajayo. Mifumo ya ufadhili wa programu ambayo ilianzishwa ilisaidiwa katika kuhakikisha kuwa shughuli nyingi za programu zinakamilika kwa wakati na kwamba malengo yanafikiwa.

9.4.3 Kuchelewa kufikia mafanikio katika programu zote muhimu

Mapitio ya ripoti nne za ukaguzi wa ufanisi zilionesha kuwa kulikuwa na kuchelewa kufikia mafanikio kwa wakati kwa programu zote muhimu ikilinganishwa na mipango iliyopangwa dhidi ya utekelezaji wake. Mikataba iliyosainiwa kati ya taasisi zinazoshiriki na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uswidi iliweka muda maalumu wa kufikia malengo katika kipindi chote cha utekelezaji wa malengo hayo.

Hata hivyo, ripoti za ukaguzi zinaonesha kuwa baadhi ya matokeo muhimu yalicheleweshwa hivyo kuathiri utekelezaji wa mipango mengine. **Jedwali 9.6** linawasilisha matokeo muhimu yaliyocheleweshwa wakati wa utekelezaji wa programu.

Jedwali 9.6: Matokeo muhimu Yaliyochelewa Kufikiwa wakati wa Utekelezaji wa Programu za Kuimarisha Utafiti

Taasisi	Malengo Muhimu ambayo Yalichelewa	Athari kwa Mpango
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	• Kukamilisha Mafunzo ya Uzamivu • Kukamilisha Masomo ya Umahiri • Kuthibitishwa kwa kozi za uzamivu na umahiri • Ombi la Fedha za Programu • Ununuzi wa Vifaa vya Utafiti	• Kuchelewesha kukamilisha mafunzo ya umahiri na uzamivu
Chuo Kikuu cha Ardhi	• Shughuli za Utafiti wa Uzamivu • Kuendesha Mafunzo ya umahiri • Kudhibitishwa kwa kozi za uzamivu na umahiri • Ombi la Fedha za Programu • Shughuli za Utafiti • Kuanzishwa kwa Kituo cha Uvumbuzi wa Utafiti na Teknolojia • Uanzishwaji wa jarida mkondoni	• Kuchelewesha Kukamilisha masomo ya Uzamivu • Kutosajiliwa kwa Wanafunzi wa Shahada ya Umahiri
Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili	• Mafunzo na Utafiti wa wanafunzi wa uzamivu • Mafunzo ya Wanafunzi wa umahiri • Kuendeleza na Kudhibitisha Programu za Uzamivu • Kuendeleza na Kudhibitisha	• Kuchelewesha kuhitimu kwa Wanafunzi wa uzamivu na umahiri

Taasisi	Malengo Muhimu ambayo Yalichelewa	Athari kwa Mpango
	Programu za uzamili	
Tume ya Sayansi na Teknolojia	• Ununuzi na Ufungaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha • Kuanzishwa kwa Hifadhi ya Usimamizi wa Utafiti	• Upatikanaji mdogo wa ripoti za utafiti • Kucheleweshwa kwa Mafunzo ya Usimamizi wa Fedha

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi wa Utendaji wa Programu ya Kuimarisha Uwezo wa Utafiti*

Jedwali 9.6 linaonesha kuwa programu ilikabiliwa na ucheleweshaji wa kufikiwa kwa matokeo muhimu hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zingine zilizofuata. Vyuo vikuu vitatu vilichelewesha kupitisha na kufanya shughuli za utafiti kuhusiana na kozi za uzamivu. Hali hii iliathiri ratiba ya kumalizika kwa masomo ya uzamivu pamoja na wanafunzi kushiriki mahafali ya umahiri na uzamivu.

Mapitio ya ripoti za ukaguzi wa ufanisi kwenye vyuo vikuu vitatu na taasisi moja ya utafiti imeonesha kuwa programu nyingi zilizochelewa kupata matokeo ilisababishwa na kutokuwepo kwa umakini wakati wa kuweka mipango ambayo haikuzingatia taratibu na mpangilio ya kawaida katika kuidhinisha na kufanya mafunzo husika.

Matokeo yake, ucheleweshaji huo uliathiri ratiba nzima ya utekelezaji wa programu na hivyo kuhitaji kuongezwa kwa muda wa programu kutoka ule uliokubalika awali. Programu zote katika vyuo vikuu vitatu ziliomba kuongezewa muda ikiwa ni ishara ya kutofanikiwa kutekeleza mipango ya mafanikio ya awali.

9.4.4 Maboresho katika mazingira ya utafiti

Lengo kuu la programu ya kuimarisha uwezo wa utafiti lilikuwa kuongeza uwezo wa tafiti katika taasisi zote nne. Uwezo wa utafiti ulitarajiwa kuongezwa kupitia hatua ambazo zilipangwa kutekelezwa kutoka ndani na nje ya taasisi nne. Mapitio ya ripoti katika taasisi nne yalibaini kuwa kulikuwa na ongezeko kubwa la uwezo wa utafiti ikilinganishwa na kabla na baada ya programu.

Licha ya ukweli kwamba mipango mengi haikufanikiwa kwa idadi kama ilivyopimwa kupitia viashiria vya utendaji, kaguzi zote zimethibitisha kuwa uwezo wa utafiti umeongezeka na kuboreshwa kwa kiwango kikubwa. **Jedwali 9.7** linaonesha uwezo mbalimbali wa utafiti ambao umeboreshwa kutokana na hatua za programu ya kuimarisha uwezo wa utafiti.

Jedwali 9.7: Maeneo ya Utafiti Yaliyoimarika ikiwa ni Matokeo ya Programu

Maeneo ya Tafiti	Maboresho
Ushiriki	•Ushiriki mkubwa wa wafanyikazi katika programu •Kiwango cha juu cha ushirikiano na watafiti wa nje na vyuo vikuu
Ubora	•Uwezo wa kusimamia ubora wa utafiti (programu ya kugundua wizi wa maarifa ya wengine, majarida yaliyopitiwa na wenzao na ushiriki wa vyuo vikuu vya nje ya nchi)
Utawala	•Uwezo wa kusimamia programu/miradi mikubwa ya utafiti •Uwezo wa kushughulikia programu za utafiti wa ubia kati ya vyuo tofauti •Uwezo uliojengwa katika usimamizi wa ushirikiano
Usambazaji/ Uwepo	•Ongezeko kubwa la idadi ya machapisho •Idadi kubwa ya semina za usambazaji wa maarifa •Uwezo wa kusambaza matokeo kwenye media tofauti (majarida ya mtandaoni n.k.)
Ufadhili	•Uwezo wa kukuza/kuandika mapendekezo ya ruzuku za tafiti kubwa •Uwezo wa kusimamia fedha zinaotegemea matokeo

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi wa Programu ya Kuimarisha Uwezo wa Utafiti kwa Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Tume ya Sayansi na Teknolojia*

Jedwali 9.7 linaonesha kuwa kumekuwa na maboresho katika maeneo matano tofauti ya uwezo wa utafiti ikiwa ni matokeo ya makakati wa programu ya kuimarisha uwezo katika taasisi nne za selimu ya juu na utafiti. Maeneo muhimu ambayo yaliboreshwa sana ni pamoja na ushiriki, usimamizi wa ubora wa utafiti, usambazaji wa matokeo ya utafiti, na ufadhili wa shughuli za utafiti.

Ukaguzi wa ufanisi juu ya uwezo wa utafiti wa Chuo Kikuu cha Ardhi ulionesha kuwa awamu ya kwanza ya programu imewezesha asilimia 25 ya wafanyakazi wake wa kitaaluma kushiriki katika utafiti. Kiwango hiki cha ushiriki kilichangia uboreshaji wa kiwango cha uwezo katika Chuo katika maeneo tofauti kama inavyooneshwa katika **Jedwali 9.7**. Kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ukaguzi wa utendaji wa uimarishaji wa uwezo wa utafiti umebaini hali hiyohiyo kama ya Chuo Kikuu cha Ardhi.

9.4.5 Maboresho ya Upatikanaji wa Mtandaoni kwa Vifaa vya Utafiti na Mafunzo

Mapitio ya ripoti nne za ukaguzi wa ufanisi juu ya uimarishaji wa uwezo wa utafiti umeonesha kuwa kumekuwa na uboreshaji wa upatikanaji wa tafiti na zana za mafunzo ukiwa ni matokeo ya mpango wa kuimarisha uwezo unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uswidi. Ripoti zilizopitiwa zilionesha kuwa taasisi zote nne zilizoshiriki zimeongeza uwezo wa usambazaji wa matokeo ya tafiti na vifaa vya mafunzo kupitia kwa njia ya mtandao na makongamano. **Jedwali 9.8** linaonesha kiwango cha maboresho ya upatikanaji wa mtandao kwa ajili ya kupata taarifa za tafiti na vifaa vya mafunzo.

Jedwali 9.8: Kiwango cha Maboresho ya Upatikanaji wa Mtandao kwa Ajili ya Kupata Taarifa za Tafiti na Vifaa vya Mafunzo

Taasisi	Kiwango cha Ongezeko
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	• Asilimia 84 ya idadi lengwa ya makala kamili za majarida ya kielekitroniki zilizopakuliwa kati ya mwaka 2015 na 2020 • Asilimia 66 ya wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walipakia data za utafiti katika hifadhi ya utafiti
Chuo Kikuu cha Ardhi	Machapisho 1384 yalipatikana kati ya 2015 na 2020
Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili	Asilimia 100 ya vipakuzi vimepangwa (vipakuzi 16,885)
Tume ya Sayansi na Teknolojia	Kuanzishwa kwa Hifadhi ya Usimamizi wa Utafiti

***Chanzo**: Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Kuimarisha Uwezo wa Utafiti*

Jedwali 9.9 linaonesha kuwa kulikuwa na ongezeko la matumizi ya machapisho ya mtandaoni kupitia majukwaa yaliyotengenezwa wakati wa utekelezaji wa mpango wa kuimarisha uwezo wa utafiti. Maeneo

yaliyopata matokeo zaidi yalijumuisha kupakua machapisho ya mtandaoni na matumizi ya majukwaa ya mtandao kupakuwa matokeo ya tafiti.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilifikia lengo la asilimia 84 ya idadi ya makala kamili za majarida ya kielekitroniki kuanzia mwaka 2015 hadi 2020. Kwa upande mwingine, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kiliweza kufikia lengo la asilimia 100 ya upakuaji wa machapisho ambapo jumla ya machapisho 16,885 yalipakuliwa katika kipindi cha miaka 4 ya fedha kuanzia mwaka 2016/17. Taasisi pia ziliweza kuanzisha majukwaa ya upatikanaji wa tafiti. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Ardhi na Tume ya Sayansi na Teknolojia zilianzisha majarida na hazina za usimamizi wa utafiti

9.5 Ufadhili wa Programu

Utekelezaji wa shughuli za programu uliwezeshwa na mtiririko wa fedha kutoka kwa mshirika wa kifedha ambaye ni Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uswidi kwenda kwa washirika watekelezaji (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, na Tume ya Sayansi na Teknolojia). Mapitio ya ripoti nne za ukaguzi wa ufanisi wa mpango wa kuimarisha uwezo ulibaini udhaifu kama ilivyoainishwa hapa chini.

9.5.1 Fedha za programu zilizoidhinishwa zilitolewa kulingana na maombi yaliyofanyika

Ripoti ya Ukaguzi wa Utendaji wa Kuimarisha Uwezo wa Utafiti katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilionesha kuwa, Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uswidi lilitoa fedha kulingana na kiwango kilichoombwa ilimradi Chuo kitimize mahitaji yaliyowekwa na mhisani kama vigezo vya malipo. Hii pia ilithibitishwa kupitia ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uswidi na Ripoti za Maendeleo za kuanzia Mwaka 2015/16 hadi 2019/20 isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2018/19 kama **Kielelezo 9.1 k**inavyoonesha.

Kielelezo 9.1: Bajeti Iliyoidhinishwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam



Chanzo: *Bajeti Iliyoidhinishwa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uswidi na Taarifa za Fedha Zilizokaguliwa za kuanzia mwaka 2015/16 - 2019/20*

Kielelezo 9.1 kinaonesha kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2019/20, Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Uswidi lilitoa asilimia 104 ya kiasi kilichoombwa. Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2017/18, Sida ilifanikiwa kutoa kiasi chote cha fedha kilichoombwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kulingana na bajeti, na lilizidisha kiasi kilichoombwa kwa miaka miwili (yaani miaka 2016/17 na 2017/18). Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2018/19, Sida ilitoa kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam asilimia 51 tu ya kiasi cha fedha za programu kilichoidhinishwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa mwaka 2018/19, Sida ilichelewa kutoa fedha kwa awamu ya pili ya Januari hadi Juni. SIDA ilitoa fedha kwenda kwenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 2019/20, ndiyo maana jumla ya fedha zilizopokelewa mwaka 2019/2020 ilikuwa Krona za Uswidi 22,261,427 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 5.4 ambazo ni pamoja na Krona za Uswidi 8,656,744 sawa na shilingi za Tanzania bilioni 2.1 kwa mwaka 2018/19. Hata hivyo, ilibainika zaidi kuwa Sida ilichelewesha kutoa fedha kwa awamu ya pili kwa sababu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilichelewa kuomba fedha kulingana na ratiba za awamu.

9.5.2 Kuchelewa kuomba fedha za programu kulingana na ratiba za awamu

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu Kuimarisha Uwezo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa kuomba fedha. Ripoti hiyo ilifafanua zaidi kuwa, barua za maombi ya fedha kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam zilizoelekezwa kwa Ubalozi wa Uswidi zilicheleweshwa hivyo kusababisha utoaji wa fedha za awamu pia kuchelewa.

Hali hii imekuwa ikijirudia kila zinapoombwa fedha katika awamu zote za utekelezaji wa programu. Kwa mfano, awamu ya pili ya 2018/19 ambayo ilikuwa Januari – Juni mwaka 2019, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliomba fedha tarehe 13 Juni 2019 kupitia barua yenye Kumb. Na. Z10/S.4 iliyoelekezwa kwa Ubalozi wa Uswidi na kutiwa saini na Makamu Mkuu wa Chuo. Mapitio ya barua za maombi ya fedha yalionesha kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hakikuweza kuomba fedha kwa wakati kutoka Sida wakati wote wa utekelezaji wa programu hadi Juni 2020. Ukaguzi ulibaini zaidi kwamba ucheleweshaji uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutuma maombi ya fedha kwa ajili ya mradi ilikuwa miezi 5 wakati wa malipo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/20 ucheleweshaji wa chini ulikuwa ni miezi 2 katika kipindi cha miaka ya fedha 2016/17 na 2017/18 na malipo ya pili ya mwaka wa fedha wa 2019/20.

Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Kuimarisha Uwezo wa Utafiti katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulibaini kuwa, ucheleweshaji ulichangiwa zaidi na sababu kama kuchelewa kwa michakato ya idhini ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na kusubiri mikutano ya Seneti ambayo inakaa mara moja kwa kila robo mwaka. Kupitia mikutano ya Seneti mipango ya utekelezaji ya kila mwaka na kwa kila bajeti ndogo ya programu huidhinishwa kulingana na vigezo vya ulipaji wa fedha za Sida. Zaidi ya hayo, matumizi chini ya fedha zilizotolewa katika kipindi kilichopangwa pia zilikuwa sababu ya ucheleweshaji wa kuomba fedha.

Ucheleweshaji uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kuomba fedha kutoka Sida ulichangia ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kwa ajili ya programu kwa kila awamu. Hii ni kwa sababu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilitarajiwa kupokea fedha zilizoombwa kutoka Sida mara mbili kwa mwaka, yaani Julai na Februari kwa kila mwaka wa fedha. Hata hivyo,

ukaguzi kupitia taarifa za benki za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na SIDA ulionesha kuwa fedha za awamu kutoka SIDA hazikutumwa kwa wakati kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo 9.2** kutokana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuchelewa kuomba.

Kielelezo 9.2: Ucheleweshaji wa Utoaji wa Fedha za Programu



Chanzo: *Taarifa za Benki za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam-SIDA na Maombi ya Fedha kuanzia mwaka 2015/16 - 2019/20*

Vivyo hivyo, ukaguzi wa ufanisi kuhusu utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha Uwezo wa Utafiti na Ubunifu wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira kwa Maendeleo Jumuishi ulibaini kuwa, kulikuwa na ucheleweshaji wa ombi la kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za programu. **Kielelezo 9.3** kinaonesha kiwango cha ucheleweshaji wa kutuma maombi ya fedha kwa kipindi cha kati ya Julai 2015 na Juni 2020.

Kielelezo 9.3: Kiwango cha Uchelewaji wa Kutuma Maombi ya Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Programu kuanzia Mwaka 2015/16 hadi 2019/20



Chanzo: *Barua za Maombi ya Malipo na Stakabadhi kwa Kipindi kati ya Julai 2015 na Juni 2020*

Kielelezo 9.3 kinaonesha ucheleweshaji wa kuomba fedha ulikuwa wa kawaida katika miaka yote ya kifedha ambayo programu hiyo ilitekelezwa. Kielelezo kinaonesha pia kuwa kilele cha kwanza cha ucheleweshaji ulikuwa mwaka 2016/17 wakati ombi la 1 na la 2 yalicheleweshwa kwa zaidi ya siku 60.

Ucheleweshaji mkubwa wa pili wa maombi ya fedha ulibainika katika mwaka wa fedha wa 2018/19. Ukaguzi wa ufanisi kuhusu uimarishaji wa uwezo wa utafiti katika Chuo Kikuu cha Ardhi unaonesha kuwa ucheleweshaji huu ulisababishwa na mrundikano wa tafiti ambazo kwa wakati huo zilikuwa zimetumia kiasi kikubwa cha fedha za programu, lakini zilikuwa hazijaandaa ripoti za uwajibikaji kuonesha jinsi fedha zilizokuwa zimetolewa hapo awali zilivyotumika (kurejesha masurufu ili kudhibitisha matumizi ya fedha).

Pia, ukaguzi wa ufanisi juu ya uimarishaji wa uwezo wa utafiti katika Chuo Kikuu cha Ardhi ulionesha kuwa, kutokana na ucheleweshaji wa maombi ya fedha, kulikuwa na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha zilizoombwa kuwezesha utekelezaji wa shughuli za programu. **Kielelezo 9.4** hapa chini kinathibitisha kuwepo kwa ucheleweshaji wa utoaji wa fedha wa kati ya miezi 2 na 6.

Kielelezo 9.4: Utoaji wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Programu kuanzia 2015/16 hadi 2019/20



Chanzo: *Barua za Maombi ya Malipo na Stakabadhi kwa Kipindi cha kati ya Julai 2015 na Juni 2020*

Kielelezo 9.4 kinaonesha kuwa kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa wa utoaji wa fedha zilizoombwa, ambapo ucheleweshaji ulikuwa wa kati ya siku 45 na 170. Takwimu hizo pia zinaonesha kuendelea kuongezeka kwa ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kwa kila mwaka wa fedha kutoka 2017/18 hadi 2019/20. Malipo ya awali ya mwaka wa fedha 2015/16 yalicheleweshwa kwa siku 45 tu, wakati malipo ya pili ya 2019/20 yalicheleweshwa kwa takribani siku 170. Kwa ujumla, fedha zilicheleweshwa kwa sababu ya urejeshaji wa masurufu kwa fedha zilizotumika katika kipindi cha malipo ya awali. Hiyo inamaanisha wakati mwingine fedha hizo zimekuwa zikipokelewa kwa kutekeleza shughuli za programu wakati muda uliohitajika kutumia (miezi sita) ulikiwa umekwisha.

9.5.3 Kutofikiwa kwa asilimia 70 ya kiwango kilichowekwa cha matumizi ya fedha zilizotolewa

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu uimarishaji wa uwezo wa tafiti katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulibaini kutofikiwa kwa kiwango cha matumizi ya fedha kilichopangwa kulingana na makubaliano yaliyosainiwa. Ukaguzi wa taarifa zilizokaguliwa za zedha za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na SIDA za miaka kuanzia 2015/16-2018/19 ulibaini kuwa Chuo Kikuu cha Dar es

Salaam hakikutumia vya kutosha fedha zote ambazo zilitolewa na SIDA kwa utekelezaji wa shughuli zilizoidhinishwa kulingana na mpango wa utekelezaji wa kila mwaka.

Chuo Kikuu ch Dar es Salaam hakikuweza kutumia kikamilifu fedha zilizotolewa kwa miaka yote minne. Uwezo wa matumizi kwa ujumla ulibainika kuwa wa asilimia 49 kwa wastani kwa miaka 4, ambao ulikuwa chini ya kiwango kilichotakiwa cha asilimia 70 (kiwango kilichopangwa). Zaidi, katika mwaka wa fedha 2017/18, fedha zilizotumiwa zilikuwa chini ya asilimia 40, ambapo inaonesha kuwa shughuli zingine zilizopangwa kwa kipindi husika hazikutekelezwa kama ilivyopangwa.

Kwa kuongezea, hadi Juni 2019, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hakikuweza kutumia fedha shilingi bilioni 4.1 (sawa na Krona za Uswidi 16,527,175). Hii ilisababisha kurudi nyuma kwa shughuli zingine za programu ambazo zilitakiwa kutekelezwa kwa sababu zilipaswa zisitekelezwe hadi mpango wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Sida ulipokuwa ukihitimishwa. Hali hii ilikilazimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuomba muda wa nyongeza ili kukamilisha utekelezaji wa shughuli ambazo hazikufanywa kabisa.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hakikupanga shughuli za programu kwa kuzingatia hali halisi. Kwa sababu hiyo, watekelezaji wa programu walikuwa wakijitahidi kutekeleza shughuli zilizopangwa ambazo zilisababisha matumizi kuwa chini ya kiwango cha matumizi ya fedha kilichopangwa.

Ukaguzi wa ufanisi juu ya Utekelezaji wa Programu ya Kuimarisha Uwezo wa Utafiti na Ubunifu wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi na Mazingira kwa Maendeleo Jumuishi pia ulionesha kuwa, fedha zilizotengwa kutekeleza shughuli zote hazikutekelezwa kwa ukamilifu. Kwa wastani, programu ndogo ilitumia chini ya asilimia 70 ya fedha zilizopokelewa kwa utekelezaji wa programu. **Kielelezo 9.5** kinawasilisha jumla ya fedha zilizotengwa na zilizotumiwa katika kiwango cha programu ndogo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2015 hadi Juni 2019.

Kielelezo 9.5: Asilimia ya kiasi kilichotengwa na Kutumika katika Kiwango cha Programu Ndogo kati ya Julai 2015 na Juni 2019



Chanzo: *Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kwa Uimarishaji Uwezo wa Kufanya Utafiti katika Chuo Kikuu cha Ardhi*

Kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo 9.5**, kiwango cha matumizi ya fedha katika programu ndogondogo kilikuwa chini ya asilimia 80. Programu ndogo zinazohusiana na Upatikanaji wa Rasilimali za Ardhi Hatarishi na VVU/UKIMWI nchini Tanzania zilitumia chini ya nusu ya bajeti zao wakati Vipengele vya Msaada wa Utafiti na Programu ya Huduma za Kitaalamu kwa Jamii na Kutafuta Njia Mbadala ya Mipango Miji kwa Mji Mdogo ilitumia zaidi ya asilimia 75 ya bajeti.

Ukaguzi ulibaini kuwa miongoni mwa sababu kubwa za ucheleweshaji wa utumiaji wa fedha zilizopokelewa ni kuchelewesha ununuzi wa vifaa vya utafiti vilivyoombwa kwa kipindi cha kati ya mwezi mmoja hadi miezi 30. Kwa kuongezea, ukaguzi ulibaini zaidi kuwa ucheleweshaji wa utumiaji wa fedha kwa kila programu ndogo pia ulisababishwa na ucheleweshaji wa kulipia fedha za wanafunzi na fedha za utafiti.

Kielelezo 9.6: Kiasi cha Ucheleweshaji wa Kulipa Posho za Wanafunzi



Chanzo: *Mapitio ya barua za maombi kwa sampuli za wanafunzi wa chini ya programu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam-SIDA na Vocha za Malipo, 2020*

Kielelezo 9.6 kinaonesha kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilichukua zaidi ya mwezi mmoja kulipa fedha za posho za wanafunzi. Ucheleweshaji ulikuwa mkubwa zaidi kwa wanafunzi wanaofanya shahada za uzamivu katika uvumbuzi na uendelezaji ambao ilikuwa siku 49. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa ucheleweshaji wa utoaji wa fedha si wa aina moja kwa wanafunzi wote. Wanafunzi wanaosoma shahada za uzamivu katika uhakika wa chakula walipokea malipo yao mapema.

Matokeo yalionesha kuwa wanafunzi wengi waliweza kupata fedha kwa muda uliowekwa. Timu ya ukaguzi ilichambua zaidi kujua idadi ya wanafunzi waliokumbwa na tatizo la ucheleweshaji. Matokeo ya uchambuzi yamewasilishwa kwenye **Mchoro 9.7.**

Kielelezo 9.7: Idadi ya Wanafunzi wa Shahada ya Umahiri ambao Walichelewa kupata Fedha



Chanzo: *Mapitio ya barua za maombi kwa sampuli za wanafunzi walio chini ya Mradi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam-SIDA na Vocha za Malipo, 2020*

Kielelezo 9.7 kinaonesha kuwa wanafunzi katika kozi zote za umahiri waliathiriwa na ucheleweshaji wa malipo ya posho za kujikimu. Wanafunzi wanaofanya kozi za umahiri katika hisabati na usimamizi jumuishi wa usafi wa mazingira walikuwa miongoni mwa walioathirika zaidi wakichukua siku 26 kupata fedha zao.

9.5.4 Matumizi ya fedha chini ya kiwango katika Chuo Kikuu cha Ardhi yalipelekea fedha kubadilishiwa matumizi

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu programu ya kuimarisha uwezo wa kufanya utafiti katika Chuo Kikuu cha Ardhi ulibaini kwamba fedha za mradi hazikutumiwa kwa kiwango kilichotarajiwa katika baadhi ya shughuli za mradi. Kulingana na ripoti, matumizi ya chini ya kiwango yalisababishwa na kutofanyika kwa baadhi ya shughuli za mradi ambazo zilifuatana kwa mtiririko mmoja baada ya mwingine. Kwa mfano, ufanyaji wa makongamano na shughuli za machapisho iliwezekana tu iwapo kazi za utafiti zingekuwa zimekamilika. **Jedwali 9.14** linaonesha matumizi ya

fedha chini ya kiwango kwa machapisho na makongamano kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2018/19.

Jedwali 9.9: Matumizi ya fedha chini ya kiwango kwa shughuli za machapisho pamoja na makongamano kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2018/19

Shughuli	Mwaka wa Fedha	Jumla ya Fedha zilizotengwa (TSh.)	Matumizi (TSh.)	Asilimia ya Matumizi (%)	Kiwango Kilichobaki (TSh.)
Machapisho	2017/18	19,123,200	-	0	19,123,200
	2018/19	28,785,723	-	0	28,785,723
Makongamano	2017/18	233,906,400	95,636,640	45	138,269,760
	2018/19	350,347,131	139,420,463	40	210,926,668

Chanzo: *Ripoti za Utekelezaji za Mwaka kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2018/19*

Jedwali 9.9 linaonesha kwamba kulikuwa na matumizi ya chini ya kiwango kwa fedha za mradi katika Chuo Kikuu cha Ardhi ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichopokelewa. Katika kipindi cha miaka miwili ya fedha ya 2017/18 na 2018/19, mradi ulifanikiwa kutumia asilimia 45 na 40 pekee, mtawalia, ya jumla ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya machapisho na makongamano. Matumizi haya ya fedha chini ya kiwango yalifanya mrundikano wa fedha wa zaidi ya shillingi milioni 300 kwa mambo mawili tu katika miaka miwili ya fedha. Mrundikano huo wa fedha ulikuwa ukitengeneza fedha zisizokuwa na matumizi ambazo zilikuwa na uwezekano mkubwa wa kuathiri kiwango cha jumla cha matumizi ya fedha zilizotolewa na hivyo kuathiri utekelezaji wa kazi nyinginezo katika mradi.

Matokeo yake, matumizi ya chini ya kiwango ya fedha za mradi yalipelekea kubadilishwa kwa matumizi ya fedha kwenda katika shughuli zingine za mradi. Kupitia majadiliano na maofisa wa mradi, ilielezwa kwamba kubadilishwa kwa matumizi ya fedha za mradi kulitokana na matumizi ya chini ya kiwango cha shughuli ambazo zilishatengewa fedha. Hii ilifanyika ili kuwezesha kufikiwa kwa kiwango cha matumizi kwa asilimia 70 ya fedha zote zilizotolewa ambayo ilitakiwa kufikiwa ili kukidhi vigezo vya kupewa fedha zingine.

9.6 Uendelevu wa Miradi katika Taasisi

Utekelezaji wa shughuli za mradi katika taasisi nne ulijumuisha matumizi ya kiwango cha kutosha cha rasilimali ndani ya nchi kutoka serikalini pamoja na wadau wa maendeleo. Katika mtazamo huo, utekelezaji wa miradi ulitakiwa kufanywa katika namna itakayohakikisha uwepo wa uendelevu wa miradi na kwamba matokeo yaliyopatikana kwa sasa yanaendelea kuzinufaisha taasisi zinazotekeleza pamoja na nchi kwa ujumla wake.

Hata hivyo, mapitio ya taarifa nne za ukaguzi kuhusu programu za kuimarisha uwezo wa kufanya utafiti katika taasisi zilizotekeleza miradi imeonesha dalili zinazoweza kuathiri kiwango ambacho matokeo ya mradi na faida zake zitakuwa endelevu. **Jedwali 9.10** linaonesha baadhi ya mambo yaliyopo hivi sasa yanayoweza kuathiri uendelevu wa matokeo ya miradi hiyo.

Jedwali 9.10: Mambo yanayoweza kuathiri uendelevu wa miradi

Taasisi	Jambo Husika
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam	Asilimia 47 ya wanafunzi wa shahada ya uzamivu hawajishughulishi na kazi za utafiti au ufundishaji.
Chuo Kikuu cha Ardhi	Hakuna waombaji wapya kwa kozi mpya za shahada za umahiri na uzamivu.
Tume ya Sayansi na Teknolojia	Hakuna mipango ya ufuatiliaji wa vituo vya ubunifu.
Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili	Hakuna waombaji wapya wa shahada za uzamivu kwenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI, afya ya uzazi ya mama na mtoto, malaria na magonjwa yasiyoambukiza

Chanzo: *Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Uimarishaji Uwezo wa Kufanya Utafiti*

Jedwali 9.15 linaonesha kwamba taasisi zote zilizotekeleza mradi zilikuwa na mambo tofauti yaliyoleta hatari ya kuwa na mwendelezo wa mradi. Moja ya mambo yaliyoonekana katika sehemu nyingi ni kutokuwepo kwa waombaji wapya kwa kozi mpya zilizoanzishwa. Jambo hili lilibainika katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Chuo Kikuu cha Ardhi, na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kutokuwepo kwa waombaji ilimaanisha kwamba kozi zilizoanzishwa zitashindwa kuendelea kwa kipindi

fulani hadi maombi yatapokelewa au mazingira mapya yatakapoongezwa ili kuwavutia waombaji.

Zaidi, ukaguzi wa ufanisi kuhusu uimarishaji wa uwezo kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ulibaini kwamba asilimia 47 ya wanafunzi wote wa shahada za uzamivu hawakuwa wafanyakazi wa Chuo na hawakuwa wakijihusisha moja kwa moja na shughuli za utafiti na ufundishaji. Jambo hili litaathiri mwendelezo wa uwezo wa kufanya utafiti katika Chuo kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wanufaika wa mradi ambao hawatajihusisha na shughuli za utafiti baada ya kumaliza masomo yao.

SURA YA KUMI

MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU USIMAMIZI WA ULIPAJI NA UREJESHAJI WA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU

10.1 Utangulizi

Ili kurahisisha sera ya uchangiaji wa gharama za elimu ya juu, mwaka 2004 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Namba 9 ya Mwaka 2004, ambayo ilianzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kusimamia mpango wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kazi ya msingi ya Bodi ya Mikopo, mbali na zingine, ni kuwezesha upatikanaji wa elimu ya juu kwa wanafunzi ambao wazazi/walezi wao hawawezi kumudu kulipia elimu ya juu. Walengwa wa mkopo wanatakiwa kulipa mikopo katika kipindi cha miaka 10 ili kuifanya Bodi ya Mikopo kuwa endelevu.

Tangu kuanzishwa kwake, Bodi ya Mikopo imekuwa ikipata changamoto kadhaa, ambazo kati ya zingine, ni ucheleweshaji wa utoaji wa mikopo, ulipaji na urejeshaji hafifu au kutolipa mikopo. Moja ya sababu za Bodi kufanya kazi chini ya uwezo ni kwamba Bodi ilikuwa ikipata ufadhili wa kiwango cha chini kutoka Serikalini kwa kipindi chote kilichoangaliwa. Pia, ilibaini kuwa kulikuwa na utendaji usioridhisha wa Bodi katika ufuatiliaji wa urejeshaji wa mikopo na hivyo kuleta shaka kubwa juu ya uendelevu Bodi katika kutoa mikopo kwa wanufaika wapya.

10.2 Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inatoa matokeo ya ukaguzi juu ya usimamizi wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kulingana na mawanda ya ukaguzi, sehemu hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni hali ya utekelezaji wa shughuli za ulipaji na urejeshaji wa mikopo; na ubunifu na mwenendo wa ufuatiliaji wa mikakati ya ulipaji na urejeshaji wa mikopo. Mapungufu yaliyobainika ni kama yanavyoelezwa hapa chini.

10.2.1 Malengo ya Ukusanyaji wa Mikopo Hayakulingana na Ukusanyaji Halisi

Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ilitoa jumla ya shilingi za trilioni 2.14 kuanzia mwaka 2012/2013 hadi 2016/2017. Hii inaonesha kuwa fedha nyingi zilitolewa kwa madhumuni ya kufadhili mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Ukaguzi ulipitia hali ya ulipaji wa mikopo kwa kuzingatia mambo anuwai ikiwa pamoja na ukusanyaji wa jumla dhidi ya malengo yaliyowekwa, ufuatiliaji, utozaji, na ukusanyaji wa mikopo kwa kipindi cha miaka mitano ya fedha kuanzia 2012/2013 hadi 2016/2017 na kubaini kuwa haukuwa wa ufanisi.

Bodi ya Mikopo haikuweza kufikia lengo la ukusanyaji wa mikopo. Tathmini ya utendaji wa Bodi ilionesha kuwa ukusanyaji wa mikopo ya kila mwaka unaofanywa dhidi ya mikopo inayostahili kulipwa kwa hesabu za jumla ilikuwa kati ya asilimia 32 na 48 kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013 hadi 2016/2017. Asilimia 35 tu ilikusanywa badala ya asilimia 70 ambayo ililengwa katika mwaka wa fedha 2013/2014. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, ni asilimia 48 tu ilifikiwa mwishoni mwa mipango mkakati husika badala ya lengo la asilimia 80.

10.2.2 Idadi ya Mikopo Iliyofuatiliwa Haikulingana na Mikopo Inayostahili

Timu ya ukaguzi ilitumia taarifa za wanufaika wa mikopo iliyotolewa kutoka kanzidata ya Bodi ya Mikopo kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013 hadi 2016/2017 na kujaribiza mwitikio wa wanufaika wa mikopo waliopatikana. Matokeo yalionesha kuwa kanzidata hiyo ilikuwa na jumla ya walengwa wa mikopo 115,819 na mikopo ya jumla ya shilingi trioni 2.4 na shilingi trilioni 2.33 ambazo hazijakusanywa. Kwa mujibu wa ripoti zake, Bodi ya Mikopo ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 221 kuanzia mwaka 2012/2013 hadi 2016/2017 kutoka kwa wanufaika wa mkopo wapatao 115,903.

Bodi ya Mikopo ilitakiwa kutunza kanzidata inayokwenda na wakati ya wanufaika wa mikopo ili kurahisisha ulipaji na urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika hao. Hata hivyo, kutokana na ugumu wa upimaji wa utendaji wa Bodi ya Mikopo na kiwango kilichokusanywa dhidi ya mikopo inayostahili, timu ya ukaguzi ilizingatia mwelekeo mwingine ambapo idadi ya wanufaika wa mikopo na mikopo inayostahili kulipwa ilizingatiwa.

Ukaguzi ulikagua taarifa kutoka kwenye kanzidata ya ulipaji wa mikopo zilizokuwa zinatumika wakati wa ripoti hii na kubainisha kuwa Bodi ilibaini asilimia 23 hadi 51 ya wanufaika wa mikopo inayostahili kulipwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 10.1.**

Jedwali 10.1: Idadi ya Wanufaika wa Mikopo na Mikopo Inayostahili Kulipwa kwa Mwaka

Mwaka wa Fedha	Idadi Jumuishi ya Wanufaika wenye Mikopo Inayostahili Kulipwa	Idadi Jumuishi ya Wanufaika wa Mikopo Waliobainishwa	Wanufaika wa Mikopo Waliobainishwa (%)
2012/2013	137,204	31,932	23
2013/2014	143,281	40,414	28
2014/2015	177,017	53,304	30
2015/2016	242,011	79,555	33
2016/2017	269,182	138,485	51

Chanzo: *Kanzidata ya Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo, Taarifa za Bodi ya Mikopo kwa Mwaka 2018*

Kwa kuzingatia uchambuzi katika **Jedwali 10.1**, Bodi ya Mikopo iliweza kubaini wastani wa asilimia 33 ya wanufaika wa mikopo inayostahili kulipwa kwa mwaka kwa kipindi cha miaka mitano. Vivyo hivyo, ilibainika kuwa kwa miaka mitatu iliyopita, kiwango cha kutafuta wanufaika wapya wa mikopo wenye mikopo inayostahili kurejeshwa kiliongezeka kutoka asilimia 28 hadi 51 ya wanufaika wa mikopo kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014 hadi 2016/2017. Hata hivyo, ongezeko hilo halikushabihiana na idadi iliyokuwa ikiongezeka ya wanufaika wenye mikopo inayostahili kurejeshwa. Pia, idadi zaidi ya wanufaika wa mkopo iliongezeka sana katika mwaka 2016/2017 hadi kufikia asilimia 51 ikilinganishwa na miaka iliyopita.

10.2.3 Kiwango cha Chini cha Mikopo Inayolipika

Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Mwaka 2004 inataka kila mnufaika wa mikopo kuwajibika kulipa mkopo baada ya miaka miwili ya kipindi cha mpito. Sehemu hiyo ya sheria pia inatoa adhabu kwa wanufaika na waajiri ambao wanashindwa kulipa mkopo au kukata makato kutoka kwa wafanyakazi bila kuwa na sababu ya msingi.

Kwa mujibu wa kanzidata ya Bodi ya Mikopo kuhusu mikopo inayostahili kulipwa, ilibainika kuwa kulikuwa na idadi ya mikopo inayostahili kulipwa ambayo haikulipwa kwa muda mrefu. Matokeo yalionesha kuwa kuanzia mwaka 1994 hadi 2017, kulikuwa na jumla ya shilingi bilioni 801.3 za mikopo isiyolipwa. Udhaifu zaidi uliobainishwa umeelezewa hapa chini.

Timu ya ukaguzi ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia taarifa za mikopo iliyobainika kama ilivyotolewa na Badi ya Mikopo ili kuona iwapo walengwa wa mikopo walikuwa wakilipa mikopo yao. Kwa kuwa taarifa iliyotolewa kwa wakaguzi haikuwa katika mwaka wa kifedha, timu ya ukaguzi ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia mwaka wa kalenda ya kawaida na matokeo yalionesha mwenendo wa ufuatiliaji kama ilivyooneshwa kwenye **Kielelezo 10.1.**

Kielelezo 10.1: Mikopo Inayostahiki kwa kila Mwaka wa Kalenda Ikilinganishwa na Idadi ya Mikopo



	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17
Kiasi cha Mikopo kwa Mujibu wa Kanzidata	29,586	29,756	35,768	28,936	68,352
Idadi ya Wadaiwa wa Mikopo Waliobainishwa	9,350	8,482	12,890	26,251	58,930
Asilimia ya Mikopo Iliyorejeshwa	32	29	36	91	86

Chanzo: *Uchambuzi wa Ukaguzi kwa Miaka ya Fedha 2012/13 hadi 2016/17*

Kielelezo 10.1 kinaonesha kuwa, Bodi ya Mikopo iliainisha idadi kubwa ya wanufaika wa mikopo pamoja na mikopo inayostahili kurejeshwa ingawa kiwango cha wastani cha mikopo iliyolipwa kwa miaka mitano iliyopita kilikuwa asilimia 55 ambapo ulipaji wa juu ukiwa asilimia 91 kwa mwaka 2015/2016 na wa chini zaidi ukiwa asilimia 29 kwa mwaka 2013/2014. Hii

inamaanisha kuwa karibu asilimia 44 ya wanufaika walikuwa wakilipa mikopo yao wakati asilimia 56 walikuwa hawalipi hadi kufikia mwaka 2017.

10.2.4 Mwenendo Usioridhisha wa Urejeshaji wa Mikopo Inayostahili Kulipwa kutoka kwa Wadaiwa

Ukaguzi ulibaini kuwa, kulikuwa na udhaifu katika urejeshaji wa mikopo iliyokuwa inastahili kurejeshwa. Uchambuzi kutoka kanzidata ya mikopo ya Bodi ya Mikopo ambayo ilitakiwa kulipwa ilionesha kuwa Bodi haikuweza kusimamia urejeshaji wa mikopo inayostahili kama ilivyooneshwa katika **Jedwali 10.2.**

Jedwali 10.2: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mikopo Inayostahili Kulipwa kwa Mwaka

Mwaka wa Fedha	Jumla ya Mikopo Ambayo Haijalipwa (Sh. Bilioni)	Jumla ya Makusanyo ya Mwaka ya Mikopo Inayostahili Kulipwa (Sh. Bilioni)	Kiwango cha Makusanyo ya Mwaka (%)
2012/2013	95.9	25.05	26
2013/2014	82.5	19.39	24
2014/2015	81.8	20.64	25
2015/2016	42.9	13.15	31
2016/2017	15.9	2.93	18
Total	**319**	**81.16**	**25**

Chanzo: *Kanzidata ya Ulipaji na Urejeshaji ya HESLB, 2018*

Jedwali 10.2 linaonesha kuwa Bodi ilikuwa na jumla ya shilingi za bilioni 319 za mikopo iliyostahili kulipwa kwa miaka mitano ya fedha. Uchambuzi wa taarifa za Bodi ya Mikopo unaonesha kuwa jumla ya ukusanyaji wa mikopo inayostahili kulipwa kuanzia mwaka 2012/2013 hadi 2016/2017 ilikuwa shilingi bilioni 198.8. Hata hivyo, malimbikizo ya mikopo iliyostahili kulipwa ilikuwa shilingi bilioni 81.16 sawa na asilimia 25 ya ulipaji wa mikopo kwa miaka mitano iliyopita.

10.2.5 Marejesho, Malimbikizo ya Ukusanyaji na Tozo zingine Hazikulipwa wakati wa Kuripoti Utendaji wa Ukusanyaji wa Mikopo

Ukaguzi ulibaini kuwa masuala kama marejesho ya mikopo yaliyotokana na makato yaliyofanywa kimakosa, ukusanyaji wa madeni ya nyuma, na

utenganishaji kati ya malipo ya ziada pamoja na kiwango cha jumla cha mikopo havikuelezwa kinagaubaga namna zilivyogawanywa wakati wa kutoa taarifa za utendaji wa makusanyo ya mikopo.

Kwa mfano, mapitio ya malipo ya mikopo inayostahili kulipwa yalionesha kuwa, Bodi ya Mikopo haikuripoti juu ya punguzo la fedha iliyokusanywa kimakosa ndani ya mwaka wa fedha husika. Kwa mujibu wa kanzidata ya mikopo inayostahili kurejeshwa, Bodi ilikuwa na jumla ya shilingi bilioni 81.16 zilizoripotiwa kukusanywa, ambapo shilingi bilioni 1.220 zilipaswa kuwa punguzo. Punguzo la kila mwaka ikilinganishwa na ulipaji wa mikopo uliofanywa ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali 10.3.**

Jedwali 10.3: Marejesho ambayo Hayakupunguzwa wakati wa Utoaji wa Taarifa ya Makusanyiko

Mwaka wa Fedha	Mikopo Ambayo Imelipwa kwa Mwaka (Sh. Milioni)	Punguzo lililooneshwa kwenye Taarifa ya Kanzidata (Sh. Milioni)	Asilimia ya Punguzo (%)
2012/2013	25,050	70	0
2013/2014	19,390	240	1
2014/2015	20,640	290	1
2015/2016	13,150	70	1
2016/2017	2,930	550	19
Total	**81,160**	**1,220**	**2**

Chanzo: *Kumbukumbu za Hesabu za Bodi ya Mikopo na Kanzidata ya Urejeshaji wa Mikopo ya Mwaka 2018*

Jedwali 10.3 linaonesha kuwa kiasi cha fedha kilichopaswa kupunguzwa kwenye makusanyo kilikuwa kati ya asilimia 0 hadi 19 ya mikopo inayostahili kukusanywa kwa mwaka. Hii inamaanisha kuwa kulikuwa na punguzo zaidi lililotakiwa kufanywa katika miaka ya fedha iliyofuata. Hata hivyo, ilibainika kuwa Bodi ya Mikopo haikutambua kiasi hiki kama punguzo kwenye makusanyo wakati wa kutoa taarifa ya utendaji kuhusu ukusanyaji wa mikopo dhidi ya malengo yaliyowekwa.

10.2.6 Hesabu ya Mikopo kwenye Kanzidata ya Bodi ya Mikopo Haikushabihiana na Kanzidata ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma

Taarifa kutoka Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora zilionesha kuwa kulikuwa na wanufaika wa mikopo wapatao 15,885 kulingana na kanzidata ya mishahara ya serikali. Wanufaika hawa walikuwa wamekamilisha malipo ya mikopo yao kupitia makato ya kila mwezi kutoka kwenye mishahara yao.

Ukaguzi ulichukua sampuli ya wanufaika wa mikopo wapatao 180 kati ya 15,885 waliokuwa wamekamilisha mikopo yao kutoka kwenye kanzidata ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kuzilinganisha na salio kwenye kanzidata ya Bodi ya Mikopo. Baada ya uchambuzi, ukaguzi ulibaini kuwa jumla ya wanufaika wa mkopo 180 walikuwa wamekamilisha mikopo yao hata hivyo taarifa za Bodi zilionesha kuwa walikuwa bado hawajamaliza mikopo yao kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 10.4.**

Jedwali 10.4: Bakaa ya Mikopo kama Ilivyoripotiwa kwenye Kanzidata ya Mishahara ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Kanzidata ya Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo ya Bodi ya Mikopo

Taaisisi ys Serikali	Idadi ya Wanafaika Waliomaliza Mikopo kwa Mujibu wa Kanzidata ya OR-UTUMISHI	Idadi ya Wanufaika Waliomaliza Mikopo yao kwa Mujibu wa Bodi	Idadi ya Wanufaika wenye Madeni ya Mikopo kwa Mujibu wa Bodi	Asilimia ya Wanufaika Wanaodaiwa
Jiji la Arusha	20	3	17	85
Jiji la Dodoma	20	3	17	85
Jiji la Mwanza	20	4	16	80
Jiji la Dar es Salaam	20	11	9	45
Wizara ya Afya	20	3	17	85
Wizara ya Elimu	20	3	17	85
TAMISEMI	20	11	9	45
UDOM	20	4	16	85
Kituo cha Elimu Kibaha	20	3	17	85

Taaisisi ys Serikali	Idadi ya Wanafaika Waliomaliza Mikopo kwa Mujibu wa Kanzidata ya OR-UTUMISHI	Idadi ya Wanufaika Waliomaliza Mikopo yao kwa Mujibu wa Bodi	Idadi ya Wanufaika wenye Madeni ya Mikopo kwa Mujibu wa Bodi	Asilimia ya Wanufaika Wanaodaiwa
Total	**180**	**45**	**135**	**75**

Chanzo: *Uchambuzi wa Ukaguzi wa Taarifa za Makato ya Mikopo kutoka Bodi ya Mikopo na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, 2018*

Jedwali 10.4 linaonesha kuwa, kwa mujibu wa kanzidata ya Bodi, wanufaika 135 kati ya 180 waliomaliza kulipa mikopo yao kwa mujibu wa Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma walikuwa bado wanadaiwa mikopo na Bodi. Hii inamaanisha kuwa ni wanufaika 45 tu kati ya 180 ambao ni sawa na asilimia 25 ya wanufaika wa mikopo waliochukuliwa sampuli ndio walilipa na kukamilisha mikopo yao kulingana na kumbukumbu za Bodi ya Mikopo. Hata hivyo, asilimia 75 ya wanufaika wote wa mikopo waliochukuliwa sampuli walikuwa hawajapelekewa ankara za madeni yao.

Kwa upande mwingine, uchambuzi zaidi ulionesha kuwa wakati Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma iliripoti wanufaika wa mikopo kwamba hawadaiwi kwa mujibu wa hati za mishahara yao, Bodi iliripoti jumla ya shilingi milioni 362 kama sehemu ya mikopo ambayo haijarejeshwa na wanufaika hao.

10.2.7 Mapungufu katika Utekelezaji wa Shughuli za Kimkakati za Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu

Mapitio hayo yalionesha kuwa kulikuwa na shughuli 39 za kimkakati kuhusu ulipaji na urejeshaji wa mikopo katika mpango-mkakati wa pili zinazohusiana na ulipaji na urejeshaji wa mikopo. Ukaguzi haukuweza kubaini hali ya utekelezaji wa shughuli hizi kwa sababu zilikuwa hazipimiki.

Uchambuzi wa utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo zilikuwa saba. 1 kati ya 7 ilitekelezwa kikamilifu wakati 4 zilitekelezwa kwa sehemu, na 2 hazikutekelezwa. Kucheleweshwa kutekeleza shughuli hizi kulizuia juhudi za Bodi ya Mikopo kutekeleza shughuli zake kama vile kutafuta, kutuma

ankara na kukusanya madeni kwa ufanisi. Miongoni mwa sababu zilizotolewa na maofisa wa Bodi ya Mikopo kuhusu kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa ni ukosefu wa vipaumbele dhahiri ambavyo shughuli zimeanza kulingana na mfuko uliopo.

Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya shughuli 39 zilizoainishwa katika mipango mkakati yote miwili, shughuli 31 hazikubuniwa kikamilifu. Hii ni kwa sababu shughuli hizi hazikuwa rahisi kuhesabika. Hii inamaanisha kuwa, shughuli hizi zilikuwa na mawanda mapana. Mbali na kuwa na mawanda mapana, pia hakukuwa na muda uliowekwa wa utekelezaji wake. Kwa kuongezea, hakukuwa na malengo au viashiria vya kupima utekelezaji wa mambo anuwai ya mipango ya kimkakati ya ulipaji wa mikopo.

10.2.8 Mapungufu katika Uangalizi na Msaada Uliotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ili Kuhakikisha Ukusanyaji Bora wa Mikopo

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikutekeleza ipasavyo jukumu lake la kuhakikisha kuwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inafanya vizuri katika ukusanyaji wa mikopo ili kuwa na chanzo endelevu cha ufadhili kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Vivyo hivyo, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia haikujadili utendaji wa Bodi ya Mikopo katika shughuli za ulipaji na urejeshaji wa mikopo. Mbali na Mkurugenzi wa Elimu ya Juu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuwa mjumbe wa bodi ya wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo, hakukuwa na ripoti rasmi za maendeleo ambazo ziliandaliwa na kuwasilishwa kwa Wizarani na Bodi ya Mikopo. Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa licha ya mkurugenzi kuwa mjumbe wa Bodi, yeye hakuwa mjumbe wa Kamati ya Bodi ambayo ilijadili masuala ya ulipaji na urejeshaji wa mikopo

10.3 Sababu ya Udhaifu Uliojitokeza kwenye Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu

Kulingana na udhaifu ulioelezwa katika matokeo ya ukaguzi chini ya Kifungu cha 10.2 kinachoonesha hali halisi ya utendaji katika usimamizi wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, zifuatazo ni sababu za udhaifu uliobainika.

10.3.1 Kushindwa Kufikia Malengo ya Ukusanyaji wa Mikopo

a) Mapungufu Katika Utoaji wa Taarifa za Mikopo Inayostahili Kulipwa

Bodi ya Mikopo haikuweka malengo ya kila mwaka kupima utendaji wake katika ukusanyaji wa mikopo kulingana na idadi ya wanufaika wa mikopo waliobainika. Ilibainika kuwa, miongoni mwa sababu za kutotimiza malengo ya ukusanyaji wa mikopo hiyo ni kukosekana kwa ripoti rasmi ambazo zilitayarishwa kuelezea idadi halisi ya wanufaika wa mikopo waliobainika kwa miaka kadhaa kwa sababu taarifa zilizalishwa moja kwa moja kutoka kwenye kanzidata ya wanufaika wa mikopo.

Kulingana na takwimu za ukusanyaji wa mikopo kwa kila mwaka, ukusanyaji wa mikopo ulifikia asilimia 53 ya kiasi cha mikopo inayostahili kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2016/17. Hata hivyo, uchambuzi kutoka kwenye mipango-mkakati ya Bodi ya Mikopo pamoja na kanzidata ya ukusanyaji wa mikopo ulionesha kuwa licha ya juhudi hizo, Bodi haikufikia malengo yake ya ukusanyaji wa mikopo kwa asilimia 70 na 80 ya mikopo kama ilivyowekwa kwenye mipango-mkakati hiyo.

b) Udhaifu katika Ufuatiliaji wa Ankara za Mikopo Zilizotolewa kwa Wanufaika

Si wanufaika wote wa mikopo waliopelekewa ankara zao walianza kulipa. Idadi ya wanufaika wa mikopo walioanza kulipa mikopo yao dhidi ya ankara zilizotolewa ilionekana kuongezeka katika miaka miwili ya fedha ikilinganishwa na miaka ya nyuma ya fedha yaani 2012/13 na 2014/15. Sababu za idadi ndogo ya ulipaji katika miaka ya fedha ya 2012/13 na 2014/15 ni juhudi hafifu za ufuatiliaji wa ankara zilizotolewa na kutokuwepo utunzaji wa nyaraka na ufuatiliaji wa shughuli za malipo ya mikopo dhidi ya idadi ya wanufaika wa mikopo waliopewa ankara. Kwa kuongezea, ilikuwa ngumu kuweza kubaini kiwango halisi cha ankara zilizotolewa dhidi ya kiwango cha mikopo kilichokusanywa.

Vilevile, timu ya ukaguzi iligundua kuwa kushuka kwa idadi ya kiwango cha ulipaji kwa asilimia 26 yaani kutoka asilimia 98 hadi 72 ya wanufaika wa mikopo waliopewa ankara kati ya mwaka wa fedha 2015/16 na 2016/17 kulitokana na juhudi kubwa zilizowekwa katika kutoa ankara kuliko kufuatilia ukusanyaji kutoka kwenye ankara hizo zilizotolewa.

Pia, ilibainika kuwa walengwa wa mikopo waliobainika kwa mwaka hawakuhusiana na wanufaika wa mikopo waliotozwa ankara. Kuanzia mwaka wa fedha 2012/13 hadi 2014/15, kulikuwa na juhudi ndogo katika utoaji wa ankara kwa wanufaika wa mikopo. Kwa miaka hiyo ya fedha, utoaji wa ankara ulifanywa kwa mikono na kumbukumbu hazikutunzwa vya kutosha.

c) Mapungufu Katika Utoaji wa Adhabu kwa Wadaiwa Sugu wa Mikopo

Kanzidata ya ukusanyaji wa mikopo ilibainisha idadi kubwa ya wadaiwa sugu. Hivyo, ukusanyaji wa mikopo inayostahili kulipwa ulitarajiwa kusimamiwa vizuri kuhakikisha kuwa mikopo yote inayostahili kulipwa imelipwa kikamilifu au wadaiwa sugu kupatikana. Ukaguzi ulibaini kuwa, kulikuwa na udhaifu katika urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wadaiwa sugu.

Kwa kuongezea, ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Mikopo kupitia idara yake ya ulipaji na urejeshaji wa mikopo haikuandaa au kuwasilisha kwa kitengo cha sheria orodha ya wadaiwa sugu wa mikopo kwa hatua zaidi za kisheria. Ukaguzi umebaini kuwa kushindwa kuhudhuria kesi nyingi kama ilivyopangwa ilitokana na ukosefu wa watumishi kwenye idara ya sheria. Hadi wakati wa ukaguzi huu, idara ya sheria ilikuwa na mtumishi mmoja tu ambaye hata hivyo alikwua akikaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Huduma za Sheria.

d) Kutotumia Ipasavyo Wadhamini wa Wanufaika wa Mikopo Wakati wa Kubaini Wadaiwa Sugu

Bodi ya Mikopo haikutumia kikamilifu wadhamini wa wanufaika wa mikopo wakati wa kubaini wadaiwa sugu wa mikopo haswa wale walioshindwa kubainika kwa njia za kawaida. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 1997 hadi 2015, Bodi iliweza kufuatilia jumla ya wadhamini 254 lakini ni 109 tu (sawa na asilimia 43) walijitokeza.

Mapitio ya kanzidata na mahojiano na maofisa wanaohusika na ukusanyaji wa mikopo yalifichua kuwa haikuwezekana kutumia wadhamini kikamilifu kwa sababu kanzidata ya Bodi haikuweza kutunza maelezo ya wadhamini wakati wa kuandikisha maelezo yao kwenye kanzidata. Hata hivyo, kati ya wadhamini wote waliojitokeza, hakukuwa na kiasi chochote cha mikopo kilichoweza kulipwa au kurejeshwa kutoka kwao au wadhaminiwa.

10.3.2 Idadi ya Mikopo ambayo Hailingani na Mikopo Inayostahili Kulipwa

Tofauti kati ya Idadi ya Wanufaika wa Mikopo dhidi ya Ankara Zilizotolewa

Sababu ya tofauti kati ya mikopo iliyobainishwa na mikopo inayostahili ilitokana na kutolingana kwa wanufaika wa mikopo iliyobainishwa kwa mwaka husika na walengwa wa mikopo waliopewa ankara za malipo ya mikopo. Kuanzia mwaka wa fedha 2012/13 hadi 2014 / 2015, kulikuwa na juhudi ndogo katika kutoa ankara kwa wanufaika waliopatikana. Utoaji wa ankara ulifanywa kwa mikono na kumbukumbu zake hazikutunzwa. Hata hivyo, kwa miaka miwili ya fedha iliyopita ya 2015/2016 na 2016/2017, Bodi ya Mikopo iliweza kutoa asilimia 100 ya ankara kwa wanufaika wa mikopo waliobainishwa. Hii ni kwa sababu shughuli za ulipaji wa mikopo ziliunganishwa kwenye kanzidata ya ulipaji na urejeshaji wa mikopo.

10.3.3 Kiwango cha Chini cha Mikopo Inayolipika

Idadi ya Mikopo Inayopaswa Kuanza Kulipwa lakini Haijalipwa kwa Muda Mrefu

Kanzidata ya Bodi ya Mikopo ilihifadhi jumla ya wanufaika wa mkopo 112,922 ambao walikuwa na madeni ya mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 706.70 na hawakurejesha kwa zaidi ya miaka mitano. Kwa mujibu wa Mwongozo wa Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo wa Mwaka 2008, wanufaika hawa walikuwa kwenye orodha ya wadaiwa sugu. Hata hivyo, Bodi ya Mikopo haikuwa na sehemu inayoonesha idadi ya wadaiwa sugu kwenye kanzidata iliyokuwepo pamoja na kwamba kiasi kinachodaiwa na Bodi kutoka kwa wadaiwa sugu hao kilikuwa kikubwa. Hapakuwa pia na uchambuzi wa muda wa urejeshaji wa mikopo ili kuwezesha Bodi kubaini uwezekano wa kukusanya mikopo hiyo.

10.3.4 Mwenendo Usioridhisha wa Urejeshaji wa Mikopo Inayostahili Kurejeshwa

a) Utafutaji Usioridhisha wa Wadhamini wa Mikopo

Tangu ianzishwe, Bodi ya Mikopo haikuwashirikisha vya kutosha wadhamini wa wanufaika wa mikopo katika kutafuta wanufaika wa mikopo au wanaokaidi kulipa mikopo yao. **Jedwali 10.5** linaonesha wadhamini kadhaa waliowasiliana na Bodi katika miaka iliyopita ikilinganishwa na idadi ya wadaiwa sugu wa mikopo kwa mwaka.

Jedwali 10.5: Idadi ya Wadhamini Waliotafutwa Ikilinganishwa na Jumla ya Idadi ya Wadaiwa Sugu wa Mikopo

Mwaka	Jumla ya Wadaiwa Sugu wa Mikopo kwa Mujibu wa Kanzidata	Idadi ya Wadhamini wa Wadaiwa Sugu wa Mikopo Mikopo Waliofikiwa	Kiwango cha Asilimia ya Wadhamini Waliofikiwa
1997-2012	112,856	42	0.04
2013	29,586	12	0.04
2014	29,756	32	0.11
2015	35,768	168	0.47
Jumla	**207,966**	**254**	**0.12**

Chanzo: *Taarifa za Ulipaji na Urejeshaji Mikopo wa HESLB, 2018*

Jedwali 10.5 linaonesha kuwa kwa ujumla, idadi ya jumla ya wadhamini waliowasiliana na Bodi ya Mikopo katika shughuli za kurejesha mkopo ilikuwa chini ya asilimia moja (asilimia 0.12). Katika kupitia kiwango cha mwitikio wa wadhamini waliowasiliana na Bodi ya Mikopo, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa idadi ya wadhamini waliotoa mrejesho ilikuwa tofauti kwa kati ya asilimia 31 hadi 63.

Mapitio zaidi ya kanzidata na mahojiano baina ya maofisa wa sehemu ya ulipaji na urejeshaji walionesha kuwa haiwezekani kuwatumia kikamilifu wadhamini kwa sababu kanzidata ya Bodi ya Mikopo haikuweza kuzingatia taarifa za wadhamini wakati wa kurekodi taarifa hizo kwenye kanzidata. Pia, taarifa za mawasiliano ya wadhamini kwenye kanzidata hazikuhuishwa mara kwa mara ili kuzingatia mabadiliko yoyote ya taarifa za mawasiliano.

b) Mwenendo Hafifu wa Adhabu Iliyotolewa kwa Wakaidi wa Malipo ya Mikopo

Timu ya ukaguzi iligundua kuwa Bodi ya Mikopo haikuwa na utaratibu wa kutunza orodha iliyohuishwa ya idadi ya wadaiwa wakaidi. Kulingana na takwimu zilizotolewa kwa timu ya ukaguzi za mwaka wa fedha 2015/2016 na 2016/2017, na kulingana na uchambuzi wa mikopo isiyolipwa, Bodi ilikuwa na jumla ya wanufaika 163,394 na 291,672 waliokaidi kurejesha mikopo katika miaka miwili ya fedha, mtawalia. Hii inamaanisha kuwa kulikuwa na ongezeko la wadaiwa sugu wa mikopo wapatao 128,278 kulingana na uchambuzi wa taarifa hizo. Hata hivyo, taarifa zilizotolewa na Bodi zilionesha kuwa kulikuwa na wadaiwa sugu wa mikopo wapato 18 pekee. Kwa mujibu wa kumbukumbu za Bodi, ni wadaiwa sugu wawili tu waliokiuka masharti ya ulipaji wa mikopo waliofikishwa mahakamani.

c) Kiwango Kidogo cha Punguzo la Mikopo na Adhabu Zinazotolewa kwa Waajiri

Kutopunguzwa kwa makato ya mikopo inayotakiwa kupunguzwa na waajiri kutoka kwa wafanyakazi ambao ni wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu ilikuwa sababu ya ukusanyaji usioridhisha wa mikopo inayostahili kulipwa. Kutopunguzwa kwa kiasi hicho kunastahiki adhabu kwa mwajiri sawa na kiwango cha makato ambayo hayajalipwa. Uhakiki na uchambuzi wa orodha ya waajiri wanaokosa malipo kama ilivyotolewa na Bodi inaonesha kuwa asilimia 34 ya waajiri ambao walipewa adhabu hawakulipa adhabu zilizotozwa.

Mapitio zaidi ya adhabu iliyotolewa kwa waajiri ambao walishtakiwa kwa kuchelewa kufanya malipo ilionesha kuwa kati ya waajiri 70 ni 14 tu walikuwa waajiri wa taasisi za umma.

10.3.5 Kutokuwepo kwa Usawa wa Mikopo Iliyoko Bodi ya Mikopo na Kanzidata ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma

Ukaguzi ulibaini kuwa kwa sababu ya njia zisizo wazi za kukusanya na kuchambua taarifa za ukusanyaji wa mikopo kwa kupima utendaji wa malengo ya ukusanyaji na kumbukumbu za mikopo katika kanzidata ya ukusanyaji wa madeni kwa mujibu wa Bodi ya Mikopo, kulikuwepo na

tofauti ya kitaarifa baina ya Bodi na Ofisi ya Rais – Menejeiment ya Utumihsi wa Umma.

10.3.6 Utekelezaji Hafifu na Ufuatiliaji wa Mikakati ya Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo

a) Kipaumbele Kidogo Kilitolewa Katika Shughuli za Ulipaji na Urekeshaji wa Mikopo

Hii ni kwa sababu kulikuwa na jumla ya shughuli 39 zilizohusu ulipaji na urejeshaji wa mikopo chini ya malengo yote mawili ya kimkakati haswa katika mpango-mkakati wa mwaka 2014-2017. Ilibainika kuwa shughuli hizo hazikutengwa katika sehemu mbili za ukusanyaji wa mkopo kwa maana ya ulipaji wa hiari na urejeshaji wa kisheria.

Kwa kuongezea, hakukuwa na mikakati ya kutafuta mikopo ambayo ililingana na shughuli za urejeshaji wa mikopo. Hii inamaanisha kuwa suala la kubaini wakaidi wa urejeshaji wa mikopo kwa lengo la kuandaa mipango na kuboresha usimamizi wa ukusanyaji wa mikopo lilikuwa hafifu. Ukaguzi ulibaini kuwa ni asilimia 1.6 tu ya shughuli za urejeshaji wa mikopo ndio ilitengwa kwa shughuli za urejeshaji wa mkopo wakati asilimia 97.4 iliyobaki ilitengwa kwa shughuli za ulipaji wa mikopo.

b) Kutokuwepo kwa Mfumo Madhubuti wa Ufuatiliaji

Kitengo cha ufuatiliaji na tathmini hakikuweza kutoa miongozo kwa vitengo au sehemu zingine kuhusu aina ya taarifa ambazo zingeweza kukusanywa na kuchakatwa kwa ajili ya kupima utendaji wa idara husika.

Kwa mfano, vitengo vya ufuatiliaji na tathmini vilitegemea kukusanya tu taarifa kwa kutumia malengo mapana ambayo hayatekelezeki. Kitengo hakikuandaa mpango wa ufuatiliaji ambao ulizingatia ufuatiliaji wa shughuli za ukusanyaji wa mikopo katika kipindi chote cha ukaguzi. Hii ilikuwa kinyume na mipango-mkakati ambayo ilionesha kuwa Bodi ya Mikopo ilitakiwa kufuatilia shughuli zake kupitia kitengo cha ufuatiliaji na tathmini.

c) Udhaifu Katika Mipango na Utoaji Taarifa za Matokeo ya Ukaguzi

Ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2016/2017 ya Bodi ya Mikopo ilionesha kuwa utendaji ulikuwa asilimia 92. Hata hivyo, ripoti ya ukaguzi haikupitishwa na uongozi wa Bodi kwani hakukuwa na udhibitisho wa idhini hiyo.

Pia, udhaifu katika muundo na uandaaji wa mikakati ya ukusanyaji kama vile ukaguzi kutoka kwenye mipango-mkakati ulichangia kutokutekelezwa kwake. Mipango-mkakati yote miwili haikuonesha idadi ya ukaguzi unaostahili kufanywa pamoja na maeneo kwa kuzingatia viashiria hatarishi au umuhimu wa maeneo hayo kwenye ukusanyaji wa mikopo. Kwa hiyo, hali hii iliathiri utekelezaji wa shughuli za ukusanyaji wa mikopo kwani hakukuwa na malengo ya haraka kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

Mipango ya ukaguzi haikuandaliwa na Bodi ya Mikopo. Utaratibu pekee ambao ulitumika ulikuwa kwa njia ya dharura. Mkakati huu hata hivyo haukuoneshwa kwenye mwongozo wa ukusanyaji wa mikopo wa mwaka 2008. Pia, mipango ya ukaguzi ilikosa viashiria vya kupima utendaji kwa ajili ya kupima na kutoa taarifa za mafanikio yaliyopatikana katika shughuli za ukaguzi zilizofanywa.

d) Kanzidata Haitumiki wakati wa Kupanga Ubainishaji wa Wanufaika wa Mikopo

Hakukuwa na ushahidi ulioonesha matumizi ya kanzidata ya wadaiwa wa mikopo katika kupanga mbinu za utekelezaji wa kubaini wanufaika wa mikopo. Mwongozo wa ukusanyaji wa mikopo haukueleza jinsi ya kuchagua njia sita zilizoko kwenye mikakati kwa msaada wa uchambuzi wa kanzidata. Timu ya ukaguzi ilitarajia kuwa kabla ya kutumia mbinu yoyote ya ukusanyaji wa mikopo, uamuzi unapaswa kuzingatia eneo la wanufaika wa mikopo, idadi ya wakopaji na ofisi za waajiri watakaotembelewa, kiwango kinachoweza kukusanywa, viashiria vya hatari vinayohusishwa na njia iliyopendekezwa, na gharama au tija katika kutekeleza mbinu hiyo.

10.4 Athari za Mapungufu Yaliyobainika

Sehemu hii inazungumzia kwa ufupi madhara yanayoweza kusababishwa na usimamizi mbaya wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Athari za mapungufu hayo yamelenga maeneo makuu mawili

ambayo ni utekelezaji wa shughuli za ulipaji na urejeshaji wa mikopo, pamoja na ufuatiliaji wa uandaaji na utekeleaji wa mikakati ya ukusanyaji wa mikopo.

10.4.1 Udhaifu wa Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo

Usimamizi wa Shughuli za Ulipaji wa Mikopo

a) Jumla ya malimbikizo ya mikopo inayostahili kulipwa ya shilingi bilioni 244 hazikukusanywa kwa mwaka wa fedha 2016/17. Kiasi hiki, ikiwa kingekusanywa, kingetumika kufadhili wanafunzi wengine wa masomo ya juu katika miaka inayofuata. Kwa hivyo, kulikuwa na idadi kadhaa ya wanafunzi wa elimu ya juu ambao wangekosa mikopo.

b) Kutokana na uwezo finyu wa kubaini wanufaika wa mikopo, Bodi ya Mikopo haikuweza kubaini malimbikizo ya wanufaika wa mikopo wapatao 130,697. Hii ilimaanisha kuwa mikopo haikulipwa na wanufaika ambao wangeweza kubainika hivyo kukwamisha ukusanyaji wa mikopo kwa ajili ya kufadhili wanufaika wengine wa mkopo wa elimu ya juu.

c) Idadi ya ankara zilizotolewa kwa wanufaika wa mikopo ambazo hazikujibiwa wala kulipwa ilikuwa 16,416 kati ya 58,930. Hii itaathiri kiwango cha ukusanyaji wa mapato na hivyo itazuia idadi ya wanafunzi wa masomo ya juu ambao wangestahili kupata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo.

Usimamizi na Udhibiti wa Shughuli za Urejeshaji wa Mikopo

a) Hadi mwaka 2017, takribani asilimia 44 ya wanufaika wa mikopo walikuwa wakilipa mikopo yao wakati asilimia 56 ilikuwa bado. Hivyo, serikali ilikuwa ikipoteza asilimia 56 ya mikopo ambayo ilitakiwa kukusanywa.

b) Bodi ya Mikopo iliweza kupata marejesho pungufu ikilinganishwa na kiasi cha mikopo ambacho kilikuwa hakijalipwa. Hii inamaanisha kwamba, bado kutakuwa na ongezeko la wakaidi wa urejeshaji wa mikopo na hivyo kuathiri ukusanyaji wa mikopo ambayo haijalipwa

kwa wakati. Bodi ya Mikopo ilifanikiwa kurejeshewa asilimia 25 tu ya jumla ya mikopo yote iliyostahili kurejeshwa.

c) Kuwepo kwa mfumo usioridhisha wa urejeshaji wa mikopo inayostahili kulipwa kutoka kwa wadaiwa sugu wa mikopo ikiwa pamoja na kutowachukulia hatua za kisheria kumepunguza uwezekano wa ukusanyaji zaidi wa mikopo ikilinganishwa na makusanyo ya sasa. Hii ingeweza kuwakumbusha wakaidi wa urejeshaji wa mikopo ili kurahisisha urejeshaji wa hiari.

10.4.2 Ubunifu na Ufuatiliaji wa Mikakati ya Ukusanyaji wa Mikopo

a) Kutokana na mapungufu ya muundo wa ufuatiliaji wa mikakati ya makusanyo, kulikuwa na uwezekano kuwa, kwa kutotumia kanzidata katika kuandaa mipango, kutekeleza na kufuatilia ubainishaji, utozaji na ukusanyaji wa mikopo kungeweza kuongeza gharama za kiutekelezaji.

b) Ukosefu wa mwongozo uliathiri shughuli za ufuatiliaji wa ukusanyaji mikopo kwani hakukuwa na uthabiti katika mbinu zilizotumika kukusanya mikopo na kuchambua taarifa za kupima utendaji ulioendana na malengo ya ukusanyaji wa mikopo. Hii ilisababisha tofauti kwenye hesabu za makusanyo ambazo zilioneshwa kwenye taarifa ya fedha, kitengo cha uhasibu, pamoja na kanzidata ya Bodi.

c) Bodi ya Mikopo haikuwa katika nafasi nzuri ya kubuni mbinu ambazo zingekuwa nafuu katika shughuli za kubaini wanufaika wa mikopo ambao hawajalipa au kurejesha mikopo. Hivyo, kutokuweka kumbukumbu na kufanya uchambuzi wa gharama zinazotumika katika mbinu mbalimbali za ubainishaji wa wanufaika wa mikopo kulikwamisha ufanisi katika mgawanyo wa rasilimali wakati wa kufanya shughuli za ubainishaji wa wanufaikaji wa mikopo.

SURA YA KUMI NA MOJA

URATIBU NA UFUATILIAJI WA UTOAJI WA ELIMU

11.1 Utangulizi

Uratibu ni kazi ya usimamizi ambayo inahakikisha kuwa idara na wakala mbalimbali hufanya kazi kwa kushirikiana. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilikuwa na jukumu la kuhakikisha kunakuwepo uratibu mzuri kati yao, sekretarieti za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa. Uratibu ni muhimu katika kufikia malengo yanayotekelezwa na wizara tofauti, sekretarieti za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa. Jambo muhimu katika uratibu ni maelewano ya pamoja ya malengo, ukamilishaji wa pamoja wa malengo hayo, rasilimali na ufanisi, uhusiano mzuri wa kijamii, na muundo wa wafanyakazi.

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi kuhusu uratibu, ufuatiliaji na tathmini kwenye shughuli zinazohusu utoaji wa elimu nchini.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni (a) uratibu baina ya wadau kuhusu utoaji wa huduma za elimu; na (b) ufuatiliaji wa shughuli za utoaji wa huduma za elimu.

11.2 Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inaelezea matokeo ya ukaguzi kuhusu uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za utoaji wa elimu nchini. Kimsingi, inafafanua kiwango cha uratibu ndani ya muundo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na vilevile kati ya Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI na pia katika ngazi ya tawala za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa. Sehemu hii pia iliangalia uratibu unaofanywa na taasisi zinazotoa huduma za elimu kama vile shule za msingi na sekondari, vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi, pamoja na vyuo vikuu.

Matokeo ya ukaguzi katika sehemu hii yamegawanywa katika sehemu kuu tatu ambazo ni uratibu kati ya watendaji katika sekta za elimu, sababu zilizopelekea uratibu usiofaa katika ngazi mbalimbali za uendeshaji wa sekta ya elimu, na athari zitokanazo na uratibu duni wa huduma za elimu.

11.2.1 Uratibu duni wa kusimamia Watendaji katika Sekta za Elimu

Ripoti za ukaguzi wa ufanisi zimebainisha kuwa kulikuwa na uratibu hafifu katika ngazi tofauti za Serikali. Hii inadhihirishwa na ushirikiano duni kati ya taasisi zinazohusika na utoaji wa aina mbalimbali za elimu kama inavyoainishwa hapa chini.

a) Uratibu Usiofaa katika Ngazi za Wizara

Ukaguzi ulionesha kuwa kulikuwa na uratibu usiotosheleza katika ngazi za wizara kama vile Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI. Kaguzi zifuatazo ziliripoti udhaifu kuhusu uratibu wa utoaji wa huduma za elimu nchini.

Ukaguzi wa ufanisi juu ya utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini ulibaini kuwa mfumo wa majadiliano uliotumika kama jukwaa la uratibu kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloji na OR-TAMISEMI haukufanyika kwa ufanisi. Hii ni kutokana na kwamba kwa mujibu wa mifumo iliyowekwa inayojumuisha vikundi vitatu vya kitaalamu na Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ambazo zilitakiwa kukutana kila robo mwaka kujadili masuala ya kitaalamu ikiwa pamoja na hatua za kuwajengea uwezo walimu walio kazini. Hata hivyo, ukaguzi uligundua kuwa mijadala hii haikufanyika kama ilivyopangwa na wakati mwingine muda wa vikao vyao kamati hizi zilikuwa zinafanya majadiliano ya masuala yasiyohusiana na kuwajengea uwezo walimu.

Pia, ukaguzi wa ufanisi katika utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini ulibainisha pia uratibu duni uliofanywa na OR-TAMISEMI na kupelekea kurudiwa kwa mafunzo ya stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa walimu walio kazini. Mafunzo yalitolewa katika mikoa 3 ambayo ni Njombe, Songwe na Mbeya kwa jumla ya walimu 4,309, 1,118 na 3,260 mtawalia. Mafunzo haya yalitolewa chini ya msaada wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto licha ya kuwa mafunzo hayohayo yalishatolewa chini ya programu ya mafunzo ya kusoma, kuhesabu na kuandika (LANES) ndani ya kipindi hichohicho cha miaka yaani, 2016/17 na 2018/19.

Vilevile, ukaguzi wa ufanisi kuhusu Upatikanaji na Utunzaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi ulibaini kuwa OR-TAMISEMI haikuanzisha

mipango ambayo iliruhusu uratibu wa Idara mbalimbali katika ngazi za wilaya na mkoa katika maendeleo na matengenezo ya miundombinu ya shule za msingi. Hakukuwa na ushahidi kuhusu mipango iliyoratibiwa kati ya idara za uhandisi, afya, maofisa wa elimu, pamoja na mazingira ambao walikuwa na taaluma ya elimu ya ufundi juu ya viwango na usimamizi wa miundombinu ya shule za msingi katika halmashauri.

Ukaguzi wa ufanisi kuhusu upatikanaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ulibaini kuwa hakukuwa na uratibu katika upangaji na utekelezaji wa sera ya maendeleo ya ujuzi haswa juu ya mafunzo ya ufundi stadi kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu. Kupitia mahojiano na maofisa wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ukaguzi ulibaini kuwa uandaaji wa mipango na utekelezaji wa sera ya uendelezaji wa ujuzi ikiwemo ujuzi wa stadi za kazi havikutekelezwa kwa pamoja.

Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa, vikao katika kanda zote zilizohusu watoahuduma za elimu na mafunzo ya ufundi stadi, havikufanywa kikamilifu katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2013/14 hadi 2018/19 kwa sababu ni kanda mbili kati ya saba ndizo zilifanya vikao, ambayo bado ilikuwa chini ya malengo. Kanda mbili, hata hivyo, za kusini mashariki na magharibi zilifanya kikao kimoja kati ya vikao sita ambavyo pia bado havikutosheleza.

b) Uratibu Usiofaa katika Ngazi ya Mkoa

Ukaguzi ulibaini kuwa uratibu katika ngazi ya mkoa haukufanywa kikamilifu. Kulikuwa na ukosefu wa mtiririko mzuri wa taarifa kati ya sekretarieti ya mkoa na wadau wake kama vile OR-TAMISEMI na mamlaka za serikali za mitaa. Hii ni kwa sababu OR-TAMISEMI haikuandaa mipango ambayo iliruhusu uratibu katika ngazi za mkoa na wilaya katika utekelezaji wa shughuli za kufikia malengo yaliyowekwa. Maelezo ya uratibu katika ngazi ya mkoa ni kama inavyofafanuliwa hapa chini.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu ulibainisha kuwepo kwa kiwango kidogo cha kupeana taarifa za elimu ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu kutoka ngazi za halmashauri hadi ngazi ya OR-TAMISEMI. Hii ni kwa sababu taarifa kama vile idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na mahitaji yao ya

vifaa na vitabu kwa ajili ya kujifunza au idadi walimu wa mahitaji maalumu katika ngazi ya taifa zilipatikana kwa urahisi kutoka shuleni na halmashauri, lakini taarifa hizohizo hazikupatikana katika ngazi za taifa ambayo inahusisha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na OR-TAMISEMI. Hali hii ilionesha kuwa hakukuwa na mfumo mzuri wa taarifa kuhusu wanafunzi walio na mahitaji maalumu kutoka shuleni, halmashauri, hadi ngazi ya taifa.

Ukaguzi huohuo ulionesha kuwa mahitaji na taarifa muhimu kuhusu elimu maalumu hazikuwasilishwa kwa ufasaha katika ripoti zilizokuwa zinaandaliwa na hamalshauri na ofisi za mikoa husika. Kwa mfano, katika Mkoa wa Lindi, ukaguzi ulibaini kuwa ni halmashauri tatu tu kati ya sita ndizo ziliwasilisha taarifa za elimu ya wanafunzi wenye mahitaji maalmu. Halmashauri hizo ni Liwale, Ruangwa na Kilwa. Hata hivyo, ripoti hizo za halmashauri hazikuwasilisha kikamilifu taarifa hizo kwa sababu hazikuonesha mahitaji ya walimu, aina na idadi ya vifaa, na idadi ya vifaa vinavyotumiwa na wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambavyo viliharibika hivyo vinahitaji matengenezo.

c) Uratibu usiofaa katika ngazi ya halmashauri

Ukaguzi ulibaini kuwa uratibu katika ngazi ya halmashsuri haukufanyika ipasavyo kwa sababu, hakukuwepo na mipango ya uratibu ndani ya halmashauri ili inayofanana na malengo yao.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Upatikanaji na Utunzaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi ulibaini kuwepo kwa uratibu duni miongoni mwa maofisa wakuu katika ngazi ya halmashauri ambapo uratibu wa shughuli zinazohusiana na utoaji wa elimu zilifanywa kunapokuwepo malalamiko. Licha ya kuwa na wahandisi na mafundi katika mamlaka husika za serikali za mitaa, miundombinu na vifaa vya shule za msingi vilisimamiwa na maofisa elimu ambao hawakuwa na taaluma ya ujenzi. Wafanyakazi waliokuwa na ujuzi wa ufundi kama wahandisi hawakufanya kazi kwa pamoja kwa kushirikiana na maofisa elimu kushughulikia masuala ya maendeleo na matengenezo ya miundombinu ya shule za msingi.

d) Uratibu katika Ngazi ya Elimu ya Vyuo Vikuu

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na uratibu usiojitosheleza katika shughuli za kuimarisha utafiti katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ardhi, na Tume ya Sayansi na Teknolojia.

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Kuimarisha Ushirikiano wa Utafiti na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili ilibainisha kuwepo kwa uratibu duni wa mfumo wa uidhinishaji wa mitaala baina ya mamlaka zenye jukumu hilo. Udhaifu huu ulianzia ngazi ya idara hadi seneti ambako kulipelekea kucheleweshwa kwa ukamilishaji wa mchakato wa kuandaa mtaala wa uanzishaji wa programu mbili za shahada ya umahiri zinazohitajika.

Pia, ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Kuimarisha Ushirikiano wa Utafiti na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilibainisha kuwepo kwa uratibu duni wa taarifa za wanafunzi kutoka kwa wasimamizi wao na kwa waratibu wa programu uliohusishwa na uchelewaji wa kumaliza masomo ya shahada za umahiri, pamoja na uratibu wa taarifa kulichukua muda mrefu kukamilika.

Kwa kuongezea, Ukaguzi wa Utendaji wa Programu ya Mifumo ya Kuimarish Ubora wa Utafiti Unaofaa na Ubunifu nchini Tanzania ulibaini kuwa, uratibu duni kati ya washirika wa programu ndogo ndogo kama vikundi, halmashauri, Tume ya Sayansi na Teknolojia, pamoja na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogovidogo ulitokana na utekelezaji wa shughuli za vituo vya uvumbuzi bila kusainiwa makubaliano ambayo yangetoa mwongozo wa jinsi kazi za vikundi zitakavyotekelezwa.

11.2.2 Sababu za Uratibu Duni katika Ngazi mbalimbali za utoaji wa Elimu

a) Kutokuwepo kwa Sera ya Kitaifa

Ilibainika kuwa kukosekana kwa sera ya kitaifa ya uratibu na ufuatiliaji ni moja ya sababu za uratibu duni wa watendaji katika ngazi tofauti za sekta ya elimu. Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Upatikanaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Stadi ilibainisha kuwa kukosekana kwa Sera ya Kitaifa katika upangaji na utekelezaji wa ukuzaji wa stadi katika Mafunzo

ya Ufundi na Mafunzo katika Wizara zote kulichangia uratibu duni katika upangaji na utekelezaji wa ukuzaji wa mafunzo haswa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Waziri Mkuu inayohusika na Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Walemavu.

b) Kutoshirikisha Wadau kuhusu Malengo Yanayotarajiwa Kutimizwa

Kaguzi za Ufanisi katika Kuimarisha Uhusiano wa Kitafiti Vyuoni zilibaini kutokuwepo kwa ushirikiano wa malengo yanayotakiwa kutimizwa kwa pamoja baina ya wahusika wakuu kuwa ndiyo sababu kuu ya uratibu duni kati ya watendaji.

Kwa mfano, katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, uratibu duni ulitokana na kutoshirikisha wadau kuhusu muda wa kukamilisha utoaji wa idhini za uendeshaji wa programu ndogondogo. Hii ingesaidia kuoanisha muda uliopangwa wa utoaji idhini na ratiba nzima ya waratibu wa programu ndogo kwa ajili ya kuoanisha ratiba za idhini na kuzipa kipaumbele kufikia muda uliotengwa. Hii ni kwa sababu mamlaka za uidhinishaji zilikuwa na jukumu la utoaji wa idhini kwa programu zingine mbali na zile zinazohusiana na mradi huu.

11.2.3 Athari za Uratibu Duni katika Utoaji Elimu

Athari za uratibu usiofaa zimeorodheshwa hapa chini.

a) Ukosefu wa njia rasmi za kushirikikiana taarifa kati ya wadau

Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Utoaji wa Mafunzo kwa Walimu Walio Kazini ulibaini kuwa hakukuwa na njia rasmi za kupeana taarifa kati ya wadau juu ya maendeleo ya shughuli za kuwajengea uwezo walimu walio kazini ambako kulitokana na uratibu duni.

Taarifa zinazopatikana kutoka kwenye ripoti za udhibiti ubora hazitumiki kikamilifu katika kushughulikia na kubuni hatua za kujenga uwezo. Kwa kuongezea, utaratibu wa kuripoti katika sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa haukuzingatiwa kikamilifu na hivyo hakukuwa na mtiririko mzuri wa taarifa juu ya shughuli za kuwajengea uwezo walimu walio kazini kwa sababu hii ilikuwa matokeo ya uratibu usiofaa wa wadau.

b) Kutoshabihiana kwa Mahitaji na Wafanyakazi Waliopo Wenye Ujuzi katika Soko la Ajira

Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Utoaji wa Mafunzo kwa Walimu walio kazini ulibaini kuwa kutokana na uratibu duni katika uundaji wa sera na mapitio ya uendelezaji ulisababisha tofauti kati ya mahitaji na wafanyakazi waliopo wenye ujuzi katika soko.

c) Kujirudia kwa Jitihada kwenye Eneo Moja

Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Utoaji wa Mafunzo kwa Walimu walio kazini ulibaini kuwa uratibu usiofaa ulisababisha kuwepo kwa juhudi za kujirudia katika eneo moja kama inavyothibitishwa kupitia mafunzo ya kusoma, kuandika na kuhesabu ambayo yalitolewa chini ya msaada wa Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani na Programu ya Kusoma, Kuhesabu na Kuandika katika kipindi hichohicho cha mwaka na maeneo yaleyale kwa kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2018/19.

11.3 Ufuatiliaji wa Shughuli za Utoaji wa Huduma ya Elimu Chini

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa utoaji wa huduma ya elimu ni jambo muhimu katika kutoa mrejesho juu ya ufanisi na tija katika kufikia mikakati ya kitaifa ya utoaji wa huduma ya elimu nchini. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na TAMISEMI wana wajibu wa moja kwa moja wa kufuatilia utendaji kazi wa taasisi zinazowajibika kwenye wizara hizo juu ya utoaji wa huduma ya elimu nchini.

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi kuhusu ufuatiliaji wa utoaji wa huduma ya elimu. Matokeo ya ukaguzi yamegawanywa katika maeneno matatu ambayo ni ufuatiliaji wa utendaji kazi wa taasisi zinazojihusisha na shughuli za utoaji wa huduma ya elimu, sababu zilizopelekea uwepo wa ufuatiliaji usiojitosheleza wa shughuli za utoaji wa huduma ya elimu na athari zitokanazo na ufuatiliaji na tathmini usiotosheleza.

11.3.1 Ufuatiliaji Usioridhisha wa Shughuli za Utoaji wa Huduma ya Elimu Nchini

(a) Ukosefu wa Viashiria Muhimu vya Utendaji katika Kupima Utendaji

Ukaguzi uliofanyika ulibaini kuwepo kwa viashiria muhimu visivyoridhisha katika kupima utendaji wa taasisi za utoaji wa huduma ya elimu nchini. Hii ni kwa sababu baadhi ya viashiria havikujitosheleza ili kupima kufikiwa kwa malengo yaliyopangwa. Kwa upande mwingine, viashiria hivyo vya kupima utendaji havikuandaliwa kabisa.

Kwa mfano, Ukaguzi wa Ufanisi katika Upatikanaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ulibaini kuwa, mipango ya VETA kwa mwaka kuanzia 2014/14 hadi 2017/18 haikuwa na viashiria vya utendaji ili kupima iwapo malengo yaliyowekwa kwa ajili ya kupata elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi yamefikiwa.

Ukaguzi ulionesha pia kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haina mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Wizara imetengeneza viashiria mtambuka kama sehemu ya hatua iliyochukuwa kwa ajili ya kuhamasisha mchakato wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji. Hata hivyo, hakukuwa na viashiria vya utendaji vinavyoweza kupima maeneo husika ya kiutendaji katika utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

Ukaguzi wa Ufanisi katika Utoaji wa Mafunzo kwa Walimu Walio Kazini ulibainisha pia kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikutengeneza viashiria vya utendaji ambavyo ni mahususi kwa ajili ya ufuatilaiaji wa utoaji wa mafunzo kwa walimu walio kazini. Pia, ilibainika kuwa pamoja na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu kuonesha umuhimu wa kuwa na viashiria vya utandaji kwa ajili ya kupima utendaji wa taasisi za elimu, mapitio ya mpango huo, mipango ya Wizara ya Elimu pamoja na OR-TAMISEMI yalionesha kuwa wizara zote hazikutengeneza viashiria vikuu kwa ajili ya kupima utendaji wa taasisi za elimu.

Hii ilikuwa kinyume cha matakwa ya Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mwaka 2016-2021 ambao unataka wizara zote kuwa na viashiria vya

utendaji kwa ajili ya kupima utendaji au meandeleo ya miradi kwa kulinganisha na mikakati iliyowekwa.

Kwa kuongezea, Ukaguzi wa Utendaji juu ya Usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania, haikuweka viwango na taratibu za kutosheleza kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Pia, Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ulibaini kuwa Wizara ya Fedha na Mipango licha ya kuwa msimamizi mkuu wa kazi zinazofanywa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, haijatengeneza mfumo wenye viashiria vya kupima utendaji ambao ungeweza kutumika kama mwongozo au mbinu ya ufuatiliaji kwa ajili ya kupima utendaji wa Bodi katika shughuli za usimamizi wa ulipaji na urejeshaji wa mikopo.

(b) Kufanyika kwa Ufuatiliaji Usioridhisha

Kaguzi zilizofanyika zimebaini kuwa ufuatiliaji na tathmini haukufanywa kikamilifu na wahusika wote wanaohusika katika sekta ya elimu. Ilibainika kuwa, si shughuli zote za ufuatiliaji zilizopangwa kutekelezwa zilifanyika.

Kwa mfano, Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Upatikanaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo Stadi ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikufanya ufuatiliaji na tathmini wenye tija na ufanisi katika kuhakikisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi inatekeleza shughuli zilizopangwa za kuhakikisha upatikanaji bora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini. Aidha, ilibainika kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikufanya tathmini huru kuangalia utendaji wa Mamlaka hiyo katika kuhakisha upatikanaji wa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi.

Ilibainika pia kuwa, ufuatiliaji ulifanywa kwa vyuo vilivyomilikiwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi pekee huku ikiwaacha watoahuduma wengine wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Vyuo vingine vya utoaji huduma ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi vilitembelewa tu wakati wa usajili, upandishaji hadhi au wakati wa kupata idhini ya kutoa huduma hiyo na si kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji wa utekelezaji wa utoaji huduma ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Uchunguzi zaidi ulionesha kuwa mipango ya mwaka ya ofisi za kanda haikuwa na kipengele

cha ufuatiliaji ambao ungetekelezwa kwenye vyuo vingine vya utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Sababu zilizotajwa za upungufu huo ni ukosefu wa wafanyakazi wa kutosha na changamoto za kifedha ambazo zilikuwa na athari kubwa katika shughuli za ufuatiliaji kwa ufanisi.

Ukaguzi wa ufanisi uliofanyika ulibaini pia kuwa, licha ya ukweli kwamba viashiria vya utendaji vinapatikana katika Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu na Mipango ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, viashiria hivyo havikutumika kwa ufanisi kupima utendaji na maendeleo ya usimamizi wa upatikanaji wa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi nchini.

Pia, Ukaguzi wa Ufanisi juu Utendaji wa Programu ya Mifumo ya Uendelezaji wa Ubora wa Utafiti na Ubunifu nchini ulibaini kuwa Tume ya Sayansi na Teknolojia na Shirika la Uendelezaji wa Viwanda Vidogo halikuwa na utaratibu au mfumo wa kufuatilia na kutathmini utendaji wa vituo vya uvumbuzi na kushughulikia kukuza maendeleo yake.

Ripoti ya ukaguzi imeonesha zaidi kuwa, ofisi za mikoa za Shirika la Uendelezaji wa Viwanda Vidogo zilikosa mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kwa vituo vya uvumbuzi, ubunifu pamoja na mfumo wa usimamizi wa ubora kwa vituo vya wabunifu. **Jedwali 11.1** linaonesha hali ya utendaji wa Shirika katika kufanya ufuatiliaji na tathmini.

Jedwali 11.1: Hali ya Ofisi za SIDO katika Suala la kufanya Ufuatiliaji na Tathmini

Ofisi za Mikoa za Shirika la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi	Ufuatiliaji na Tathmini Uliofanyika	Zana za Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya Vituo vya Uvumbuzi	Uwepo wa Mfumo wenye Ubora wa Usimamizi pamoja na Sera	Upatikanaji wa Mfumo na Sera ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi
Kilimanjaro	Fomu ya Ripoti ya Maendeleo	Dodoso kukusanyia Takwimu za Msingi	Ipo	Ipo

Ofisi za Mikoa za Shirika la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi	Ufuatiliaji na Tathmini Uliofanyika	Zana za Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya Vituo vya Uvumbuzi	Uwepo wa Mfumo wenye Ubora wa Usimamizi pamoja na Sera	Upatikanaji wa Mfumo na Sera ya Usimamizi wa Viashiria Hatarishi
Shinyanga	Kufanya ufuatiliaji wa utoaji wa ripoti ukianza na ripoti ya kila mwezi kwa mwaka	Ripoti za kila mwezi, robo mwaka, nusu mwaka na za kila mwaka	Hakuna	Mwongozo wa Usimamizi wa viashiria vya Hatari za Uhasibu
Morogoro	Ripoti za mara kwa mara	Hakuna	Ipo	Ipo
Singida	Kuripoti na kutembelea maeneo kwa ajili ya kutoa ithibati	Hakuna	Hakuna	Hakuna
Manyara	Kuripoti na kutembelea maeneo kwa ukaguzi na kufanya mikutano katika maeneo hayo	Hakuna	Hakuna	Hakuna
Dodoma	Ripoti za za kuonesha maendeleo	Hakuna	Hakuna	Hakuna

Chanzo: *Ripoti ya Utafiti wa Msingi, (2018)*

Kama inavyooneshwa katika **Jedwali 11.1**, njia za kufuatilia jinsi shughuli zilivyofanywa kutoka ngazi ya kituo cha uvumbuzi hadi mamlaka za serikali za mitaa zilikuwa hazishabihiani. Ni mikoa ya Shinyanga na Kilimanjaro pekee ndiyo ilikuwa na aina fulani ya zana za ufuatiliaji na tathmini za shughuli za vituo na wavumbuzi. Mikoa yote iliyobakia ambayo ilitembelewa haikuwa na njia zinazojulikana za kufanya ufuatiliaji na tathmini ya vituo vya uvumbuzi pamoja na wavumbuzi.

Ukaguzi wa Ufanisi Juu ya Utekelezaji wa Mpango wa Uwezeshaji wa Utafiti na Ubunifu kwa Ardhi Endelevu na Usimamizi wa Mazingira kwa Maendeleo ya Pamoja ulibaini kuwa ufuatiliaji dhaifu wa maendeleo ya

utafiti kwa waratibu wa programu ulikuwa miongoni mwa vyanzo vilivyosababisha kuchelewa kukamilika kwa tafiti ndogo wakati wa utekelezaji wa programu hiyo.

Kwa kuongezea, Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ulibaini kuwa, kulikuwa na udhaifu katika ufuatiliaji na utekelezaji wa adhabu kwa wanufaika wa mikopo waliokaidi kurejesha mikopo yao wakati wa kuandaa mikakati ya urejeshaji wa mikopo. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa kitengo cha ufuatiliaji na tathmini hakikuweza kutoa miongozo kwa vitengo na idara za Bodi ya Mikopo kuhusu taarifa zinazopaswa kukusanywa na kuchakatwa ili kupima utendaji wa idara hizo.

Kwa mfano, vitengo vya ufuatiliaji na tathmini vilitegemea kukusanya taarifa kwa kutumia malengo mapana sana. Kitengo hakikuandaa mpango wa ufuatiliaji ambao ulizingatia ufuatiliaji wa shughuli za ukusanyaji wa mikopo katika kipindi chote cha ukaguzi. Hii ilikuwa kinyume na matakwa ya Mipango-mkakati miwili ya mwaka 2011 hadi 2014 na 2014 hadi 2017 ambayo iliainisha kwamba Bodi ya Mikopo ilitakiwa kufuatilia shughuli zake kupitia kitengo cha ufuatiliaji na tathmini.

Ukaguzi huu wa ufanisi pia ulibaini kuwa, hakukuwa na ukaguzi binafsi wa kitaasisi na mapitio huru ya shughuli za ulipaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa uwezo wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ambao ungeiwezesha Bodi ya Mikopo kutathmini uwezo na udhaifu wake kuhusu shughuli za ukusanyaji wa mikopo. Pia, ukaguzi uligundua kuwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2012/13 hadi 2016/17, Bodi ya Mikopo ilishindwa kutathmini utendaji wake katika kuhakikisha ulipaji na urejeshaji wa mikopo unafanyika kama inavyotakiwa.

(c) Kutokuwepo kwa Utoaji Unaoridhisha wa Taarifa za Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Ukaguzi wa ufanisi uliofanyika pia ulibaini kutokuwepo kwa utoaji unaoridhisha wa taarifa za matokeo ya ufuatiliaji na tathmini. Kwa mfano, Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Upatikanaji wa Elimu Bora ya Ufundi na Mafunzo Stadi ulibaini kutokuwepo kwa utaratibu wa utoaji wa taarifa za utendaji katika utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

Pia, Ukaguzi wa ufanisi kuhusu Usimamizi wa Ulipaji na Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu ulibaini kuwa mbali na mkurugenzi wa elimu ya juu kutoka wizara ya elimu kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo, Wizara haikuwa na taarifa zozote za mwaka za utendaji kutoka Bodi ya Mikopo kwa kipindi chote cha miaka mitano ya fedha.

Ukaguzi wa Ufanisi juu Utendaji wa Programu ya Mifumo ya Uendelezaji wa Ubora wa Utafiti na Ubunifu nchini ulibaini kuwa taarifa zilizokuwemo kwenye taarifa za utendaji za kila mwaka hazikuwiana. Mambo yaliyoripotiwa hayakulenga kushughulikia malengo yaliyowekwa ya kuboresha uwezo wa utafiti, mafunzo, na uzalishaji wa tafiti. **Jedwali 11.2** linaonesha hali ya utoajia wa wa ripoti katika kila mwaka wa fedha yaani kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2018/19.

Jedwali 11.2: Mapungufu katika Kuripoti Maendeleo ya Programu

Mipango	Kuripoti mafanikio			
	2015/16	2016/17	2017/18	2018/19
Ongezeko la idadi ya tafiti zilizoshinda ruzuku kutoka vyanzo vya nje kwa taasisi za utafiti na maendeleo (angalau 2-4 kila mwaka) kufikia mwaka 2020	Imeripotiwa (Uundaji wa kikundi)	Haijaripotiwa	Imeripotiwa (Uundaji wa kikundi)	Imeripotiwa (timu 1-2 za watafiti wadogo walipokea misaada)
Kuongezeka kwa bidhaa na huduma (10-20) kutoka kwa Taasisi za Utafiti na Maendeleo ambazo	Haijaripotiwa	Haijaripotiwa	Haijaripotiwa	Haijaripotiwa

zinatoa vipaumbele vya maendeleo endelevu ifikapo Juni 2019				
Ongezeko la usambazaji na upokeaji wa matokeo ya utafiti (angalau 3 kwa mwaka)	Haijaripotiwa	Haijaripotiwa	Haijaripotiwa	Haijaripotiwa

***Vyanzo**: Mipango ya Mwaka na Ripoti za Maendeleo (2015 / 16-2019 / 2020)*

Jedwali 11.2 linaonesha kuwa katika mwaka wa fedha 2016/17, ripoti ya maendeleo haikujumuisha mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo ya programu. Pia, hakukuwa na mwaka wowote wa fedha ambapo taarifa zilitolewa kwa kuzingatia matakwa ya mkataba wa programu.

(d) Utekelezaji wa Kiwango cha Chini cha Mapendekezo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Ukaguzi wa ufanisi uliofanyika ulibaini kuwepo kwa kiwango cha chini cha utekelezaji wa mapendekezo ya ufuatiliaji yaliyotolewa. Hii ilibainika katika Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Upataji wa Elimu na Mafunzo Bora ya Ufundi Stadi ambapo ulionesha kuwa mapendekezo mengi yaliyotolewa kwa vyuo vinavyotoa elimu na mafunzo ya ufundi stadi hayakutekelezwa ipasavyo. Mapitio ya ripoti za ufuatiliaji na tathmini ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi yalibaini kuwa Mamlaka ilikuwa ikitoa mapendekezo yanayofanana kwa vyuo vyote kwa takribani miaka mingi bila kuwepo kwa mabadiliko makubwa, au utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa.

11.3.2 Sababu za Ufuatiliaji Usiofaa wa Shughuli Zilizofanywa wakati wa Utoaji wa Huduma za Elimu

(a) Ukosefu wa viashiria vikuu vya utendaji

Viashiria vya utendaji ni sehemu muhimu ya mfumo wowote wa ufuatiliaji na tathmini kwani hutumika kama kigezo cha kupima kiwango kilichofikiwa kuhusu malengo yaliyowekwa. Kwa hiyo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, na OR-TAMISEMI na watekelezaji wengine walihitajika kuunda viashiria hivyo ili kupima utendaji wa vyombo vilivyoko chini ya Mamlaka yao.

Mapitio ya taarifa za ukaguzi zilibaini kuwa hakukuwa na viashiria vya utendaji vilivyowekwa ili kupima kiwango na hali ya utekelezaji wa utoaji wa huduma ya elimu nchini. Hii ilibainika hasa katika eneo la uimarishaji wa utafiti na ubunifu.

(b) Kutokuwepo kwa Kanzidata

Ukosefu wa kanzidata uliripotiwa kama sababu ya kuwepo kwa ufuatiliaji duni. Kwa mfano, Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Upatikanaji wa elimu Bora ya Ufundi na Mafunzo Stadi ulibaini kuwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya UFundi Stadi haikutengeneza kanzidata ili kurahisisha ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa wakati wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini.

11.3.3 Matokeo ya Ufuatiliaji Usiofaa wa Shughuli za Utoaji wa Huduma za Elimu

Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Utoaji wa Mafunzo kwa Walimu Walio kazini ulibaini kuwa, kukosekana kwa viashiria vya utendaji kwa ajili ya kupima utendaji wa utoaji wa mafunzo ya walimu walio kazini kuliathiri utoaji wa maamuzi wakati wa utoaji wa huduma za elimu. Ukaguzi pia ulibaini kuwa, vyombo kama vile Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu na vikundi vya wataalamu vilishindwa kubaini ufanisi wa mafunzo yanayotolewa kwa walimu walio kazini. Pia, ukaguzi huo ulibaini kuwa, ukosefu wa ufuatiliaji mzuri wa utoaji wa elimu kulipelekea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kushindwa kufuatilia jinsi maarifa yalivyorithishwa kwa watu.

Pia, Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Upatikanaji wa Elimu Bora ya Ufundi na Mafunzo Stadi ulionesha kuwa kutofanyika kwa ziara kwa watoahuduma ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi kuliongeza hatari ya kukiuka viwango vya usajili na hivyo kuathiri ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

SURA YA KUMI NA MBILI

HITIMISHO

12.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha mahitimisho yaliyotokana na mapitio na uchambuzi wa masuala yaliyojadiliwa katika ripoti tisa za ukaguzi wa ufanisi katika sekta ya elimu nchini.

12.2 Hitimisho la Jumla

Kwa ujumla, kaguzi za ufanisi zilizofanyika zinatambua mchango wa Serikali katika kuendeleza sekta ya elimu nchini. Hata hivyo, mambo yaliyobainika katika ripoti hizi zilizojumuishwa yanapelekea kuhitimisha kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa bado hazijasimamia utoaji wa huduma za elimu katika namna yenye kuleta tija katika ngazi zote kuanzia elimu ya msingi, sekondari, ufundi, pamoja na vyuo vikuu.

Hii ni kwa kuwa Wizara hizo mbili hazikutekeleza kwa tija shughuli zinazohakikisha uwepo wa miundombinu toshelezi katika ngazi zote za elimu kuanzia msingi hadi chuo kikuu ili kuwa na mazingira rafiki ya kujifunzia kwa wanafunzi wote ikiwa pamoja na wale wenye mahitaji maalumu.

Juhudi zaidi inahitajika ili kuboresha utoaji wa mafunzo ya kujenga uwezo ili kuboresha ushindani wa walimu katika ngazi zote za elimu. Shughuli nyingi zilizofanyika zilihusu utoaji wa mafunzo na kusahau mambo mengine ya ujengaji wa uwezo kama vile programu za walimu wapya, usimamizi, pamoja na msaada mwingine wa kitaaluma kupitia miongozo ya mafunzo na majarida ya kujifunzia.

Zaidi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haijatekeleza jukumu lake ipasavyo la kuhakikisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inatekeleza majukumu yake kiutendaji katika ukusanyaji wa mikopo ili kuhakikisha uwepo wa chanzo endelevu cha ufadhili wa elimu ya juu. Vilevile, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikufuatilia utendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika shughuli za ukusanyaji na urejeshaji wa mikopo. Hali hii ilizuia upatikanaji kwa usawa

wa elimu ya juu kwa wanafunzi wenye vigezo kutokana na mikopo ambayo haijalipika ambayo ingetumika kufadhili wanafunzi wengine.

Pia, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikuweza kuhakikisha kuna upatikanaji wa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi ili kuwa na ukuaji wa ujuzi na kukidhi mahitaji ya soko na ya nchi kwa ujumla.

12.3 Hitimisho Maalumu

12.3.1 Rasilimali Zisizotosheleza Zilitolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja na OR-TAMISEMI kwa ajili ya Utoaji wa Elimu

Imehitimishwa kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI hazikuweka mipango, hazikutenga bajeti, na hazikutenga rasilimali zinazotosheleza ili kuwezesha shughuli anuwai zinazolenga kuimarisha utoaji wa huduma bora za elimu.

Hii ilisababisha utekelezaji wa shughuli kwa kutegemea maamuzi ya siku husika. Kwa mfano, OR-TAMISEMI haikuwa na mipango ya muda mrefu ya kudhibiti changamoto mbalimbali za elimu juu ya maendeleo na matengenezo ya miundombinu. Hakuna wizara, kati ya hizi mbili, iliyopanga na kuweka bajeti ya kutosha kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Vivyo hivyo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI hazikuwa na mikakati na mipango endelevu ya kuwajengea uwezo walimu walio kazini. Hatua za kuwajengea uwezo walimu walio kazini zilitegemea zaidi miradi inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo ambayo ilichukua muda wa miaka mitatu hadi minne kuhitimishwa.

Licha ya ulipaji wa mikopo kuwa miongoni mwa vyanzo vya fedha vya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikutoa maagizo, mwongozo, au maelekezo kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo kuhusu mafanikio yasiyoridhisha ya ukusanyaji wa mikopo au ucheleweshaji wa utekelezaji wa shughuli za kurejesha mikopo. Badala yake, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilijikita zaidi kufanya ufuatiliaji wa karibu wa masuala ya bajeti na utoaji wa mikopo ili iweze kutolewa kwa wanafunzi waliohitimu.

12.3.2 Udhibiti wa Ubora wa Elimu

Ukaguzi unahitimisha kwamba mifumo ya udhibiti na uhakiki ubora katika utoaji wa elimu ya msingi na sekondari haifanyi kazi ipasavyo kutokana na uchache wa wahakiki ubora wenye ujuzi. Vivyo hivyo, mapendekezo kutoka kwa wakaguzi wa shule hayatekelezwi kwa ukamilifu kutokana na kwamba ni asilimia 39 pekee ya mapendekezo yalikuwa yakitekelezwa huku asilimia 61 yakiwa hayajatekelezwa. Vivyo hivyo, kumekuwa na ukaguzi hafifu wa miundombinu ya shule za msingi kutokana na shule za msingi na sekondari kutokaguliwa.

Ukaguzi unahitimisha zaidi kwamba mifumo ya uhakiki ubora katik ngazi ya elimu ya juu imeundwa lakini inahitaji maboresho zaidi. Kwa mfano, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kiliimarisha na kukipandisha hadhi kitengo kuwa idara kamili ikiwa na miongozo ya utendaji na ilianza kufanya kazi kuanzia mwaka 2017. Hali hii ni tofauti na ya Chuo Kikuu cha Ardhi kwa kuwa zana za uhakiki ubora hazifanyi kazi ipasvyo na hasa zile zinazohusu shughuli za utafiti.

12.3.3 Utoaji Hafifu wa Elimu ya Msingi na Sekondari

Ukaguzi ulihitimisha kwamba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI hazikuhakikisha utoaji bora wa elimu ya msingi na sekondari. Hii ni kwa sababu hazikuhakikisha uwepo wa mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wote.

Shule za msingi na sekondari hasa za umma zilikuwa na miundombinu isiyokidhi mahitaji na chakavu, ambayo mara nyingi haikuzingatia mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Kwa mfano, wanafunzi milioni 4 sawa na asilimi 48 wa shule za msingi hawakuwa na vyumba vya madarasa; wakati wanafunzi milioni 5.4 sawa na asilimi 65 ya wanafunzi wa shule za msingi hawakuwa na matundu ya vyoo.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI hazikuwa na mikakati ya kuwajengea uwezo walimu. Mafunzo yalitolewa kwa walimu wachache waliokuwa na mahitaji fulani ya taaluma na kuwaacha walimu wengine wenye mahitaji sawa. Kwa kuongezea, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI hazikuwa na mikakati ya kuhakikisha uendelevu wa uwezo waliojengewa walimu, kwa kuwaendeleza wakiwa

kazini ili waweze kuhamisha maarifa waliyopata kwa walimu wenzao kwa njia ilivyopangwa.

Zaidi ya hayo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI hazikuwa na kanzidata iliyoratibiwa hivyo hakukuwa na utaratibu maalumu wa usimamizi wa kazi zilizopangwa kwa elimu ya shule za msingi na sekondari.

12.3.4 Mapungufu katika utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu

Bila kujali matakwa ya kuwepo kwa mazingira rafiki ya utoaji wa elimu maalumu, bado Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI hazikusimamia utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Hii ni kwa sababu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI hazikuhusisha ipasavyo shughuli za elimu maalumu katika mipango yao. Hali hii imeathiri mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Katika ngazi ya taifa, hakuna taarifa za kina kuhusu idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na walimu wa elimu maalumu. Taarifa hizo zingeweza kusaidia kuboresha utoaji na uratibu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia elimu maalumu.

Aidha, shughuli za udhibiti ubora wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hazichangii kwa kiwango cha kutosha kuboresha utoaji wa elimu maalumu, na utungaji na usimamizi wa mitihani. Ufundishaji na utahini wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu hauhusishi kwa kiwango cha kutosha mahitaji yao.

12.3.5 Ujengaji Uwezo Usioridhisha kwa Walimu Walio Kazini

Licha ya jitihada za Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI za kuboresha ujengaji uwezo kwa walimu walio kazini hatua zaidi zinahitajika ili kuimarisha zaidi. Hii ni kwa sababu, katika ngazi ya taifa, ni asilimia 18 tu ya walimu walio kazini ndio wamejengewa uwezo tena kwa kuzingatia masomo ya stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu kwa madara awali na ya chini ya elimu ya msingi.

Kwa ujumla, mafunzo yaliyotolewa kama sehemu ya kujengea uwezo walimu walio kazini hayakushughulikia masuala yote ya taaluma ya ualimu, kama vile tathmini, elimu jumuishi, maudhui, na mbinu za kufundishia Zaidi ya hayo, aina zingine za kujenga uwezo kama vile ushauri-elekezi na msaada wa kitaaluma endelevu hazikutolewa.

12.3.6 Utoaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Pamoja na juhudi zilizofanywa, ukaguzi unahitimisha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haijawahakikishia kwa ufanisi Watanzania kupata elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi ili kuimarisha maendeleo ya ujuzi wao na kukidhi mahitaji ya soko la ajira na mahitaji mapana ya kiuchumi.

Bado kuna upatikanaji mdogo wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi miongoni mwa waombaji wanaokidhi sifa za kujiunga. Vilevile, wanafunzi wachache wenye ulemavu wamedahiliwa katika vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi ikilinganishwa na wale wasio na ulemavu.

Hakuna fedha za kutosha na kwa wakati za kushughulikia elimu na mafunzo ya ufundi stadi. vilevile, hakuna ufuatiliaji na tathmini ya kutosha ya utendaji wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika utekelezaji wa jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi.

12.3.7 Utekelezaji wa Miradi ya Tafiti katika Taasisi za Elimu ya Juu

Ukaguzi ulihitimisha kwamba licha ya kuwa na uchelewaji wa kufikia malengo ya miradi ya elimu na utafiti katika taasisi za elimu ya juu na utafiti, kulikuwa na matumizi ya fedha chini ya kiwango tarajiwa katika ngazi ya miradi kwa ujumla na kwa vipengele vya miradi. Hii ni kwa kuwa baadhi ya miradi na vipengele vya miradi havikutekelezwa ipasavyo. Matokeo yake, fedha ambazo hazikutumika zilibadilishiwa matumizi na kutumika kufadhili masomo na utafiti kwa wanafunzi.

Udhaifu wa kudhibiti ubora wakati wa kuandaa mipango ya miradi na kutengeneza malengo na viashiria vya utekelezaji wa miradi ulipelekea taaasisi za elimu ya juu kuwa na malengo na viashiria visivyo na uhalisia. Hali hii ilipelekea kuwa na ugumu katika kuainisha mafanikio ya mradi.

Inahitimishwa zaidi kwamba taasisi za elimu ya juu hazikufanya kazi ipasavyo kuhakikisha uwepo na matumizi ya matokeo ya tafiti kwa kuongeza machapisho na majarida yanayopatikana mitandaoni kitaifa na kimataifa.

12.3.8 Mikopo ya Wanafunzi Elimu ya Juu

Utekelezaji wa shughuli za ulipaji na urejeshaji mikopo haukuwa wa kuridhisha. Kwa mfano, kati ya shughuli 39 ambazo zilipangwa na Bodi ya Mikopo kupitia mipango-mkakati yake miwili, ni shughuli 4 tu ndizo zilitekelezwa kikamilifu, shughuli 20 zilikuwa zikiendelea kutekelezwa, na shughuli 15 haikutekelezwa kabisa. Baadhi ya shughuli hizi zililenga kutoa ushirikiano na wadau wengine ili kuboresha ufuatiliaji wa wanufaika wa mikopo na kuboresha na kupanua wigo wa njia za ulipaji na ukusanyaji wa mikopo.

Malengo ya Bodi ya mikopo hayakuwa mahususi kuhusu ulipaji na urejeshaji wa mikopo. Kwa upande mwingine, kutathmini utendaji wa ukusanyaji wa mkopo kwa kutumia malengo ya jumla ya Bodi bila kuyahusisha na ukusanyaji wa mikopo ilileta hatari ya kupuuza shughuli zingine zihusuzo marejesho ya mikopo. Kwa mfano, shughuli za urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wadaiwa sugu hazikupewa umakini wa kutosha katika ukusanyaji wa mikopo. Vivyo hivyo, idadi ya wanufaika wa mkopo kutokujulikana ndani ya kanzidata na malengo ya Bodi ya Mikopo imepunguza wigo wa uchambuzi na ufafanuzi wakati wa kupima utendaji.

Kutotumia vihatarishi na kanzidata katika kusimamia ulipaji na urejeshaji wa mikopo kulichangia kushindwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mikopo. Bodi haikuweka maelezo ya vihatarishi kwa walengwa wake wote katika kanzidata ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Hivyo, uchaguzi wa njia za kutumia kutafutia walengwa wa mikopo hazikuongozwa na viwango cha vihatarishi vilivyowekwa kwa wanufaika wa mikopo.

Usimamizi Mdogo wa Wizara ya Elimu katika Kusimamia Majukumu ya Bodi ya Mikopo

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikutekeleza jukumu lake katika kuhakikisha kuwa Bodi ya Mikopo inafanya vizuri katika ukusanyaji wa

mkopo ili kuwa na chanzo endelevu cha ufadhili wa elimu ya juu. Vivyo hivyo, Wizara haikufuatilia na kufanya tathmini juu ya utendaji wa Bodi ya Mikopo katika shughuli za ulipaji na urejeshi wa mikopo. Pamoja na Mkurugenzi wa Elimu ya Juu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo, hakukuwa na ripoti rasmi za utekelezaji za mwaka ambazo ziliandaliwa na kuwasilishwa Wizarani na Bodi ya Mikopo. Pamoja na kuwa mjumbe wa Bodi, Mkurugenzi wa Elimu ya Juu hakuwa mjumbe wa Kamati ya Bodi ambayo ilijadili masuala ulipaji na urejeshaji wa mikopo.

12.3.9 Uratibu Duni katika Utoaji wa Elimu

Wakaguzi walibaini uratibu duni katika ngazi mbalimbali za utoaji wa elimu na miongoni kwa watendaji wa elimu ikiwemo ngazi ya wizara, mikoa, halmashauri, vyuo vikuu, na shule. Taarifa mbalimbali za elimu hazikushirikishwa kwa wadau muhimu kutoka wizarani. OR-TAMISEMI haikuanzisha mipango iliyoruhusu uratibu katika ngazi za wilaya na mikoa katika utekelezaji wa shughuli za elimu ili kufikia lengo lililowekwa. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa sera ya taifa ya kupanga na kutekeleza maendeleo ya ujuzi katika elimu na mafunzo ya ufundi stadi katika Wizara, pamoja na wadau kutoshirikishwa malengo yatakayotimizwa pamoja nao.

Ukaguzi umebaini ufuatiliaji hafifu wa utendaji wa utoaji wa huduma za elimu ambao ulichangiwa na kutokuandaa viashiria muhimu vya utendaji na idadi isiyotosha ya shughuli za ufuatiliaji ambazo zilitekelezwa. Pia, ilibainika kuwa njia za kufuatilia jinsi shughuli zilivyofanywa kutoka ngazi ya vituo vya uvumbuzi hadi halmashauri hazikuwa sawa. Aidha, ukaguzi ulibaini taarifa zisizoridhisha za matokeo ya ufuatiliaji na tathmini hali iliyosababisha utekelezaji wa kiwango cha chini cha mapendekezo katika ufuatiliaji na tathmini.

SURA YA KUMI NA TATU

MAPENDEKEZO

13.1 Utangulizi

Ili kutatua changamoto katika utoaji wa elimu, mapendekezo kadhaa, yametolewa kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na OR-TAMISEMI kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

13.2 Mapendekezo Maalumu ya Ukaguzi

13.2.1 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapaswa:

1. Kuanzisha utaratibu endelevu wa kufadhili shughuli zote za elimu maalumu na kuhakikisha shughuli za mapitio ya mtaala, utunzi na usimamizi wa mitihani, udhibiti ubora wa shule, na mafunzo kwa walimu wa elimu maalumu yanapatiwa kipaumbele na kutengewa fedha katika bajeti;

2. Kuhakikisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaanzisha mfumo wa utambuzi wa mikopo hatarishi na kuunganisha na mikakati yake ya ulipaji na urejeshaji wa mikopo ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali hususani katika kufuatilia na kukusanya madeni ya mikopo;

3. Kuhakikisha taasisi za elimu ya juu nchini zinaboresha mifumo yao ya usimamizi wa rasilimali-fedha na kuanzisha utaratibu utakaowezesha maombi na utolewaji wa fedha kufanyika kwa wakati ili shughuli za utekelezaji wa shughuli za programu zifanyike kwa wakati;

4. Kuhakikisha kuwa taasisi za elimu ya juu zinaboresha uwezo wao wa kusimamia miradi hasa inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo ili kupunguza ucheleweshaji na kushindwa kufikia malengo ya programu husika;

5. Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini za elimu na mafunzo ya ufundi stadi ili kuhakikisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi inatoa elimu na mafunzo bora ya ufundi stadi; na

6. Kuhakikisha kuwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi inaanzisha na kutekeleza mpango endelevu wa kuboresha majengo na upatikanaji wa vifaa vya kisasa katika vyuo vyote vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

13.2.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja na OR-TAMISEMI

Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja na OR-TAMISEMI zinapaswa:

1. Kuhakikisha kuwa rasilimali zilizotengwa (fedha pamoja na wafanyakazi wataalamu) kwa ajili ya utoaji wa elimu na mafunzo zinatolewa kama ilivyopangwa na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa;

2. Kuanzisha utaratibu na kupanga kwa ajili ya kuimarisha uratibu baina ya watendaji katika ngazi zote za utoaji elimu ili kuhakikisha taarifa zinafika kwa urahisi katika ngazi zote za kiutendaji;

3. Kuimarisha uwajibikaji katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na wadhibiti ubora wa shule ili kuwezesha utoaji wa elimu bora nchini;

4. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa wahusika katika utoaji wa elimu; na

5. Kufuatilia kwa ukaribu na kutekeleza matumizi ya mafunzo ya mara kwa mara kwa wataalamu, huku msisitizo zaidi ukiwekwa kwenye kuhakikisha hatua endelevu zinawekwa kwenye kuwaendeleza walimu shuleni.